

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA ISHIRINI**

**Kikao cha Nane – Tarehe 16 Juni, 2010**

*(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:**

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka 2009/2010 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZAN:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**MASWALIA NA MAJIBU**

Na. 55

## **Serikali Kuimarisha Barabara Wilayani Rungwe**

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Rungwe ni mionganoni mwa Wilaya zenye mvua nyingi hapa nchini hadi kufikia kati ya mm 900 – mm1250 kwa mwaka, na kwa kuwa mvua nyingi husababisha uharibifu mbaya wa barabara hasa za Vijijini na kukwamisha usombaji wa chai mbichi kutoka kwa wakulima wadogo wa wilaya hiyo:

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha barabara hizo zinaimarishwa na kupitika kwa mwaka mzima?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIKOA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ina mtandao wa barabara wenye jumla ya urefu wa kilomita 1,033.3. Mchanganuo wa barabara hizo ni kama ifuatavyo.

Barabara Kuu (*Trunk Road*) - km 64.4

Barabara za Mkoa (*Regional Roads*) - km 205.8

Barabara za Wilaya (*District Roads*) - km 463.1

Barabara za Mjazio (*Feeder Roads*) - km 300

Mheshimiwa Spika, barabara kuu (*Trunk Roads*) na za Mkoa (*Regional Roads*) zinahudumiwa na Wakala wa barabara yaani *TANROADS* Mkoa wa Mbeya, barabara za Wilaya yaani *District Roads* na za Mjazio yaani *Feeder Roads* zinahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe. Aidha, barabara za jamii zinahudumiwa na wananchi wenywewe.

Mheshimiwa Spika, barabara zinazotumika kukusanya chai ziko katika kundi la barabara za mjazio (*Feeder Roads*) na kwa kiasi kikubwa haziko katika hali ya kutengenezeka (*Non – maintenance*). Hivyo kuhitaji ukarabati. Hata hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kwa kushirikiana na wakulima wa chai inajitahidi kuzifanyia barabara hizo matengenezo madogo madogo ya sehemu korofii ili ziweze kupitika kwa wakati wote.

Mheshimiwa Spika, lengo la matumizi ya fedha za Mfuko wa barabara kwa Halmashauri ni kuhakikisha kuwa barabara zilizo katika hali ya kutengenezeka

(*Maintanance Roads*) zinapata matengenezo ili ziweze kupidika na kudumu kwa muda mrefu. Kwa barabara ambazo haziko katika hali nzuri (*Non – maintenable Roads*) na hivyo kuhitaji ukarabati, ninaishauri Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kuziweka katika vipaumbele vyake na kuzitengea bajeti kutoka vyanzo mbalimbali mfano TASAF, fedha za ruzuku za maendeleo, mapato ya Halmashauri na kadhalika. ili kuzifanya barabara hizo ziwe katika hali nzuri na wakulima waweze kusafirisha chai.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009 bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ilikuwa ni Sh. 439,965,000/= na katika mwaka 2009/2010 bajeti ilikuwa ni shilingi 485 na zote zinatokana na Mfuko wa Barabara. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Halmashauri ya Rungwe imetenga shilingi milioni 730, kutoka mfuko wa barabara. Ninaishauri Halmashauri iweke kipaumbele katika kutengeneza barabara hizo zinazohusika katika kusafirisha zao la chai.

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii, nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Hizi barabara za mazao kama Chai, Kahawa na kadhalika ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. Kwa nini inapofikia hatua kubwa namna hii na uwezo wa Halmashauri ukawa mdogo kwa nini Serikali isiingilie kati na kuweza kuchangia fedha ya kutosha ili barabara hizi ziwe *maintainable*?

Kwa kuwa, barabara ya Katumba – Tukuyu iliyohidiwa na Mheshimiwa Rais kutengenezwa kwa kiwango cha lami na ambayo inasidia sana kusomba Chai kutoka kwa wakulima kupeleka katika viwanda vya Mwakaleli na Katumba nayo pia ingeweza kusaidia sana kama ingeweza kutengenezwa. Je, Serikali hivi sasa katika mipango yake imefikia hatua gani ili barabara hii ifikiwe kutengenezwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIKOA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swalii la kwanza na la pili nitaeleza majibu yake kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa mimi kabla ya kuja hapa ninataka niseme kwamba nilifanya ziara katika Mkoa wa Mbeya, na ninataka nithibitishe kwamba Mheshimiwa Cynthia Ngoye anachozungumza hapa ni kweli kwa sababu Rungwe nilikwenda na nikakaa pale siku tatu na hizi barabara anazozizungumzia ni kweli zinaonekana kwamba zina hali mbaya.

Kwa faida ya Bunge hili nataka nithibitishe hapa kwamba zao linalozungumzwa hapa si kama mazao mengine, ni zao la Chai. Chai ikikuchenga siku moja kama umevuna leo imekuchenga basi inaharibika. Kwa hiyo, *the Member of Parliament* anachosema hapa ni *correct* kabisa hiyo naiona na ninajua anachozungumza hapa.

Sasa analiza swalii hapa anasema kwamba kama ninyi mnajua hivyo ni kwa nini basi msitoe kipaumbele katika jambo hili? Nimeeleza humu ndani kwamba Bajeti ya Wilaya ya Rungwe wanaaoi-determine ni watu wa Rungwe wenyewe, wao ndiyo wanaosema sisi hiki ni kipaumbele wanapeleka pale. Fedha iliyotengwa sasa hivi tunavyozungumza hapa ni shilingi milioni 540 ni hela kidogo sana hazitoshi, nikasema

kwamba unaweza ukachukua hela za maendeleo ukazipeleka katika hizi barabara anazosema, unaweza ukachukua hela za *TASAF* kwani *TASAF* unaweza ukasema kwamba sisi kipaumbele kwetu ni barabara akapeleka pale, anaweza akafika mahali akasema lakini pamoja na hayo hazitoshi. Mimi nataka niseme hivi, tuombe basi Bunge hili lipitishe Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ili hayo yote ambayo Mbunge anazungumza hapa yaweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili ameuliza swali ambalo liko kwenye barabara ya *TANROAD* na mimi hapa najibu maswali yanayomhusu Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa hii barabara anayoisema hapa ni barabara kubwa ya lami ambayo Mheshimiwa Rais alikuwa ametoa. Sasa naomba kama utakubali kwa sababu na mhusika mwenyewe nina hakika kwamba yuko hapa aweze kufanya hivyo, lakini kama nitatakiwa kusema hivyo basi nitapeleka hiyo taarifa kwa Waziri halafu Waziri akinijibu nitampelekea majibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kwa majibu ya ziada!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hilda Cynthia Ngoye, kama ifuatavyo.

Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpa hongera yeye Mheshimiwa Mbunge pamoja na Mheshimiwa Prof. Mwakyusa na Prof. Mwadosya ambao kwa mara nyingi sana walikuwa wanafuutilia kuhusu barabara hii kwa karibu kila mara.

Niseme kwamba kila mara barabara hiyo tumeitambua kwamba ni barabara muhimu sana, Mheshimiwa Rais aliitolea ahadi na tumeshafanya kazi kubwa pamoja na kuifanyia upembuzi yakinifu pamoja na usanifu wa barabara hiyo. Katika mchakato wa mwaka unaokuja wa fedha tumependekeza kutengea fedha na tutaanza na ujenzi wa madaraja mawili Mbaka na Malisi.

Mheshimiwa Spika, kama Bunge lako Tukufu litapitisha Bajeti hiyo basi kazi hiyo tutaianza ndani ya mwaka wa fedha ujao. (*Makofî*)

**SPIKA:** Tunaendelea sasa kwani tumechukua muda mrefu kwa swali hili na swali linalofuata linalekezwa Ofisi ya Makamu wa Rais na linaulizwa na Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis wa Magogoni.

Na. 56

**Mambo Yaliyoorodheshwa Katika Hati ya  
Muungano ya Mwaka 1964**

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa mnamo mwaka 1964 Hayati Baba wa Taifa na Hayati Mzee Karume walitia saini Hati ya Muungano ili kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar:-

- (a) Je, ni mambo mangapi yaliyoanishwa katika Hati hii kama mambo ya Muungano?
- (b) Je, mambo mengine ya ziada katika orodha ya mambo ya Muungano yaliongezwa lini na kwa utaratibu gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis Mbunge wa Magogoni lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika mwaka 1964 Hati ya Muungano iliorodhesha mambo kumi na moja ya Muungano ambayo ni:-

- (i) Katiba ya Serikali ya Muungano.
- (ii) Mambo ya Nchi za Nje.
- (iii) Ulinzi.
- (iv) Polisi.
- (v) Mamlaka juu ya mambo yanayohusu hali ya hatari.
- (vi) Uraia.
- (vii) Uhamiaji.
- (viii) Mikopo na Biashara ya Nchi za Nje.
- (ix) Utumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano.
- (x) Kodi ya Mapato inayolipwa na watu binafsi na mashirika, ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa zinazotengenezwa nchini Tanzania unaosimamiwa na Idara ya Forodha.

- (xi) Bandari, mambo yanayohusika na usafiri wa anga, posta na simu.
- (b) Kuongezeka kwa mambo ya Muungano. Mambo ya Muungano yaliongezeka kutoka kumi na moja (11) hadi (22) kutokana na mahitaji ya ndani pamoja na mabadiliko yaliyokuwa yanaendelea ndani ya nchi na ulimwengu baada ya Muungano kuasiwi. Mambo mengine 11 yaliyoingizwa ni kama yafuatavyo:-
- (i) Mwaka 1965, jambo la kumi na mbili linalohusu mambo yote yanayohusika na sarafu na fedha kwa ajili ya malipo yoyote halali (pamoja na noti); Mabenki (pamoja na mabenki ya kuweka akiba na shughuli zote za mabenki), fedha za kigeni na usimamizi juu ya mambo yanayohusika na fedha za kigeni liliongezeka na kuingizwa katika Katiba ya muda ya mwaka 1965. Sababu ilikuwa ni kuwa na sarafu ya pamoja, kurahisisha usimamizi wa fedha za kigeni na mabenki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- (ii) Katika mwaka 1967 kufuatia kuundwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, mambo matatu (3) yaliongezwa katika orodha ya mambo ya Muungano ambayo ni Leseni za viwanda na takwimu, Elimu ya Juu na Usafirishaji wa anga.
- (iii) Katika mwaka 1968, Maliasili ya Mafuta, pamoja na mafuta yasiyochujwa ya motokaa na mafuta ya aina zote za petrol na aina nyinginezo za mafuta au bidhaa na gesi asilia yaliongezwa kwenye orodha ya mambo ya Muungano.
- (iv) Mwaka 1977 liliongezwa jambo la Baraza la Mitihani la Taifa na mambo yote yanahuksika na kazi za Baraza hilo.
- (v) Kutokana na kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki mwaka 1977, mambo matatu (3) yaliyokuwa na upande wa Tanganyika na Zanzibar yaliyokuwa yakisimamiwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki yalikuwa yakisimamiwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki, yalikabidhiwa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na yaliingizwa katika orodha ya mambo ya Muungano. Mambo yaliyoongezwa ni haya yafuatayo:- Utafiti, Utabiri wa Hali ya Hewa na Takwimu.
- (vi) Mwaka 1979 liliongezwa jambo la Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano.
- (vii) Mwaka 1992 kufuatia mabadiliko ya mfumo wa siasa nchini suala la ishirini na mbili la uandikishaji wa vyama vya siasa na mambo mengine yanayohusiana nayo yaliongezwa kwenye orodha ya mambo ya Muungano.

Utaratibu uliotumika kuongeza orodha ya mambo ya Muungano na uliopo Kikatiba ni ule wa Serikali kupeleka Mswada Bungeni ili watoe baraka zao kwa kura kwa mujibu wa taratibu. Kwa mambo yote yaliyoongezwa Wabunge wa pande zote za Muungano walikubali kwa kupiga kura kwa kila upande kwa idadi ya kura za Wajumbe wasiopungua theluthi mbili kutoka kila upande.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, Serikali inapoongeza au kupunguza kitu kwenye mambo ya Muungano utaratibu wake unakuwaje?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:**  
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo.

Kwanza ninaomba Waheshimiwa Wabunge waelewe kwamba muungano huu ni wa ubia na wa hiari kwa hiyo kila Serikali ni lazima ishiriki katika mabadiliko yoyote yanayotokea.

Utaratibu wa kwanza ni kwamba imejengwa hoja ama Serikali ya Muungano au Serikali ya Zanzibar na hoja inapokubalika inakwenda kwenye Baraza la Mawaziri la Muungano au Serikali ya Zanzibar na hoja hii baada ya kukubalika inakwenda kwenye Baraza la Mawaziri la Muungano ambalo ndani yake kunakuwa na Mawaziri kutoka Zanzibar na kutoka Bara, inajadiliwa na baadaye unaundwa Muswada ambao unaletwa Bungeni hapa na baadaye Bunge linapiga kura na kwa taratibu zetu za Katiba yetu kwa mambo yote yale ambayo ni ya Muungano huwezi kuyandoa au kuyaweka bila kupiga kura theluthi mbili kwa kila upande na hivyo kupigwa kura hapa Bungeni na jambo hilo huondolewa au huingizwa.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi na pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake sahihi. Pia imefurahi kusikia kwamba Wizara ya Mambo ya ndani imo katika mambo ya Muungano na Mungu aijaalie iendelee hivyo hivyo. Lakini ndani ya Wizara hii ya Mambo ya ndani kuna vikosi maalum ambavyo vinajumuisha Wizara hii, moja ni Magereza.

Mheshimiwa Waziri, hivi nani aliyetoa Magereza Zanzibar kuwa isiwemo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kama ni hivyo lini itarudishwa Magereza Zanzibar kuwa ndani ya Wizara ya Mambo ya ndani?

**SPIKA:** Lakini kama ungemfuatilia vizuri Mheshimiwa hakuna suala la Mambo ya Ndani kuna Polisi tu, kwa hiyo Magereza haipo toka mwanzo. Mheshimiwa Jussa!

**MHE. ISMAIL JUSSA LADHU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninaomba nimwulize Mheshimiwa Waziri swali la nyongeza.

Kwa kuwa Hati hii ya Muungano ambayo ni mkataba wa kimataifa inazifunga Tanganyika na Zanzibar katika Muungano huu haikutoa nafasi popote kwa kuongeza mambo ya Muungano. Haonikama utaratibu uliotumika kuongeza mambo haya ulikuwa siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mkataba wa kimaita na kwamba haoni kama ni busara haikuchukua hatua za kuyaondoa mambo hayo ili kuweka Muungano wetu uliokubaliwa na waasisi wetu wa Muungano mwaka 1964?

**SPIKA:** Swalii hili siliruhusu kwa sababu ni la malumbano na uchokozi tu hata halina maana. Basi nimpe nafasi Mheshimiwa Yahya Kassim Issa.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa mambo ya Muungano yalikuwa 11 na kufikia hadi 22, huoni kwamba mambo mengi haya kuyaingiza kwenye Muungano ni kuipunguza nguvu Serikali ya Mapinduzi Zanzabari kujitegemea?

**SPIKA:** Leo Waheshimiwa Sijui mkoje? Haya yote mnayolalamika yameletwa humu ndani ya Bunge na taratibu za Kikatiba zikafuatwa ndiyo maana yakapitishwa.

Leo sisi kukaa tena tunahoji siyo sahihi hata kidogo. Kama ipo hoja mathalani, hasa kwa Ndugu zangu Wabunge kutoka Zanzibar. Kama mtu anataka sarafu iwe ya Zanzibar si alete hoja! Ndiyo yako hapa! Kama kuna Mbunge anataka Baraza la mitihani Zanzibar, Zanzibar iwe na mitihani yake peke yake, mlele hapa hoja, hakuna tatizo. (*Makofii*)

Tunaendelea Waheshimiwa, sasa ni Wizara ya Maji na Umwagiliaji swalii linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila, Mbunge wa Kwimba.

Na. 57

### **Kero ya Maji ya Wilaya ya Kwimba**

**MHE. BUJIKU P. SAKILA** aliuliza:-

Kwa kuwa, moja ya kero za Wilaya ya Kwimba ni ukosefu wa maji na kwamba Serikali ilikubali kuvunganisha vijiji kumi na saba (17) katika tarafa ya Mwamashimba katika mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Shinyanga na Kahama (KASHWASA) ili kupunguza makali ya ukame katika tarafa hiyo:-

- (a) Je, ni lini KASHWASA itaanza na kumaliza shughuli za kusambaza mabomba ya maji katika vijiji kumi na saba vinavyohusika na mradi huo?
- (b) Je, Serikali inatoa maelekezo gani kwa Kamati za watumiaji wa maji za Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba ambazo zimeshaundwa na zinasubiri kazi ili wananchi wa vijiji hivyo wapate maji?
- (c) Je, wakala wa KASHWASA itakuwa na shughuli zipi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Bujiku Philipo Sakila, Mbunge wa Kwimba, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoleze Bunge lako Tukufu mwaka jana, katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2009, Serikali ilikamilisha ujenzi wa mradi mkubwa wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria hadi miji ya Kahama na Shinyanga kwa gharama ya shilingi bilioni 252.

Mradi huo ulizinduliwa rasmi tarehe 30 Mei, 2009 na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu ambao ulisanifiwa kuhudumia watu 1,000,000 tayari unahudumia watu 430,000 katika miji na Kahama na Shinyanga na vijiji 40 ambavyo tayari vimeunganishwa kati ya lengo la vijiji 76 katika Mikoa ya Mwanza na Shinyanga. Aidha, ujenzi wa tanki kubwa la Mhalo nao umekamilika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2010/2011 Wizara yangu itaendelea kufanya usanifu katika vijiji vilivyobaki ikiwa ni pamoja na kuongeza vituo ya kuchochea maji. Vijiji 17 katika Tarafa ya Mwamashimba ambavyo Mheshimiwa Mbunge anaviulizia, ni sehemu ya kazi itakayofanywa na wakazi wake watapata maji kutoka katika tanki la Mhalo. Wizara yangu inaendelea na utaratibu wa kumwajiri mtalaam mwelekezi atakayefanya usanifu na kusimamia ujenzi wa mfumo wa usambazaji maji katika vijiji hivyo.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu Kamati ya watumia maji, napenda kukumbusha kwamba kamati za maji zilizopo ni ngazi tu ya muda ya kuelekea kwenye uundaji wa vyombo huru vya kuendesa mradi. Halmashauri na wananchi wasiishie kwenye uundaji wa Kamati za maji za vijiji. Kamati ya maji siyo chombo huru kwani ni sehemu ya Serikali ya Kjiji. Kwa vile uundaji na usajili wa vyombo vya watumiaji maji sasa unafanya katika ngazi ya Halmashauri natumia fursa hii kuielekeza Halmashauri ya Kwimba pamoja na Halmashauri zote nchini zihakikishe miradi iliyopo na mingine itakayojengwa ikiwa ni pamoja na ile itakayojengwa kupitia programu ya Maji Vijijini, inaudiwa vyombo huru vya watumiaji maji.

Kanuni za usajili wa vyombo vya watumiaji maji tayari zimetolewa kisheria kupitia Gazeti la Serikali *GN. 21* la tarehe 22 Januari, 2010. Katika mwaka 2010/2011 Halmashauri zinatakiwa ziandae mipango kazi ya kuhamasisha wananchi kuanzisha na kusajili vyombo vya watumiaji maji.

(c) Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya kuendesa mradi wa maji inayojulikana kama Kahama Shinyanga *Water Supply Authority* (KASHWASA) inafanya kazi kama mamlaka nyingine zinazotoa huduma ya maji safi na maji taka nchini. Tofauti kubwa iliyopo kati ya KASHWASA na Mamlaka nyingine ni kwamba KASHWASA inauza maji kwa vyombo vingine vinavyotoa huduma moja kwa moja kwa watumia maji. Vyombo hivyo ni pamoja na Mamlaka za Maji Safi na Majitaka za Shinyanga na Kahama na Jumuiya za Watumia maji na vijiji vilivyo kandokando ya Bomba Kuu.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia sana jambo hili, lakini pia nawoomba wananchi wa tarafa ya Mwamashimba kuwa na subira

kidogo kwa kuwa sasa Serikali inatekeleza mpango utakaokamilisha upatikanaji wa maji katika vijiji vyao.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza, nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana ambayo yanatia moyo watu wa Tarafa ya Mwamashimba, lakini vijiji 17 ambavyo vimetajwa katika swali la msingi pamoja na majibu ya Naibu Waziri, vilitambuliwa miaka ya 1975 na tangu wakati ule kuna wananchi wengi ambao wameongezeka pamoja na vijiji vingine vipyta, mradi huo utakapokamilika utakuwa umepita karibu na wananchi ambao hawakuwemo katika mradi wa zamani.

(a) Je, katika kuwasaidia wananchi hawa, Serikali itakuwa na mpango gani sasa ili kuwafikishia wananchi ambao hawakuwepo katika mpango wa awali?

(b) Kama nilivyosema katika swali la msingi, Wilaya ya Kwimba ina shida kubwa sana ya maji, hii ni pamoja na Makao Makuu yake Ngudu, mara kwa mara tumekuwa tukiomba mradi huu upelekwe mpaka Ngudu na majibu yalikuwa kwamba mtalaam mwelekezi angeweza kutoa maelekezo kama ingewezekana, ningependa kupata majibu ya Serikali kama ingewezekana, Serikali, wamefikia wapi katika ombi la wakazi wa Ngudu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli vijiji hivyo 17 anavyovisema vilanza tangu zamani, na si hivyo 17 tu ni vijiji vingi hapa Tanzania na katika vijiji vingi ongezeko la watu limekuwa kubwa. Sisi tunachokifanya siku zote katika kusanifu miradi tunaangalia ongezeko la watu, tukisema tunaandaa mradi tunaangalia pia miaka mingine mingi mbele.

Kwa hivyo, naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Bujiku Sakila kwamba wakati tunatayarisha mipango ya kuendelea kusambaza maji haya, maana yake siyo kwamba mchakato umekwisha huu ni mchakato endelevu, tutakuwa tunaendelea kuangalia ongezeko la watu na kila linapoongezeka basi tunaangalia tuweke tena Miundombinu gani ya kuongeza maji kwa ajili ya watu wanaoongezeka.

Hili pia litakuwa ni jukumu la Hal mashauri ya Wilaya ya Kwimba kuangalia watu wake wanavyoongezeka na kuweka katika mipango ya maendeleo ya Maji ya kila mwaka, hili ni tatizo ambalo ni endelevu siyo la siku moja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mji wa Ngudu naomba nimtaarifu Mheshimiwa Sakila kwamba, kazi hii bado inaendelea kama nilivyosema hatuwezi tukafanya kazi siku moja tu ikakamilika, utaratibu wa kuandaa mipango hii ni utaraibu ambao unachukua muda, kwa hivyo kazi ya kuandaa mradi wa maji wa Ngudu na usambazaji wake itakapokuwa tayari kama ilivyofanyika katika vijiji hivi 17 basi nao tayari tutam Warifu Mheshimiwa Bujiku Sakila.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira tu kazi hii inaendelea.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona, kwa kuwa tatizo la Wilaya ya Kwimba na tatizo la Jimbo la Ubungo hasa katika Kata za Kimara na Makuburi linafanana, na katika kutatua tatizo hili sasa Serikali iliingia mkataba na kampuni ya kichina ambapo walisambaza mabomba maeneo mengi sana, lakini cha kushangaza imepita miezi minne hakuna maji yanayotoka, sasa kuna fununu zinazosemekana kwamba Wachina mmewafukuza.

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na hili, maji yatatoka ama Wachina mmewafukuza kwa hiyo maji hatutapata?

**SPIKA:** Nilidhani Mheshimiwa unagombea Kawe, kumbe sasa unagombea Ubungo! (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza jana alikuwa amesema angekuja tuwasiliane sijui kama ilikuwa suala hili. Sasa mimi naomba tu kwa kifupi tu niseme kwanza; mradi ule unaendelea, maji yatatoka na ninamwomba Mheshimiwa Mdee aache kufanyakazi na fununu. Kama alivyokuwa ameahidi kuja kuonana na mimi basi angekuja kuonana na mimi. Llakini habari za fununu za kufukuza Wachina hizo hatuwezi kuzifanya kazi. (*Kicheko/Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge swali hili limechukua muda mrefu sana na bado tupo Wizara ya Maji kwa swali linalofuata ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mbunge wa Nzega.

Na. 58

### **Kuondoa Kero ya Ukosefu wa Maji Nchini**

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:-

Kwa kuwa, huduma ya maji ni muhimu sana kwa maisha ya kila siku ya binadamu; na kwamba upatikanaji wa maji nchini hasa katika maeneo ya vijijini ni wa taabu sana hususani wakati wa kiangazi:-

- Je, ni mikakati gani mahsusiliyopo ya kuhakikisha kero ya maji inakwisha au kupungua?
- Je, ni wakati gani maalum uliowekwa kwa vijiji vya Wilaya ya Nzega kuondolewa adha hiyo ya ukosefu wa maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini safari hii ujibu siyo uahidi kukutana huko, sisi hatuwezi kujua mnafanya nini huko. (*Kicheko/Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne ilidhamiria kupunguza umaskini kama ilivyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo, 2005 na Mkakati wa Taifa wa Kuondoa Umaskini na Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2005. Lengo ni kuwawezesha wananchi wanaishi mijini na vijiji kupata maji safi, salama na ya kutosha kwa matumizi yao ya kawaida karibu na sehemu wanapoishi. Ili kufikia malengo hayo, Serikali katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2010 iliendelea kuboresha huduma ya maji vijiji kwa kujenga miradi mipy, kukarabati miradi iliyopo, kuchimba visima vipy na kufufua vilivyopo kujenga mabwawa na kushirikisha wananchi katika kupanga, kujenga na kuendesha miradi ya maji.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, kama zilivyo Halmashauri nyingine inatekeleza programu ya maji na usafi wa mazingira. Kwa bahati nzuri, Halmashauri ya Wilaya ya Nzega ni moja kati ya Halmashauri 123 ambazo tayari zimeajiri wataalam washauri ambao wameanza kazi ya kuainisha vyanzo vya maji na kufanya usanifu wa miundombinu ya maji. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, Mtaalam Mshauri *M/S Howard Humphrey* ameanza kazi mwezi Novemba, 2009 na matarajio yangu ni kwamba ataimaliza kazi hiyo ifikapo Agosti, 2010 ambapo kazi ya ujenzi wa miundombinu ya maji itafuata. Katika awamu hii vijiji 10 vinavyohusika na mradi ni Nawa, Nata, Ndala, Mahene, Nkiniziwa, Upungu, Buhondo, Figili, Itobo na Ikindwa.

Wakati tukiendelea na maandalizi ya utekelezaji wa programu ya maji na usafi wa mazingira, Serikali kwa makusudi iliamua kukarabati na kujenga miradi midogo ya maji inayoweza kutoa matokeo ya haraka ili kupunguza tatizo la upatikanaji wa maji. Kati ya mwezi Julai, 2007 na Desemba, 2009 Halmashauri ya Wilaya ya Nzega ilipewa jumla ya shilingi 413,017,000/= kutekeleza miradi midogo ya aina hii. Fedha hiyo ilitumika kukarabati bomba za maji katika Vijiji vitatu vya Bukene, Sojo na Undomo; kufunga pampu 50 za mkono kwenye visima vya asili, kujenga vituo 25 vya kuchotea maji na kuchimba visima virefu viwili (2).

Mheshimiwa Spika, matarajio yangu ni kwamba katika mwaka 2010/2011 ujenzi wa miundombinu ya maji katika vijiji 10 chini ya programu ya maji na usafi wa mazingira utaanza. Pamoja na matarajio hayo, ni dhahiri kwamba viko vijiji vingine ambavyo havitakfikiwa na programu hiyo. Namshukuru Mheshimiwa Mbunge, Selelii kwa juhudzi zake za kuendelea kuibua miradi ya maji.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, ahsante! Ukubwa wa tatizo la upatikanaji wa maji vijiji kwa nchi nzima ni kubwa sana na hasa kwenye mikoa ambayo inapata ukame wa mara kwa mara. Lakini, juhudzi zinazofanywa na Serikali hazikidhi haja kwa haraka kuondoa hilo tatizo.

Je, Serikali iko tayari kufanya juhudini za makusudi kuanzisha mipango maalum kama ilivyoanzisha Mpango wa Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari, Zahanati na kuanzisha Mpango Maalum wa Maji uitwe MMA ili kuondoa matatizo hili?

Mheshimiwa Spika, swali la pili Mheshimiwa Waziri anasema atatupatia maji katika vijiji 10, Wilaya ya Nzega ina vijiji 150 kwa hiyo, hivi vijiji 10 ni vichache sana kwa wilaya kubwa kama Nzega. Je, kwenye mgao wa fedha unaotolewa na Serikali hususani katika kuondoa matatizo ya maji haiwezekani ukazingatia ukubwa wa maeneo na upatikanaji wa maji katika eneo hilo ili maeneo kama Nzega yakapewa upendeleo maalum?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Selelii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama anavyosema ni kweli juhudini bado hazijakidhi haja, na mimi nasema juhudini zinaendelea kwa sababu haya ni maendeleo na si matukio. Kwa hiyo, tunaendelea kufanya juhudini ili tuweze kutatua matatizo haya yanayotokana na maji. Lakini kuhusu mipango maalum mimi naomba niseme kwa kifupi tu kwamba, hata hivi sasa tunavyoendelea na kazi hii tukitegemea programu hizi za Serikali peke yake hatuwezi kutatua matatizo ya maji katika nchi hii, lazima tutumie pia vyanzo vingine na fursa nyingine zilizopo.

Mheshimiwa Spika, ipo mifano hai ambayo mimi nimeiona katika maeneo mengi, nimekwenda Manyoni nimeona Shirika la Damu ya Yesu pale Manyoni linashirikiana na Mamlaka ya Maji na wanaupatia maji Mji wa Manyoni vizuri sana. Nimeona pia huko Kigoma nafikiri Mheshimiwa Rais yuko kule na wakipata nafasi watampa leo fursa ya kutembelea mradi wa Makongoro II. Huu umejengwa kwa kushirikiana na Wahandisi wasio na mipaka.

Mheshimiwa Spika, zote hizi ni fursa ambazo zipo na nikianza kuzitaja ni nyingi mno, labda niseme tu kwamba kinachotakiwa ni kuangalia kwamba tunawezaje kutumia fursa zilizopo za vyanzo vingine vya fedha vilivyopo katika nchi hii ikiwa ni pamoja na mashirika ya dini, taasisi fulani fulani, *NGOs*, Mashirika yasiyo ya kiserikali ili kwa pamoja tusaidiane kutatua matatizo haya ya maji.

Kuhusu hivi vijiji 10 nadhani jibu mojawapo ni hilo nililolisema. Lakini nataka nimwarifu Mheshimiwa Selelii kwamba, vijiji 10 ni vijiji vichache tu katika Halmashauri ya Nzega, viko vingi labda zaidi ya 100 nadhani. Lakini, baada ya hapa tutakuwa tena na awamu nyingine itakayofuata, lakini tusingoje hivyo vijiji 10 vya programu ya Serikali naomba tuendelee kutumia hizi fursa nilizozitaja na mimi Wizara yangu inao uwezo wa kuwasaidia kuandaa michakato, kuandaa maandishi ili tuweze kuomba fedha kutoka katika vyanzo vingine na mimi mwenyewe nina hakika nina uwezo wa kusaidia katika masuala kama haya. (*Makofi*)

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la maji kwa Wilaya ya Nzega ni tatizo ambalo lipo kwa mkoa mzima wa Tabora, na kwa kuwa wilaya ya Urambo ambayo ina misitu mingi minene ambayo ndiyo vyanzo vya maji ina tatizo sugu la maji kwa wananchi wake, wapo wananchi ambao kwa muda wote wa uhuru hawajawahi kuona maji yanatoka bombani. Waziri anatwambia nini kuhusu mpango maalum kwa Wilaya ya Urambo kupata maji safi na salama?

**SPIKA:** Na wewe pia unatafuta...basi bwana!(*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba uwe chonjo. Lakini niseme tu kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ni moja ya Halmashauri zote 132 katika nchi hii ambazo zimo katika programu yetu ya vijiji 10 na tunaendelea kutekeleza miradi. Sidhani kama majibu yanatofautiana na haya niliyompa Mheshimiwa Selelili, pale ambapo vijiji 10 hatukuvifikasi ni lazima tuendelee kutazama fursa zingine ambazo tunazo katika nchi hii ili tuendelee kutatua matatizo ya Urambo.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka pia kwamba Waziri Mkuu alipotembelea Urambo, tulikuwa pamoja na wewe na ninakumbuka uliomba kwa makusudi kabisa kwamba tuangalie uwezekano wa kwanza kutengeneza maeneo yale ambayo miradi midogo midogo inahitaji kuweka vitu vidogo na maji yakatoka. Nimeanza kulifuatilia hilo na ninaamini baada ya muda si mrefu pale Urambo nako kutakuwa kuzuri.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, basi mchangamke maana yake hawa vijana wananyatia.(*Kicheko*).

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swalii moja tu la nyongeza;

Mheshimiwa Spika, pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri na kuipongeza Serikali kwa ule mradi wa maji vijijini ambao Wilaya ya Kongwa ni mojawapo ya Wilaya zilizohudumiwa katika awamu ya kwanza, japo baadhi ya vijiji havikukamilika na bado tunafanya kazi vizuri na Wizara kurekebisha hilo, lakini sasa tuna vijiji 10 vya awamu ya pili wananchi wanajiuliza.

Je, kuna mikakati ya kuhakikisha kwamba safari hii katika awamu ya pili utekelezaji utakuwa ni wa uhakika na haraka, kule Njoge, Makawa, Mkoka, Mlali na maeneo mengine tofauti na ilivyokuwa awamu ya kwanza kwamba sasa mradi huu utatekelezwa kwa wakati huu wa awamu ya pili?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, najua Mheshimiwa Ndugai na wananchi wa Kongwa wanakumbuka matatizo waliyoyapata katika mradi wao ule. Kwa sababu utekelezaji kweli uligubikwa na matatizo mbalimbali ya kiutekelezaji. Sasa tu nimhakikishie kwamba tayari tulikwishajifunza yale yalitokea katika utekelezaji ule na hasa hasa katika Menejimenti ya mikataba yale tumeyaangalia

na tutayarekebisha katika awamu hii ya pili, basi kama hayatakuwa yameisha kabisa na nataka nimpe matumaini kwamba awamu ya pili itatekelezwa kwa ufanisi zaidi kuliko ile awamu ya kwanza.

Na. 59

### **Usikivu wa Simu za Mkononi Shinyanga Mjini**

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna usikivu hafifu sana wa simu za mkononi kwenye baadhi ya maeneo ya Jimbo la Shinyanga Mjini kama vile Kizumbi, Chibe na kadhalika:-

Je, ni lini Serikali itashawishi Makampuni ya Simu za Mkononi kuongeza nguvu za mitambo yao ili kuboresha usikivu wa simu za mkononi katika jimbo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako kabla sijajibu suala la Dr. Mlingwa, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu na wananchi kwa jumla kwamba siku za kuandikisha simu zetu zinakaribia kumalizika. Nakuombeni sana mkaandikishe simu zenu na watu wa kuandikisha wapo hapo nje na kule kwenye majimbo yenu muwakumbushe wananchi wenu kwamba waandikishe simu ili baadae kusije kuwa na lawama.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Charles Ogesa Mligwa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuhamasisha kampuni za simu za Mkononi kuimarisha huduma za mawasiliano ya simu ikiwa ni pamoja na kuongeza nguvu za mitambo.

Ni kweli kwamba kulikuwa na matatizo ya kutokuwepo usikivu mzuri katika baadhi ya maeneo ya Jimbo la Shinyanga Mjini yaliyopelekea na kampuni ya ZAIN kufanya marekebisho kwa kanda ya Ziwa ya kubadilisha mitambo ya zamani aina ya ALCATEL na kuweka mitambo mingine mipya ya aina ya HUAWEI. Baada ya marekebisho hayo baadhi ya maeneo ya Shinyanga Mjini usikivu umeboreka ila bado eneo la Kizumbi na Chibe usikivu ni hafifu, hivyo uboreshaji zaidi unahitajika.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu huo kampuni ya VODACOM tayari imejenga mnara katika eneo la Buhangija ili kuboresha mawasiliano ya simu katika maeneo yanayozunguka Buhangija. Aidha, kampuni inaendelea na jitihada za kuhakikisha mawasiliano yenye usikivu mzuri yanapatikana katika maeneo yote nchini yakiwemo maeneo ya Shinyanga Mjini ikiwa ni pamoja na maeneo ya Kizumbi na Chibe ili kuwawezesha wananchi wengi kunufaika na huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *TIGO* na *ZANTEL* zimeahidi kuyaweka maeneo ya Kizumbi na Chiba katika malengo yale ya kuyafanyia tathmini ya kibashara mwakani. Napenda nimpongeze Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla kwa juhudini za kufuatilia ahadi mbalimbali za makampuni ya simu ili kusaidia upatikanaji wa mawasiliano katika majimbo hayo.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza naipongeza Serikali kwa kuyahamasisha makampuni haya ya simu za mkononi kutoa huduma ya simu kwa wananchi. Lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana yanayotia matumaini.

Mheshimiwa Spika, ninalo swali moja lenye sehemu mbili. Ningelipenda kuelewa nini maendeleo ya mkonga wa Taifa wa Mawasiliano. Je, Serikali inatuhakikishia hapa kuwa ni kweli mkonga huu wa Taifa wa Mawasiliano utaleta unafuu katika gharama za mawasiliano ili wananchi wetu waweze kupata huduma hizo kwa gharama nafuu?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nimfahamishe Mheshimiwa Dr. Mlingwa na kupitia kwake kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwamba maendeleo ya Mkonga wa Taifa yanaendelea vizuri sana.

Tumemaliza *Phase I* ambayo ni *Northwing* na hivi leo ninavyozungumza wataalamu wetu kutoka Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na wataalamu wa Rwanda wako mpakani baina ya Rwanda na Tanzania wakiunganisha mawasiliano. Tayari nchi sita za jirani tumeshafikia mipakani mwao lililobaki ni nchi za jirani kuwasiliana na sisi katika kuunganisha mawasiliano hayo. Tunavyozungumza sasa tuko kwenye *Phase II* ya maendeleo haya na mkongo umeshapita Shinyanga. Mawasiliano katika maeneo yaliyopita yameteremsha gharama za simu na hasa *internet* vibaya sana na tunategemea tukikamilisha mawasiliano hayo ya mkongo hali ya mawasiliano itaboreka na wananchi watanufaika na faida hasa ya mawasiliano nchini. (*Makofii*)

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa tatizo la mawasiliano hafifu haliko Shinyanga tu, na tatizo la mawasiliano hafifu limejaa katika kisiwa cha Pemba na Unguja. Na kwa kuwa katika jibu lako Mheshimiwa Naibu Waziri ulisema kwamba katika hizo baadhi ya sehemu ni kubadilishwa mitambo kutoka *ALCATEL* na kwenda *HUAWEI*, na kwa kuwa katika jimbo langu la Mkanyageni mnara wa *ZANTEL* upo na mawasiliano hayapatikani yana shida sana. Je, nao wamebadilisha hii mitambo yao kutoka *ALCATEL* kwenda *HUAWEI* ndio tatizo la mawasiliano likatokea?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, napenda nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba mnara uliopo

pale ni mnara wa ZANTEL na hali ya Mkanyageni sisi tunaiona kutokana na milima na mabondebonde kidogo inawezekana *penetration* sio nzuri. Na kwa sababu umenieleza sasa hivi siku zote hujawahi kuniambia mimi nitalishughulikia ipasavyo.

Lakini ni kwa kisiwa cha Pemba labda niseme kwamba hivi karibuni Mheshimiwa Rais wa Zanzibar alizindua masuala ya umeme Pemba, kitu ambacho tunakishukuru sana. Waya ule wa umeme ambao unapita baharini una mkongo wa mawasiliano. Sasa kilichobaki kwetu sisi ni kuhakikisha tunakaa pande hizi mbili kuona ni namna gani wananchi wa Pemba watafaidika na mkongo huu wa mawasiliano kwa kuunganishwa na mkongo wa baharini. Tunategemea kwamba waya wa mawasiliano ya umeme utakaopita Zanzibar pia utakuwa na mkongo wa mawasiliano kitu ambacho kitatusaidia sana kuboresha mawasiliano hapa nchini. (*Makofi*)

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Tatizo la usikivu hafifu wa simu za mkononi lina changamoto kubwa zaidi Wilaya ya Kyela pengine kupita sehemu zingine Tanzania kwa sababu ukiingia tu Wilaya ya Kyela kuititia Kata ya Busare, Ngana, Katumbasongwe, Ikolo, Bujonde, Ngonga unakaribishwa na ujumbe unaosema “*CELTEL Malawi Welcomes you to Malawi*”.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali itachukua hatua gani za haraka kturejesha wana-Kyela Uraia wetu kimawasiliano wa kuongeza nguvu zaidi ya *CELTEL Tanzania* iweze nayo kusema “*Welcome to Tanzania*”? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, bahati nzuri Muungano huu umenifanya kujua maeneo mengi sana na nimefika Kyela kwa Mheshimiwa Mbunge. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hili tutalifuatilia kwa karibu haipendezi sana kusikia ukifika pale unakaribishwa na “*CELTEL Malawi*” tunataka ukaribishwe na *ZAIN Tanzania Limited* ambayo ndiyo Kampuni yako unayoichangia siku zote.

Lakini na *training* ya Kyela wewe mwenyewe unaifahamu inawezekana milima na mabonde yale inafanya hali ya mawasiliano kuwa dhaifu kidogo. Lakini tutawaambia wanaohusika kwamba waweke kama ni *booster* au ni kitu chochote ambacho kitaboresha mawasiliano katika jimbo lako. Mheshimiwa Mbunge tunakushukuru sana kwa ufuutiliaji wa karibu. (*Makofi*)

Na. 60

### **Mapato Yatokanayo na Mawasiliano**

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA** aliuliza:-

Eneo la mawasiliano ni la muhimu sana kwa mapato ya nchi, kwani linaingiza mapato mengi ikiwa ni pamoa na Tanzania Zanzibar ambapo licha ya mawasiliano duni lakini inaingiza zaidi ya shilingi bilioni sita (6) kwa mwaka:-

Je, Tanzania Zanzibar inafaidika vipi na mapato hayo na kwa utaratibu upi?  
**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa sekta ya mawasiliano ni moja kati ya sekta muhimu sana kwa ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Sekta hii huchangia asilimia 2.3 ya pato la Taifa na pia huchangia mapato ya Serikali kupitia kodi mbalimbali kama ifuatavyo:-

- (i) Ushuru wa bidhaa (*Exercise Duty on Airtime*) – 10% ambayo siyo kodi ya Muungano.
- (ii) VAT – 18% ambayo siyo kodi ya Muungano.
- (iii) Skill Development Levy – 6% kwa Tanzania Bara na 5% kwa Zanzibar ambayo siyo kodi ya Muungano.
- (iv) Cooperate Tax – 30% ambayo ni kodi ya Muungano.
- (v) PAYE – ambayo ni kodi ya Muungano.
- (vi) Kodi ya Kiwanja - ambayo siyo kodi ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kodi ambazo siyo za Muungano, kila upande wa Jamhuri unakusanya na kufaidi wenyewe. Kwa upande wa kodi za Muungano ambazo ni mbili:-

(i) Cooperation Tax – 30%. Kodi hii inakusanywa na TRA upande ambao Kampuni iliposajiliwa. Kwa upande wa Zanzibar, TRA huziwasilisha HAZINA Zanzibar kwa ajili ya matumizi ya SMZ.

(ii) Kodi ya Mapato (*PAYE*). Kodi hii ni mionganini mwa maswali ambayo yanajadiliwa na Serikali zetu mbili kuitia Kamati ya Makamu wa Rais.

Kutokana na matokeo ya kikao cha tarehe 2/5/2010, tunatarajia kupata ufumbuzi mapema iwezekanavyo juu ya kodi hii. Kwa sasa kodi hii inakusanywa na kuwasilishwa HAZINA ya Muungano. (*Makofi*)

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake, ila naomba nimwulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa kodi ya mapato (*PAYE*) ambayo inakusanywa inapelekwa HAZINA na kwa kuwa tunasubiri matokeo ya kikao cha Kamati ya Mheshimiwa Makamu wa Rais. Je, baada ya kupatikana ufumbuzi makusanyo hayo ambayo ni makusanyo ya Muungano yaani yapelekwe HAZINA ya Muungano utafanywa ukokotoaji ili makusanyo hayo yaweze kugaiwa kulingana na mapato yaliyopatikana tangu huko nyuma?

La pili, kwa kuwa suala hili la mapato ya Muungano yatokanayo na shughuli za Muungano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar alipewa mshauri mwelekezi kazi ambayo alipewa na Tume ya Pamoja ya Fedha. Je, hadi hii leo mapendekezo hayo hayajafanyiwa kazi ni lini mapendekezo hayo yatafanyiwa kazi yaliyotolewa na mshauri mwelekezi ili kero hii ya mgawanyo wa mapato iondoke? Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba kodi ya *PAYE* ni moja ya mambo ambayo yanazungumzwa katika Kamati ya Muungano ya Mheshimiwa Makamu wa Rais.

Nini kitafanyika, itategemea jinsi itakavyokubalika katika kikao cha Makamu wa Rais. Lakini haina maana kwamba Zanzibar kwa miaka yote hii haijapata chochote. Katika mapato yote yanayohesabika kwamba ni ya Kimuungano, Zanzibar inapata asilimia 4 na nusu. (*Makofi*)

Na. 61

**Mradi wa Chuma na Makaa ya Mawe  
Kuwa Nishati Mbadala**

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI** aliuliza:-

Upo uhaba mkubwa wa nishati katika maeneo mbalimbali nchini.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia nishati za Makaa ya Mawe huko Ludewa na Ruvuma (Mbinga) ili kukabiliana na tatizo la umeme nchini?

### **NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkakati uliopo ni kujenga mitambo ya kuzalisha umeme ya megawati 600 kwa kutumia makaa ya mawe ya Mchuchuma na megawati 400 kwa kutumia makaa ya mawe ya Ngaka.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mawaziri, kupitia Waraka Na. 14/2007, lilielekeza kuwa utekelezaji wa miradi ya makaa ya mawe ya Mchuchuma na chuma cha Liganga iliyoko Wilaya ya Ludewa, Mkoani Iringa ifanyike kwa njia ya ubia kati ya Serikali, kupitia Shirika la Taifa la Maendeleo (*NDC*) na wawekezaji wenye uwezo wa kifedha na kiufundi.

Aidha, waraka huo uliagiza kuwa wawekezaji wateuliwe kwa njia ya ushindani na uwazi na Kamati ya wataalamu iliundwa ili kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo. Hatua ya kwanza imeshafanyika ambapo zabuni zilitangazwa mwezi wa Desemba 2009 Kampuni 48 zililitokeza ambapo Kampuni 21 ziliwasilisha nia ya awali ya kushiriki katika ujenzi (*Express of Interest*).

Mheshimiwa Spika, Kampuni 21 zilifanyiwa tathmini na Kampuni 9 zilipendekezwa kuwasilisha maombi rasmi kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa Mchuchuma. Kampuni tano (5) zilipendekezwa kuingia katika hatua ya pili kwa mradi wa Liganga.

Kwa sasa Shirika linamalizia maandalizi ya makabrasha ya zabuni (*Request for Proposal*) kwa ajili ya kuwapatia wazabuni waliochaguliwa kutoka hatua ya kwanza ili wawasilishe zabuni zao kwa ajili ya kufanyiwa tathmini hatua ya mwisho.

Sehemu ya nishati na umeme itakayozalishwa kutokana na makaa ya mawe ya Mchuchuma utakuwa kichocheo cha kuendeleza mradi wa chuma cha Liganga ili uweze kuzalisha aina mbalimbali za chuma kwa matumizi ya ujenzi na katika viwanda vyetu hapa nchini na nje.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa makaa ya mawe ya Ngaka Wilayani Mbinga, katika Mkoa wa Ruvuma kwa ajili ya kuzalisha umeme, mwaka 2008. *NDC* iliingia ubia na Kampuni ya *Pacific Corporation East Africa (PCEA)*, ambayo ni Kampuni Tanzu ya *Atomic Resources Limited* ya Australia na kuanzisha Kampuni ya *Tancoal Energy Limited*.

Kampuni ya *Tancoal Energy Limited* imekwishaanza kazi na imebainisha kiasi cha makaa ya mawe yaliyopo. Uchorongaji wa miamba (*Diamond Drilling*) uliofanyika umebainisha kiwango cha akiba ya makaa ya mawe ya kutosha kuzalisha umeme MW 400.

Kwa sasa Kampuni inakamilisha tafiti mbalimbali kuhusiana na mgodi wa makaa ya mawe, kituo cha kuzalisha umeme pamoja na athari za mazingira na matumizi mengine ya makaa ya mawe kama kwenye viwanda vya Saruji. (*Makofi*)

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nataka kusema hivi kwamba mradi wa Makaa ya mawe ya Ludewa na Ruvuma (Mbanga) umechukua miaka mingi sana karibu sasa zaidi ya miaka 10 na mradi huu kwa kweli upo katika *Mtwara Corridor* ambao inahusika na mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Iringa na Rukwa. Mimi nataka tuambiwe tu ni lini hasa huu mradi utakuwa tayari?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mradi huu wa Mchuchuma na Liganga kama sehemu ya Mtwara Corridor umekuwa unazungumzwa kwa muda mrefu na nadhani tatizo lililokuwepo kwa muda huo wote ulikuwa ni mkakati wa namna ya kuendeleza suala lile. Kwa sababu uwekezaji uliokuwepo pale ni uwekezaji mkubwa na kusema kweli badala ya kufanya kwa kudonyoa donyoa ili kupata thamani kamili ya mradi ule ni lazima ufanywe na mwekezaji ambaye kwanza ana uwezo wa kifedha wa kiufundi lakini pia kimkakati kwa sababu mradi wa Mchuchuma na Liganga kama Prof. Mwalyosi anavyoweza kuthibitisha tulipokwenda kule mwaka juzi ni mradi ambao unatakiwa uwe na mikakati mikubwa ya kimiundombinu ya nishati na kadhalika. Kwa hiyo ni integrated project mkubwa sana. Kuufanya kwa kudonyoa donyoa kwa kweli ni kutokuutendea haki. Kwa hiyo Serikali imengia mikakati hiyo na ndiyo maana sasa hivi mkakati ni kuufanya maendeleo unavyostahili na ninaamini kwa sababu tunafikia hatua za mwisho za kuwachuja hawa wazabuni tumbeki nao watano tutapata mzabuni ambaye anauwezo wa kutupatia maslahi makubwa kutokana na mradi huu kwa nchi yetu.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Miradi hii ya umeme kusema kweli inachukua muda mrefu sana na hata ile sehemu ambayo umeme umeshapatikana tayari kwa mfano kama ule wa Somanga-Fungu. Lakini mpaka leo umeme haujawaka na Mheshimiwa Naibu Waziri alishakuja na akasema kwamba umeme utawaka siku fulani lakini hadi leo kimya. Je, kulikoni?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mwezi uliopita tulikwenda Kilwa na tulikuwa na Mheshimiwa Dr. Mpanda na kimsingi mradi anaouzungumzia ni katika miradi ambayo imo kwenye Mtwara Corridor lakini ni mradi wa kutumia gesi kwa ajili ya Wilaya ya Kilwa na Wilaya ya Rufiji moja kwa moja ukishatoka pale Songsongo na ukafikia pale Somanga bomba linatoka pembeni na kuna kituo cha umeme cha Somanga-Fungo ambacho kimeshakamilika. Kwa hiyo kwa sasa

hivi naomba nimhakikishie Mheshimiwa Dr. Mpanda kwamba pana matatizo mawili makubwa. Moja ni kwamba bado Songas na TANESCO hawajakubaliana kuhusu matumizi ya gesi kwa sababu pale tatizo la mita lilisahaulika kwa hiyo sasa hivi Songas wanasema wakiwapa umeme TANESCO watashindwa kuupima. Kwa hiyo sasa hivi tupo kwenye suala hilo la kukabiliana na tatizo la mita ambalo tumezungumza na Mkuu wa Mkoa wa Lindi na nadhani litakwisha muda wowote kuanzia sasa. (*Makofi*)

Lakini suala la pili ni suala la fidia, kuna baadhi ya wananchi ambao wako pale tatizo la fidia halijakamilishwa kwa hiyo wamezuia ukamilishaji wa nyaya. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda pamoja na ahadi ambayo Serikali iliweka kituo cha kuzalisha umeme kimekwisha na kiko tayari kuanza kazi hata leo. Lakini matatizo ya fidia nadhani ni bora zaidi viongozi wa Kilwa na Rufiji wakashirikiana na Serikali ili twende kwa wananchi na tuwazungumzie umuhimu wa kukamilisha mradi huo na pamoja na kukamilisha tatizo hilo la kulipa fidia ambalo liko mikononi mwao.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ingawa muda wa maswali umepita kidogo lakini mtakumbuka kulikuwa na uwasilishaji mezani wa taarifa kadha wa kadha. Kwa hiyo, najaribu kufidia ili tumalize haya maswali mawili. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Ruth Msafiri, kwa niaba yake namwita Mheshimiwa Wilson Massilingi.

Na. 62

#### **Utumiaji wa Nishati ya Umeme wa Jua Nchini.**

**MHE. WILSON M. MASILINGI (K.n.y. MHE. RUTH B. MSAFIRI)** atauliza:-

Kwa kuwa nchi yetu ni ya kitropiko yenyе vipingi virefu vyā jua kali lenge uwezo wa kutoa nishati ya umeme unaoweza kutumika popote hadi vijijini kwa matumizi mbalimbali ya wananchi.

- (a) Je, Serikali inafanya jitihada gani za kuweka nguvu katika upatikanaji wa nishati hii mbadala na kuisambaza vijijini?
- (b) Je, Serikali ina mpango wowote wa kupelekea nishata hiyo kwenye shule zetu za Sekondari na zahanati vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naona unaondoka na nilikuwa na ujumbe kidogo. Mambo ya kuchelewesha fedha za Mfuko Maalum wa Bunge, hayapendezi kabisa. Kwa hiyo, nilitaka ujue hilo tu. (*Kicheko*)

Sasa hata ukitaka kwenda unaweza kwenda na pengine kama unakwenda basi ulishughulikie hilo. (*Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Hajajibu Hoja.

**SPIKA:** Hakuna haja ya kujibu. Wewe lifanyie kazi tu, tuone mchana watu wanatabasamu humu ndani. Naibu Waziri wa Nishati na Madini majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kabla ya kujibu swal la Mheshimwa Ruth Blasio Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Nchi yetu inapata mwanga wa jua kwa wastani wa zaidi ya saa sita (6) kwa siku na kufanya wastani wa mnururisho kuwa *watt* 218 kwa kila meta ya mraba. Mnururisho huo kitaalam unatosha sana kuzalisha umeme. Teknolojia za kuzalisha umeme kutumia mionzi ya jua zimethibitishwa. Vikwazo vyta undelezaji matumizi ya teknolojia husika ya uzalishaji umeme kwa kutumia mionzi ya jua kwa hapa Tanzania ni pamoja na gharama kubwa ya vifaa, uelewa ndogo kuhusu chanzo hiki cha nishatai, kutokuwepo mafundi wa kutosha kuhudumia teknolojia husika, vyombo vyta fedha kutojihushisha na teknolojia za nishati jiaidifu na soko kuingiliwa na vifaa visiviyokidhi viwango vyta ubora.

Baada ya maelezo ya kiutangulizi naomba kujibu swal la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutekeleza mikakati na miradi mbalimbali kuhusu uendelezaji wa matumizi ya umeme nuru nchini. Mikakati iliyotekelizwa ni pamoja na Serikali kuondoa kodi zote kwenye vifaa vyta nishati ya jua mwaka 2005, pamoja na kuunga mkono juhudhi za wadau kama vile *TATEDO* na *Tanzania Solar Energy Association (TASEA)*.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuhamasisha upolekaji wa umeme wa jua katika shule za Sekondari na Zahanati zilizopo mbali na gridi ya Taifa imeingiza vipengele vyta kujenga mifumo ya maonesho katika baadhi ya shule na vituo vyta afya. Kupitia mradi wa *UNDP/GEF* unaofadhaliwa na *World Bank*, mitambo ya maonesho imefungwa katika baadhi ya shule za sekondari katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara na Kagera. Mradi umefunga mitambo ya maonesho katika jumla ya vituo vyta afya 51 katika mikoa ya Mara, Shinyanga, Mara na kigoma na Mwanza. Aidha mtaala wa umeme nuru kwa ajili ya mafunzo ya vyuo vyta *VETA* umeandalishi na vifaa vyta mafunzo kutolewa kwa *VETA* Mwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa nishati kwa ajili ya maendeleo ya elimu nchini ningependa kutumia fursa hii kuishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na wadau wa sekta ya Elimu na Afya, kuhakikisha kuwa masuala ya nishatai yanaingizwa katika mipango ya uanzishaji shule na vituo vyta afya wakati wa ukarabati wa shule na zahanati hizo ili kusaidia katika kuongeza ubora wa elimu itolewayo na vituo vyta afya. Aidha, nitoe mwito kwa sekta zote kuzingatia mahitaji ya nishati katika mipango na Bajeti ili malengo ya maendeleo yafikiwe kama ilivyotarajiwa.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza nikupongeze kwa ujasiri wako na umakini katika kuongoza Bunge kama ulivyodhihirisha dakika mbili zilizopita. Nina swali moja la nyongeza. (*Makofii*)

Kwa kuwa Serikali imekuwa inatoa ushirikiano wa karibu sana hasa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kuimairisha elimu ya sekondari katika Wilaya ya Muleba na Mkurugenzi wa Halmashauri wa Wilaya ya Muleba na Afisa Elimu wa Sekondari ya Wilaya ya Mleba wanachapa kazi kwelikweli na haijapata kutokea. Je, huu ushauri ambao Waziri wa Nishati na Madini kuitia kwa Naibu wake ameutoa kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kwamba vifunguliwe vituo vya maonesho ya nishati ya nguvu ya jua utazingatiwa kwa kukipatia kipaumbele Wilaya ya Muleba ambapo mwuliza swali Mbunge mwenzako anatokea?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi nimesema kwamba huu mradi wa *UNDP/GEF* ambao ni mradi wa majaribio ambao unafadhiliwa na *World Bank* kwa sasa hivi uko kwenye Mikoa ya Mwanza, Shinyanga Mara na Kagera. Kwa hiyo, ni kwa sababu ni mradi wa majaribio lengo ni kwamba bada ya *pilot study* hii kufanikiwa na kukamilika, Serikali sisi wenyewe sasa tuendelee na mpango huu kama sehemu ya kupata umeme na nishati kwenye shule na zahanati.

Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba nina hakika na wenzangu wamenisikia. Kwa hiyo tutakapokamiliha *project* hii na kuhakikisha kwamba inakidhi mahitaji nadhani ni mradi ambao utaenda kwenye shule na zahanati zingine. (*Makofii*)

Na. 63

### **Ufugaji Nyuki**

**MHE. JOYCE M. MASUNGA (K.n.y. MHE. FELIX N. KIJKO)** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Kibondo ina wafugaji wengi wa nyuki na kwa kuwa shughuli za ufugaji nyuki hufanyika ndani ya Hifadhi kwa vibali maalum vinavyotolewa na Serikali; na kwa kuwa kumekuwepo na tatizo la utoaji vibali hivyo bila kuzingatia misimu ya urinaji wa asali kwa kisingizio kuwa ni msimu wa uwindaji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa vibali kwa kuzingatia matakwa ya wavunaji asali ambao ni wana chama chao kiitwacho UKI Wilayani Kibondo ili kuwa na uhuru wa kufanya kazi zao kwa wakati ikiwa ni pamoja na kuwapa ulinzi askari wa wanyamaporii?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mbunge wa Muhambo, kama ifuatavyo:-

Wizara yangu inatambua na kukubaliana na Mbunge kuwa Sekta ya ufgaji nyuki inao mchango mkubwa kwa wananchi wengi wanaofuga nyuki katika Wilaya ya Kibondo. Shughuli nyingi za ufgaji nyuki nchini hufanyika katika misitu ya asili, misitu iliyokuwa kwenye ardhi ya jumla, misitu ya hifadhi na katika mapori ya akiba kwa kuzingatia mpango maalum wa usimamizi unaokuwa umeandaliwa. Uvunaji wa asali katika Wilaya ya Kibondo kufanyika kwa misimu miwili, msimu mkubwa huwa kati ya mwezi Mei na Julai na msimu mdogo katika miezi ya Novemba na Desemba. Pia pori la Muyowosi Kigosi lina vitalu vya wawindaji ambao nao hutumia maeneo hayo hayo na katika kipindi kilekile cha msimu mkubwa wa uvunaji. Ili kudhibiti shughuli zinazofanyika katika kipindi kimoja, uongozi wa pori hutoa vibali kulingana na kalenda ya ufgaji nyuki ya msimu wa uvunaji. Aidha katika kurahisisha utoaji wa vibali wafugaji nyuki wameshauriwa kufanya mambo yafuatayo:-

1. Kuunda vikundi.
2. Kuanisha maeneo yeny uwezo mkubwa wa uzalishaji wa asali.
3. Kuweka bayana muda sahihi wa kuingia katika pori la akiba kwa ajili ya shughuli za ufgaji nyuki kwa kuzingatia kalenda ya ufgaji nyuki.
4. Kuwasilisha katika Ofisi ya Pori la Akiba la Muyowosi Kigosi mapendekezo ya jinsi ya kufanya shughuli za ufgaji katika pori hilo.

Katika kutekeleza hayo vikundi vimeundwa na hatua hii imesaidia sana, kuwapatia ulinzi kwa usalama wao wenyewe na pia kwa uwepo wao unasaidia kuzuia ujangili wa wanyamapori kwenye maeneo husika. Aidha, hali hii imeturahisishia kazi ya Askari wa Wanyamapori ya kulinda kikundi badala ya mfugaji nyuki mmoja mmoja. Kwani pori la Akiba la Muyowosi Kigosi lina askari wachache ambao hawatoshi kumlinda kila mmoja. Aidha kuunda vikundi kumesaidia kupata takwimu za uzalishaji wa asali katika mapori ili kubaini mchango wake kwa jamii na Taifa kwa ujumla. Kutokana na hali niliyoelezea ni matumaini yangu kwa utaratibu uliopo hivi sasa ni mzuri. Hata hivyo iwapo bado Mheshimiwa Mbunge anaona kuna dosari basi Wizara yangu iko tayari kushirikiana naye pamoja na wafugaji nyuki katika kuboresha utaratibu wa kuingia hifadhini kwa vikundi na kwa muda maalum lakini kwa kuzingatia mazingira niliyobainisha. (*Makofi*)

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa na majibu mazuri ya Naibu Waziri naomba niulize swal moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa maelekezo ya Wizara ambayo yametolewa hivi karibuni, nchi nzima na kwa baadhi ya maeneo yametafsiriwa vibaya na baadhi ya watendaji na kuleta usumbufu mkubwa kwa walina asali na wavuvi kuwalazimisha kuanza shughuli zao tarehe 1 Julai bila kuzingatia ile ratiba ambayo kwa kweli ilikuwa inawasaidia kupata mavuno yao vizuri katika vipindi vilivyopita. Je, Sasa Wizara itakuwa tayari kutoa maelekezo mapya ambayo hayataleta usumbufu kwa walina asali na wavuvi nchi nzima?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba ili kuhakikisha tunakuwa na udhibiti katika watu wanaoingia kwenye hifadhi wananchi wameshauriwa kuunda vikundi pamoja na mambo mengine pia wameshauriwa kuweka bayana muda sahihi wa kuingia katika pori. Katika kuweka bayana si lazima iwe Julai, tunachotaka sisi ni kikundi kusema kwamba kwa eneo hili msimu unaofaa kwa uvunaji wa asali ni muda fulani na kwa maana hiyo si lazima iwe Julai tu ila ni muda wowote ili mradi mawasiliano yawe yamefanyika. (*Makofi*)

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la wafugaji wa nyuki wa Kibondo linalingana na tatizo la wafugaji wa nyuki wa Kahama ambao wana-share shamba lile la pori la akiba la Kigosi Muyowasi; na kwa kuwa kwa ufahamu wangu pori hili lina maeneo machache sana na pori hili lina zaidi ya kilomita za mraba 20,000, lina maeneo ya machache sana ya uwindaji.

Je, hili tatizo la mgongano kati ya wawindaji na wafugaji wa nyuki linatokea wapi kama si ukiritimba na kuzalisha eneo la rushwa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, tatizo ambalo tunalo si mgongano kati ya wawindaji na wafugaji wa nyuki. Tatizo lililoko kwa ujumla ni la usalama wa binadamu wenyewe na wanyamapori. Kwenye maeneo mengine imeleta shida kwamba hawa hawa warinaji wa asali kuna maeneo ambapo unakuta kuna ujangili unafanyika. Kuna maeneo tumewahi kukamata silaha zimefichwa kwenye mizinga ya nyuki na kadhalika.

Kwa hiyo, inaleta taabu sana ndiyo maana tukasema ni vizuri waende katika utaratibu ambao ni *coordinated* lakini vilevile ni kwa usalama wao wenyewe wananchi kwa sababu wanapokwenda kule warinaji wa asali hatutegemei waingie na silaha na hairuhusiwi. Kwa hivyo wakiingia kule na kupambana na wanyama wakali pia inakuwa ni tatizo. Kwa hiyo, migongano si kati ya wawindaji wa kitalii na warinaji asali pakee bali pia ni pamoja na wadau wengine wakiwemo wanyama wenyewe. Kwa hiyo, hakuna mgongano katika maeneo mawili ila tatizo la mgongano liko pana zaidi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umepita na maswali yamekwisha. Ninayo matangazo leo marefu kidogo kwa sababu ya uzito wa shughuli inayofuata. Sasa wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, ni hawa wafuatao.

Ndugu Paniel Lyimo - Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bibi Maimuna Tarishi - Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ndugu Fanuel Mbonde, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bwana Eliakim Maswi - Naibu Katibu Mkuu, TAMISEMI na Ndugu Jumanne Sagini - Naibu Katibu Mkuu, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima na taadhima napenda niwatambulische kwenu Wakuu wetu wa Mikoa, ambao kwa kweli ndiyo mhimili wetu mkubwa sana wa maendeleo ya nchi yetu kwa sababu katika maeneo yao ndiyo wanaosimamia sekta zote kwa niaba ya Rais. Wakuu wetu wa Mikoa ambao wako hapa, waliotangulia ni Wabunge wenzenetu; sijui ndiyo upendeleo huu? Mheshimiwa Dr. James Msekela wa Dodoma hayupo leo.

Mheshimiwa William Lukuvi - Dar es Salaam, Mheshimiwa Monica Mbega - Kilimanjaro; au wako kwenye mikutano hawa? Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz Iringa, Mheshimiwa Dr. Christine Ishengoma - Ruvuma, Mheshimiwa Meja Jenerali Mstaafu Said Kalemba - Tanga, Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Daudi Balele - Shinyanga, Mheshimiwa Kanali Mstaafu Anatoli Tarimo - Mtwara, Mheshimiwa Kanali Mstaafu Enos Mfuru - Mara, Mheshimiwa Kanali Mstaafu Joseph Simbakalia - Kigoma; Ooh! ana ugeni wa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Luteni Kanali Mstaafu Issa Machibya - Morogoro, Mheshimiwa Mohamed Babu - Kagera, Mheshimiwa Isidori Shirima - Arusha, Mheshimiwa Daniel Ole Njoolay - Rukwa, Mheshimiwa Abbas Kandoro - Mwanza; pamoja na maandalizi ya kwenda Kalenga lakini ndiyo hivyo tena, Mheshimiwa John Mwakipesile - Mbeya, Mheshimiwa Hajjat Amina Mrisho - Pwani; ahsante sana na maandalizi ya kwenda Kiteto, Mheshimiwa Parseko Kone - Singida, Mheshimiwa Abeid Mwinyimsa - Tabora, Mheshimiwa Sadik Meki Sadik - Lindi, Mheshimiwa Henry Shekiffu - Manyara; Mheshimiwa Shekiffu sijapata taarifa zako rasmi lakini karibu sana Dodoma. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mheshimiwa Celina Kombani, ambao kwanza ni mume wake Ndugu Tongolani na Watoto wao wawili; Joel na Shaaban; wale pale karibuni sana. Pia wageni wake wengine ni Wachungaji wanne, nadhani hawa ni Wachungaji wa mambo ya dini siyo wale akina Laizer; wachungaji wanne kutoka Dodoma ahsanteni sana.

Mzee wetu, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, ana mgeni wake anaitwa Ndugu Simwita ni Kada wa CCM na Diwani kutoka Tarafa ya Kamsamba, Wilaya ya Mbozi; ahsante sana na karibu sana.

Pia mionganoni mwa Wageni wetu leo ni Makatabu Tawala wote wa Mikoa ya Tanzania Bara. Ninaomba wasimame pale walipo kwa pamoja; ahsanteni sana. Hawa ndiyo Watendaji Wakuu katika Mikoa, tunawashukuru kwa kazi yenu kubwa mnayoifanya.

Wapo Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu; Ndugu Rajab Kiravu - Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Ndugu John Tendwa - Msajili wa Vyama vya Siasa, Dr. Fatuma Mrisho - Mwenyekiti Mtendaji wa TACAIDS, Bwana Martin Kitila - Mkurugenzi Mkuu wa CDA, Bwana Emmanuel Ole Naiko - Mkurugenzi Mtendaji wa TIC na Bwana Christopher Shekiondo - Kamishna wa Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya.

Wapo pia Bwana Eliud Sanga - Mkurugenzi Mkuu wa LAPF, Bwana Dunstan Mrutu - Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Biashara , Bwana William Kabisama - Katibu wa Bodi wa Mfuko wa Serikali za Mitaa na Kanali Mstaafu Ferdinand Swai - Mkurugenzi wa Shirika la Elimu Kibaha.

Vilevile wapo Wakurugenzi wa Idara mbalimbali ila kwa majina yupo Bwana Ramadhan Khalfan - Mkuu wa Bodi ya Biashara za Nje, Bwana Majid Kikula - Afisa Usalama wa Serikali, wametajwa hapa Mwenyekiti wa Bodi ya Wazamini wa Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, lakini hawakuandika jina; Mwenyekiti yule pale ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, wageni wa Mheshimiwa Mwinchoum Msomi ni wanafunzi 27 na watumishi 3 kutoka Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, wakiongozwa na Ndugu Everline Mpasha - Afisa Uhusiano wa Chuo; karibuni sana tunawatachia mema katika mafunzo yenu kwa sababu kadiri mnavyojituma katika mafunzo, basi mnakuja kuwa watumishi bora katika Taifa na tunawatachia mema.

Wageni wa Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini ni Bibi Gaudensia Mathayo, ambaye ni Mama Mzazi wa Mheshimiwa Mbunge. Mama yetu tunaomba usimame pale ulipo; ahsante sana. Ndugu Gati Joel Musira ni dada yake ambaye ni Mtumishi wa TRA, watoto wake yeche sasa Evodia Joel, Edith Joel, Justus Joel , Miriam Vedastusi na Thomsoni Vedastusi; wale pale asanteni sana.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Castor Ligallama, ambao ni wafugaji 18 na Maafisa Ugani 3 kutoka Vijiji vya Chita, Namwawala, Mkangawalo, Merera, Sagamaganga na Kiberege; asanteni sana na karibuni sana ndugu zetu wafugaji pamoja na maafisa ugani.

Mgeni wa Mheshimiwa George Simbachawene, ambaye ni Ndugu Erasto Badiel - Afisa Mikopo wa NMB. Hakusema ni NMB ya wapi, inaweza kuwa ni ya Mpwampwa nadhani; karibu sana.

Pia ninaye mgeni wangu amekaa wapi sasa; Frt John Kasembo ambaye anasomea upadri katika Seminari Kuu Peramiho Songea. Frt uko wapi? Ahsante sana; karibu sana tutaongea baadae. Waheshimiwa Wabunge ni lazima kuwa na watu wa dini nyakati kama hizi. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya kazi. Leo saa saba mchana kikao kimeitishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Alhaji Mohammed Missanga, Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu mkutane katika Ukumbi wa *Basement* hapa katika jengo jipya saa mchana. Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji mkutane saa saba mchana katika Ukumbi Namba 231, Jengo la Utawala.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwisho wa matangazo. Nimepata barua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba, mambo yanakamilishwa leo; yale mambo yale, kwa hiyo, kesho watu watafurahi tu. Waheshimiwa, taarifa ndiyo hiyo. Sasa namwita Katibu kwa shughuli inayofuata.

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011 - Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2010/2011**

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, iliyochambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2010/2011. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu, likubali kuitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, kumekuwepo na matukio mbalimbali ambayo yamewagusa Watanzania. Waheshimiwa Wabunge, watakumbuka kuwa ni katika kipindi hiki Bunge lilipata Msiba wa aliyekuwa Mbunge wa Ruangwa, Marehemu Sigifrid Seleman Ng'itu, aliyefariki Dunia tarehe 2 Novemba, 2009. Aidha, Nchi yetu ilipata msiba mkubwa wa kuondokewa na Mzee wetu, Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa, Waziri Mkuu Mstaafu na Makamu wa Pili wa Rais aliyefariki Dunia tarehe 31 Desemba, 2009. Matukio mengine ni ajali za barabarani na mafuriko yaliyosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali za Wananchi wengi. Tunamwomba Mwenyezi Mungu, awaponye haraka majeruhi wote na aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2009 na Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011. Napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo (Mb), Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa Hotuba nzuri na ufanuzi fasaha wa hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa kujadili Hotuba hiyo. Vilevile, napenda kuwapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa kuzijadili kwa kina Hotuba hizo na hatimaye kuitisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2010/2011. Serikali inathamini ushauri mlioutoa na itauzingatia wakati wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti hiyo.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa michango na ushauri waliotoa wakati wa kuitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara za Serikali Zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kipekee, nitumie nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kwa mchango wao mkubwa wakati wa

uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Bunge. Maoni na Ushauri wao umesaidia sana kuboresha Makadirio ya Bajeti ninayowasilisha leo.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu limepitisha Bajeti ya Serikali ambayo inakamilisha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005. Hivyo, katika Hotuba yangu, nitaelezea kwa muhtasari baadhi ya mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Nne kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita. Katika kipindi hicho, Serikali ilitekeleza kazi zake kwa kuzingatia Ahadi zilizopo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, MKUKUTA na Malengo ya Milenia. Kwa ujumla, Serikali imepata mafanikio makubwa ambayo matokeo yake yanajidhihirisha katika Ukuaji Uchumi, Kuimariika kwa Huduma za Kiuchumi na Kijamii na Utawala Bora. Nitumie fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake makini na kusimamia vizuri Serikali na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005. Aidha, nawashukuru Wananchi wote kwa kutekeleza Ilani hiyo kwa mafanikio.

Mheshimiwa Spika, hali ya Siasa Nchini ni shwari. Nchi yetu imekuwa mfano bora wa kuendesha Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa kwani tumeendelea kukosoana na kupingana bila kupigana. Jambo hilo limeifanya Nchi yetu iendelee kuwa na amani na kuwezesha watu wetu kufanya kazi za kujiletea maendeleo. Hali hii imeiletea Nchi yetu heshima kubwa Kikanda na Kimataifa. Natoa wito tuendelee kudumisha utamaduni na sifa hizo njema ili tuweze kuendelea kuwa nchi ya amani na utilivu. Tunapoelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2010, tuendelee kutumia majukwaa yetu vizuri, tutumie lugha zenye staha na kuzingatia maadili na heshima ya Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Siasa: Katika kukuza Demokrasia na kusimamia Siasa za Vyama Vingi Nchini, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa imetua usajili wa kudumu kwa Vyama vya Siasa 18 Nchini. Vyama viwili vya Siasa vya *National Coalition for Democratic Movement (NCDM)* na Chama cha Jamii (CCJ), vimepata usajili wa muda. Aidha, Vyama vya *Peoples Democratic Movement (PDM)* na *Democratic National Congress* vilifutiwa usajili baada ya kushindwa kutimiza masharti ya usajili wa kudumu. Kanuni za Maadili ya Vyama zimetungwa na Vyama vyote vya Siasa vimekubaliana kuzifuata na kuziheshimu. Aidha, ili kuiwezesha Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kutoa huduma zake karibu zaidi na Wadau wake, Ofisi tatu mpya za Kanda za Mwanza, Arusha na Mbeya zimefunguliwa. Vilevile, Serikali imepanua wigo wa Vyama vya Siasa vinavyopata ruzuku kwa kujumuisha vile vyenye Madiwani. Kwa sasa Vyama vinavyopata Ruzuku ni CCM, CHADEMA, CUF na UDP. Vingine ni TLP, NCCR-MAGEUZI, PPT-Maendeleo na CHAUSTA.

Mheshimiwa Spika, Sheria mpya ya Gharama za Uchaguzi ya Mwaka 2010 inayoweka udhibiti na ukomo wa matumizi ya fedha wakati wa kura za maoni na Kampeni za Uchaguzi imepitishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Aprili, 2010. Dhana kubwa katika Sheria hiyo ni Kudhibiti Rushwa katika Siasa ili kupata Viongozi ambao wamechaguliwa kwa ridhaa ya Wananchi pasipo Rushwa. Nichukue nafasi hii, kuwapongeza Wananchi kwa kushiriki kutoa mawazo yaliyowezesha kutungwa kwa

Sheria hiyo yenyе umuhimu wa pekee katika kuimarisha Demokrasia na kuweka uwanja sawa wa ushindani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa itaendelea kutoa Elimu kwa Umma kuhusu Sheria ya Gharama za Uchaguzi, kukagua shughuli na uhai wa Vyama vya Siasa na kukagua Taarifa zitakazotolewa na Wagombea pamoja na Vyama vya Siasa kabla na baada ya Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali ilifanikisha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika ngazi ya Kitongoji, Kijiji na Mtaa uliofanyika mwezi Oktoba 2009. Katika uchaguzi huo, Chama cha Mapinduzi (CCM) kiliongoza kwa asilimia 92, kikifuatiwa na CUF asilimia 4 na CHADEMA asilimia 3. Vyama vingine vilivyoshiriki ni CHAUSTA, NCCR-Mageuzi, TLP, UMD, UPDP, UDP, PPT-Maendeleo, SAU, DP, NLD na NRA ambavyo kwa pamoja vilipata asilimia moja. Nichukue fursa hii, kukipongeza kwa dhati Chama cha Mapinduzi kwa kupata ushindi mkubwa. Aidha, navishukuru Vyama vyote vilivyoshiriki katika Uchaguzi huo na kwa utulivu walioonesha wakati wote wa Kampeni na Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba, 2010 ni wa nne tangu kuanzishwa kwa Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa Nchini. Hatua mbalimbali zimechukuliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kufanikisha Maandalizi ya Uchaguzi huo. Hatua hizo ni pamoja na kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, kutoa Elimu ya Mpiga Kura na kufanyika kwa marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi.

Hatua nyininge zilizochukuliwa ni kugawa Majimbo Saba ya Uchaguzi ambayo ni Ukonga, Tunduru, Singida Kusini, Kasulu Mashariki, Bukombe, Maswa na Nkasi. Vilevile, Kata mpya 808 zimeanzishwa na zitahusishwa katika Uchaguzi Mkuu ujao. Natoa wito kwa Viongozi na Wadau wote kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi wakati wote wa zoezi zima la Uchaguzi Mkuu wa Mwaka huu. Wote tunalo jukumu la kuhakikisha kwamba, Uchaguzi unafanyika kwa hali ya amani na utulivu na kila mwenye sifa ajitokeze kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005 – 2010, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeimarisha na kuondoa baadhi ya vikwazo katika utekelezaji wa mambo yanayohusu Muungano. Vikao vinne vya Kamati ya pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar vilifanyika chini ya Uenyekiti wa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein. Katika Vikao hivyo, hoja tisa zilijadiliwa na kati ya hizo, hoja mbili zilipatiwa ufumbuzi na kuondolewa katika orodha ya Kero za Muungano. Hoja saba zinaendelea kufanyiwa kazi. Aidha, jumla ya Vikao 75 vya ushirikiano wa Serikali mbili kwa masuala yasiyo ya Muungano vilifanyika.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuimarisha Muungano, miradi ya pamoja ya maendeleo imetekeliza katika pande zote mbili za Muungano. Miradi hiyo ni *TASAF*, *MACEMP*, *PADEP* na *SELF*, pamoja na uimarishaji na ukarabati wa njia ya umeme kutoka Dar es Salaam hadi Fumba – Zanzibar. Vilevile, utekelezaji wa Mradi wa Umeme

kutoka Pangani kwenda Pemba ulikamilika na kuzinduliwa tarehe 3 Juni, 2010 na Mheshimiwa Dkt. Amani Abeid Karume, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Aidha, maandalizi ya ujenzi wa barabara tano za Pemba yanafanyika chini ya ufadhili wa *Millenium Challenge Corporation (MCC)*. Serikali pia imekamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Dar es Salaam na inaendelea na ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Tunguu – Zanzibar. Aidha, ujenzi wa Ofisi Ndogo ya Bunge, Tawi la Benki Kuu na Ofisi ya Uhamiaji – Zanzibar umekamilika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Vikao vya Kamati ya pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar vitaendelea kufanyika na kutekeleza miradi ya pamoja ya maendeleo ya pande zote za Muungano. Aidha, Wizara zisizo za Muungano, zitahimizwa kukutana mara kwa mara kujadili masuala ya Sera na kubadilishana uzoefu ili kuimarisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Desemba 2005 hadi Juni 2010, Bunge limefanya Mikutano 20 yenye Vikao zaidi ya 340. Katika Mikutano hiyo, Miswada ya Sheria 93 ilipitishwa na Maazimio 49 kuridhiwa. Vilevile, Maswali ya Msingi 3,411 na ya Nyongeza 5,129 ya Waheshimiwa Wabunge yamejibiwa na Serikali. Hoja mbalimbali za Kamati za Kudumu za Bunge pamoja na hoja Binafsi za Wabunge ziliwasilishwa na kujadiliwa. Aidha, Waziri Mkuu alijibu Maswali ya Msingi 270 kwa utaratibu wa Maswali ya Papo kwa Papo. Bunge letu liliandaa kwa mafanikio makubwa Mkutano wa 55 wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola uliofanyika Arusha kuanzia tarehe 29 Septemba hadi 5 Oktoba 2009. Mkutano huo ambao ulikuwa na Kaulimbiu ya “Kukabiliana na Changamoto Mbalimbali Zinazoikabili Dunia” ulilettea Nchi yetu sifa na kujulikana Duniani.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge hili kwa Kasi na Viwango vya hali ya juu pamoja na umakini mkubwa. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa kutimiza wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga Sheria na kuishauri Serikali. Nawashukuru pia kwa michango yao ambayo imesaidia kuboresha utendaji wa Serikali na kuimarisha utoaji wa huduma kwa Wananchi. Nawatakieni wote kila la kheri katika Uchaguzi Mkuu ujao ili sote turudi tena Bungeni tuendelee kuwatumikia Wananchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2008, Uchumi umeendelea kuimarika na Pato la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 7.2 kwa mwaka. Mwaka 2009, Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 6.0 ikilinganishwa na asilimia 7.4 mwaka 2008. Kushuka kwa ukuaji wa Uchumi kunatokana na athari za Mtikisiko wa Uchumi Duniani pamoja na ukame ulioikumba Nchi yetu kwa misimu miwili mfululizo. Pia, katika kipindi hicho, Mfumko wa Bei ulipanda kutoka wastani wa asilimia 5 mwaka 2005 hadi 12.2 Desemba 2009. Hali hii ilitokana na kuongezeka kwa bei ya mafuta katika Soko la Dunia na ukame mkubwa uliotokea katika maeneo mengi Nchini na kusababisha ukosefu wa chakula na hivyo bei zake kupanda. Hata hivyo, kutokana na juhudzi zilizochukuliwa na Serikali, Mfumko wa Bei umeanza kupungua hadi kufikia asilimia 7.9 mwezi Mei 2010. Serikali itaendelea kuandaa na kusimamia Sera za Uchumi, Mapato na Matumizi ya Serikali ili kujenga Uchumi imara na endelevu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania kama zilivyo Nchi nyingi Duniani, hufanya Sensa ya Watu na Makazi kila baada ya miaka kumi. Sensa nyingine itafanyika mwezi Agosti 2012. Ili kufanikisha zoezi hili, mwezi Mei 2010, Serikali ilitoa Waraka kuhusu kuundwa kwa Kamati mbalimbali za Sensa kuanzia ngazi ya Wilaya, Mkoa hadi Taifa. Napenda kuchukua fursa hii kusositiza kwamba, Kamati za Sensa katika ngazi zote ziundwe na zianze mara moja utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, kila Kiongozi na Mtendaji ahakikishe kuwa, anazungumzia umuhimu wa Sensa kila anapopata nafasi ya mkutano au mkusanyiko wowote wa kikazi. Vilevile, kila Mwananchi afahamu kwamba, Sensa ya Watu na Makazi ni zoezi la Kitaifa linalohitaji ushirikiano mkubwa, hivyo kila mmoja awe ni mhamasishaji ili zoezi hilo lifanikiwe.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2005 – 2010; Serikali imeweka Mazingira Wezeshi ya Biashara na Uwekezaji ili kuimarisha ushiriki na ushindani wa Sekta Binafsi. Lengo ni kuhakikisha kuwa, Sekta Binafsi inakua na kuhimili ushindani katika Masoko ya Ndani na Nje.

Katika kufikia azma hiyo, Serikali ilitekeleza Programu na Mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania na Mradi wa Kuimarisha Ushindani wa Sekta Binafsi. Aidha, Serikali imeboresha Mifumo ya Kitaasisi na Kisheria kwa lengo la kuimarisha Uwekezaji, ikiwa ni pamoja na kuundwa kwa Kitengo Maalum cha kushughulikia Malalamiko ya Wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuweka Mazingira Wezeshi ya Biashara Nchini, bado tunahitaji kuchukua hatua zaidi. Taarifa za Wepesi wa Kufanya Biashara inayochapishwa kila mwaka na Benki ya Dunia, inaonesha kuwa, Tanzania ilishuka kutoka nafasi ya 126 kati ya Nchi 178 mwaka 2008, hadi 131 kati ya Nchi 183 mwaka 2010. Ili kukabiliana na hali hii, Serikali inatekeleza Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira Wezeshaji ya Uwekezaji na Biashara katika maeneo ya Usajili wa Biashara na Kampuni; Usajili wa Rasilimali na Ajira ya Wafanyakazi. Maeneo mengine ni Upatikanaji wa Mikopo; Usuluhishi wa Migogoro ya Kibiashara; Vibali vya Ujenzi; Ulinzi kwa Wawekezaji; Ulipaji Kodi; Urahisi wa Kuendesha Biashara ya Ndani na ya Nje; na Masuala ya Utawala Bora. Napenda kusositiza kuwa, wahuksika wote katika utekelezaji wa shughuli zilizoainishwa katika Mpango huo, wawajibike ipasavyo ili kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha Sera ya Ubina baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Sera hiyo imeweka bayana mfumo na taratibu za ushirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Lengo ni kuwezesha Sekta Binafsi kuchangia zaidi katika kutoa huduma za Kiuchumi na Kijamii kwa viwango bora na gharama nafuu. Serikali pia imeendelea kuwa na mawasiliano ya karibu na ya mara kwa mara na Wadau wa Sekta Binafsi kuititia Baraza la Taifa la Biashara. Serikali inakamilisha mapendelekezo ya Muswada wa Sheria ya Ubina baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na inatarajia kuyawasilisha katika Mkutano huu wa Bunge la Bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005 – 2010, jitihada za kuvutia uwekezaji wa ndani na nje ya Nchi, zimekuwa na mafanikio mbalimbali. Kituo cha

Uwekezaji kilisajili Miradi 3,458 yenyе thamani ya Dola za Kimarekani milioni 22,704. Kati ya Miradi hiyo, Miradi 1,768 ni ya Watanzania, 833 ya Wageni na 857 ni ya Ubia kati ya Watanzania na Wageni. Miradi hiyo kwa pamoja, inatarajiwa kuchangia upatikanaji wa ajira mpya 407,737 kwa Watanzania katika Sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha Sekta ya Kilimo chini ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo katika maeneo ya kugharamia Ruzuku ya Mbolea, Mbegu Bora, Miche na Madawa. Maeneo mengine ni kusimamia utoaji wa mikopo kupitia Mfuko wa Pembejeo za Kilimo, kuongeza uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora, kuimarisha huduma za ugani, utafiti na mafunzo ya kilimo, kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao na kuendeleza matumizi ya zana bora za kilimo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiongeza Ruzuku ya Pembejeo za Kilimo ili kuhakikisha kwamba, Wakulima wanazipata kwa bei nafuu na kwa wakati unaotakiwa. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali iliongeza fedha kwa ajili ya ruzuku ya pembejeo za Kilimo kwa asilimia 1,361 kutoka Shilingi bilioni 7.5 mwaka 2005/2006 hadi Shilingi bilioni 109.6 mwaka 2009/2010. Kutokana na ongezeko hilo, matumizi ya mbolea yameongezeka kwa asilimia 244 kutoka Tani 77,557 mwaka 2005/2006 hadi Tani 267,076 mwaka 2009/2010. Vilevile, katika kipindi hicho matumizi ya majembe ya kukokotwa na ng'ombe yameongezeka kutoka 585,240 hadi 819,360, sawa na ongezeko la asilimia 40.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ununuzi wa Zana za Kilimo, hadi mwezi Mei 2010, jumla ya matrekta makubwa 518 na matrekta madogo 162 yamekopeshwa kupitia Mfuko wa Pembejeo za Kilimo. Katika mwaka 2009/2010 pekee, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimenunua matrekta madogo 2,154 na makubwa 53. Kutokana na juhudhi hizo, tija imeongezeka katika uzalishaji wa baadhi ya mazao. Kwa mfano, uzalishaji wa mahindi umeongezeka kutoka wastani wa Tani 1.5 kwa Hekta mwaka 2005/2006 hadi Tani 3.8 kwa Hekta mwaka 2008/2009. Pia, uzalishaji wa Mpunga uliongezeka kutoka Tani 1.8 kwa Hekta hadi wastani wa Tani 5 kwa Hekta.

Mheshimiwa Spika, nazikumbusha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa matrekta kila mwaka. Aidha, Serikali imekamilisha taratibu za kupata Mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 40 kutoka Serikali ya India kwa ajili ya ununuzi wa Zana za Kilimo. Meli ya kwanza yenyе shehena ya Zana hizo itawasili Nchini mwezi Julai 2010.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, Sekta ya Kilimo imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali kama ukame, uwekezaji mdogo kwenye miundombinu, hasa katika kilimo cha umwagiliaji, usindikaji na masoko. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Serikali ilizindua Azma ya Kilimo Kwanza ambayo ni hatua thabiti ya kuleta Mapinduzi ya Kijani kwa kushirikisha Sekta Binafsi. Katika kutekeleza Azma hiyo, Wadau wameelimishwa lengo na madhumuni ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imetoa Shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kuanzisha Dirisha Maalum la Mikopo ya Kilimo katika Benki ya Rasilimali Tanzania na

inaendelea na matayarisho ya kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo. Nawahimiza Waheshimiwa Wabunge kuendelea kuelezea Azma ya Kilimo Kwanza popote mtakapokutana na Wananchi kama kichocheo cha kuongeza uzalishaji katika kilimo na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Serikali itaongeza upatikanaji wa pembejeo na zana za kilimo ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya Chakula na Biashara. Aidha, itaimarisha utafiti, mafunzo na huduma za ugani kwenye kilimo. Vilevile, usimamizi na uwajibikaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambao ni watekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo kuititia Sera ya Kupeleka Madaraka kwa Wananchi utaimarishwa.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji kinawawezesha wakulima wengi kulima na kuvuna hata mara mbili kwa mwaka kutegemea aina ya mazao. Aidha, kinawezesha kulima mazao mengine yenye soko na bei nzuri hasa kipindi cha ukame. Kutohana na hali hiyo, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2005 hadi Machi 2010, Serikali ilichukua hatua mbalimbali za kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Hatua hizo ni pamoja na kuandaa Sera ya Umwagiliaji, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Skimu za Umwagiliaji 244 na Mabwawa 24, kutoa mafunzo kwa Wakulima na Wataalamu katika maeneo ya matumizi bora ya maji, utunzaji wa miundombinu na Teknolojia mbalimbali za Umwagiliaji. Aidha, miongozo ya Uibuaji wa Miradi ya Umwagiliaji katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya ilikamilishwa na kuanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Serikali itajenga Skimu mbalimbali za Umwagiliaji kwa Wakulima Wadogo na wa Kati ili kuongeza uzalishaji na ufanisi wa matumizi ya maji. Aidha, itakamilisha uandaaji wa Mkakati na Sheria ya Umwagiliaji ili kutekeleza Sera Mpya ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo ina fursa kubwa katika kukuza Uchumi na kupunguza umaskini. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeanzisha Mpango wa kutoa Ruzuku ya Chanjo na Dawa za Kuogesha Mifugo ili kuongeza uzalishaji wenye tija na mapato kwa Wafugaji. Kati ya Mwaka 2006 hadi 2009, jumla ya lita 887,992 za dawa ya kuogesha mifugo zenye thamani ya Shilingi bilioni 13.5 zilinunuliwa na kusambazwa kwenye Mikoa yote, ambapo Wafugaji walizinunua kwa asilimia 60 ya bei ya Soko baada ya Serikali kutoa ruzuku ya asilimia 40. Aidha, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufutiliaji wa Mifugo ya Mwaka 2010 na Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo ya Mwaka 2010. Kupitishwa kwa Sheria hizo, kutaimarisha usimamizi wa Sekta ya Mifugo hasa katika biashara ya mifugo na mazao yake. Aidha, zitasaidia kupunguza tatizo la migogoro kati ya Wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Serikali itatoa kipaumbele katika kutekeleza Mpango wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi ili kubainisha maeneo ya ufugaji na matumizi mengine ya ardhi. Vilevile, itaimarisha utafiti na miundombinu ya mifugo ikiwemo majosho, malambo, mabwawa, minada, vituo vya afya ya mifugo na

machinjio. Aidha, Serikali itaanza kufanya maandalizi ya Sensa ya Mifugo itakayofanyika mwaka 2012 ili kupata takwimu sahihi za mifugo Nchini.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uvuvi inatoa mchangano mkubwa katika kuwapatia Wananchi ajira, lishe, kipato na kuiingizia Nchi fedha za kigeni. Kati ya mwaka 2006 – 2009, jumla ya tani milioni moja za samaki zenye thamani ya Shilingi bilioni 783 zilivunwa. Hata hivyo, usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi bado unakabiliwa na tatizo sugu la Uvuvi Haramu unaoendeshwa na baadhi ya Wavuvi pasipo kuzingatia Sheria na Kanuni zilizopo. Kutokana na hali hiyo, Serikali imeendesha zoezi la kupiga vita Uvuvi Haramu pamoja na kuwaelimisha Wananchi kuhusu athari za Uvuvi Haramu.

Natoa wito kwa Viongozi na Watendaji katika ngazi zote za Serikali na Wadau wa Uvuvi, wahusike kikamilifu katika kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya samaki. Aidha, elimu ya uvuvi endelevu itolewe kwa Wavuvi, Wawekezaji na Wadau wengine.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Serikali itasimamia uvunaji endelevu wa rasilimali za uvuvi katika maeneo yote ya maji hapa Nchini ili kuongeza mapato yatokanayo na Sekta ya Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2010, Serikali imetekeleza Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika. Programu hii imeweka mazingira mazuri ya kuwa na Vyama vya Ushirika vinavyoendeshwa kibiashara. Idadi ya Vyama vya Ushirika imeongezeka kutoka 5,730 mwaka 2005/2006 hadi 9,510 Desemba 2009, na Wanachama kutoka 291,368 hadi 795,482 katika kipindi hicho, sawa na ongezeko la asilimia 173. Akiba na Amana za Wanachama zimeongezeka kutoka Shilingi bilioni 65.7 mwaka 2005 hadi Shilingi bilioni 385.5 mwaka 2009. Aidha, mikopo iliyotolewa kwa Wanachama kuititia Vyama vya Akiba na Mikopo kwa ajili ya shughuli za Kilimo, Ufugaji, Usafirishaji, Ujenzi na Biashara iliongezeka kutoka Shilingi bilioni 54.1 hadi Shilingi bilioni 463.4. Katika mwaka 2010/2011, Serikali itaendelea kuvijengea uwezo Vyama vya Ushirika ili viwe endelevu na vyenye nguvu kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Uendelezaji wa Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo, ilikamilisha rasmi utekelezaji wa shughuli zake katika Wilaya 30 za Mikoa minane tarehe 31 Desemba, 2009. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuvijengea uwezo Vikundi 1,202 vyenye Kaya 43,000 za Wakulima, Wasindikaji wa Mazao ya Kilimo na Wafanyabiashara Wadogo; na kuviunganisha na masoko. Programu pia, imehamasisha na kuanzisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani katika Halmashauri za Wilaya tisa za Babati, Hanang, Mbarali, Mbeya Vijijini, Sumbawanga Vijijini, Kyela, Ileje, Mufindi na Mbozi.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Mfumo huo kumewezesha bei ya mazao yaliyohifadhiwa ghalani kupanda kwa zaidi ya mara mbili wakati wa kuuza. Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani pia umewawezesha Wakulima katika Kaya zaidi ya 7,000 kujipatia mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 12.5. Vilevile, Programu imewezeesa ukarabati wa Miundombinu ya Masoko Vijijini zikiwemo barabara zenye urefu wa

Kilomita 957.3 katika Wilaya 30 na Masoko ya kisasa 24 kwenye Wilaya 24 kwa ushirikiano na Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Huduma za Kifedha Vijijini imeboresha usimamizi na uendeshaji wa Asasi Ndogo za Kifedha 276 na kuimarisha Mifumo ya Kifedha Vijijini kwa kutoa mafunzo mbalimbali kwa Wanachama, Viongozi na Watendaji wa Asasi hizo. Mafunzo yalitolewa kwa Wanakamati 828 wa Kamati za Usimamizi na Maafisa Ushirika 51 kutoka Wilaya 22 na Mikoa 7 ambako Programu inatekelezwa. Aidha, Programu imeimarisha Benki ya Wananchi Mufindi, Benki ya Ushirika Kilimanjaro na Benki ya Wananchi Mwanga. Vilevile, uanzishwaji wa Benki za Wananchi Kyela na Mbeya Vijijini upo kwenye hatua za awali na Benki ya Wananchi Njombe imepatiwa Leseni.

Mheshimiwa Spika, Miradi hii imeonesha mafanikio makubwa katika kuchangia juhudhi za Serikali kupambana na umaskini. Mafanikio hayo yameibua chachu ya Wananchi wa Mikoa mingine kuomba kufikishiwa huduma za Miradi hii. Serikali imezingatia maombi hayo na imeanzisha mchakato wa kuendeleza shughuli za miradi hii katika Wilaya zote za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Wabia wa Maendeleo kama vile Shirika la Kilimo la Umoja wa Mataifa (*IFAD*), Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) na *Alliance for Green Revolution in Africa (AGRA)*, wameonesha nia ya kutoa fedha kwa ajili ya upanuzi wa shughuli za Miradi hii. Hatua za mwanzo za kuangalia jinsi Miradi hii itakavyoendelezwa zimeshaanza ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa fedha za uendeshaji. Hadi sasa warsha za Kikanda na Kitaifa zimefanyika na Taarifa ya Andiko la kina imekamilika. Mradi huo mpya utajulikana kama *Marketing Infrastructure, Value Addition and Rural Finance Support Programme* na utekelezaji wake utakuwa wa miaka mitano na unatarajiwa kuanza rasmi mwezi Julai, 2011.

Mheshimiwa Spika, ardhi ni msingi wa Uchumi wa Taifa lolote Duniani. Hata hivyo, ili ardhi iweze kutumiwa na makundi yote katika jamii, inahitaji mpango mzuri. Kwa kuzingatia ukweli huo, Serikali imeandaa Mpango wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi wa Miaka 20 kuanzia mwaka 2009 hadi 2029. Mpango huo unalenga kutenga ardhi katika ngazi ya Taifa, Wilaya na Kijiji kwa kuwashirikisha Wadau.

Programu 12 za Utekelezaji wa Mpango huo zilitayarishwa na jumla ya Vijiji 516 viliandaliwa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 64. Pamoja na hatua hizo, Serikali bado inakabiliwa na changamoto ya kupima ardhi yote Nchini na kuitayarishia Ramani ikiwa ni pamoja na kupima mashamba kwa kila Mkulima. Ili kukabiliana na tatizo hilo, Serikali imeanza kuweka alama za msingi za upimaji ardhi na utayarishaji ramani ambazo zitawezesha kuharakisha upimaji wa ardhi na kuandaa ramani kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Serikali itatekeleza Programu za Mpango wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Ardhi katika Wilaya na Vijiji mbalimbali Nchini. Mkazo utawekwa kwenye upimaji wa mashamba ya wakulima; ardhi kwa ajili ya Wawekezaji na kuweka mipaka kati ya Vijiji na Hifadhi za Wanyamapori, Misitu na Vijiji vyenye migogoro ya ardhi. Kazi hizi zitafanyika sambamba na utoaji wa Elimu kwa Umma kuhusu Sera, Sheria na Matumizi Bora ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, Makazi bora ni moja ya vipaumbele vya Serikali katika kuondoa umaskini. Hivyo, Serikali imehamasisha wananchi kujenga nyumba bora kwa kutumia vifaa na teknolojia rahisi za ujenzi. Aidha, kwa kuzingatia mazingira halisi ya Mijini na kasi ya ukuaji wa Miji, Sheria ya Miliki ya Sehemu za Jengo Na.16 ya Mwaka 2008 (*The Unit Titles Act No. 16 of 2008*) imetungwa. Sheria hiyo inawezesha mwananchi kupata Hatimiliki ya sehemu ya jengo. Hii itawezesha kipande kimoja cha ardhi hasa Mijini kuwanufaisha Wananchi wengi na kuongeza Soko la Nyumba na Mapato ya Serikali. Vilevile, Sheria ya Mikopo ya Nyumba Na. 17 ya Mwaka 2008 (*The Mortgage Financing Act No. 17 of 2008*) imetungwa ili kuondoa tatizo la kupata mikopo ya ujenzi na ununuzi wa nyumba.

Serikali pia, imetekeleza Programu ya Kurasimisha Makazi yaliyojengwa bila kupimwa kwa kutambua Miliki za Nyumba 290,000 katika Miji ya Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma, Tanga na Moshi. Wamiliki wamepewa Leseni za Makazi ambazo wameanza kuzitumia kuombea Mikopo katika Taasisi za Fedha.

Mheshimiwa Spika, kutokuwepo kwa mfumo wa Kiutawala kuhusu uendelezaji wa Nyumba katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, kumedumaza maendeleo ya ujenzi katika ngazi hizo. Uendelezaji wa Nyumba umebaki kuwa ni jukumu la mtu mmoja mmoja bila uratibu, miongozo na udhibiti wa Mamlaka husika. Ili kukabiliana na tatizo hilo, Serikali inakusudia kuanzisha Idara ya Nyumba katika ngazi za Halmashauri. Katika mwaka 2010/2011, Serikali itahimiza uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika wa Ujenzi wa Nyumba Nchini na kuvutia Makampuni Binafsi kuwekeza kwenye ujenzi wa Makazi Bora na Viwanda vya kutengeneza vifaa vya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma ya kuifanya Tanzania kuwa kiungo Kikuu cha Mawasiliano Kikanda na Kimataifa, Serikali inaendelea na Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Mkongo huo hivi sasa umeunganishwa na Mikongo ya Kimataifa ya Baharini ya *SEACOM* na *EASSy*. Nchi za Rwanda na Uganda pia zimeunganishwa na Mkongo huo. Aidha, Mkongo huo umeunganishwa kwenye Mikoa 13 ambayo ni Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Iringa, Dodoma, Singida, Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Tanga, Shinyanga, Mwanza na Kagera. Kuunganishwa huko kumeweza Mawasiliano ya Simu na Intaneti kuwa mazuri zaidi na gharama za Mawasiliano zimepungua.

Aidha, katika mwaka 2009, Serikali ilianzisha Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kwa lengo la kufikisha Mawasiliano katika maeneo yasiyo na mvuto wa kibashara hasa Vijijini. Huduma za Mawasiliano zitakazoshughulikiwa na Mfuko huo ni pamoja na Simu za Viganjani, Intaneti na Radio za Jamii. Katika mwaka 2010/2011, Serikali itaanza ujenzi wa Awamu ya Pili ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha ujenzi wa eneo la Viwanda vya kuzalisha bidhaa kwa ajili ya kuuza nje na kuweka miundombinu yote muhimu katika eneo la *Benjamin William Mkapa Special Economic Zone* lililopo Mabibo Jijini Dar es Salaam. Eneo hili lilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 17 Mei, 2010. Tayari Wawekezaji 24

wamewasilisha maombi ya kuwekeza katika eneo hilo ambapo Wawekezaji watano wamepewa Leseni za Uwekezaji na kuanza kufunga mitambo ya uzalishaji. Aidha, Serikali kupitia *SIDO* ilitoa mafunzo kwa Wajasiriamali katika Mikoa ya Tanga, Kigoma, Lindi na Mtwara ili kuendeleza usindikaji wa mazao mbalimbali ya Kilimo. Changamoto tuliyonayo ni kuzalisha bidhaa bora zinazokidhi Viwango vya Kimataifa. Natoa rai kwa Wenye Viwanda Nchini kuzalisha kwa kuzingatia Ubora na Viwango vya Kimataifa ili kuhimili ushindani wa Masoko ya Nje na ndani na kuiongezea Serikali fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, mauzo ya bidhaa nje ya nchi yaliongezekwa kwa asilimia 84.4 kutoka Dola za Kimarekani Milioni 1,679 mwaka 2005 hadi Dola za Kimarekani milioni 3,096 mwaka 2009. Hayo ni mafanikio yanayotokana na fursa za Masoko za Kikanda kama Afrika Mashariki na *SADC* na za Masoko ya Upendeleo Maalum (*Preferential Market Access*). Nawahimiza Wafanyabiashara kutumia fursa hizo vizuri ili kuongeza mauzo ya bidhaa zetu nje. Katika mwaka 2010/2011, Elimu ya Ujasiriamali itatolewa kikamilifu ili kuongeza ushiriki wa Wajasiriamali Wadogo katika kukuza Uchumi.

Aidha, Serikali itaimarisha uhusiano wa Kikanda na Kimataifa katika biashara ili kuongeza wigo wa Masoko ya bidhaa zinazozalishwa hapa Nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali imepiga hatua katika kufanikisha lengo la kuwa na mtandao mzuri wa babarara za lami na zinazopitika wakati wote wa mwaka ili kurahisisha usafiri na usafirishaji.

Serikali ya Awamu ya Nne imekamilisha Miradi ya ujenzi wa Barabara zilizoanzishwa na Serikali ya Awamu ya Tatu. Miradi hiyo ni Tinde – Mwanza/Shinyanga Border (km 96), Nzega – Tinde – Isaka (km 73), Singida – Shelui (km 109), Mbwenkuru – Nangurukuru – Mingoyo (km 190), Mkuranga – Kibiti (km 60), Tarekeea – Rongai – Kamwanga (km 32), Kyamyorwa – Buzirayombo – Geita (km 220) na Dodoma – Manyoni – Singida (km 245) isipokuwa kipande cha kilomita 20 kutoka Mkiwa hadi Manyoni ambacho kinaendelea kukamilishwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na kazi ya kukamilisha ujenzi wa barabara hizo, Serikali ya Awamu ya Nne ilianzisha Miradi mipy 27 ya ujenzi wa Barabara za Lami zenye urefu wa Kilomita 1,745. Kati ya Barabara hizo, jumla ya Kilomita 212 zimekamilika na nyingine zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

Katika mwaka 2010/2011, Serikali itaendeleza ujenzi wa Barabara zote zinazoendelea na ujenzi pamoja na kukamilisha mchakato wa kutafuta Wakandarasi wa Miradi mipy.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazopelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa zote Nchini kwa ajili ya matengenezo ya barabara za vijiji na mijini zimeongezeka kwa asilimia 264 kutoka Shilingi bilioni 23.4 mwaka 2005/2006 hadi Shilingi bilioni 85.5 mwaka 2009/2010.

Ongezeko hilo limewezesha Barabara zenyе hali nzuri kuongezeka kutoka Kilomita 12,623 mwaka 2005 hadi Kilomita 29,298 mwaka 2009. Hili ni ongezeko la Kilomita 16,675, sawa na asilimia 132.

Kutokana na ongezeko hilo la fedha katika Mfuko wa Barabara, kiasi kinachopelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa pia kimeongezeka na hivyo Mtandao wa Barabara nyingi umeimarishwa. Barabara nyingi Vijijini zimeweza kufanyiwa matengenezo ya muda maalum na yale ya kawaida kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hiso, changamoto kubwa inayoikabili Sekta ya Barabara Nchini ni kuongezeka kwa kasi kwa gharama za ujenzi ikilinganishwa na uwezo mdogo wa kifedha wa Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kutokana na hali hiyo, ni vyema Mamlaka zote zinazohusika zihakikishe kwamba, fedha kidogo zinazopatikana kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu zinatumika kwa uangalifu mkubwa ili kupata thamani halisi ya fedha za kodi za Wananchi.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2005 hadi sasa, Serikali imekamilisha ujenzi wa madaraja makubwa na ya kati zaidi ya 284 katika Barabara Kuu na za Mikoa. Nafurahi kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, moja ya madaraja muhimu yaliyokamilika ni ujenzi wa Daraja la Umoja lenye urefu wa mita 720 ambalo linaunganisha Tanzania na Msumbiji. Daraja hilo ambalo limefunguliwa kwa pamoja na Wakuu wa Nchi za Tanzania na Msumbiji tarehe 12 Mei 2010, litakuwa kichocheo muhimu cha kukuza biashara, kuvutia uwekezaji na kuimarisha uhusiano baina ya Nchi yetu na Msumbiji. Ni imani yangu kuwa, Watanzania na hasa Wananchi wa Mikoa ya Kusini watachangamkia fursa nyingi za kiuchumi na kijamii zinazotokana na kukamilika kwa kiunganishi hicho muhimu. Serikali itakamilisha miundombinu mingine muhimu katika eneo hilo la daraja ili kuwawezesha wananchi wa nchi hizi mbili kufanya biashara na kutembeleana bila vikwazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali ilikamilisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Reli ya Isaka – Kigali – Musongati na Isaka - Dar es Salaam. Kazi nyingine zilizokamilika katika Reli ya Kati ni utandikaji wa reli na mataruma mapya kati ya Malongwe na Itigi (Kilomita 47) na kukamilisha ununuvi wa mashine tano za kunyanyulia vitu vizito.

Aidha, kufuatia utendaji mbovu wa Kampuni ya Reli Tanzania (TRL), Serikali imeamua kununua hisa zote (asilimia 51) za Kampuni ya RITES ya India na kuchukua jukumu la kuendesha TRL kwa muda wakati akitafutwa mwendeshaji mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kazi ya ukarabati wa Miundombinu ya Reli ya Kati iliyoaribiwa na mafuriko katika Mikoa ya Morogoro na Dodoma imekamilika. Mwishoni mwa mwezi Mei 2010, treni ya mizigo ilianza kufanya majaribio ya kusafirisha mizigo kuanzia Dar es Salaam kwenda Mwanza na Kigoma.

Napenda kuwashukuru kwa dhati Askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Wahandisi wa Wizara ya Miundombinu na Kampuni ya TRL, kwa kazi nzuri waliyofanya ya kurejesha miundombinu hiyo katika hali ya kawaida kwa muda mfupi.

Katika mwaka 2010/2011, Serikali itaendelea kuisimamia Kampuni ya TRL ili kuhakikisha kuwa, inaboresha huduma zake na kukarabati kilomita 150 za reli Kati ya Dodoma na Tabora.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeimarisha na kuboresha huduma za Viwanja vya Ndege Nchini. Kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere kimefanyiwa ukarabati kwa kujenga barabara za kuruka na kutua ndege na viungio vyake. Aidha, kazi ya kuweka mitambo ya kisasa ya ukaguzi wa abiria na mizigo katika Viwanja vya Ndege vya Julius Nyerere, Mwanza na Arusha imekamilika.

Kazi za Usanifu wa Awali wa Viwanja vya Ndege vya Tabora, Bukoba, Shinyanga, Arusha, Sumbawanga na Kigoma kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami zimekamilika. Katika mwaka 2010/2011, ujenzi wa Viwanja vya Ndege vya Bukoba, Kigoma na Tabora kwa kiwango cha lami utaanza kwa mkopo wa Benki ya Dunia. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Wakimbizi (*UNHCR*), itajenga Uwanja wa Ndege wa Mpanda kwa kiwango cha Lami ili kukuza Utalii katika Hifadhi ya Taifa ya Katavi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeimarisha huduma zinazotolewa na Mamlaka ya Bandari kwa kuanzisha Vituo 8 vya kuhifadhi makasha nje ya Bandari ya Dar es Salaam pamoja na kuboresha mfumo na taratibu za uondoshaji wa mizigo Bandarini. Aidha, Mamlaka ya Bandari imeandaa Mpango Kabambe wa Kuendeleza Bandari na tayari kazi ya upanuzi wa maeneo ya kuhudumia mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam, Mtwara na Tanga imeanza.

Katika mwaka 2010/2011, Mamlaka ya Bandari itaanza kazi ya ujenzi wa Vituo vipya vya kuhudumia Makasha katika Gati Namba 13 na 14 katika Bandari ya Dar es Salaam. Pia, Serikali itajenga Magati katika Bandari za Mafia, Kasanga na Pangani pamoja na kujenga Magati Matano ya Karema, Kalya, Kirando, Lagosa na Kibirizi katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2010, Serikali iliweka mikakati imara ya kuhakikisha kwamba, Maliasili tulizonazo za Misitu na Wanyamaporini zinahifadhiwa na kuwanufaisha Wananchi.

Halmashauri zenye maeneo ya hifadhi ziliendelea kupata mgao wa asilimia 25 ya mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii na kugharamia mipango mbalimbali ya maendeleo inayoibuliwa na Jamii.

Aidha, katika kipindi hicho, *TANAPA* imetoa Shilingi bilioni 5.8 kugharamia Mipango ya Maendeleo ya Wananchi katika maeneo mbalimbali. Vilevile, Serikali imejenga uwezo wa wafugaji nyuki kwa kutoa mafunzo na mbinu za Ufugaji Bora wa Nyuki na kuwawezesha kupata vifaa vya kisasa vya Ufugaji Nyuki. Uimarishaji wa Sekta Ndogo ya Nyuki umezingatia ukweli kwamba, urinaji wa asali ni moja ya shughuli muhimu za kuongeza kipato na kupunguza umaskini mionganoni mwa Wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, ili kulinda ubora wa asali inayozalishwa Nchini, Viongozi wa Mikoa yote ambayo ina Wananchi wengi wanaojishughulisha na Ufugaji wa Nyuki wachukue hatua ya kutenga maeneo maalum kwa ajili ya Ufugaji wa Nyuki.

Aidha, Kilimo cha Tumbaku katika maeneo ya Wafugaji Nyuki kisiruhusiwe ili kulinda ubora wa asali yetu katika Masoko ya Kimataifa. Katika mwaka 2010/2011, Serikali itaimarisha usimamizi na matumizi endelevu ya Misitu na Wanyamapori.

Aidha, juhudu zaidi zitaongezwa kwenye kutoa mafunzo ya Ufugaji Nyuki na utafutaji wa Masoko ya uhakika ya asali na nta inayozalishwa nchini. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu utalii. Serikali kwa kushirikiana na Wadau imetangaza Utalii wa Tanzania kwa njia mbalimbali ikiwemo matumizi ya Vyombo vya Habari vya Kimataifa, Ofisi zetu za Ubalozi, safari na ziara mbalimbali za Viongozi na kupitia Makongamano ya Kimataifa. Watalii kutoka Masoko mapya ya Nchi za Asia zikiwemo China, Japan, Singapore, India na Urusi wameongezeka kutoka watalii 23,542 mwaka 2006 hadi 32,973 mwaka 2008. Kwa ujumla, idadi ya watalii walitembelea Tanzania iliongezeka kutoka 612,754 mwaka 2005 hadi 770,376 mwaka 2008. Hata hivyo, idadi ya Watalii kwa mwaka 2009 ilipungua na kufikia 714,367 kutokana na athari za M dororo wa Uchumi Duniani. Mapato yatokanayo na biashara ya utalii yaliongezeka kutoka Shilingi Bilioni 948.6 mwaka 2005 hadi Bilioni 1,610 mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, tunavyo vivutio vingi vinavyoweza kutuingizia mapato na kuinua uchumi wetu. Hivyo, hatuna budi kuelekeza nguvu zetu zaidi katika kuimarisha Sekta hii muhimu ya Utalii kwa kuitangaza kwa nguvu zaidi na kuimarisha huduma kwa watalii wetu. Natoa wito kwa kila mmoja katika nafasi yake ajione ana wajibu wa kuitangaza nchi yetu kila inapotokea nafasi. Katika mwaka 2010/2011, Serikali itaainisha na kutangaza vivutio vya Utalii ndani na nje ya nchi pamoja na kuhamasisha uwekezaji kwenye maeneo mapya ya Utalii. Aidha, itaimarisha miundombinu katika vituo na maeneo ya rasilimali za kale.

Mheshimiwa Spika, nishati na madini. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 iliveka malengo ya kufikisha umeme katika Miji Mikuu ya Wilaya mbalimbali, kuongeza kasi ya kupeleka umeme Vijijini kuitia Mfuko wa Nishati Vijijini na kuvutia uwekezaji wa Sekta Binafsi katika uzalishaji na usambazaji wa umeme. Katika kipindi hicho, umeme umefikishwa katika Makao Makuu ya Wilaya tisa za Serengeti, Ukerewe, Mbinga, Simanjiro, Uyui, Ludewa, Mkinga, Kilolo na Bahi. Aidha, Sheria ya Umeme ya mwaka 2008 ilitungwa. Sheria hiyo inaruhusu ushiriki wa Sekta Binafsi katika kuzalisha na kusambaza umeme.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza tatizo la upatikanaji wa umeme, Serikali ilikamilisha ujenzi wa mtambo wa kuzalisha umeme unaotumia gesi asilia wenyewe uwezo wa kuzalisha *MW* 45 katika eneo la Tegeta, Dar es Salaam. Aidha, ilinunua na kufunga mashine tano za kufua umeme wa *MW* 6.25 kwa ajili ya Mji wa Kigoma – Ujiji. Serikali pia inakamilisha usambazaji wa umeme wa gesi asilia kutoka Mnazi Bay kwenda katika Mikoa ya Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo niliyoyataja, upatikanaji wa nishati ya uhakika umekuwa ni moja ya changamoto kubwa zinazotukabili. Kukosekana kwa nishati ya uhakika na kwa bei ya ushindani kunaathiri uwekezaji na mazingira ya ufanyaji biashara kwa ujumla. Taarifa ya wepesi wa kufanya biashara Tanzania ya mwaka 2010 inaonyesha kwamba, wazalishaji na wafanyabiashara wengi wadogo na wa kati wanalamika kuhusu upatikanaji wa nishati ya uhakika kama moja ya kikwazo kikubwa katika shughuli zao. Changamoto hiyo ni lazima itafutiwe ufumbuzi wa kudumu ili kuhakikisha kwamba uzalishaji wa bidhaa unaongezeka katika viwanda vyetu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Serikali itajenga mtambo wa kufua umeme wa *MW* 100 Ubungo, Dar es Salaam na *MW* 60 Jijini Mwanza. Vilevile, itayapatia umeme Makao Makuu ya Wilaya nane za Namtumbo, Loliondo, Longido, Nkasi, Bukombe, Kishapu, Kasulu na Kibondo. Serikali pia, itatekeleza miradi ya kupeleka umeme Vijijini na kuimarisha miundombinu ya mifumo ya usafirishaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini. Serikali ilikamilisha na kuptisha Sera Mpya ya Madini ya mwaka 2009 na Sheria ya Madini ambayo ilipitishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Aprili 2010. Sheria hiyo mpya, pamoja na mambo mengine, imeweka bayana namna ambavyo Serikali na wananchi watashiriki katika shughuli za madini. Serikali pia, ilianzisha Wakala wa Ukaguzi wa Madini ambao utawajibika kukagua madini yatakayouzwa nje ya nchi. Uzoefu uliopatikana katika kipindi kifupi tangu kuanzhishwa kwa Wakala huo na kuanza kukagua dhahabu umeonyesha kwamba, tuna uwezo wa kufanya kazi hiyo na Serikali inaokoa fedha nyingi kutokana na utaratibu huo. Natoa wito kwa Watanzania kutumia fursa ya Sheria mpya ya Madini ili washiriki kikamilifu kwenye biashara ya uchimbaji madini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga maeneo kwa ajili ya Wachimbaji Wadogo wa Madini nchini ili wafanye shughuli zao kwa uhakika na usalama. Aidha, Serikali

imetenga Shilingi bilioni moja kama kianzio cha Mfuko wa Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo na kuanzisha Kitengo maalum cha kuwaendeleza Wachimbaji hao. Vilevile, Wachimbaji Wadogo wamepewa mafunzo juu ya Utunzaji wa Mazingira, Afya na Usalama katika maeneo yao ya kazi. Pamoja na hatua hizo, bado kuna tatizo la Wachimbaji Wadogo kutozingatia Taratibu za Kisheria na hivyo kuwepo uvamizi wa maeneo, ajali za Migodini, uharibifu wa mazingira na migogoro kwenye Migodi. Natoa wito kwa wachimbaji wadogo kufanya shughuli zao kwa kufuata Sheria, Taratibu na Kanuni za Usalama Migodini ili kuzuia ajali na migogoro isiyo ya lazima. Katika mwaka 2010/2011, Serikali itaimarisha Wakala wa Ukaguzi wa Madini kwa kuupatia Watumishi mahiri na vitendea kazi vya kisasa. Aidha, itatoa elimu kwa Wachimbaji Wadogo na kufanya kaguzi katika migodi yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji. katika kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini, Serikali imeandaa na kupitisha Mkakati na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Aidha, Sheria Na. 11 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji na Sheria Na. 12 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira za mwaka 2009 zilitungwa. Kwa mujibu wa Sheria hizo, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Bodi za Maji za Mabonde zimepewa jukumu la kusajili Vyombo vya Watumiaji Maji.

Hatua hiyo imesaidia kuharakisha uandikishaji Kisheria wa Vyombo hivyo na kupanua wigo katika kusimamia huduma ya maji na kutunza rasilimali za maji kwa njia endelevu. Aidha, Serikali imejenga na kukarabati miradi ya maji na kuchimba visima virefu na vifupi. Kutokana na hatua hizo, upatikanaji wa Maji Vijijini umeongezeka kutoka asilimia 57.1 mwaka 2007 hadi 61 Desemba 2009 na Maji Mijini kutoka asilimia 78 hadi 84 kwa kipindi hicho. Vilevile, upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam umeongezeka kutoka asilimia 50 mwaka 2005 hadi 68 mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Serikali itaendelea kutekeleza Program ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa lengo la kuboresha usimamizi wa rasilimali za maji na kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji Vijijini na Mijini. Serikali itaandaa na kutekeleza Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji katika Mabonde yote ya Maji. Aidha, itaimarisha Maabara za Maji na kujenga Miradi mipy ya Maji. Natoa wito kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zihamasishe uvunaji wa maji ya mvua kwa kutumia teknolojia nyepesi na rahisi ya kukinga na kutunza maji. Aidha, ziweke Sheria Ndogo kwa ajili ya Taasisi na Kaya kuvuna maji ya mvua kwenye mapaa ya nyumba na zisimamiwe kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na elimu. Serikali imeongeza kasi ya uandikishaji wa wanafunzi na kuimarisha miundombinu ya elimu katika Shule za Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ufundu Stadi. Kutokana na jitihada hizo, katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2009, uandikishaji katika Shule za Msingi umeongezeka kutoka wanafunzi 6,499,581 hadi kufikia 8,441,553, sawa na ongezeko la asilimia 30. Uandikishaji wa wanafunzi wa Kidato cha Kwanza kwa Shule za Sekondari za Serikali uliongezeka kutoka wanafunzi 134,963 hadi 477,554 sawa na ongezeko la asilimia 254. Vilevile, idadi ya wanafunzi wanaoingia Kidato cha tano iliongezeka kutoka wanafunzi

9,710 hadi 33,169 sawa na ongezeko la asilimia 242. Kwa upande wa mafunzo ya Ufundu Stadi, idadi ya wanafunzi wote iliongezeka kutoka 78,586 hadi 114,295.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepiga hatua kubwa katika kupanua elimu ya juu kwa kushirikiana na Sekta Binafsi. Miiongoni mwa mafanikio ya hatua hizo ni kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Dodoma pamoja na Vyuo Vikuu Vishiriki vya Elimu vya Dar es Salaam na Mkwawa. Pia, Sekta Binafsi imepanua na kuanzisha Vyuo mbalimbali. Kutokana na juhudhi hizo, idadi ya Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki vya Umma na Binafsi vimeongezeka kutoka 26 mwaka 2005/2006 hadi 32 mwaka 2009/2010. Aidha, Udhili wa wanafunzi wanaojiunga na Vyuo vya Elimu ya Juu umeongezeka kutoka wanafunzi 40,719 mwaka 2005/06 hadi 117,068 mwaka 2009/2010, sawa na ongezeko la asilimia 188. Ongezeko hili limetokana na Serikali kuongeza Mikopo ya Elimu ya Juu kutoka wanafunzi 42,726 mwaka 2005/2006 hadi 69,442 mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuyapongeza Madhehebu mbalimbali ya Dini na Sekta Binafsi kwa kuitikia wito wa Serikali wa kuongeza fursa za wanafunzi wengi kupata Elimu ya Juu nchini. Kipekee nampongeza Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa ahadi ya Serikali ya Awamu ya Nne ya kuanzisha Chuo Kikuu cha Dodoma. Chuo hiki ambacho ni cha kihistoria na kikubwa hapa nchini kitakapokamiliaka kinatarajiwaa kuchukua wanafunzi 40,000. Hadi sasa Chuo hiki kimedahili wanafunzi 15,121. Kuanzishwa kwa Chuo hiki ni kielelezo kuwa Watanzania tukidhamiria tunaweza kujiletea maendeleo wenyewe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, Sekta ya Elimu bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo uhaba wa Walimu, Maabara, Nyumba za Walimu, Hosteli, upungufu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia pamoja na ufaulu mdogo wa masomo ya Hisabati, Sayansi na Kiingereza. Changamoto nydingine ni mazingira magumu ya kazi katika baadhi ya maeneo ya Vijijini na uchakavu wa miundombinu katika Shule za Sekondari za Bweni, Vyuo vya Ualimu na Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hizo katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Serikali itaongeza ajira ya Walimu wapya katika Shule za Msingi wapatao 14,800 na Sekondari Walimu 11,140. Vilevile, itaongeza vifaa vya kufundishia na kujifunzia na ujenzi wa Maabara za Masomo ya Sayansi na Lughaa. Aidha, Serikali itatoa mafunzo kazini kwa Walimu wa Masomo ya Sayansi, Hisabati na Kiingereza, kuimarisha Vituo vya Walimu na kuimarisha miundombinu ya elimu katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza Sera ya Afya ya mwaka 2007 inayolenga kuimarisha huduma za kinga na tiba. Serikali ilielekeza jitihada zake katika kuzuia na kudhibiti magonjwa mbalimbali ikiwemo Malaria ambayo inasababisha vifo vya Watanzania wengi. Hadi sasa, Serikali imesambaza vyandarua milioni 3.8 vyenye

viuatilifu kwa wanawake wajawazito na vyandarua milioni 1.3 kwa watoto wachanga. Aidha, vyandarua milioni 5.6 viligawanywa kwa kila Kaya yenye watoto wa umri chini ya miaka mitano bila malipo. Vilevile, Serikali ilinunua na kusambaza Dawa Mseto ya Malaria kwa Vituo vyote vya Tiba vya Umma vipatavyo 5,000.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeimarisha mfumo wa utoaji wa huduma za afya kwa kuendelea kuongeza Vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Katika kipindi cha miaka mitano, Hospitali za Mikoa zimeongezeka kutoka 17 hadi 21, Vituo vya Afya vimeongezeka kutoka 382 hadi 468 na Zahanati zimeongezeka kutoka 3,292 hadi 4,559 ikiwa ni pamoja na kuimarike kwa huduma za chanjo. Ongezeko hilo limesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza vifo vya watoto wadogo. Aidha, ujenzi wa Hospitali ya Magonjwa ya Moyo Muhimbili umeanza, na inategemewa kukamilika mwezi Mei 2011. Hospitali hiyo itakapokamilika itapunguza idadi ya wagonjwa wa moyo wanaopelekwa nje ya nchi kwa matibabu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudhi hizo, Sekta ya Afya inakabiliwa na upungufu wa Watumishi wa Afya. Upungufu huo umeathiri zaidi maeneo ya Vijijini ikilinganishwa na Mijini. Katika kukabiliana na upungufu huo, Serikali imeandaa mikakati ya kuendelea kuongeza wataalam ambayo ni pamoja na kuanzishwa kwa mafunzo ya masafa na kuongeza fedha za kugharamia mafunzo ya utarajali na uzamili. Hatua hii itaongeza Wahitimu wa Vyuo Vikuu na Vyuo vya Uuguzi na Sayansi Shirikishi za Afya hapa nchini kutoka 4,900 mwaka 2010 na kufikia 22,540 mwaka 2015. Katika mwaka 2010/2011, Serikali itajenga Vituo zaidi vya kutolea Huduma za Afya na kutoa Dawa na vifaa vya Tiba.

Mheshimiwa Spika, Watu Wenye Ulemavu na Wazee. Serikali imeridhia Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki kwa Watu Wenye Ulemavu na kutunga Sheria Jumuishi ya Watu wenye Ulemavu na Wasiojiweza nchini. Hatua hizo zimeweka mfumo mzuri wa kusimamia na kutoa huduma kwa Watu Wenye Ulemavu. Serikali pia, imefanya utafiti kuhusu idadi ya watu wenye ulemavu kwa lengo la kupata takwimu sahihi na kubaini mahitaji yao ili waweze kuhudumiwa kwa urahisi zaidi. Vilevile, imegharlamia mahitaji muhimu katika baadhi ya shule za wanafunzi wenye Ulemavu wa Ngozi. Aidha, Serikali imeanzisha utaratibu wa kila Hospitali na Vituo vya Afya kuwa na Kliniki pamoja na watoa huduma Maalum kwa ajili ya kuhudumia Wazee. Vilevile, kuanzia mwaka 2010/2011, Serikali imeamua kusamehe Kodi ya Majengo kwenye nyumba wanazoishi Wazee wenye umri wa zaidi ya miaka 60 ambaa uwezo wao kiuchumi ni mdogo kuweza kulipa kodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya wanawake na watoto. Serikali imetekeleza kwa dhati dhamira ya kuongeza uwakilishi wa wanawake katika ngazi mbalimbali za maamuzi kuelekea uwiano wa asilimia 50 kwa 50. Idadi ya wanawake katika ngazi mbalimbali za maamuzi imeongezeka kutoka wastani wa asilimia 26 mwaka 2005 hadi asilimia 31 mwaka 2009. Aidha, Serikali ilianzisha Benki ya Wanawake Tanzania ambayo inalenga kuwapatia wanawake mikopo yenye masharti nafuu. Hadi sasa, zaidi ya akaunti 9,902 zimefunguliwa na kiasi cha shilingi milioni 135 zimekopesha kwa

wajasiriamali wa jinsia zote. Serikali pia, ilitoa mikopo yenyeye thamani ya Shilingi milioni 928 kwa Vikundi vya Wanawake katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika mwaka 2010/2011, Serikali itahamasisha jamii na taasisi mbalimbali kununua hisa za Benki ya Wanawake na kusimamia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa Sera mpya ya Maendeleo ya Mtoto Tanzania ya mwaka 2008 inayotoa Mwongozo wa Haki za Mtoto. Aidha, Serikali imeratibu na kuwezesha kuundwa kwa Mabaraza ya Watoto ambayo hadi sasa yameanzishwa katika Mikoa 15 ya Tanzania Bara na katika Wilaya 87. Uanzishwaji wa Mabaraza hayo ni njia mojawapo ya ushirikishwaji wa watoto katika kutoa mawazo yao kuhusu haki zao na wajibu wao katika ujenzi wa Taifa. Vilevile, Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 ambayo inajumuisha Sheria nyingi za watoto zilizokuwepo awali ilitungwa. Sheria hiyo imetilia mkazo kuhusu Maendeleo, Ulinzi na Haki za Watoto.

Mheshimiwa Spika, kuhusu habari na utamaduni. Sekta ya Habari ina umuhimu mkubwa katika kuiunganisha jamii na kuleta maendeleo nchini. Kwa sababu hiyo, Serikali imeimarisha na kuendeleza uhuru wa kupata, kutoa na kusambaza habari nchini ili ziweze kuwafikia wananchi wote. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imepanua uhuru na wigo wa kupashana habari kwa kiwango kikubwa. Kutokana na jitihada hizo, kumekuwepo na ongezeko la Magazeti na Majarida, Vituo vya Redio, Televisheni na Mitando. Napenda kuchukua nafasi hii kuwakumbusha Wamiliki na Wahariri wa Vyombo vyote vya Habari kuandika na kutangaza habari zilizo sahihi na zinazoelimisha wananchi kuhusu masuala muhimu ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha Lughya ya Kiswahili kama kielelezo cha Utamaduni wetu. Moja ya kielelezo hicho ni kuanzishwa kwa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kiswahili sasa ni mojawapo ya Lughya rasmi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Afrika. Kwa mantiki hii, nachukua nafasi hii kusisitiza umuhimu wa matumizi ya Lughya ya Kiswahili katika shughuli rasmi za Serikali. Vilevile, nahimiza Taasisi za Elimu Nchini ziweke mkazo katika kufundisha Kiswahili Sanifu ili Watanzania waweze kunufaika na fursa nyingi za ajira ya Kiswahili za ndani na nje. Katika mwaka 2010/2011, Serikali itaendeleza mazungumzo ya kukiwezesha Kiswahili kuwa mojawapo ya Lughya rasmi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*).

Mheshimiwa Spika, ulinzi na usalama. Serikali imeimarisha Jeshi la Ulinzi kwa kulipatia vifaa na mafunzo. Hatua hiyo imelenga kuimarisha utendaji na kuwapatia mbinu za kisasa za kivita. Jeshi letu limeweza kushiriki katika Operesheni za Kulinda Amani huko Darfur - Sudan na Lebanon. Vilevile, Serikali imeboresha Makambi na Makazi ya Askari wa Jeshi la wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kujenga jumla ya nyumba mpya za makazi 336. Aidha, ukarabati wa mabwalo, mabweni, ofisi, madarasa, Hospitali na Miundombinu ya Maji Safi na Taka, umeme na mawasiliano umefanyika katika Makambi mbalimbali ya Jeshi nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza ahadi ya Serikali ya kurejesha Jeshi la Kujenga Taifa, ukarabati wa miundombinu umefanyika katika makambi 12 yenyewe uwezo wa kuchukua vijana 7,110 kwa wakati mmoja. Makambi mawili ya Kanembwa na Masange yenyewe uwezo wa kuchukua vijana 2,000 yanaendelea kukarabatiwa. Katika mwaka 2010/2011, Serikali itayaongeza uwezo wa utendaji kivita Majeshi ya Ulinzi kwa kuyanunulia vifaa na Zana za Kisasa, kukarabati miundombinu na mitambo ya Vituo vya Utafiti, Viwanda na Karakana za Kijeshi. Mwelekeo huo utahusu pia uendelezaji wa ukarabati wa Makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa ajili ya kuyaandaa kuchukua Vijana wengi kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia, itaimarisha Jeshi la Magereza kwa kulipatia vitendea kazi. Katika kutekeleza Azma ya Kilimo Kwanza, Jeshi hilo limetenga sehemu ya maeneo yake ili kuzalisha mbegu bora ambazo zitasambazwa kwa wakulima katika maeneo mbalimbali nchini. Kazi hiyo, imeanza katika Mikoa mitano ya Arusha, Dodoma, Lindi, Manyara na Morogoro. Mbegu zinazozalishwa ni za mazao ya mpunga, mahindi, alizeti, mtama, karanga, ufuta na mbaazi.

Mheshimiwa Spika, katika miaka mitano iliyopita, Jeshi la Polisi, limetoa mafunzo ya Utawala Bora na Haki za Binadamu kwa askari 12,536 na wengine 1,169 katika taaluma ya upelelezi. Nyumba za kisasa za kuishi 293 zimejengwa na vitendea kazi mbalimbali vimenunuliwa yakiwemo magari 516. Katika jitihada za kuendeleza dhana ya Polisi Jamii, wananchi wamehimizwa kuanzisha Vikundi vya Ulinzi Shirikishi ambapo vikundi 2,174 vimeanzishwa. Kuanzishwa kwa vikundi hivyo kumelisaidia Jeshi la Polisi kudhibiti vitendo vya uhalifu pamoja na kuimarisha usalama wa raia na mali zao. Aidha, jumla ya silaha haramu 3,010 zimekamatwa. Katika mwaka 2010/2011, Serikali itaimarisha Jeshi la Polisi kwa kulipatia Vitendea Kazi muhimu, mafunzo na kuboresha mazingira ya kazi.

Mheshimiwa Spika, maboresho katika mamlaka za Serikali za Mitaa, Program ya kuboresha mfumo wa Serikali za Mitaa. Serikali imekuwa ikitekeleza Program za maboresho kwa lengo la kuboresha utendaji katika Sekta ya Umma. Pamoja na Programu hizo ni ile ya kuboresha mfumo wa Serikali za Mitaa. Kupitia Programu hiyo, Serikali imefanikiwa kujenga uwezo wa Serikali za Mitaa na kuwawezesha wananchi kushiriki katika upangaji wa Mipango kwa kutumia mbinu Shirikishi Jamii na kuhakikisha kuwa thamani ya fedha inapatikana kutokana na utekelezaji wa Mipango hiyo. Aidha, imeongeza kiasi na uwazi katika ugawaji wa rasilimali Fedha kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kufuata vigezo maalum.

Hatua hiyo imekuwa ni kichocheo cha kuleta maendeleo ya haraka kwenye Mamlaka hizo. Hata hivyo, katika baadhi ya Halmashauri kumekuwepo na usimamizi hafifu wa rasilimali za umma. Natoa wito kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuongeza nidhamu na kuimarisha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya Fedha za Umma. Aidha,

Viongozi na Watendaji wawashirikishe wananchi kikamilifu katika kuibua na kutekeleza Miradi ya Maendeleo na kufanya maamuzi mbalimbali katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, tarehe 7 Juni, 2010 nilizindua Mradi wa Mabasi ya Kusafirisha Wanafunzi Jijini Dar es Salaam. Mradi huo unalenga kupunguza kero ya muda mrefu ya usafiri wa wanafunzi wapatao 500,000 ambaao wanahitaji usafiri wa kila siku wa kwenda na kurudi shulenii. Benki ya *CRDB* imetoa mabasi matano yenye uwezo wa kubeba wanafunzi 100 kila moja. Mabasi hayo yamekabidhiwa kwa Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) kwa Mkataba maalum wa uendeshaji. Changamoto kubwa iliyoko mbele yetu ni kuhakikisha Mradi huo unakuwa endelevu kwa kushirikisha Wadau wengine wa Sekta Binafsi na Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba tunahitaji mabasi mengi ili kuondoa tatizo hilo. Hivyo, Makampuni na Mashirika ya Umma na ya Binafsi yajitekeze kwa wingi kuiga mfano huo mzuri ili tuweze kupunguza tatizo hilo katika Jiji la Dar es Salaam na Miji mingine nchini. Serikali kwa upande wake itaangalia suala la ushuru unaotozwa kwa mabasi hayo ili kuwatia moyo wale wote wanaopenda kuchangia mabasi kwa ajili ya wanafunzi na nitumie fursa hii tena kuipongeza Benki ya *CRDB* kwa ubunifu huo mzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ushirikiano wa Kimataifa, Tanzania imeendelea kudumisha uhusiano mzuri na Mataifa na Mashirika mbalimbali duniani kuititia Balozi zetu. Aidha, ziara za Viongozi wa Kitaifa zimetumika kuitangaza Tanzania, kuvutia Wawekezaji na kuwapa fursa wafanyabiashara wa Tanzania kutafuta Masoko ya Nje. Mahusiano mazuri yaliyojengeka yameiwezesha nchi yetu kupata heshima kubwa na kufungua milango ya biashara na uwekezaji na nchi mbalimbali. Aidha, kazi kubwa aliyoifanya Rais wetu ya ziara za kikazi zimesaidia kupatikana kwa misaada na mikopo nafuu na kutambulika Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kutoptaka na hali hiyo, Tanzania ilipewa heshima ya kuwa Mwenyeji wa Mkutano wa Jukwaa la Uchumi la Dunia kwa Afrika uliofanyika Dar-es-Salaam tarehe 5 hadi 7 Mei, 2010. Moja ya matokeo mazuri ya Mkutano huo ni pamoja na Makampuni nane ya Kimataifa kuonyesha dhamira ya kuwekeza katika Ukanda Mpya wa Kilimo ambaao ni eneo lililounganishwa na Reli ya *TAZARA* na Mikoa ya Pwani, Morogoro, Mbeya na Rukwa. Napenda kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutuongoza vyema katika kufanikisha Mkutano huo ambaao ni mara ya kwanza kufanyika katika Nchi za Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umeimariika. Mnamo tarehe 20 Novemba 2009, Wakuu wa Nchi za Jumuiya walitia saini Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki ambayo utekelezaji wake unategemewa kuanza

ifikapo mwezi Julai 2010. Soko la Pamoja litatoa uhuru wa kufanya biashara, fursa za kupata ajira bila usumbufu usio wa lazima na uhuru wa raia wa kuwekeza mitaji katika nchi yoyote ndani ya Jumuiya. Natoa rai kwa wananchi wote na hasa wafanyabiashara hapa Tanzania kutambua fursa za kiuchumi, biashara na kijamii zinazotokana na kuimarka kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuzitumia kikamilifu kwa manufaa ya mtu mmoja mmoja na Taifa letu kwa ujumla. Watanzania sasa hatuna budi kuhakikisha tunauza bidhaa nyingi zaidi katika Jumuiya badala ya kuwa soko tu la bidhaa kutoka kwa jirani zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, masuala mtambuka, mapambano dhidi ya rushwa, suala la kupambana na rushwa limepewa kipaumbele katika kipindi cha miaka mitano iliyopita kwa kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa. Aidha, tafiti mbalimbali kuhusu rushwa na utawala bora zilifanyika na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 16 ya mwaka 2007 ilipitishwa. Nawakumbusha Viongozi na wananchi wote kwamba, rushwa ni adui wa haki, hivyo, tuikatae kwa nguvu zetu zote. Tunapoelekea kwenye Uchaguzi Mkuu, wananchi wajiepushe na vitendo vya kupokea na kutoa rushwa. Vyombo vyote vinavyohusika vinapaswa kuongeza Mapambano dhidi ya rushwa ili kunusuru Taifa letu lisiteketee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mazingira, Serikali inatekeleza Sera ya Taifa ya Mazingira na kusimamia Sheria ya Mazingira kwa kuhakikisha kuwa masuala ya Mazingira yanazingatiwa katika Sekta zote. Vilevile, Mkakati wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na Vyanzo vya Maji umeandaliwa pamoja na Kanuni za kufanya tathmini ya athari kwa mazingira katika miradi yote ya maendeleo. Pia, Serikali imeandaa Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali imeimarisha utoaji wa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira. Ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, Serikali imeanza kuandaa Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa ya Ukaa kutokana na ukataji miti ovyo na uharibifu wa misitu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Serikali itatekeleza Mpango wa Taifa wa kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi. Aidha, elimu ya mazingira itaendelea kutolewa kwa wananchi wote. Vilevile, Serikali itaandaa na kutekeleza Program Maalum ya Kujenga Uwezo wa Halmashauri Kusimamia na Kudhibiti Taka Ngumu ambazo zinaziba mifumo ya majitaka hasa katika maeneo ya Mijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ilikumbwa na maafa mengi ambayo yameleta athari kwa maisha ya wananchi wetu. Maafa hayo ni pamoja na ukame uliosababisha upungufu mkubwa wa chakula, tetemeko la ardhi, mafuriko, ajali na milipuko ya mabomu katika Kituo cha Kijeshi Mbagala pamoja na maporomoko ya ardhi Wilayani Same na kwenye baadhi ya Migodi. Katika kukabiliana na maafa hayo, Serikali ilitoa misaada mbalimbali ya chakula, mbegu, vifaa na fedha. Misaada iliyotolewa katika kipindi cha mwaka 2006 hadi 2010 ni pamoja na tani 252,000 za mahindi yenye thamani ya Shilingi bilioni 96.2 kwa Mikoa iliyokumbwa na upungufu wa Chakula.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia, ilitoa Shilingi bilioni 3.7 kwa Mikoa ilioathirika na ukame kwa ajili ya kununulia mbegu. Aidha, Serikali ilitoa jumla ya Shilingi bilioni 8.5 kwa ajili ya kulipa fidia kwa waathirika wa maafa yaliyosababishwa na mlipuko wa mabomu katika Kambi ya Jeshi Mbagala, Jijini Dar es Salaam. Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali imezipatia kaya 2,397 zenye waathirika 8,177 wa mafuriko Wilayani Kilosa, vifaa na huduma muhimu. Serikali imeanza zoezi la kupima Viwanja katika maeneo mapya kwa ajili ya kuvigawa kwa wananchi walioathirika.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba tatizo la ukame, pamoja na kusababisha upungufu mkubwa wa chakula, limeathiri sana baadhi ya wafugaji ambao wanategemea mifugo kwa kipato pamoja na usalama wa chakula. Serikali inalifanya kazi tatizo hilo kwa lengo la kuona namna ambavyo itaweza kusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kujenga uwezo wa Taifa wa kukabiliana na maafa, Serikali imetoa mafunzo kwa Kamati za Maafa za Mikoa 16 na Wilaya zote. Aidha, mafunzo maalum ya kuijandaa kukabiliana na Janga la *Tsunami* yalifanyika kwa Mikoa yote inayopakana na Bahari ya Hindi. Serikali imeanzisha maghala ya kutunza vifaa vya kuijandaa kukabiliana na maafa katika Kanda Nne za Dar es Salaam, Shinyanga, Dodoma na Mbeya. Nichukue fursa hii kuwashukuru Wadau waliota misaada mbalimbali kusaidia wananchi waliopatwa na maafa nchini. Natoa rai kwa Kamati za Maafa za Mikoa, Wilaya zote na Vijijini hapa nchini kusimamia kikamilifu misaada yote inayotolewa na kuhakikisha inawafikia waathirika.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2010/2011, Serikali itafanya mapitio ya Sera ya Maafa na kuandaa Sheria mpya ya Maafa ambayo itaweka Muundo mpya wa kushughulikia maafa nchini. Aidha, Serikali itatoa elimu ili kuhamasisha umma kuchukua hatua za kuzuia, kuijandaa na kukabiliana na maafa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI kwa kutoa elimu na kuhamasisha upimaji wa hiari wa Virusi Vya UKIMWI (VVU). Utafiti uliofanyika nchini wa kubainisha viwango vya maambukizi ya UKIMWI ulionyesha kupungua kwa maambukizi kutoka Asilimia saba mwaka 2003/2004 hadi Asilimia 5.7 mwaka 2007/2008. Hata hivyo, kuna tofauti kubwa ya viwango vya maambukizi kati ya Mkoa na Mkoa. Mikoa yenye kiwango kikubwa zaidi ya wastani wa Kitaifa ni Iringa (asilimia 15.7), Dar es Salaam (asilimia 9.3) na Mbeya (asilimia 9.2). Mikoa yenye kiwango kidogo ni Manyara (asilimia 1.5), Arusha (asilimia 1.6) na Kigoma (asilimia 1.8).

Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI, Serikali kwa kushirikiana na Wadau imesogeza huduma ya Ushauri Nasaha na Upimaji wa Virusi vya UKIMWI karibu na wananchi katika Hospitali zote na baadhi ya Vituo vya Afya na Zahanati hapa nchini. Hadi kufikia mwezi Desemba 2009, Vituo vya kutolea Dawa za kupunguza makali ya UKIMWI vimefika 900. Jumla ya Watu 559,472 wamesajiliwa na kati ya hao takriban Watu 302,000 wameanza kutumia Dawa hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Serikali itaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI, kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya UKIMWI na kukamilisha mapitio ya Sera ya UKIMWI. Aidha, itaendelea kutoa Dawa za kupunguza makali ya UKIMWI, kutoa ushauri nasaha, upimaji wa VVU na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji takwimu.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa dawa za kulevyta, katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2010, Serikali iliendelea kudhibiti upatikanaji na matumizi ya Dawa za Kulevya nchini. Operesheni za kuteketeza mashamba ya bangi ziliendeshwa katika Mikoa ya Mara, Morogoro, Tanga, Iringa na Arusha ambapo jumla ya ekari 1,864 ziliteketewa. Aidha, ukamataji wa Dawa za Kulevya uliimarishta na kufanikiwa kukamatwa kwa tani 540 za bangi, tani 36.5 za mirungi, kilo 126.5 za *Heroin* na kilo 18.6 za *Cocaine* na jumla ya watuhumiwa 30,761 walikamatwa wakihusishwa na biashara ya dawa hizo. Pia, elimu ilitolewa kwa umma juu ya athari za dawa za kulevya kijamii na kiuchumi kupitia vyombo vya Habari, machapisho na matukio mbalimbali ya Kitaifa. Aidha, Miongozo ya Tiba kwa watumiaji wa Dawa za Kulevya iliandaliwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Serikali itaimarisha Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya na kuelimisha umma juu ya madhara ya biashara haramu na matumizi ya dawa za kulevya hasa kwa vijana. Aidha, uboreshaji wa huduma za tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya utapewa kipaumbele. Serikali pia, itaendeleza operesheni za kukamata dawa za kulevya pamoja na kuteketeza mashamba ya bangi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeimarisha Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kununua mitambo mipyaa nane (8) itakayowezesha kuchapa nyaraka kwa viwango vya ubora na usalama unaokubalika. Aidha, Idara imepata kiwanja chenye ukubwa wa hekta nne (4) kwa ajili ya kujenga Kituo kipyaa kikubwa cha Uchapishaji hapa Dodoma ambacho kitakuwa Makao Makuu ya Idara ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali. Katika mwaka 2010/2011, Idara ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali itachapa nyaraka mbalimbali za Serikali ziliwemo za Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2010. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu, katika kipindi cha mwaka 2005 hadi Aprili 2010, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu iliandaa Michoro ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi yenye jumla ya viwanja 17,505 vya Msongo Mdogo katika maeneo mbalimbali ya Mji wa Dodoma. Mamlaka pia imepima Viwanja vipyaa 21,893 katika maeneo mbalimbali, kukamilisha upimaji wa viwanja 3,584 vya zamani na kuandaa Hati 5,187 za kumiliki viwanja. Aidha, imepiga Picha za Anga eneo lote la Uendelezaji la Mji Mkuu na kutayarisha Mipango kwa maeneo yenye kuhitaji matumizi makubwa ya ardhi kama vile, Chuo Kikuu cha Dodoma na maeneo ya uwekezaji mkubwa wa Taasisi na Mashirika mbalimbali ya Umma na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Mamlaka itakamilisha kutayarisha Ramani za Msingi za maeneo mapya ya Makazi, Taasisi na biashara, kusanifu na kutenga maeneo ya ujenzi wa huduma za kijamii, kuandaa maeneo mapya ya uendelezaji shughuli za kiuchumi na kufanya mapitio ya Mpango Kabambe wa Mji wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu wa shughuli za Serikali katika sekta zote. Ofisi yangu ina jukumu la kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za kila siku za Serikali pamoja na maelekezo na maamuzi mbalimbali ya Serikali na ushauri unaotolewa na Bunge lako Tukufu. Katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2005, Mipango na taarifa za utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi kwa kila sekta kwa vipindi tofauti iliandaliwa na kusambazwa kwa Wadau. Vile vile, imeratibu maandalizi ya Sera na Mikakati mbalimbali ya Kitaifa na kufuatilia utekelezaji wa maagizo na maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bado kuna changamoto kwa baadhi ya Watendaji Wakuu wa Serikali kuchelewa kutatua kero za wananchi na kutowasilisha taarifa sahihi na kwa wakati. Natoa wito kwa Watendaji Wakuu wa Wizara, Mikoa na Idara Zinazojitegemea kuwasilisha taarifa sahihi za utekelezaji kwa Mamlaka husika na kwa muda uliopangwa pamoja na kuzipatia kero za wananchi ufumbuzi mapema. Katika mwaka 2010/2011, Serikali itaimarisha uratibu wa shughuli za Serikali kwa kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na kufanya tathmini za mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, nimeeleza kwa muhtasari baadhi ya shughuli ambazo Serikali imetekeleza kwa kipindi cha miaka mitano. Aidha, nimetoa mwelekeo wa kazi zitakazofanyika katika mwaka 2010/2011. Ningependa kusisitiza mambo muhimu yafuatayo:-

(a) Ili nchi yetu iendelee, ni lazima tukuze uchumi wetu kwa kuongeza uzalishaji na tija katika Sekta zote. Sekta inayopaswa kupewa kipaumbele ni kilimo, kwa maana ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, ufügaji, uvuvi, na matumizi sahihi ya misitu yetu. Hii ni kwa sababu zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wanaishi kwa kutegemea kilimo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, azma ya Kilimo Kwanza iwe ni kichocheo cha kuhimiza mipango na mikakati tuliojiwekea ya kuendeleza kilimo katika nchi yetu. Natoa wito kwa Viongozi na Wadau wote wa maendeleo kushirikiana na Serikali kuwashimiza wananchi wetu kuhusu matumizi ya teknolojia sahihi yaani (mbolea, mbegu bora na zana za kisasa za kilimo) ili kuongeza uzalishaji katika kilimo.

Tuwahimize pia kuhusu umuhimu wa kutumia Wataalam wa Kilimo wachache waliopo katika maeneo yao. Aidha, Serikali itaweka mazingira mazuri ya kuvutia uwekezaji kutoka Sekta Binafsi, kuimarisha masoko pamoja na utafiti na kuhimiza kilimo cha umwagiliaji, ujenzi wa Viwanda vya Kusindika mazao na kuweka utaratibu madhubuti wa mikopo.

(b) Mwezi Julai 2010, tutaanza utekelezaji wa Awamu ya Pili ya MKUKUTA kwa kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika Awamu ya Kwanza. Ili tufikie malengo tuliyojiwekea, hatuna budi kutumia rasilimali adimu tulizonazo kwa umakini na uangalifu mkubwa. Hivyo, ni lazima Fedha zilizoidhinishwa kwenye Bajeti ya Serikali zitumike kwa kazi zilizopangwa na thamani halisi ya fedha hizo ione kane bayana. Maafisa Masuuli wote waimarishe usimamizi na udhibiti wa fedha za Serikali. (*Makofi*)

(c) Tulianza vizuri kujenga madarasa ya Shule za Sekondari kwa ajili ya wanafunzi waliofaulu mtihani wa darasa la saba. Kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa ijipange vizuri kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanaofaulu wanapata nafasi ya kujiunga na Kidato cha Kwanza. Aidha, ujenzi wa madarasa uende sambamba na ujenzi wa Nyumba za Walimu, Maabara na Vyoo vya kutosha. Nazihimiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa kipaumbele katika ujenzi wa nyumba za Walimu, Maabara na Hosteli za Wanafunzi ili kupanua na kuimarisha miundombinu ya shule nchini. (*Makofi*)

(d) Ardhi tuliyonayo ni hazina kubwa inayohitaji kuwa na Mpango wa Matumizi Bora. Hivyo, nazihimiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuandaa na kutekeleza kwa kasi Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi katika maeneo yao ikiwemo kupima Vijiji, Mashamba na Viwanja. Aidha, nawakumbusha wananchi kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za Ardhi zilizopo ili kuepuka migogoro ya ardhi hasa ile ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. (*Makofi*)

(e) Bado tunayo changamoto ya kusaidia makundi maalum katika jamii yetu, kama vile watu wenyewe ulemavu wa ngozi na vikongwe, ambao bado wanaendelea kuuawa kikatili. Tuendelee kushirikiana kumaliza kabisa tatizo hilo kwa kuwafichua wale wanaofanya vitendo hivyo ili wachukuliwe hatua za kisheria. Naomba tusichoke kuwasaidia watu wenyewe ulemavu kwa kuwapa moyo, kuwaondolea hofu na kuwasaidia pale inapobidi ili waweze kujiletea maendeleo. (*Makofi*)

(f) Tunaelekea katika Uchaguzi Mkuu, mwezi Oktoba 2010, Serikali itahakikisha amani, utulivu na umoja katika nchi yetu unadumishwa. Natoa wito kwa wale wote watakaogombea nafasi mbalimbali za uongozi na wananchi wote kuepuka kujuhusisha na vitendo vya rushwa wakati wa uteuzi, kampeni na uchaguzi mkuu. Aidha viongozi wa Vyama vya Siasa na wagombea wao, wanashauriwa wakati wa kampeni kunadi sera na mikakati ya vyama vyao, badala ya kutumia lugha za kejeli zinazowenza kusababisha uvunjifu wa amani na utulivu hapa nchini.

(g) Tanzania ni nchi yenye fursa tele za kuleta maendeleo, kwa kila mwananchi. Changamoto kubwa ni kwa kila Mtanzania kujitahidi kufanya kazi kwa bidii na maarifa na kutumia muda wa kazi kikamilifu kwa lengo la kuboresha maisha yetu. Hata katika misahafu ya dini zetu imeandikwa, kwamba lolote tufanyalo kwa mikono yetu, hatuna budi kulifanya kwa bidii. Nawahimiza Watanzania wote tutambue kwamba kila mmoja ana wajibu wa kufanya kazi, Serikali itakuwa na jukumu la kuwawezesha wananchi wanaojituma kuinua ubora wa maisha yao. (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha hoja yangu, nimwombe Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, atoe maelezo ya mapitio ya kazi zilizofanyika katika mwaka wa 2009/2010 na mwelekeo wa kazi za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa 2010/2011. Ni matumaini yangu kwamba maelezo hayo yatawezesha Waheshimiwa Wabunge na wananchi kufahamu kwa upana shughuli zinazotekelawa na mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, asante sana. Waheshimiwa hoja hajahitimishwa, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu, ataihitimisha baada ya kusikia maelezo ya utendaji wa Ofisi ya Waziri wa Nchi – *TAMISEMI*, ambaye anazo dakika zisizozidi 30.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika siku hii ya leo. Kipekee namshukuru Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kunitewa kuiongoza Wizara hii. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa hotuba nzuri iliyotoa mwelekeo na malengo ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2010/2011. Pia napenda nimshukuru Mheshimiwa Mustapha Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi kwa Hotuba yake kuhusu hali ya uchumi na mapendekezo ya Serikali ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2010/2011. Hotuba hizi zimeweka misingi ya utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa ujumla kwa mwaka wa fedha 2010/2011. (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kuwasilisha maelezo ya kiutendaji ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, katika kipindi cha mwaka 2009/2010 na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya mpango wa bajeti Ofisi ya Waziri Mkuu – *TAMISEMI*, mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2010/2011, yamezingatia malengo yaliyomo katika mipango mikakati Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005/2010, malengo ya maendeleo ya milenia na mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini Tanzania. Aidha, maelekezo ya mwongozo wa mpango wa bajeti kwa mwaka 2010/2011 hadi 2012/2013 yamezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu ya kisera na ya kiutendaji ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imeendelea na umoja na mshikamano wa Kitaifa na kuhakikisha kwamba amani na utulivu vinakuwepo. Aidha, imehakikisha kwamba demokrasia na utawala bora vinaendelea kujengwa na kuimarishwa. Pia ofisi yangu inaratibu na kusimamia utekelezaji wa sera, programu, miradi na taasisi zilizoko chini yake.

Mheshimiwa Spika, mikoa inalo jukumu kubwa la kujenga uwezo na kutoa ushauri wa kitaalam katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Pia kuhakikisha amani na utulivu vinakuwepo na kudumishwa na kuratibu miradi mbalimbali na programu mbalimbali na kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinateneza majukumu yake kwa kuzingatia utawala bora.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Serikali za Mitaa, ni watekelezaji wa shughuli za Serikali kwa kuhakikisha kuwa zinatoa huduma bora kwa wananchi katika sekta zote katika ngazi za msingi. Mamlaka hizo zina jukumu kubwa la kuwashirikisha wananchi katika kupanga, kufuatilia na kutekeleza mipango ya maendeleo katika maeneo yao. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa, zina wajibu wa kuendeleza ddemokrasia na Utawala Bora, kwa kuendesha chaguzi za viongozi wa ngazi za msingi na kujenga uwezo wa watendaji ili waweze kusimamia rasilimali za umma kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa majukumu kwa Mwaka 2009/2010, madaraka kwa umma, chimbuko la kupeleka madaraka kwa wananchi linatokana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sura ya 8, Ibara ya 145 na 146. Upelekaji wa madaraka hayo kwa wananchi unapitia katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na ndio maana Serikali za Mitaa na Ushirikishwaji wa wananchi katika mchakato wa maendeleo, vinatambuliwa katika Katiba na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ufanuzi wa dhana hii umeelezwa kwa kina katika Sera ya Uboreshaji wa mfumo wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 1998. Katika Sera hii, Mamlaka za Serikali za Mitaa, zimepewa uhuru wa kufanya maamuzi mbalimbali yahusuyo utoaji wa huduma kwa wananchi walio katika Mamlaka hizo na kuwashirikisha wananchi katika kujileta maendeleo na ustawi wao kwa ujumla. Pamoja na kupewa uhuru huo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuutumia kwa kuzingatia Katiba na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika kutekeleza uamuzi wa Serikali wa kupeleka madaraka kwa wananchi, awamu ya pili ya programu ya uboreshaji wa mfumo wa Serikali za Mitaa, yaani kupeleka madaraka kwa wananchi, iliidhinishwa na Serikali mwezi Juni 2009 na imeanza rasmi utekelezaji mwaka 2009 na itakamilika mwaka 2014. Mambo yanayokusudiwa kutekelezwa katika awamu hii ni pamoja na:-

- (i) Kujenga mazingira ambayo yatawezesha Serikali kutekeleza wajibu wake wa Kikatiba wa kupeleka madaraka kwa wananchi.

(ii) Kuzijengea Mamlaka za Serikali za Mitaa uwezo wa kutekeleza majukumu yake.

(iii) Kuimarisha ushirikishwaji wa wananchi katika kupambana na umaskini.

(iv) Kujenga uwezo kwa Viongozi na Watendaji wa ngazi za msingi za mamlaka za Serikali za Mitaa.

(v) Kujenga uwezo wa kitaasisi wa kusimamia na kuratibu utekelezaji wa programu katika ngazi zote Serikalini.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango huo, matokeo yanayotarajiwa ni pamoja na:- Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa vyombo imara vya kusimamia na kuratibu shughuli za kijamii na kimaendeleo, utoaji huduma na kutekeleza *agenda* ya kuondoa umaskini; Wizara za kisekta kuainisha majukumu yake chini ya mahusiano mapya kati ya Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sera na Sheria za Kisekta kuendana na kuzingatia Sera ya Serikali ya kupeleka madaraka kwa wananchi na wananchi kuwa na uelewa wa madaraka waliyonayo na wajibu wao katika kujiletea maendeleo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utawala bora, ili kuimarisha utendaji katika ngazi za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imeendesha vikao mbalimbali vya kazi. Kikao cha kwanza kilifanyika hapa Dodoma kati ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa, kilichofanyika mwezi Machi 2010 na mada kubwa zilizojadiliwa ni pamoja na utekelezaji wa dhana ya Kilimo kwanza, kukabiliana na maafa, kuinua kiwango cha ufaulu wa wanafunzi wa darasa la saba pamoja na kidato cha nne na maandalizi ya kuwapokea wakimbizi 172,000 waliopatiwa uraia wa Tanzania. Kikao cha pili kilifanyika kati ya uongozi wa Ofisi ya Waziri Mkuu, – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wakurugenzi wote katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kupima utendaji wa Mamlaka hizo pamoja na namna ya kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika mwaka 2009/2010, nilielezea kwamba suala la kupeleka madaraka kwa wananchi ni suala la Wizara za kisekta, zina wajibu wa kuhakikisha kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zinakuwa na watumishi wenyewe sifa za kitaaluma na uzoefu ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Aidha, ili kuhakikisha Serikali inapunguza tatizo la uhaba wa watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, jumla ya watumishi 22,215 walijiriwa katika sekta ya kilimo, elimu, fedha na uhasibu, afya na mifugo kwa mchanganuo ufuatao:-

(ii)	Elimu	19,981
(iii)	Afyा	2,245
(iv)	Mifugo	322
(v)	Fedha	392

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi 2010, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikuwa zimejaza nafasi zilizokuwa wazi sita za Wakurugenzi na nafasi wazi 110 za Wakuu wa Idara hazijajazwa. Aidha, mchakato wa uteuzi ili kujaza nafasi hizo unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maeneo mapya ya utawala. Katika mwaka wa fedha 2009/2010 nilieleza kwamba Ofisi imekuwa ikipokea maombi mengi ya kuanzisha Mikoa, Wilaya, Tarafa, Halmashauri, Kata Na Vijiji. Ofisi imeyafanyia kazi maombi hayo yote yaliyowasilishwa. Kuanzisha maeneo mapya ya utawala ni lazima Serikali iwe na uwezo wa rasilimali fedha, watu na vigezo vingine vilivyowekwa. Katika mwaka wa fedha 2009/2010 Serikali imesajili Kata 808, Vijiji 944, Mitaa 120 na Vitongoji 4,958 katika mikoa mbalimbali. Aidha, mamlaka za miji midogo ya Handeni, Nzega, Masasi na Kahama zimepandishwa hadhi na kuwa Halmashauri za Miji. Pia Halmashauri ya Mji wa Lindi, imepandishwa hadhi na kuwa Manispaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukarabati na ujenzi wa Hospitali za Mikoa. Ili kuendeleza kuboresha hospitali zetu za mikoa, hospitali za Singida, Manyara na Mbeya, zinaendelea kujengwa na ujenzi upo katika hatua mbalimbali. Aidha hospitali mbalimbali zimekarabatiwa ikiwa ni pamoja na hospitali ya mkoa wa Morogoro, Arusha, Kilimanjaro, Mtwara, Mwanza na Ruvuma, umefanyika. Aidha katika mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imepokea kiasi cha shilingi bilioni tano, kwa ajili ya ununuzi wa magari ya kubebwa wagonjwa yapatayo 50, ambayo yatapelekwa kwenye mamlaka ya Serikali za Mitaa ambazo hazina kabisa magari hayo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010 Ofisi yangu imeendelea kushughulikia migogoro ya mipaka kati ya Wilaya na Wilaya na kati ya Vijiji na Vijiji. Aidha, tarehe 22/04/2010 kilifanyika kikao cha kutafuta suluhu ya mgogoro wa mpaka kati ya Wilaya ya Sikunge na Manyoni. Wadau wa pande zote walishirikishwa na walikubaliana kimsingi kwamba ramani ya upimaji wa Kijiji cha kilangali irekebishwe ili Makao Makuu ya Kata ya Kipili, Wilaya ya Sikunge, ibaki katika Wilaya ya Sikunge. Aidha, sehemu iliyobaki baada ya ramani ya upimaji wa kijiji cha kilangali, kurekebishwa ibaki katika eneo la Wilaya ya Manyoni. Yote hayo ni kwa manufaa ya maendeleo ya wananchi. Kwa mwaka 2010/2011 tutaendelea kutatua migogoro ya mipaka ya Wilaya ya Kiteto na Wilaya ya Kondoa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuimarisha ulinzi na usalama kwa kushirikisha jamii. Kwa mwaka 2009/2010, nilieleza kuhusu utekelezaji wa mpango wa miji salama kwa

lengo la kuimarisha uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, kutekeleza jukumu hili. Mikoa mbalimbali imeshirikishwa na imepatiwa uwezo na mikoa hii imeelezwa vizuri katika aya ya 16. Utekelezaji huu utafanyika kuitia bajeti ya Halmashauri zenyewe.

Mheshimiwa Spika, Vikao Vya Ushirikiano Kati ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ikishirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi, Zanzibar, imekuwa ikifanya vikao vya ushirikiano mwaka hadi mwaka. Vikao hivi, kutokana na agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alilolitoa kwa viongozi wa Serikali ili kudumisha na kuendeleza Muungano. Madhumuni ya vikao vya ushirikiano ni kujifunza, kubadilishana uzoefu na mafanikio katika nyanja mbalimbali kutoka pande zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009/2010 ilikuwa ni zamu ya wenzetu wa upande wa Zanzibar na tarehe 26 na 27/11/2009 wajumbe walipata fursa ya kutembelea miradi mbalimbali ya maendeleo iliyokuwa inatekelezwa Tanzania, Zanzibar. Miradi hiyo imejumuisha ujenzi wa Ofisi ya Wakuu wa Mikoa ya Unguja Kaskazini na Unguja Kusini, ujenzi wa Ofisi za Wabunge, ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais na miradi ya wananchi ya ufugaji wa mbuzi wa maziwa. Aidha, mada mbalimbali zilijadiliwa katika kikao hicho kwa lengo la kubadilishana uzoefu. Yote hayo yanafanyika ili kudumisha Muungano.

Mheshimiwa Spika, maeneo yenye mazingira magumu. Kwa mwaka jana wakati natoa taarifa yangu nilieleza kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa 34, zimeainishwa na kuonekana kwamba ziko katika mazingira magumu zaidi. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Mamlaka hizo zimetengewa fedha ili kushughulikia matatizo ya miundombinu, mawasiliano, huduma za kiutumishi na huduma nyingine za kijamii. Jumla ya shilingi bilioni 22.3 zilitolewa na kazi ambazo ziko katika hatua mbalimbali ni ujenzi wa nyumba 304 za kuishi kwa ajili ya watumishi, ujenzi wa hosteli mbili na ununuizi wa boti nane kwa ajili ya usafiri katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizohusika.

Mheshimiwa Spika,, Mfumo wa kuzipelekea ruzuku ya maendeleo Mamlaka za Serikali za Mitaa(*Local Government Development Grant System*), unaendelea kutekelezwa hapa nchini. Katiika mwaka wa 2009/2010 jumla ya shilingi bilioni 264.5 ziliidhinishwa na kupelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kuitia mfumo huu. Ruzuku iliyopelekwa kwa mwaka huo ni shilingi bilioni 141, ambazo ni fedha za kigeni na shilingi bilioni 61.6 ni mchango wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, aidha, shilingi bilioni 26.2 zimepelekwa kwa ajili ya kujenga uwezo na shilingi bilioni 31 ni ruzuku ya maendeleo kwa upande wa maeneo ya elimu. Pia ruzuku hiyo imetumika kuboresha miundombinu ya elimu ya msingi na sekondari katika nyanja mbalimbali. Kwa upande wa afya, ruzuku ya shilingi bilioni 29.2 imetumika kutekeleza miradi iliyobuliwa na wananchi ikiwa ni pamoja na kukarabati na

kujenga vituo vya afya na zahanati. Kwa mwaka 2010/2011, fedha za ruzuku ya maendeleo isiyokuwa na masharti kiasi cha shilingi bilioni 324, zitapelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mtiririko wa mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa miaka minne unaonesha kuwa mwaka 2006/2007 makisio ya makusanyo yalikuwa ni shilingi bilioni 63.4 na makusanyo halisi yalikuwa ni shilingi bilioni 61.4 sawa na 69.9%. Mwaka 2007/2008 makisio yalikuwa shilingi bilioni 90.1 na makusanyo halisi yalikuwa ni shilingi bilioni 79.8 sawa na 88.5%. Mwaka 2008/2009 makisio yalikuwa ni shilingi bilioni 109.3 na makusanyo halisi yalikuwa ni shilingi bilioni 100.1 sawa na asilimia 91.6%.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2009/2010 hadi kufikia Machi 2010, jumla ya shilingi bilioni 86.3 zimekusanya sawa na 62.4% ya makadirio ambayo yalikuwa ni shilingi bilioni 138.1. Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato unaonesha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashindwa kufikia malengo wanayojiwekea ya ukusanyaji mapato. Kutokana na hali hii, Serikali inaendelea kuzisaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa katika suala zima la ukusanyaji mapato na usimamizi wa matumizi.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonesha kuwa hali ya usimamizi na utunzaji wa vitabu vya hesabu za fedha kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa inaendelea kuwa ya kuridhisha. Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizopata hati inayoridhisha mwaka 2004/2005 zilikuwa 62 kati ya 117. hadi kufikia mwaka 2008/2009 hati safi zilikuwa 77 kati ya 133. Kwa upande mwingine kwa miaka miwili ya 2006/2007 na 2007/2008 hapakuwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizopata hati isiyoridhisha. Hata hivyo, mwaka 2008/2009 Halmashauri ya Wilaya moja imepata hati isiyoridhisha. Halmashauri hii itaendelea kujengewa uwezo ili kuimarisha utendaji wake na utunzaji wa vitabu vya fedha.

Mheshimiwa Spika, tathmini zinaonesha hati chafu zimezidi kupungua mwaka hadi mwaka, lakini changamoto iliyopo hivi sasa ni kuhakikisha kuwa thamani ya fedha inapatikana katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ukaguzi uliofanyika katika mwaka 2008/2009, katika maeneo maalum, umeonesha mapungufu mengi. Serikali imeziagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya marekebisho kwa kuzingatia na kuhakikisha kunakuwa na thamani ya fedha kwenye maeneo yote katika matumizi ya kawaida na fedha za maendeleo wanatumia kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, hatua ambazo tunazichukua kukabiliana na udhibiti wa fedha za Serikali za Mitaa. Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha usimamizi na udhibiti wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kutoa mafunzo na kuajiri wahasibu na wakaguzi wa ndani, pamoja na kuhakikisha kuwa Kamati za ukaguzi zinafanya kazi kama inavyotakiwa. Mafunzo ya Viwango Vya Kimataifa Vya Uandishi, Utunzaji na Utoaji wa Taarifa za Hesabu kwa Umma (*International Public Sector Accounting Standard - IPSAS*), yametolewa kwa watumishi mbalimbali wa Serikali za Mitaa wa kada mbalimbali ili kuimarisha usimamizi wa fedha.

Aidha, Serikali itahakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zote zinatumia mfumo wa *EPICOR*. Katika mwaka 2010/2011 Serikali imetenga shilingi bilioni tano ili kusimika mfumo wa *EPICOR* kwenye Halmashauri 47 ambazo zilikuwa hazijaingia kwenye mfumo huu. Aidha, mfumo huu unasaidia kuboresha na kuongeza uwazi na uwajibikaji katika masuala yote yanayohusu fedha, ikiwa ni pamoja na kurahisisha utoaji wa taarifa za hesabu zinazojitosheleza na ufungaji wa vitabu kwa usahihi na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, aidha, kanuni za fedha za Serikali za Mitaa, na mwongozo wa fedha za Serikali za Mitaa ni nyaraka muhimu ambazo ziliandaliwa zaidi ya miaka 28 iliyopita. Kwa kuzingatia mazingira ya sasa nyaraka hizi zinahitaji kufanyiwa mapitio. Lengo ni kutumia mfumo wa sasa unaozingatia viwango vya Kimataifa, vya uandishi utunzaji na utoaji wa taarifa katika sekta za umma yaani *IPSAS*. Wizara imekamilisha rasimu ya kwanza ya kanuni za fedha za Serikali za Mitaa pamoja na mwongozo wa fedha kwenye ngazi za Halmashauri. Mchakato unaendelea wakuwasilisha nyaraka hizo kwa wadau mbalimbali ili kupata maoni.

Mheshimiwa Spika, miradi na program za Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ujenzi wa Ofisi za Wabunge, kwa mwaka 2009/2010 Serikali imeendelea na ujenzi wa Ofisi za Wabunge, lengo lilikuwa kujenga Ofisi za Wabunge katika Majimbo 25 Tanzania Bara na Ofisi tano Tanzania Zanzibar. Jumla ya shilingi bilioni moja zimeidhinishwa na mpaka mwezi Aprili zimekwishatolewa shilingi milioni 700 ili kutekeleza mpango huu. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kiasi cha shilingi bilioni moja zimetengwa kwa ajili ya kujenga Ofisi za Wabunge 20 katika Tanzania Bara na tano Tanzania visiwani. Mradi huu ni endelevu na kila mwaka fedha zitatengwa kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa Miji Tanzania, Tanzania *Strategic Cities Project*, Serikali inakusudia kuanzisha mradi kuboresha Miji kwa mwaka wa fedha 2010/2011 jumla ya dola za Kimarekani milioni 175 zitatumika katika mradi huo. Mradi huo ni ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania, Benki ya Dunia na Serikali ya Denmark. Madhumuni ya mradi huu ni kuboresha miundombinu za utoaji huduma za jamii katika Miji. Mradi huu utahusisha Halmashauri za Manispaa za Arusha, Kigoma Ujiji, Dodoma, Mtwara na Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Mbeya na Tanga.

Mheshimiwa Spika, katika Mji wa Dodoma mradi utahusisha Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma na Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu *CDA*. Vigezo vilivyotumika kuchagua Miji hiyo ni hali ya ukuaji wa uchumi katika Mji, mahitaji ya huduma za jamii, ongezeko la idadi ya watu na vitu muhimu vinavyohitaji kuendelezwa. Mradi wa kuboresha Miji pia utahusika na maandalizi ya mradi mkubwa wa kusaidia Jiji La Dar es Salaam kuboresha miundombinu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu utakuwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2010/2011 hadi 2014/2015 na shughuli ambazo zitatekelezwa zimeelezwa vizuri katika aya ya 28 na aya ya 29.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi utakuwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2010/2011 hadi 2014/2015. Shughuli zitakazotekelawa katika Miji kwa upande wa miundombinu ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa barabara, uboreshaji wa dampo za taka ngumu ili ziwe za kisasa, kununua vifaa vya kuzolea taka na ujenzi wa vituo vikubwa vya mabasi.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa maendelo ya Miji nchini yanasmamiwa kwa karibu zaidi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imeanza mchakato wa kuanzisha idara ya uendelezaji wa Miji na kuanza maandalizi ya sera ya kusimamia maendeleo ya Mijini.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa kuzisaidia mamlaka za Serikali za Mitaa, yaani *Local Government Project*, mradi huu ulianzishwa mwaka 2004/2005 na ilivyokuwa katika makubaliano kati ya Serikali na Benki ya Dunia, mradi huu utafikia kikomo mwezi Juni, 2010. Aidha, kwa kushirikiana na Wabia wa Maendeleo, Serikali imeziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kupata ruzuku ya maendeleo na ya kujenga uwezo ili hatimaye ziweze kutekeleza miradi ya maendeleo. Katika Jiji la Dar es Salaam mradi huu uliboresha miundombinu na usimamizi na ukusanyaji wa mapato. Fedha zilizotolewa mwaka 2009/2010, zitaendelea kutumika hadi kufikia mwezi Desemba 2010. Utekelezaji wa shughuli hizi katika Jiji la Dar es Salaam zitaendelea hadi mwezi Juni, 2011, mradi huu tangu umeanza mpaka kufikia kikomo umetumia jumla ya dola za Kimarekani milioni 152.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano na takwimu katika kutekeleza shughuli za Serikali. Serikali imepitisha sera ya matumizi ya TEKNOHAMA ya mwaka 2003 iliyoelekeza matumizi ya teknolojia hii ili kuboresha shughuli za Serikali. Aidha, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2005 katika ibara ya 46 ilieleza kuongeza kasi ya kukua kwa TEKNOHAMA. Katika kutekeleza suala hili ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imeweka na inaendelea kuboresha mfumo wa habari za menejimenti inayotumia teknolojia ya kompyuta kwa ajili ya kuandaa mipango ya bajeti, (*Planning and Reporting Database - PlanRep2*) na kukusanya takwimu ya sekta mbalimbali na katika mamlaka za Serikali za Mitaa.

Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itashirikiana na ofisi ya Taifa ya takwimu katika kuimarisha mpango kabambe wa Taifa wa Takwimu (*Tanzania Statistical Master Plan - TSMP*).

Mheshimiwa Spika, katika kuunga mkono jitihada za Serikali za kudhibiti matumizi ya fedha za umma katika mamlaka ya Serikali za Mitaa, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iko katika zoezi la kuuhisha mfumo wa kudhibiti matumizi ya fedha wa *EPICOR*. Katika Halmashauri 86 ambazo tayari ziko katika mfumo huu. Uhusishaji wa mfumo wa *EPICOR* utasaidia mfumo wa *IPSAS* ambao unatumika kufunga vitabu vya hesabu uweze kufanya kazi kwa urahisi zaidi. Ili kuifanya

mifumo hii kuwa endelevu na kupunguza gharama za kutumia wataalam washauri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imeanzisha timu ya Kitaifa ya uwezeshaji kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa watumiaji wa mifumo hii na kutoa huduma za kiufundi.

Mheshimiwa Spika, aidha, ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inauhisha tovuti yake ili iweze kupokea taarifa nyingi zaidi na kuzitoa kwa wakati kwa wadau mbalimbali. Aidha, ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na mikoa imewezesha kuanzisha tovuti na inaendelea kuboresha tovuti za mikoa. Tovuti hizi zinaiwezesha mikoa kuweka taarifa mbalimbali zikiwemo za fedha na bajeti, mipango, kilimo na mifugo, elimu, afya, mazingira na maliasili, maji, ushirika na biashara, vivutio vya mikoa husika na taarifa nyingine kulingana na mahitaji ya wadau mbalimbali na maelezo yametolewa katika aya ya 33.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 Ibara ya 57 imetambua kuwa rasilimali watu ndio nyenzo kuu ya maendeleo yote ya nchi. Hivyo, kwa kutambua hilo Serikali imegatua shughuli za uendeshaji na usimamizi wa elimu ya sekondari kwenda katika mamlaka za Serikali za Mita. Sababu kubwa ya kufanya hivyo ililenga kupeleka huduma karibu na walengwa. Aidha, hivi sasa liko ongezeko kubwa la shule za sekondari, walimu na wanafunzi kuliko ilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Spika, ongezeko hilo limetokana na maamuzi ya Serikali ya kutekeleza mpango wa maendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM) ambao utekelezaji wake ulianza mwaka 2001. Katika mpango huo wanafunzi takribani 1,000,000 wenye umri wa kwenda shule wamekuwa wanaandikishwa kila mwaka. Kuongeza idadi ya shule za sekondari ni kuongeza uwezo wa kupokea wanafunzi wanaomaliza na kufaulu elimu ya msingi. Imeshaelezwa vizuri na Mheshimiwa Waziri Mkuu, maelezo zaidi yako kwenye aya ya 34, 35 pamoja na aya ya 36 mpaka 37. Mafanikio ya ugatuaji wa shule za sekondari, kwenda katika Serikali za Mitaa pia yameonyesha katika aya ya 36 kwa changamoto zake ziko kwenye aya 37.

Mheshimiwa Spika, baada ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanza kutekeleza jukumu la kusimamia na kuendesha shughuli za elimu ya sekondari mafanikio mbalimbali yameanza kuonekana. Mafanikio hayo ni pamoja na:-

- (i) Walimu wapya kulipwa posho ya kujikimu na mishahara kwa wakati kuanzia mwezi wanaporipoti kituo cha kazi;
- (ii) Fedha za chakula cha wanafunzi kutolewa kwa wakati na kutokuwepo kwa malimbikizo ya madeni ya wazabuni. Aidha, bei za vyakula ambazo awali zilikuwa

zikipandishwa kiholela zimedhibitiwa baada ya mamlaka za Serikali za Mitaa kusimamia wazabuni wanaotoa huduma na shule husika kuthibitisha ubora na usahihi wa huduma inayotolewa;

(iii) Bajeti ya chakula imeongezeka kutoka shilingi 450 hadi shilingi 1500 kwa siku kwa wanafunzi. Kiasi hiki cha fedha kinagharamia chakula chenyewe, kulipia umeme, maji, kuni au gesi na ukarabati wa mfumo wa kupikia. Jumla ya shilingi bilioni 29.5 zimepelekwa katika mamlaka za Serikali za Mitaa hadi kufikia mwezi Machi, 2010 kwa ajili ya chakula cha wanafunzi;

(iv) Kupungua kwa migomo ya wanafunzi inayosababishwa na ukosefu wa huduma bora za chakula, maji, umeme na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Hadi mwezi Machi, 2010 jumla ya shilingi bilioni 8.8 zimepelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia;

(v) Kupunguza kwa utoro wa walimu kutokana na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzuia mishahara yao inapogundulika kuwa hawapo katika maeneo yao ya kazi kwa wakati unaotakiwa; na

(vi) Kutokana na kupata huduma za kuridhisha, kiwango cha ufaulu katika shule za sekondari kimeongezeka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio ambayo yameanza kuonekana bado ziko changamoto mbalimbali ambazo zinahitaji kuendelea kufanyiwa kazi. Changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

(i) Ukosefu wa vyombo vya usafiri katika idara ya elimu ya sekondari ngazi ya Halmashauri na katika shule za sekondari hususan za bweni. Hata shule zenye magari inaonesha magari hayo ni chakavu na gharama za matengenezo ni kubwa;

(ii) Miundombinu chakavu katika shule za sekondari (vyumba vya madarasa, maabara, nyumba za walimu, mabweni, mifumo ya maji safi na maji taka na vifaa kwa ajili ya wanafunzi wenyewe mahitaji maalum);

(iii) Upungufu wa walimu hususan katika masomo ya Hisabati, Sayansi na Kiingereza; na

(iv) Baadhi ya walimu kutopenda kufanya kazi katika mazingira ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hizo Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitafanya yafuatayo:-

(i) Kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatenga bajeti ya kutosha kuongeza rasilimali watu, vitendea kazi na nyenzo nyingine za utendaji;

(ii) Kutumia kwa uangalifu ruzuku ya uendeshaji na maendeleo kwa kuainisha na kutekeleza vipaumbele veya elimu;

(iii) Kuendelea kuboresha mazingira ya kufanya kazi kwa walimu na wanafunzi kujifunza hasa katika maeneo ya vijiji ili yawe vivutio kwa walimu na wanafunzi. Kwa mfano, ujenzi wa nyumba na mabweni na kuweka nishati ya jua na kuhimiza wazazi au jamii kutoa chakula cha mchana kwa wanafunzi; na

(iv) Serikali kuwezesha udahili wa wanafunzi wengi kujiunga na vyuo veya ualimu na hatimaye kupata idadi kubwa ya walimu wanaofuzu.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES II), maelezo yake yameainishwa katika aya ya 36 pia inaendelea mpaka aya ya 38 na Mpango wa Maendeleo ya Msingi (MMEM) yameainishwa vizuri katika aya ya 41, 42 na 43.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari, Awamu ya Kwanza uliana mwaka 2004 na kumalizika mwaka 2009 chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii. Mpango ulikuwa na malengo ya kuongeza uandikishaji wa wanafunzi katika kidato cha kwanza na tano kwa kujenga vymba veya madarasa, nyumba za walimu, maabara, majengo ya utawala, maktaba na hosteli.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari, Awamu ya II itaanza kutekelezwa Julai, 2010 na unalenga kuinua ubora wa elimu kwa kuajiri walimu wanaomiliza masomo vyuoni, kununua vifaa veya kufundishia na kujifunzia na kuboresha miundombinu ya elimu. Mpango ni wa miaka mitano kuanzia Julai, 2010 hadi mwaka 2014 ambapo utajikita katika kuongeza uandikishaji wa wanafunzi katika kidato cha tano. Gharama za kutekeleza mpango zitatokana na mkopo kutoka Benki ya Dunia, mchango wa Serikali, wadau wa Maendeleo ya elimu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2010/2011, mpango umetengewa fedha kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa miundombinu katika shule yaani ujenzi wa nyumba 450, maabara 200, kununua vifaa veya maabara na ukarabati wa shule pamoja na fedha za uendeshaji (*capitation Grant*). Aidha, Serikali itaendesha mafunzo kwa ajili ya Bodi za Shule kwa lengo la kuzipatia mwongozo wa usimamizi wa shule na matumizi ya fedha zinazopelekwa na Serikali. Fedha za ujenzi zimetengwa chini ya mafungu ya kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa kupitia mfumo wa kuzipatia Serikali za Mitaa fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) ili kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 Ibara ya 60(c) Mamlaka za

Serikali za Mitaa zimeendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) kwa kujenga vyumba vya madarasa 510, nyumba za walimu 402 na kutengeneza madawati 12,362. Hadi mwezi Machi, 2010 jumla ya wanafunzi 1,252,724 wameandikishwa kuanza darasa la kwanza kati yao wavulana 626,621 na wasichana 626,103.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009/2010, Serikali imewapanga walimu wa daraja la IIIA 9,111 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kufundisha katika shule za msingi. Kwa utaratibu wa sasa mwalimu akiripoti katika kituo chake cha kazi analipwa posho ya kuanza kazi ya siku saba na uhakika wa kupata mshahara kwa mwezi huo. Utaratibu huu umewasaidia walimu kutekeleza majukumu yao na kupunguza malalamiko yiliyokuwa yanajitokeza kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki Serikali imeendelea kulipa madeni ya walimu wa shule za msingi na sekondari baada ya uhakiki kufanyika. Jumla ya shilingi bilioni 32.2 zilipelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa mwezi Septemba, 2009 kwa ajili ya kulipa madeni ya walimu wa shule za msingi na kiasi kilicholipwa ni shilingi bilioni 22.4. Jumla ya shilingi bilioni 9.7 zillibaki kutokana na madeni ya malimbikizo ya mishahara kulipwa kwa utaratibu wa kawaida wa malimbikizo ya mishahara. Kwa upande wa walimu wa sekondari jumla ya shilingi bilioni 12.5 zimelipwa. Uhakiki wa madeni ya watumishi wasio walimu umekamilika.

Mpango wa maendeleo ya kilimo yaani *DADPs* nayo yameainishwa vizuri sana katika hotuba katika aya ya 44 na aya 45 na programu ya maendeleo ya sekta ya ngozi yameainishwa katika aya ya 46 na aya ya 47.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009/2010, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimepokea jumla ya shilingi bilioni 83.6 kwa ajili ya utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya na shilingi bilioni 2.6 zimepokelewa katika Sekretarieti za Mikoa kwa ajili ya kuratibu shughuli za kilimo. Mamlaka za Serikali za Mitaa zimetumia fedha hizo kuboresha miundombinu, kutoa mafunzo kwa wakulima na wafugaji na kuimarisha uwezo wa taasisi katika kuboresha utoaji wa huduma za kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 zimetengwa shilingi bilioni 1000 kwa ajili ya utekelezaji wa mipango ya kilimo ya Wilaya. Katika fedha hizo Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya imetengewa shilingi bilioni 73 kwa ajili ya kilimo, mifugo, uvuvi na umwagiliaji umetengewa shilingi bilioni 27. Hivyo kuna ongezeko la asilimia 14.1 kwa fedha za umwagiliaji ukilinganisha na shilingi bilioni 23.8 kwa mwaka 2009/2010. Fedha hizi zitatumika kutekeleza miradi ya maendeleo ya sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, programu ya Maendeleo ya Sekta ya Ngozi, Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta ya Ngozi ulibuniwa na wadau mbalimbali wa sekta ya ngozi kwa kushirikiana na Serikali ili kukabiliana na kuendelea kushuka kwa maendeleo ya sekta ya ngozi nchini. Mkakati huu unalenga kufufua na kuendeleza sekta ya ngozi ili zipatikane ngozi zenyе ubora unaotakiwa kwa ajili ya viwanda vya hapa nchini

vinavyosindika na kutengeneza ngozi na bidhaa zake. Mkakati wa kufufua na kuendeleza sekta ya ngozi unatekelezwa katika mikoa 17 ya Arusha, Dar es Salaam, Shinyanga, Kagera, Kilimanjaro, Maogoro, Manyara, Dodoma, Singida, Mwanza, Tabora, Mara, Pwani, Iringa, Mbeya, Ruvuma na Rukwa yenye Halmashauri 65. Lengo la baadaye mikoa yote itatekeleza mkakati huu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, pamoja na Chama cha Wadau wa Ngozi (*Leather Association of Tanzania -LAT*) zitaendelea kuratibu utekelezaji wa mkakati huu katika mamlaka za Serikali za Mitaa. Jumla ya shilingi bilioni 1.3 zimepangwa kutumika kuendeleza sekta ya Ngozi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, shilingi milioni 73.0 zitatumika katika ngazi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na shilingi milioni 51.0 katika ngazi ya sekretarieti za mikoa kuratibu utekelezaji wa mkakati huo.

Mheshimiwa Spika, programu ya maji na mazingira vijijini nayo imeainishwa vizuri sana utekelezaji wake katika aya ya 48 na aya ya 49. na Mpango wa Afya ya Msingi (MMAM) umeainishwa vizuri katika aya ya 50 na aya ya 51 na upande wa usimamizi wa hifadhi ya mazingira imeelezwa vizuri katika aya ya 52 na Waziri mwenye dhamana ya mazingira ataaeleza vizuri katika hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira ilianza kutekelezwa mwaka wa fedha 2007/2008. Utekelezaji wa programu hii unaongozwa na Mkakati wa Sera ya Maji ya Taifa ya mwaka 2002 na programu ya Taifa ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Hadi kufikia Desemba 2009 jumla ya Miradi ya Maji 3,791 yenye vituo vya kuchottea maji 7,988 vimejengwa au kufanyiwa ukarabati wa watu wapatao 1,738,542 katika vijiji mbalimbali wanapata maji safi na salama. Vilevile, Ofisi 46 za maji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekarabatiwa na nyingine 41 mpya zimejengwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imehamasisha wananchi kuhusu usafi wa mazingira na wa mtu binafsi. Hadi kufikia Desemba 2009 wananchi wapato 1,976,992 walikuwa wamehamasishwa kuhusu usafi wa mazingira na usafi wa mtu binafsi na vyoo vya shimo vya mfano 2,224 vimejengwa katika maeneo mbalimbali. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Serikali itaendelea kutekeleza programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kushughulikia changamoto zilizopo ili kuweza kutosheleza mahitaji ya upatikanaji wa huduma za maji na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM), mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM) ni utekelezaji wa sera ya Afya ya mwaka 2007 ya kuongeza na kusogeza huduma bora ya afya ya msingi kwa kila mwananchi katika ngazi ya zahanati, vituo vya afya na hospitali za Wilaya. Mpango huu

unahusu ukarabati, upanuzi na ujenzi wa majengo ya vituo vya kutolea huduma za afya zikiwemo nyumba za watumishi na upelekaji wa vifaa vya kitaalam na samani kwenye Hospitali za Wilaya, vituo vya afya za zahanati. Mpango unazingatia pia upatikanaji wa watumishi, kuboresha huduma za afya ya uzazi wa mama na mtoto, kupunguza maambukizi na kuwapa dawa za kupunguza makali ya ugonjwa wa UKIMWI, elimu ya afya na kinga. Hadi sasa vituo vya afya 200 na zahanati 1,334 zimekarabatiwa. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, shilingi bilioni 29.2 zilitengwa ili kutekeleza mpango huu na shilingi bilioni 9.2 zilitengwa na washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi ni mwendelezo wa juhudzi za Serikali za kutoa huduma za afya zilizoanza kupitia Mfuko wa Pamoja na Ukarabati (*Joint Rehabilitation Fund*) wa vituo vya kutolea huduma za afya. Kwa mwaka 2009/2010, miongozo na michoro ya vituo vya kutolea huduma za afya, mahitaji ya ukarabati wa hospitali za Wilaya, mahitaji ya vifaa-tiba katika hospitali za Wilaya yaliandaliwa na mafunzo kwa watumishi wa ngazi mbalimbali yaliyotolewa. Miongozo na michoro hiyo ndiyo inayotumika sasa katika kutekeleza mpango wa MMAM. Mwezi Aprili, 2010 Mamlaka za Serikali za Mitaa zimepokea shilingi bilioni 18.0 kwa ajili ya kuendelea kutekeleza mpango wa MMAM. Utekelezaji wa ukarabati wa vituo vya afya, zahanati na hospitali za Wilaya upo katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira, suala la hifadhi ya usimamizi wa mazingira limekuwa mjadala mkubwa duniani kote, kuhusiana na hali ya mabadiliko ya tabianchi. Kwa mujibu wa Mkakati wa Hifadhi ya Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji wa 2006, jamii yote ya Tanzania inalo jukumu la kuhifadhi mazingira. Mamlaka za Serikali za Mitaa zina wajibu wa kutunga, kusimamia na kutekeleza sheria ndogo za hifadhi ya mazingira katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 ibara ya 81(a) na (b) kwa mwaka 2009/2010 Mirada ya Hifadhi Mazingira na Ardhi-Oevu na Usimamizi Shirikishi wa Misitu iliendelea kutekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 62 katika Mikoa 11. Fedha zilizoidhinishwa kutekeleza Miradi hiyo ni shilingi bilioni 2.73, fedha zilizotolewa hadi Machi, 2010 ni shilingi milioni 974.4. Fedha hizo zimetumika kufundisha wananchi namna ya kutayarisha vitalu, ufugaji bora wa nyuki, upandaji miti na wananchi kuotesha misitu kwa njia shirikishi.

Mheshimiwa Spika, katika juhudzi za kupambana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi, eneo la hekta 1,030 limehifadhiwa na miti 253,709,000 imepandwa katika maeneo yanayotekelzwa mradi. Katika mwaka wa 2010/2011 Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itaendelea kuratibu utekelezaji wa Miradi ya Hifadhi Mazingira na Ardhi-Oevu na Usimamizi Shirikishi wa Misitu.

Mheshimiwa Spika, Mashirika na taasisi yaliyoko chini ya ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, utekelezaji wake umeanishwa vizuri katika aya ya 55, 56, 57 na aya ya 58.

Mheshimiwa Spika, Mashirika na Taasisi, Chuo cha Serikali za Mitaa - Hombolo (*LGTI*), katika mwaka 2009/2010 Chuo cha Serikali za Mitaa kimeendelea na mipango yake ya kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa kozi nne zilizopo ambazo ni Astashahada na Stashahada ya Utawala na Uhasibu na Fedha. Kuandaa kozi mpya katika ngazi ya Stashahada ya Shahada. Chuo pia kimeendelea na mikakati ya kutoa ushauri na kufanya tafiti katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Chuo kwa sasa kina jumla ya wanafunzi 476 ambaao mafunzo yao yanaendeshwa katika kampasi za Hombolo, Kimvi na Mtumba. Idadi hii ni ongezeko la wanafunzi 233 sawa na asilimia 96 ya wanafunzi waliodahiliwa mwaka 2008/2009. Kati ya idadi hiyo wanaume ni 257 na wanawake ni 219 sawa na asilimia 46 ya wanafunzi wote. Kuhusu ikama ya watumishi, Chuo kina Wahadhiri 26 na watumishi waendeshaji 44, idadi inayofanya watumishi wote kuwa 70 katika mwaka 2009/2010. Kwa mwaka 2010/2011, Chuo kimepanga kuongeza udahili kufikia jumla ya wanafunzi 800 na kuongeza ikama kufikia jumla ya watumishi 108.

Mheshimiwa Spika, Chuo katika mwaka wa fedha 2008/2010, kimejenga majengo mapya matatu kwa gharama ya shilingi bilioni 2.7 ikiwa ni kupunguza pengo la uhaba wa mabweni, vyumba vya kutolea mihadhara na ofisi za watumishi. Majengo ambayo yamekamilika kwa kiwango cha asilimia 100 ni:-

- (i) Bweni moja lenye uwezo wa kulaza wanafunzi 200;
- (ii) Kumbi mbili za kutolea mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 200 kila moja na ofisi nne za watumishi; na
- (iii) Bohari moja yenye ofisi sita za watumishi.

Mheshimiwa Spika, katika maelezo yangu mwaka 2009/2010 nilieleza kuwa, mradi wa upanuzi wa Chuo utagharimiwa na Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (*LAPF*) kwa gharama za shilingi bilioni 39.8 kwa mpango wa dhamana ya Serikali. Gharama hizi zinahusisha malipo ya wakandarasi, wataalam elekezi, uendeshaji wa mradi na riba. Miundombinu inayojengwa ni majengo na huduma nyingine ambazo ni:-

- (i) Mabweni 2 (wanafunzi 200 kwa kila moja);
- (ii) Maktaba moja (wanafunzi 300);
- (iii) Ukumbi wa mihadhara moja (wanafunzi 200);
- (iv) Madarasa tisa (wanafunzi 40 kila moja);

- (v) Ofisi 6 za wahadhiri;
- (vi) Maabara ya Kompyuta (wanafunzi 300);
- (vii) Nyumba za kuishi watumishi (tano za daraja la A na 10 za daraja B); na
- (viii) Viwanja vya michezo na burudani, barabara za ndani, mabwawa ya maji taka, kuboresha miundombinu ya umeme na maji na sehemu ya kuegesha magari.

Utekelezaji wa mradi huo umeanza tangu mwezi Februari, 2010 na unatarajiwu kukamilika mwezi Novemba, 2010.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 chuo kimepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa upanuzi wa chuo;
- (ii) Kukarabati baadhi ya miundombinu ya zamani, kujenga miundombinu ya kuvuna maji ya mvua na kuweka samani katika majengo mapya;
- (iii) Kufanya tathmini ya eneo jipya la ekari 750; na
- (iv) Kutoa mafunzo ya utawala bora kwa watendaji katika ngazi za msingi za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Elimu Kibaha, utekelezaji wake umeainishwa katika aya ya 59, 60, 61,62, 63 na 65.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Elimu Kibaha lina jukumu kubwa la kupambana na maadui ujinga, umaskini na maradhi. Shirika hutekeleza majukumu yake kwa njia ya kushabikiana (*synergy*) na kushabihiana (*integration*).

Mheshimiwa Spika, katika kupambana na adui ujinga mwaka 2009/2010, shirika lilikuwa na lengo la kutoa elimu na malezi bora kwa wanafunzi 2,706. Wanafunzi wote walipitiwa elimu na malezi bora. Pia, Shirika lilikuwa na lengo la kuendelea kutoa huduma za maktaba kwa wadau 48,500 utekelezaji ulikuwa, wadau 52,392 walipatiwa huduma ya kujisomea vitabu, magazeti, majarida mbalimbali; pamoja na huduma ya mtandao.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, wanafunzi 768 walihitimu masomo yao katika asasi za Shirika. Aidha, Shule za Shirika zimekuwa zikifanya vizuri katika mitihani ya Kitaifa, kwa mfano, mwaka 2010 Shule ya sekondari

Kibaha imekuwa ya nne Kitaifa katika matokeo ya kidato cha sita na kushika nafasi ya kwanza katika masomo ya Hisabati na Kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Shirika kupitia chuo chake cha Maendeleo ya wananchi liliendelea kutoa mafunzo katika fani mbalimbali. Fani hizo ni pamoja na kilimo na mifugo, ujenzi na useremala, umeme na magari, upishi na ushonaji, uungaji vyuma pamoja na udereva. Wanachuo 220 walipatiwa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, shirika pia lilitoa elimu ya nadharia na vitendo juu ya ufugaji bora wa kuku. Shirika liliwauzia wananchi vifaranga wa nyama 630,917 na vifaranga wa mayai 30,965. Aidha, wataalam wa ugani wa Shirika waliwatembalea wafugaji 380 ili kutoa ushauri juu ya ufugaji bora wa kuku. Shirika pia liliendelea kutoa elimu kwa vitendo kwa wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA). Kutokana na mfumo wa kushabihiana na kushabikiana wanachuo 34 wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha walipatiwa mafunzo ya kilimo na ufugaji kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa shamba la ng'ombe wa maziwa pamoja na kuwauzia wananchi maziwa (lita 120,000) kwa ajili ya lishe bora, pia lilitoa mafunzo ya nadharia na vitendo kuhusu ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa kwa wakulima wadogo. Aidha, katika uboreshaji wa ng'ombe wa kienyeji, shirika liliendelea kusimamia na kutoa elimu ya ufugaji wa ng'ombe bora kwa maziwa katika maeneo ya jirani. Ndama 23 (madume 13 na majike 10) walizaliwa kutokana na madume ya mbegu bora yiliyopelekwa kwa wafugaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010 shirika lilikuwa na lengo la kuhudumia wagonjwa 200,000 katika hospitali ya Tumbi. Wagonjwa 232,000 wamehudumiwa. Aidha, shirika lilikuwa na lengo la kutoa elimu ya utabibu kwa wanachuo 120 na wanachuo 118 walipatiwa mafunzo hayo. Katika kuhudumia wahanga wa ajali za barabarani kwa mwaka 2009/2010, shirika limehudumia wahanga 1,873 katika hospitali ya Tumbi.

Mheshimiwa Spika, mradi wa upanuzi wa hospitali ya Tumbi, ulianza mwaka 2008/2009 na mpaka sasa Serikali imetua shilingi bilioni tano kwa kazi hiyo. Kazi ya upanuzi awamu ya kwanza imefikia asilimia 75. Mwaka 2010/2011 shilingi bilioni 1.5 zimetengwa ili kukamilisha awamu ya kwanza na kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2010/2011 shirika limepanga kufanya yafuatayo:-

- (i) Kuendelea na Upanuzi wa Hospitali ya Tumbi;
- (ii) Kuendelea kutoa mafunzo ya maafisa tabibu 228;

(iii) Kuendelea kutoa elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Malezi Bora kwa wanafunzi 2,786;

(iv) Kuendelea kutoa elimu katika fani mbalimbali katika chuo cha maendeleo ya wananchi Kibaha kwa wastani wa wanachuo 320;

(v) Kuendelea kutoa huduma za Maktaba kwa wastani wa kuhudumia wadau 52,419;

(vi) Kuendelea kutunza mazingira, ikiwa ni pamoja na kupanda miti na kuitunza miti 3,684 ambayo imepandwa tayari;

(vii) Kuendelea kutoa elimu ya nadharia na vitendo juu ya ufugaji bora wa kuku na ngombe wa maziwa;

(viii) Ukarabati wa miundombinu ya shirika;

(ix) Uboreshaji wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha ili kutekeleza dhana ya Kilimo Kwanza; katika uzalishaji na uuzaji wa vifaranga na kuwauzia wananchi. Majogoo 4,000 kwa ajili ya kubadilisha kuku wa kienyeji kuwa wenye tija; na

(x) Kuendelea na utekelezaji wa mpango kabambe wa matumizi ya ardhi ya shirika 2006 - 2007.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa pia maelezo yake yameainishwa vizuri sana katika aya ya 67, 68 mpaka aya ya 69.

Mheshimiwa Spika, jukumu la msingi la Bodi ya Mikopo ya Serikali ya Mitaa kama ilivyoanishwa katika Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 (Sura ya 290 R.E 2000), ni kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kutekeleza miradi ili kusaidia kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010 hadi Machi, 2010 ruzuku ya shilingi milioni 251 imetolewa na Serikali sawa na asilimia 62.8 ya shilingi milioni 400 zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Kwa upande wa marejesho ya mikopo pamoja na riba, jumla ya shilingi milioni 162.9 zimerejeshwa na kulipwa ikilinganishwa na shilingi 265 zilizokadiriwa kulipwa mwaka wa fedha 2009/2010. Kwa ujumla marejesho yote ya mikopo na malipo ya riba yamefika shilingi bilioni 1.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 2.9 zinazopaswa kurejeshwa na kulipwa riba.

Mheshimiwa Spika, katika mwelekeo wa Sera za Chama cha Mapinduzi Ibara ya 18(b) umeelekeza kutekeleza sera ya kuwawezesha wananchi kiuchumi. Hadi kufikia

tarehe 15 Aprili, 2010 mikopo ya jumla ya shilingi milioni 451.4 imetolewa kwa ajili ya miradi miwili ya upimaji viwanja, ujenzi wa vituo viwili vya mabasi, mradi wa ujenzi wa soko, na ujenzi wa ukumbi wa mikutano katika Halmashauri za Wilaya za Mvomero na Monduli, Halmashauri za Manispaa za Musoma na Moshi na katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya. Mikopo yote iliyokwishatolewa imefikia jumla ya shilingi bilioni 4.02 ikilinganishwa na maombi yaliyopokelewa ya jumla ya shilingi bilioni 12.4.

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya fedha za kuendeshea huduma ya mikopo zinatokana na michango ya akiba ya Halmashauri pamoja na ruzuku kutoka Serikalini. Hadi tarehe 15 Aprili, 2010, jumla ya shilingi milioni 558.6 zimechangwa na Halmashauri sawa na asilimia 61.4 ya shilingi milioni 910 zilizokadiriwa kuchangwa kwa mwaka 2009/2010 na kufanya michango yote ya akiba kufikia jumla ya shilingi bilioni 2.9 sawa na asilimia 52.7 ikilinganishwa na kiasi kinachopaswa kuchangwa cha jumla ya shilingi bilioni 5.5.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Bodi itaendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kutoa mikopo kwenye mamlaka ya Serikali za Mitaa. Utaratibu umewekwa wa kufanya ufuatiliaji ili kuhakikisha kuwa marejesho ya mikopo yanafanya na michango ya akiba inawasilishwa ili kuongeza mtaji wa bodi. Lengo ni kuhakikisha kuwa Halmashauri nyingi zaidi zinanufaika na huduma ya mikopo ya bodi.

Mheshimiwa Spika, maombi ya mikopo kutoka kwenye Halmashauri yamekuwa mengi, lakini uwezo wa Bodi wa kukidhi mahitaji ni mdogo kutokana na kiwango kidogo cha mtaji. Changamoto kubwa iliyopo ni namna ya kuifanya Bodi iweze kutoa mikopo ya kutosha na ufanisi zaidi. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali inaangalia upya muundo wa bodi hiyo. Hivyo, katika mwaka wa 2010/2011, kati ya mambo yanayotarajiwa kufanya ni pamoja na kuanzisha mchakato wa kuufanya marekebisho muundo wa bodi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wakala wa Usafiri wa Haraka Dar es Salaam yaani Dar es Salaam *Rapid Transit*. Maelezo yake yameainishwa katika aya ya 72.

Mfuko wa Pensheni za Serikali za Mitaa maelezo yake yameainishwa katika aya ya 73, 74, na 75 nimefanya masahihisho na aya ya 76.

Mheshimiwa Spika, katika maelekezo ya Ilani ya uchaguzi ya chama cha mapinduzi ya mwaka 2005 Ibara ya 45(h) inaelekeza kutekeleza mradi wa mabasi yaendayo haraka katika jiji la Dar es Salaam. Katika mwaka wa fedha 2009/2010 wakala wa mradi wa mabasi yaendayo Haraka kwa kushirikiana na wakala wa Barabara umekamilisha kufanya usanifu mpya wa miundombinu ya mfumo wa usafiri wa haraka wa mabasi ambao umelenga kugawa kazi za ujenzi kwenye mafungu ambayo wakandarasi wa ndani na nje ya nchi baada ya kukosa mkandarasi kwa matangazo ya Julai, 2008.

Mheshimiwa Spika, usanifu ulikamilika mwezi Oktoba, 2009 na kugawa kazi zote kwenye zabuni saba katika vituo mbalimbali vya mabasi yatakayohusika. Mzabuni wa ujenzi wa kituo kikuu cha Kivukoni na mzabuni wa kuhamisha nguzo za umeme wanatarajia kuanza kazi mwezi Juni, 2010 wakati zabuni nyingine zikiendelea kukamilisha tayari kwa ujenzi.

Mheshimiwa Spika, hatua za kuhakikisha mfumo huu unawafikia wananchi wengi kwa haraka zabuni ya usanifu wa miundombinu ya awamu ya pili utakaohusu Barabara ya Kilwa na awamu ya tatu Barabara ya Nyerere zimetangazwa na kufunguliwa tarehe 30 Aprili, 2010. Pia mwezi Machi, 2010 wakala umetangaza zabuni ya ujenzi wa kituo cha mawasiliano ya mfumo wa *DART* ambao utaongozwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa; ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi Oktoba, 2010.

Mheshimiwa Spika, shughuli nyingine zilizofanyika ni kutekeleza mradi mdogo wa elimu kwa jamii kuhusu mfumo bora wa mabasi na mahitaji ya nishati safi mradi ambao ulishirikisha wadau wote muhimu. Wakala wa usafiri wa Haraka kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (*EWURA*) na Baraza la mazingira la Taifa (*NEMC*) katika kutekeleza mradi huu wataendeleza juhudzi za kuhakikisha kuwa matumizi ya nishati safi kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira inazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, wakala umefanya utafiti kuhusu utoaji huduma ya mabasi ambayo imewezesha kueleweka kwa mfumo wa watoa huduma uliopo na kubaini uwezo wa kifedha na kielimu kumudu uwekezaji kwenye mfumo mpya wa *DART*. Wakala kwa kushirikiana na Wataalam Waelekezi (*consultants*) umeandaa mikakati ya kuwezesha Watanzania kupata fursa na kipaumbele kuwekeza kwenye mfumo wa Mabasi ya Haraka. Mwitikio wa wadau kwenye tafiti zilizofanyika ni mzuri hivyo mikakati iliyoandalila inazingatia maoni ya watoa huduma ya usafirishaji. Jitihada zinafanyika kuhakikisha mfumo wa *DART* awamu ya kwanza unaanza kufanya kazi rasmi ifikapo mwezi Agosti, 2012,

Mheshimiwa Spika, mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa, Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 2006 iliuboresha Mfuko huo na kuufanya pamoja na mafao mengine, kutoa mafao ya pensheni kwa wanachama wake. Katika kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai, 2009 hadi Machi 2010, Mfuko umeweza kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 41.34 sawa na asilimia 114 ya lengo lililowekwa la shilingi bilioni 36. Katika kipindi hicho Mfuko umewalipa wastaafu 714 na warithi wa wanachama 245 waliofariki kiasi cha shilingi bilioni 12.7. Katika kipindi hicho mfuko ulilipa jumla ya mafao ya kila mwezi kwa wanachama 2,320 jumla ya shilingi bilioni 1.6.

Mheshimiwa Spika, aidha, mfuko umeongeza wanachama 4,986 sawa na asilimia 93 ya lengo la kuandikisha wanachama 71,380 na idadi hii inatarajiwa kuongezeka kwa kiwango cha asilimia nane kila mwaka hasa baada ya kuanza kuandikisha madiwani, walimu na makundi mengine kwenye mfuko.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu ya Mfuko kwa mwaka wa fedha 2010/2011, shughuli na malengo mbalimbali yameainishwa kama ifuatavyo:-

- (i) Kuongeza idadi ya mafao kutoka manne mpaka sita kwa kutoa mafao mapya mawili ambayo ni fao la uzazi na fao la msaada wa mazishi;
- (ii) Kuandikisha wanachama wapya wapatao 6,030;
- (iii) Kukusanya michango ya wanachama shilingi bilioni 57.7;
- (iv) Kulipa mafao ya kiasi cha shilingi bilioni 21.8 ikiwamo mafao mapya mawili; na
- (v) Kukusanya shilingi bilioni 29.75 kutoka kwenye vitega uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 Ibara ya 52 ilielekeza Serikali kuona umuhimu wa kufikiria uwezekano wa kutumia uwezo mkubwa wa fedha katika Mashirika ya Hifadhi ya Jamii. Mfuko huu wa Pensheni wa Serikali za Mitaa kwa 2010/2011 umepanga kuwekeza kiasi cha shilingi bilioni 153.04 katika maeneo mbalimbali ikiwemo miradi ya ubia na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Mwanza, Manispaa ya Morogoro na miradi inayodhaminiwa na Serikali kama Upanuzi wa Chuo cha Serikali za Mitaa - Hombolo na Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela Arusha. Ujenzi wa awamu ya kwanza ya Chuo Kikuu cha Afya cha Dodoma umeshakamilika. Aidha, Mfuko unaendelea kutoa mikopo ya riba nafuu kwa SACCOS za Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuziwezesha kuwakopesha wanachama.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 15.06 pamoja na riba kwa ajili ya Mfuko huu wa LAPF ikiwa ni utekelezaji wa maamuzi yaliyopitishwa mwaka 2006 ya kuupatia shilingi bilioni 107.3 kwa awamu kumi ili kuuwezesha kumudu mabadiliko ya kuubadili kuwa na pensheni.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, napenda kushukuru Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa michango yao na maelekezo yao kuhusu utendaji wa Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kamati hizi mbili zimekuwa za msaada mkubwa kwangu na kufanya kazi yangu kuwa nyepesi. Napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuniongoza na kwa kunishauri kwa busara na naomba Mungu ambariki.

Aidha nawashukuru Waheshimiwa, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Naibu Waziri; Katibu Mkuu, Maimuna Tarishi; Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Maswi na wote ambao wanansaidia katika kazi zao. Naomba niwashukuru Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala na Wakuu wa Wilaya pamoja na Wakurugenzi kwa kazi zao nzuri kwa ushirikiano mzuri na wananchi, naomba niwashukuru wote ambao wanafanya kazi bega kwa bega na Serikali katika maeneo yao ya utawala.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naishukuru familia yangu, mume wangu na watoto kwa kunisaidia katika shughuli mbalimbali. Nisiwasahau wapiga kura wangu wa Ulanga Mashariki na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano wenu kwa muda wa miaka mitano hii, naomba mungu awabariki wote turudi tena hapa Bungeni ili tuweze kushirikiana.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ila katika salamu kwa ndugu zako umewasahau mawifi sijui. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuhitimisha hoja.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii sasa kuwashukuru timu zima ya Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa ushauri wao ambao umewezesha Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu Rais na Waziri Mkuu kutekeleza majukumu yao ya Kitaifa kwa ufanisi katika kipindi cha miaka iliyopita. Kwanza nawashukuru wafanyakazi wote wa Serikali na taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu kiongozi, bwana Philemon Luhanjo pamoja na vyombo vyote vya dola kwa kuiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuiwezesha kukamilisha maandalizi yote ya bajeti ya Serikali ya mwaka 2010/2011 pamoja na makadirio ya matumizi ya fedha ya kila Wizara, Mikoa, Wakala na Taasisi za Serikali zinazojitegemea. Nawashukuru Watanzania wote na Washirika wetu wa Maendeleo kwa michango yao ambayo imewezesha Serikali kufanikisha kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuwashukuru Mheshimiwa Philip Sanka Marmo, Mbunge wa Mbulu, Waziri wa Nchi Sera, Uratibu na Bunge; Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani, Mbunge wa Ulanga Mashariki, Waziri wa Nchi wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Mheshimiwa Aggrey Joshua Mwanri wa Siha, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa msaada mkubwa na ushirikiano walionipa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri. Shukrani za pekee kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwa jitihada walizoonyesha katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru vilevile wafanyakazi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu chini ya uongozi wa Makatibu Wakuu Bwana Peniel Moses Lyimo na bibi

Maimuna Kibenga Tarishi na Manaibu Makatibu Wakuu bwana Fanuel Zebius Mbonde pamoja na bwana Eliachim Chacha Maswi na bwana Jumanne Abdallah Sagini kwa ushauri wao wa kitaalam ambao wamenipa mimi na Waheshimiwa Mawaziri wa nchi katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, vile vile nawashukuru kwa kukamilisha maandalizi yote ya makadirio ya fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa mwaka 2010/2011. Katika mwaka 2009/2010, nchi yetu imepata misaada kutoka kwa wahisani wetu mbalimbali. Misaada na mikopo imetoka kwa nchi rafiki, nchi fadhili, Taasisi za Fedha Duniani, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Mifuko mbalimbali ya Fedha Duniani, Madhehebu ya Dini na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Misaada na mikopo hiyo imechangia sana katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na kuboresha utoaji wa huduma kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati na kuwahakikishia kuwa Tanzania tunathamini misaada na mikopo waliyotupatia na tutaendelea kushirikiana nao katika harakati za kuleta maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati wapiga kura wangu wa Jimbo la Mpanda Mashariki kwa imani na heshima kubwa waliyonipa ya kunichagua kuwa Mbunge wao tangu mwaka 2000. (*Makofifi*)

Aidha, nawashukuru viongozi wenzangu wa CCM na Serikali mkoani Rukwa na wananchi wote kwa ushirikiano wa dhati walionipatia katika kipindi chote cha uongozi wangu. Kipekee napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa imani kubwa kwangu na hivyo kunateua kuwa Waziri Mkuu tangu tarehe 8 Februari, 2008. Pia namshukuru Mheshimiwa Rais kwa jinsi alivyonipa ushirikiano mkubwa wa kufanya kazi naye kwa karibu na kwa upendo na hivyo kuniwezesha kujifunza mengi kutoka kwake katika kipindi hiki. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliokubali na kuthibitisha uteuzi huo wa Rais ambao umeniwezesha kuwatumikia Watanzania katika wadhifa huu kwa miaka miwili na miezi minne hadi sasa. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile niwashukuru viongozi wenzangu wote wa Kitaifa na viongozi wa ngazi nyingine zote kwa ushirikiano mlionipa ameniwezesha wa kutekeleza jukumu kubwa la kusimamia utendaji wa Serikali katika sekta zote na kuwa kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nirudie tena kukushukuru wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mkubwa mlionipa katika kipindi changu cha kuwa kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni, nasema ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, shukrani zangu za mwisho ningependa kuzitoa kwa familia yangu, mama Tunu Pinda na watoto kwa kunipa moyo, msaada na uvumilivu mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Bunge ya Mwaka 2010/2011, baada ya maelezo haya kwa muhtasari, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2010/2011 ya jumla ya Shilingi bilioni hamsini na sita, milioni mia nane tisini na tano, laki nane tisini na nane elfu (56,895,898,000) kwa ajili ya Mfuko wa Bunge na jumla ya Shilingi trilioni mbili, bilioni mia tisa kumi na sita, milioni mia tatu ishirini na tano, laki tatu sitini na mbili elfu (2,916,325,362,000) kwa ajili ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ikiwa ni Matumizi ya Kawaida na Fedha za Maendeleo za Ndani na Nje kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii, yapo Majedwali ambayo yanafafanua kwa kina Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Bunge pamoja na takwimu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Celina Kombani. Waheshimiwa Wabunge shughuli sasa inabidi tuendelee kwa mujibu wa ratiba tuliojiwekea, kanuni ya 28(2) inasema: “Hivi Bunge litakutana hadi saa saba mchana, ambapo Spika ataaahirisha shughuli yoyote itakayokuwa inafanyika hadi saa 11 isipokuwa kama akiona inafaa Bunge linaweza kuendelea kukutana kwa muda usiozidi dakika 30 au kusitishwa wakati wowote kabla ya saa saba”. Sasa ni hii ya dakika thelathini, nimeona inafaa kwa sababu tuna wachangiaji wawili Mwenyekiti wa Kamati kwa jinsi tulivyotengua kanuni amepewa nusu saa na msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani amepewa dakika zisizozidi thelathini.

Kwa hiyo itapita kidogo kama dakika kumi hivi, kwa hiyo, naona ufanisi isiwe tena tusitishe halafu turudi tena saa kumi na moja tuwasikie hao halafu kwenye saa saba na dakika kumi tutaweza kusitisha na nitawatajia sasa wachangiaji, orodha imeshapita sasa zaidi ya 80. Kwa hiyo, nitatamka wachache ambaao watachangia. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ili tuweze kupata maoni ya Kamati ya kisekta kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa George Malima Lubeleje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) na Kanuni ya 114 (11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, kwa mwaka wa fedha 2009/2010 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011, kwa Fungu 25 - Waziri Mkuu, Fungu 27 - Msajili wa Vyama vyaa Siasa, Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 42 –

Mfuko wa Bunge, Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Fungu 91 – Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevy na Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania.

Aidha, nawasilisha maoni ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, kwa Fungu 56 – Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na Mafungu 70 – 89 na 95 kwa ajili ya Mikoa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge inahusisha mafungu saba. Mafungu hayo ni Fungu 25 – Waziri Mkuu, Fungu 27 – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 42 – Mfuko wa Bunge, Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Fungu 91 – Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevy na Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge na Taasisi zake yalitolewa na Waziri Muhusika. Pamoja na mambo mengine, Kamati ilielezwa kuhusu Makusanyo ya Maduhuli hadi kufikia Mwezi Aprili, 2010 pamoja na matumizi kwa mafungu yote kama nilivyoyataja tangu awali. Aidha, Kamati ilielezwa changamoto zilizoikabili Ofisi hii na Taasisi zake katika utekelezaji wa majukumu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati iliridhika na namna Ofisi ya Waziri Mkuu ilivyotekeleza majukumu yaliyoombewa fedha katika Mwaka wa fedha wa 2009/2010 kwa mafungu yote ya Ofisi ya Waziri Mkuu kama ilivyoolezwa na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua Bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka 2009/2010, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ya utekelezaji na utendaji kazi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa sehemu kubwa ya ushauri wa Kamati ulizingatiwa na kufanyiwa kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, mbali na kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge na Taasisi zake kwa mwaka uliopita, Kamati ilipokea maelezo ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2010/2011, yakiwemo matarajio. Aidha, Kamati ilielezwa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge pamoja na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati na kwa kuzingatia dhima, azma ya Serikali na majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kamati inatoa maoni na ushauri kwa Ofisi hii na Taasisi zake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Fungu 25 - Waziri Mkuu na Fungu 37 Ofisi ya Waziri Mkuu, Kamati ilipendekeza yafuatayo:-

(i) Pamoja na ufinyu wa bajeti, bado sababu za Kuhamishia Makao Makuu Dodoma ni za msingi na zinahitaji kuzingatiwa. Kamati inashauri kuwa azma ya dhati ya kuhamia Dodoma iendelee na utekelezaji wake uharakishwe ipasavyo. Aidha, Sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu ipitiwe na kurekebishwa ili kuondoa kasoro na migongano baina ya *CDA* na *Manispaa* ya Dodoma;

(ii) Ili kuongeza Ufanisi wa Idara ya Maafa, kasi ya mchakato wa kuibadilisha Idara hii kuwa Taasisi ya Umma au Mamlaka inayojitegemea iongezwe; na

(iii) Pamoja na kuipongeza Serikali kwa uamuzi wa kujenga Jengo la Makao Makuu ya Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali Mkoani Dodoma, Kamati inashauri kuwa Serikali itoe maelekezo kwa Taasisi za Umma ili zilazimike kuipelekea kazi Idara hii na ziache mtindo wa kuchapisha kazi zao kwenye Taasisi binafsi.

Mheshimiwa Spika, Fungu 27 - Msajili wa Vyama vya Siasa. Hivi karibuni Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Gharama za Uchaguzi na kusainiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kamati inashauri kuwa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, isimamie utoaji wa elimu ya kutosha kwa wadau na wananchi wote kwa ujumla kuhusu Sheria hii. Aidha, kwa kuwa tuna Tume ya Kurekebisha Sheria nchini, Kamati inashauri kuwa Ofisi ya Msajili kwa kushirikiana na Tume hii wahakikishe kuwa Sheria husika inatafsiriwa kwa Kiswahili na kusambazwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Fungu 42 - Mfuko wa Bunge, Kamati ilipendekeza yafuatayo:-

(i) Pamoja na kuipongeza Ofisi ya Bunge kwa Mpango Mkakati uliozinduliwa kwa mwaka wa Fedha 2009, Kamati inashauri kuwa ni vizuri malengo hayo yakatekelezwa kadiri ilivyopangwa angalau hatua kwa hatua; na

(ii) Sekretarieti ya Bunge iendelee kuimarishwa zaidi katika vitendea kazi, teknohomaa na miundombinu ya kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, Fungu 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Kamati ilipendekeza yafuatayo:-

(i) Tume iendelee kujipanga vizuri katika kusimamia uchaguzi ili uwe wa haki, huru, amani na utulivu. Aidha, vifaa kwa ajili ya uchaguzi, usafiri pamoja na fedha za kuwalipa wasimamizi vifanyiwe maandalizi ya kutosha na yanayokidhi haja; na

(ii) Changamoto zote zilizojitokeza wakati wa uchaguzi Mkuu 2005 zifanyiwe kazi ili kuongeza ufanisi na kuboresha mchakato mzima wa uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Fungu 91 - Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Ili kukabiliana na athari za matumizi ya dawa za kulevya, Kamati inaishauri Tume kama ifuatavyo:-

(ii) Kuongeza kasi katika utaratibu wake wa kutoa elimu kuhusu athari za madawa ya kulevya; na

(iii) Kubuni mbinu mpya ya kuwashawishi watu hususan vijana wanaotumia dawa za kulevya waone kuwa ni kitu cha hatari na cha kuachwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ushauri huo, Tume hii iongezewe bajeti ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Fungu 92 - Tume ya Kudhibiti UKIMWI. Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya Tume hii ili iweze kufanikisha kuandaa mkakati wa Sekta mbalimbali za kitaifa za kukabiliana na kukua kwa athari ya virusi vya UKIMWI. Aidha, mtiririko wa fedha kutoka Hazina kwenda Tume hiyo uende kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa – TAMISEMI. Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi. Tarehe 3 – 4 Juni, 2010, Kamati ilikutana Dar es Salaam ili kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Katika kikao hicho, Kamati ilipokea maelezo ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii kwa Mwaka 2009/2010 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2010/2011. Maelezo hayo yaliwasilishwa na Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa akisaidiwa na Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri, (Mb) - Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo ya Mheshimiwa Waziri, Kamati pia ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu kwa Mwaka 2009/2010 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mikoa kwa Mwaka 2010/2011 kwa mafungu 70 – 89 na Fungu 95, yaliyowasilishwa na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2009/2010. Pamoja na maelezo kuhusu mpango mkakati, Dira, Dhima na Majukumu ya Ofisi hii, Kamati pia ilielezwa kazi zilizofanyika kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010. Aidha, Mheshimiwa Waziri alifafanua kuhusu kazi ziliyofanyika kwa Kipindi cha Julai hadi Aprili, 2010 na changamoto zilizojitokeza katika kipindi cha utekelezaji wa Mipango ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Halmashauri nchini.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka 2009/2010. Wakati wa kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii na Mikoa kwa Mwaka 2009/2010, kama ilivyo ada, Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala

ilitoa Maoni na Ushauri Mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba tena kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia ushauri uliotolewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezwa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa Mwaka 2009/2010. Kamati ilifahamishwa kazi mbalimbali zilizopangwa kufanyika Mwaka 2010/2011. Maeleo hayo yalihusu Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI (Fungu 56) pamoja na Mikoa na Halmashauri zote (Fungu 70 - 89 na 95). Aidha, Mheshimiwa Waziri alifafanua kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mafungu yote.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia dhima, majukumu na mipango ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, kiwezeshwe kifedha ili kiweze kutoa mafunzo, kufanya utafiti na ushauri elekezi na kuendelea kufanya kazi nzuri ya kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuwashudumia wananchi;

(ii) Serikali iache baadhi ya vyanzo vya mapato kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuziongezea wigo wa mapato na kuziwezesha kutoa huduma bora kwa wananchi;

(iii) Ofisi ya Waziri Mkuu itoe maelekezo kwa Mikoa ambayo tabia yake ya nchi inawezesha kustawi kwa Mtama ili Mikoa hiyo ihmize kilimo cha Mtama pamoja na mazao mengine;

(iv) Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, ihmize Mikoa kuwasilisha kwa wakati Ofisi ya Waziri Mkuu, Taarifa za utekelezaji wao ili zifanyiwe kazi ipasavyo;

(v) Serikali iongeze kasi katika kushughulikia suala la Mfuko wa Barabara (*Road Fund*) kuongezwa kutoka asilimia 30 ya sasa hadi angalau asilimia 40 ili kuongeza uwezo wa kufanya matengenezo ya Barabara na hasa Vijijini;

(vi) Halmashauri nchini zihimizwe kupeleka watumishi wao Chuo cha Serikali za Mitaa kwa mafunzo mahususi yanayohusu Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(vii) Ili kuboresha utendaji kazi wa pamoja, uwajibikaji wa pamoja na Uongozi wa pamoja baina ya Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa na baina ya Watendaji na Madiwani, ni vyema suala la mafunzo kwa Madiwani likatekelezwa mapema mara baada ya Uchaguzi;

(viii) Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI iweke mkakati madhubuti ili kuepuka kutokea kwa tatizo la mlundikano wa madeni ya Walimu;

(ix) Katika kusimamia misingi ya Utawala Bora, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, ijitahidi kushughulikia vyanzo vyta uvunjaji wa haki za Binadamu na ukiukwaji wa misingi ya Utawala Bora unaojitokeza katika baadhi ya Wilaya na Vijiji nchini; na

(x) Wakuu wa Mikoa na Wilaya nchini wajipange vizuri kuhakikisha kuwa hali ya usalama nchini inaendelea kuwa shwari wakati wa Uchaguzi Mkuu ili demokrasia ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adhimu kuwasilisha maoni ya Kamati yangu. Kwa kuwa hii ni hotuba yangu ya kwanza katika Mkutano huu wa mwisho na wa Ishirini wa Bunge, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, nakupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge hili la Tisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sote ni mashahidi kuwa umekuwa na umahiri na uhodari mkubwa katika kuhakikisha kuwa Bunge linazidi kuwa chombo muhimu cha uwakilishi wa wananchi, kinachobeba matazamio ya wananchi na chenyeye uwezo wa kukidhi utashi wao wa maisha bora katika mazingira ya Uhuru, Amani, Usawa na Umoja. Kwa hakika, Uongozi wako ukisaidiwa na Mheshimiwa Anne Makinda, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, umeliwezesha Bunge la Tisa kuwa Bunge halisi la Wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwanza, kwa jinsi anavyosimamia na kufuatilia kwa karibu shughuli mbalimbali zinazotekelizwa na Wizara zote. Uongozi wake kwa kipindi chote umesaidia kuweka mambo mbalimbali katika hali iliyo sawa na inayotakiwa. Pili, namshukuru kwa ushirikiano wake mkubwa kwa Kamati yangu kwa muda wote hususan wakati wa uchambuzi wa Bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia Mheshimiwa Phillip S. Marmo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge na Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa nchini, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Taasisi, Idara na vitengo pamoja na Maafisa wake, kwa maelezo na ufanuzi wa kina na walioutoa kwa Kamati.

Mheshimiwa Spika, kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio haya. Umahiri na uzoefu wa muda mrefu katika nyanja mbalimbali za Sekta ya Umma, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, ndio

uliofanikisha kazi hii. Kwa heshima kubwa, naomba niwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti na Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Makamu Mwenyekiti. (*Makofi*)

Wajumbe wengine ni Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Stephen Jones Galinoma, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa John Paulo Lwanji, Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mheshimiwa Yusuf Rajabu Makamba na Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu. (*Makofi*)

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru Ndugu Charles Mloka, Mkurugenzi wa Kamati za Bunge, Ndugu Athuman Hussein na Elihaika Mtui, Makatibu wa Kamati hii kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mpwapwa, kwa imani kubwa waliokuwa nayo kwangu na kunipa ushirikiano unaoridhisha ambao mara zote umesaidia kufanikisha utekelezaji wa majukumu yangu bila kuwaangusha. Naamini ushirikiano huu unaendelea.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zake jumla ya shilingi 2,973,221,260,000/-. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,107,701,783,000/- ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 865,519,477,000/- kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati. Waheshimiwa Wabunge, ninaomba mtambue uwepo wa Mheshimiwa Mama Tunu Pinda ambaye amejiunga nasi, karibu sana, tunathamini unapokuja hapa kuangalia shughuli zetu, ahsante na ubarikiwe sana. (*Makofi*)

Namwita sasa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu mambo ya Sekta ya Utawala, Mheshimiwa Dr. Willibroad P. Slaa. (*Makofi*)

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA - MSEMADI WA UPINZANI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuwasilisha Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Hotuba ya Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za

Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Fedha, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kifungu cha 99(3) (7) , Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, naomba nitamke kwamba, haya ni maoni ya Kambi ya Upinzani na nasema hili ili lililotokea jana lisitokee, maoni ya Kambi ya Upinzani si ya Vyama wala si ya mtu, ni maoni ya Kambi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuwashukuru sana wananchi na wapiga kura wangu wa Wilaya ya Karatu ambao kama kawaida wameendelea kuniunga mkono wakati wote, kwa njia mbalimbali na hasa kwa mshikamano wao wa kuijenga Wilaya yetu. Nawashukuru sana na hasa kwa kuionyesha Tanzania nzima kuwa kumbe maendeleo yanawezekana hata bila CCM. Nachukua fursa hii, kuwahakikishia kuwa nitaendelea kuwatumiwa kwa akili, moyo na uwezo wangu wote. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia, kuwashukuru Watanzania wote kutoka kona zote za Tanzania wenye mapenzi mema ambao kwa maelfu wameendelea kutuunga mkono na kujifunza kutoka Karatu katika jitihada zao mbalimbali za kujiletea maendeleo. Kwa wapenzi wetu wote, Mwenyezi Mungu awarudishie mara mia kwa upendo wenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa nimekosa fadhila iwapo sitatoa shukrani kwa Chama changu CHADEMA, chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Freeman Mbewe, Mwenyekiti wa Taifa. Chadema ndio kimeniwezesha kufika hapa Bungeni. Kwa waliofikiri kuwa Ubunge unapatikana kwa njia ya CCM tu, natumaini wameona kuwa Ubunge unapatikana pia kuitia Kambi ya Upinzani. Watanzania waache tu hofu na uwoga, Tanzania ni yetu sote. Vyama vyote vya siasa ni “milango na madirisha”tu ya kuwahudumia. Haitoshi kulalamika kila mwaka, mabadiliko yanawezekana kila mmoja akifanya na kutimiza wajibu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Kambi ya Upinzani wakiongozwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kwa msaada walionipa wakati wote katika kipindi chote cha miaka mitano tunayoelekea kumaliza sasa kama Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Pinda, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Celina O. Kombani, Mawaziri wa Nchi na Naibu Waziri na Makatibu Wakuu kwa kuandaa Bajeti hii, wakisaidiana na Wataalam wao wote na kwa ushirikiano walionipa wakati wote katika utekelezaji wa majukumu yangu mbalimbali hapa Bungeni na kwa Jimbo langu la Karatu.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge letu Tukufu na kuliweka katika medani ya Kimataifa kwa ubora, uongozi wa kasi na viwango vya juu na kuwa kielelezo cha kweli cha demokrasia katika nchi. Ninamwomba Mwenyezi Mungu awajalie hekima na busara na kuwapatia nguvu na afya mnazohitaji katika kuliendesha vizuri Bunge letu hasa katika kipindi hiki cha lala salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ni bajeti ya Tano na ya mwisho kwa Serikali ya Awamu ya Nne. Kwa kuwa, hii ni Hotuba yetu ya mwisho kwa Bajeti hii, tutafuata zaidi mfumo wa tathmini ya utendaji wa Serikali kwa kutathmini bajeti hii na Bajeti zilizopita za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kazi ya msingi ya Kikatiba ya Kambi ya Upinzani, siyo kuipigia Makofi Serikali ya Chama Tawala bali kuangalia zaidi upungufu katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kuwaonyesha wananchi kwa nini waendelee kuichagua Serikali iliyoko madarakani au kwa nini wasiiondoe kwa njia ya sanduku la kura kama hawajaridhika na utendaji wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanahitaji pia kuonja yale yanayopendekezwa kutolewa na vyama vingine. Huu ndio mchezo wa demokrasia japo katika demokrasia “changa” ukitamka hivyo wengine wanaona huo ni uhaini. Tathmini yetu itafuatiliwa na maoni ya Kambi ya Upinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, iwapo Vyama vya Upinzani vitaipigia Makofi Serikali ya Chama Tawala, basi vyama hivyo vitakuwa wasindikizaji tu siku zote, wakati na lengo lenyewe la kuvisajili ni kutengeneza ushindani wa sera na utendaji katika kuwaletaa matumaini mapya wananchi kwa njia ya uchaguzi wa mara kwa mara na pale Chama Tawala kinaposhindwa kutekeleza matumaini ya wananchi, wakiondoa kwa njia ya uchaguzi na kujaribu Chama kingine. Ndio maana ya utajiri wa Vyama vya Siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, demokrasia yetu sasa siyo changa tena baada ya miaka takriban 20 ya Mfumo wa Vyama Vingi, hivyo wananchi wana uwezo wa kuona, kutafakari na kufanya maamuzi yao wenyeewe kutokana na taarifa sahihi wanazopata. Wananchi baada ya miaka takriban 50, wamekwisha kuona jinsi kila kukicha wanavyoendelea kuwa masikini na wakati huo huo wamekwishakuona na kuonja baadhi ya matunda ya Mfumo wa Vyama Vingi japo kwa uchache.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii inalenga kutoa ufanuzi katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwaonyesha wapi Chama Tawala kimeshindwa kufikia malengo yake na wapi Upande wa Upinzani, japo hauna Serikali umeweza kuisukuma Serikali kwa kiwango cha kuwafanya wananchi kunufaika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa miaka minne iliyopita Kambi ya Upinzani, imekuwa ikichangia mawazo mbadala kwa kina na kwa mapana. Lengo ni kutoa mchango wetu katika kuleta maendeleo katika nchi yetu na kumnufaisha mwananchi wa kawaida. Hii ingewezezana tu iwapo Serikali ingelikuwa sikivu na kutekeleza ‘vizuri’ angalau baadhi ya ushauri na au kuchukulia hatua baadhi ya mambo ambayo Kambi ya Upinzani imekuwa ikishauri.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid, imezungumzia kwa kirefu upungufu wa kibajeti na kupendekeza Bajeti mbadala ya Kambi ya Upinzani. Sipendi kuyarudia hayo yote.

Mheshimiwa Spika, Kauli, Sera na Ilani ya Chama Tawala inapimwa kuitia vigezo vya Bajeti na utekelezaji wa Bajeti hiyo kwa kila mwaka. Vigezo vya kisiasa haviingii sana katika upimaji huu, kwani kama kauli mbiu ni “Maisha Bora kwa kila Mtanzania” basi tathmini yetu itajikita kama kweli katika kipindi cha miaka mitano Maisha Bora yamepatikana kwa kila Mtanzania au la! Vigezo muhimu katika hali hiyo ni vya kawaida kabisa yaani hali ya kawaida ya maisha ya mwananchi inavyokua.

Mheshimiwa Spika, katika tathmini hii pia nitatumia taarifa ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha aliyoitoa Machi, 2010 kwa vyombo vya habari akitoa tathmini ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM), akielezea mafanikio ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nne, Desemba, 2005 hadi Desemba 2009.

Mheshimiwa Spika, tathmini hiyo inakiri kuwa Serikali haijafanikiwa kutimiza malengo mengi yaliyokusudiwa, muda hautoshi ningeweza kufafanua yote.

Mheshimiwa Spika, mathalan, wananchi wengi wameacha kunywa chai kwa vile sukari sasa imekuwa bidhaa ya anasa wastani wa Tshs 1,200/= hadi 1,800/- wakati mwaka 2005 ilikuwa Tshs.500/= hadi 600/=, mikate iliyokuwa kimbilio la walala hoi hasa mijini imekuwa haishikiki tena kwa vile bei ya mkate unakimbilia Shs .,500/= hadi 2,000=/. Nyama inazidi kuwa hadithi ya kusadikika kwa Watanzania wengi kwani bei ya kilo inakimbilia zaidi ya Shs.4,500-5,000/- katika maeneo mengi mchele ambao ukiacha mahindi unakuwa chakula cha Watanzania wengi unakimbilia Tshs.1,500/ kwa kilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hali inakuwa ngumu pale ambao bei ya kila kitu imepanda maradufu, na kipato cha Mtanzania kimebaki pale pale na nguvu ya Mwananchi kununua nayo ikishuka kwa kasi kubwa kutohana na kuperomoka kwa thamani ya Shillingi ya Tanzania. Serikali makini ni ile isiyotafuta visingizio bali hutafuta kila siku namna ya kupunguza makali hayo kwa wananchi wake. Kuna msemo unaosema “*All Politics is local*” visingizio vya hali ya uchumi wa dunia, ukame, kuperomoka kwa thamani ya shilingi hauwahusu wananchi, kwani walijajiri Serikali kwa lengo pekee la kushughulikia matatizo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pale Serikali inaposhindwa kupunguza makali hayo ndio inaitwa “Serikali imeshindwa kulinda maslahi ya ndani ya Wananchi wake”. Katika hali hii Taarifa za Serikali za kuwa wastani wa kipato cha Mtanzania (*per capita*) kwa mwaka 2008 ni Tshs. 682,737.7/= inapoteza maana. Watu wenyewe kipato hicho wasingelishindwa kununua angalau sukari na mchele! Hata hivyo, Watanzania wenyewe ndio wanajua kama wanapata kipato hicho au hizo ni takwimu za vitabuni tu! (Taarifa ya Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha). (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tamko la Serikali la Uchumi kukua litakuwa na maana tu iwapo Watanzania wanapata chakula vizuri, wanalala vizuri, mishahara ni mizuri, lakini si kwa vitabu kuonyesha takwimu kubwa kubwa za uchumi kukua. Wananchi hawali takwimu za vitabuni, wanahitaji mahitaji yao muhimu kwa maisha yao ya kila siku. Kwa kigezo hiki ni dhahiri Serikali ya Awamu ya Nne, imeshindwa kukidhi kigezo muhimu cha kuwapatia Watanzania maisha bora katika miaka minne iliyopita. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lazima Bunge kama mwakilishi wa Wananchi lichukue nafasi yake kusimamia maslahi ya Watanzania na kulinda haki zao, kwa kusimamia vizuri fedha, mali na rasilimali za nchi yetu. Wabunge ni Wawakilishi, lakini huku vijijini kuna baba zetu, mama zetu, dada zetu, kaka zetu, shangazi zetu na kadhalika. Wao ndio wanaojuja jinsi maisha yalivyo magumu na ndio wanaotupima kwa vigezo vyâ bei nilizotaja hapo juu.

Mheshimiwa Spika, Dola moja ya Marekani inayokubalika Kimataifa kama kigezo cha umaskini wa kutupwa na kwa msingi huu tukiwa wa kweli katika takwimu zetu. Watanzania wengi zaidi ya asilimia 16 iliyotajwa katika kitabu cha hali ya uchumi, watakuwa katika kundi hili ambalo haliwezi tena kula nyama, kununua sukari, kununua mchele na hata maharage kilo sasa ni zaidi ya Shs 1,000 hivyo hata chakula ambacho ni cha mtu wa chini sana watashindwa kokinunua. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, haya ni maisha magumu, ni magumu sana kwa Watanzania hao kwa kigezo chochote kile na hayajawahi kutokea katika historia ya Tanzania tangutupate uhuru. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hili si suala la kisiasa. Maisha Bora licha ya chakula ni pamoja na kujua kama kila Mtanzania amepata mlo wa uhakika, amelala mahali pazuri, amepata huduma nzuri, hasa Afya na Elimu, na huduma zote za kijamii zinazostahili kutolewa na Serikali. Maisha Bora ni pamoja na kuona kama hali ya Mtanzania ya uchumi imeboreka kwa kiasi gani katika kipindi kinachotathminiwa. Hivi ndivyo vigezo tutakavyotumia katika tathmini hii na ninaamini hili ni jukumu letu la Kikatiba. Watanzania nao wana haki ya kujua mustakabali wa nchi yao kwa kusikiliza upande wa pili wa shilingi bila ushabiki wa kivyama au kisiasa tu.

Mheshimiwa Spika, wananchi hawali siasa, bali wanahitaji kitu cha kuingia kwenye matumbo yao waweze kuishi vizuri kama binadamu, wanahitaji mahili pazuri kujikimu japo siyo maghorofa ambayo hata wengine hata kuyaona tu hawaajaona wala hawatarajii kuyaona. Kigezo kingine cha kupima maendeleo ni kupima tulikotoka, tuliko

leo na hasa katika tathmini ya miradi mbalimbali ya maendeleo pamoja na kigezo cha kipato binafsi ambacho kinamgusa mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, ni vema tukaeleweka vizuri. Si kwamba tunapotoa tathmini hii hatuoni mambo yaliyofanywa na Serikali zetu chini ya TANU/CCM/ASP tangu tulipopata uhuru. La hasha! Tunachosema ni kuwa kwa rasilimali tulizonazo tungeliweza kufanya zaidi sana, tungeliweza kufanya mambo mengi bila kumbughudhi mwananchi kama tungeliweza kulinda vizuri rasilimali tulizonazo na kuzielekeza vizuri kwenye maeneo muhimu yanayomnufaisha mwananchi.

Mheshimiwa Spika, huu ndio mgogoro siyo kwamba Kambi ya Upinzani haina macho kuona yaliyofanyika. Lakini kwa nini tupoteze muda kuzungumzia vitu ambavyo kila mmoja anaona na wengi tunakubaliana kuwa havikidhi hali? Ndio maana kila mara tumesema kuwa vipaumbele vya Serikali vina kasoro na hata pale inapoonekana fedha zinasemekana zimetengwa, kimatendo hali siyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu na hata Mheshimiwa Waziri wa Fedha, katika hotuba yake Kifungu cha 38 cha Hotuba, anaweka bayana Misingi na Shabaha za Bajeti kwa mwaka 2010/2011. Baadhi ya misingi hiyo ni pamoja na kuendelea kuboresha mfumo wa makusanyo ya mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na kupanua wigo wa mapato kwa kuhusisha vyanzo vipyta; kuimarisha udhibiti na usimamizi wa mapato kutoka vyanzo mbalimbali; kuendelea kuchukua hatua ya kudhibiti misamaha ya kodi ili kuongeza mapato; kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa kauli mbiu ya Kilimo Kwanza na kuanzishwa kwa vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kauli hii ya kisiasa ni kauli tamu sana katika masikio ya Watanzania. Kwa bahati mbaya, Watanzania wengi wanafikiri Bajeti ni Hotuba ya Waziri na kwa kawaida hawafanyi utafiti wa kina kujua kauli hii ya Waziri inatafsiriwa vipi katika takwimu za kibajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine, tena napenda kuwashauri sana Watanzania, kabla ya kuipongeza au kuichanachana bajeti, ni vizuri wakaangalia takwimu za kibajeti yaani fedha zimetengwa kiasi gani na kwa ajili ya nini, taarifa ambayo inapatiikana katika kitabu cha kwanza hadi cha Nne cha Vitabu vya Bajeti ambacho wananchi hawana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hotuba hii inachanganua kama kweli vitabu vinaonesha ongezeko kubwa na kama ongezeko hilo linaendana na anguko la thamani ya shilingi ya Tanzania. Nitatoa mifano michache kuona kama Kauli hii tamu ya kisiasa inawiana na kilichoko katika vitabu vya Bajeti. Kitabu cha Nne, *Public Expenditure Estimates Development Votes*, kwa mfano mwaka 2009/2010, Wizara ya Kilimo ilitengewa Jumla ya Tshs.92,694,254,000/= na mwaka 2010/2011 imetengewa Tshs.103,952,371,000/=.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna ongezeko la Tshs.11,258,117,000/= lakini ikumbukwe kuwa mwaka 2009/2010 Dola ya Marekani ilikuwa inabadilishwa kwa \$1= Tshs 1200, leo \$ 1 ni sawa na Tshs.1,450. Hivyo, uwezo na nguvu ya manunuzi ya Shillingi imeshuka kwa zaidi ya Tshs. 250 hivyo kwa fedha hizo kazi unazofanya inaweza kufanana na zile za mwaka jana au hata chini ya hapo.

Mheshimiwa Spika, muhimu zaidi ni kuona fedha hizo zimetengwa hasa kufanya kazi gani ndani ya kilimo na je zitakazofika kwa mkulima kufanya shughuli za kilimo hasa ni kiasi gani? Kasma ya 43 ndiyo inayojibu swalii hili. Kifungu kidogo cha 2002 ndicho kinatengewa fedha kwa ajili ya vifaa vya kilimo (*Agricultural Mechanization*), Tshs.497,850,000/= tu. Leo hii hapa ndiyo tunasikia kutoka kwa Waziri Mkuu milioni 40 za dola zilizokopwa, takwimu hizi haziko kwenye vitabu vya bajeti. Hii ndiyo inatufanya tushindwe kusimamia bajeti za Serikali. Hii ni sawa na trekta moja tu kwa bei ya 38,000,000/= kwa Halmashauri zote 133 kama zote zingeelekezwa kununua trekta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *ASDP* ambayo inaonyesha kuwa kwa shughuli za *ASDP* ambayo ndio yenyeye kunufaisha kilimo mmoja kwa mmoja ni Tshs.97,595,807,000/= tu. Matumizi mengine ni Tshs.149 Billioni, jambo ambalo linafanya matumizi mengine kuwa makubwa kuliko hata ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kabisa hiki ni kiwango kidogo sana katika jumla ya Bajeti ya trillioni 11. Uwiano huu hauonyeshi dhahiri kuwa Kauli ya Kilimo Kwanza haioani na fedha zilizotengwa. Vivyo hivyo kwa kutazama Kasma zilizotengwa chini ya Halmashauri za Wilaya nazo hazonyesi uwiano huo.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa vipaumbele makini ndio kunakoitafuna nchi yetu. Serikali isiyoweka vipaumbele kwa wananchi wake, ni dhahiri ni Serikali isiyojali wananchi wake. Mfano halisi ni msamaha kwa Makampuni makubwa ya Madini, wakati inawatoza wananchi wake waendesha Pikipiki na Bodaboda ambao wanafanya biashara ya kujitafutia tu chakula. Wakati imetoa misamaha mikubwa ya zaidi ya Billioni 700, lakini wafanyakazi wake inawaondolea kodi ya asilimia moja tu ambayo ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, hivyo hoja ya kwamba Serikali haiwezi kuongeza mishahara haina tija na wala si ya kweli kama kweli Serikali ingelipanga vizuri vipaumbele vyake. Taarifa kamili kuhusu mishahara itatolewa na Waziri wetu kivuli wa Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, Mapato ya Serikali, yaani jumla ya Makusanyo yote yanaonekana katika kitabu cha Kwanza yaani “*Volume 1 Financial Statement and Revenue Estimates*” (for the Year from 1<sup>st</sup> July, 2010 to 30<sup>th</sup> June, 2011), ambayo sasa tunagundua kumbe si yote yameandikwa humo, haya mengine sijui yako wapi na yanadhibitiwa na nani! Makusanyo yote yameonyeshwa kwa mfumo wa asili na miaka yote mfumo huu unafanana. Kitabu hiki kinaonyesha kuwa *Vote 21 ‘Hazina’ Trillion 5.4* ya mapato yote yatapatikana kwa njia zile za kawaida, Bia, Sigara, Vinywaji Baridi vinaonyeshwa kuwa ndio vilivyongezewa kodi. Vivyo hivyo kodi ya kuingiza vitu chini *Exercise Duty, Custom Duty* na kadhalika na Kodi ya Mauzo na hata Kodi ya Magari.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi huu na Taarifa za *TRA* zinaonyesha kuwa sehemu kubwa ya kodi inalipwa na Wafanyabiashara (wenye *TIN*) wasiozidi, 570,000 kwa nchi nzima na kati ya hao asilimia zaidi ya 75 wanatoka Dar-es-Salaam. Wafanyakazi wa Serikali na Sekta Binafsi wanaolipa kodi ni takriban 1,000,000/=. Hao ni kati ya watu milioni 40 wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hivyo mzigo mkubwa wa kodi unabebwa na idadi ndogo sana ya Watanzania. Huo ndio mfumo uliokuwepo siku zote na unaendelea kuwa hivyo. Ni dhahiri maneno matamu yaliyoko katika Hotuba ya Serikali ya kupanua wigo wa mapato hayako kwa matendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wala Serikali haionekani kutafuta kodi kwenye maeneo mapya ambayo yangelipunguza sana mzigo wa kodi kwa walipa kodi wachache ambao kila mwaka wanabebeshwa mzigo huo huo au wananchi ambao ndio walaji wa mwisho kila mwaka kubebeshwa mzigo wa kulipa kodi kupitia mfumo wa VAT.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake ni kuwa watu wachache sana wanaendelea kubeba mzigo mkubwa lakini usiotosheleza mahitaji ya maendeleo na badala yake Taifa linazidi kuwa Tegemezi. Serikali ingelikuwa makini ingelifanyia kazi pendekero lake au kauli yake yenye, la kuwa na wigo mpana wa kodi, watu wengi zaidi wangeligawana mzigo na hivyo mzigo usionekane kumwelemea mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 21, Kifungu kidogo cha 2007 ambayo inahusika na Kodi ya Mapato, kwenye mapato, faida na ‘*Capital gains*’ inayoo nyesha Taifa linapata kiasi cha Tshs Billioni 463,070,200.00 tu. Kodi kutoka kwa Wafanyakazi takriban Tshs.1,000,000 inakisiwa kuwa Tshs.44,325,000.00. VAT kwenye huduma mbalimbali itaingizia Taifa kiasi cha Tshs.229,822,900.00, wakati Kodi kwenye biashara ya nje inategemewa kuingiza tu kiasi cha Tshs.96,394,800.

Mheshimiwa Spika, kwa nchi inayoingiza karibu kila kitu hata sindano ya kushona “vifungo” vya nguo, ni dhahiri kabisa kuwa kiasi hiki ni kidogo sana na inaashiria mambo mengi ikiwa ni pamoja na *under-declaration, under-invoicing* na au udanganyifu wa wazi na viashiria vya rushwa katika idara husika.

Mheshimiwa Spika, aidha, Watanzania wengi wanafikiri kuwa kodi pekee mwaka huu ni zile zilizoko kwenye kodi iliyopanda ya Sigara, Bia na Vinywaji Baridi tu. Watanzania wengi hawana elimu ya kodi. Kodi za Vinywaji na Sigara zinakatwa toka kiwandani hivyo watu wengi hawajui kuwa wavuta sigara, wanywaji wa bia na soda ndio wenge kulipa hizo kodi.

Mheshimiwa Spika, hivyo ni muhimu Watanzania waelewe kuwa siku zote kodi kwenye sigara, bia na soda inapopanda, wao ndio wanaozilipa japo hawalipi moja kwa moja, kwani kodi hizo zinakuwa ndani ya bei ya sigara, bia na soda na sukari. Lakini isitoshe, Watanzania wanalipa kodi kupitia VAT ya asilimia 18 yaani kwa kila Shs. 100 wanalipa kodi ya Shs.18 Serikalini kupitia gharama za simu za mikononi na gharama

zingine zote wanazozitumia ambazo sasa watumiaji wake wanakadiriwa kuwa 18 milioni. Wanaponunua sukari, kanga, shati, suruali, daima wanalipa kodi na hizi ndizo zinazoitwa *indirect taxes* yaani kodi isiyo ya moja kwa moja na mtu anailipa bila kujua analipa kodi. Wananchi wengi bila kujua wanalipa *Exercise Duty* kwenye bia, soda, sigara na sukari. Sasa haya yote yanapandisha bei ya bidhaa zetu. Jambo ambalo Watanzania hawajeleta ni kwamba kodi inayopandishwa katika bidhaa wao ndio wanaolipa, wafanyabiashara wao ni njia ya kuikusanya Serikali fedha hizo tu.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa mara kwa mara kwa kodi kwenye vinywaji, kunawalazimisha wananchi wengi wageukie vinywaji vyta kienyeji na hasa Gongo (Moshi, Changaa au kwa jina lolote inayojulikana), pombe ambayo siyo tu kwa sheria zetu ni harama lakini pia ni hatari kwa afya za raia wetu.

Mheshimiwa Spika, aidha asilimia 18 ya ushuru kwenye mafuta, kwenye karatasi imendikwa 20, asilimia 18 ya ushuru kwenye mafuta aina ya petroli, diesel – Kifungu cha 21 kifungu kidogo cha 2), nayo inamuathiri moja kwa moja mwananchi wa kawaida kwa kuwa bei ya petroli nayo itaendelea kuathiri gharama za usafiri na usafirishaji wa bidhaa mbalimbali, ikiwa ni pamoja na usafiri wa binadamu. Ni kweli kuwa bei ya Mafuta (Petroli na Diesel) katika soko la dunia nayo imepanda kwa mara nyngine tena. Serikali yetu imeshindwa kubuni namna ya kukata makali hayo kwa njia bunifu kama vile “*Stabilization fund*” ambayo nchi nyngine zinafanya. Tanzania tumeachia mzigo wote kwa mlaji wa mwisho ambaye kwa bahati mbaya asilimia 98 ni wananchi wa kawaida wa mijini (wakiwemo wafanyakazi ambao mshahara wao ni kiduchu mno) na wa vijiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi sasa wananchi wengi wamepata mwamko wa kujenga nyumba za kisasa na kuondokana na hali mbaya ya nyumba, za majani, udongo, na kadhalika. Mwamko huo unapata kikwazo kikubwa kutokana na bei ya bati, cementi na misumari kuendelea kuwa juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu ingeliweza kupunguza makali haya kwa kupunguza asilimia 18 ya VAT angalau ishuke kidogo kuwa 16 kulingana na nchi nyngine za Afrika Mashariki, katika bei ya bati, cementi, nondo na hata misumari. Kodi na ushuru mbalimbali kwenye vifaa hivyo ikiwa ni pamoja na bidhaa za mbaao za ujenzi, ingepunguzwa. Kwa mtindo huu, japo kuna dalili ya kuendelea na ujenzi, ni watu wenye hela ndio wenye uwezo wa kujenga na Watanzania walio wengi wataendelea kuwa watazamaji katika shughuli za maendeleo bila maendeleo ya mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, kitakwimu inaonekana fedha nyngi sana zinaenda kwenye miradi mbalimbali hasa ngazi ya Wilaya. Maswali mengi ya kujiuliza ni kama tunapata thamani halisi ya fedha zinazoelekezwa kwenye miradi hiyo? Isitoshe, Maneno, Usimamizi na Udhhibiti yaliyotamkwa mwaka huu kama ilivyo miaka mingine yamekuwa wimbo wa kila Siku.

Mheshimiwa Spika, taarifa za CAG za kila mwaka, ni ushahidi wa wazi kuwa Serikali pamoja na kutamka maneno haya matamu, imeshindwa kutekeleza lengo lake

hili. Taarifa za kila mwaka zinaonyesha upotevu wa mabilioni ya shilingi, lakini hakuna hatua madhubuti zinazochukuliwa, kama zinachukuliwa za sirisiri sisi hatujui na ni jukumu la Bunge kuzijua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, taarifa za *CAG* zinaongezewa nguvu na Taarifa za Kamati tatu za Bunge ambazo zimethibitisha matumizi makubwa na mabovu ya Fedha za Umma. Kwa mwaka wa Fedha wa 2008/2009 ambao ndio ukaguzi wa mwisho wa *CAG* na pia Kamati za Bunge za Hesabu, Kamati hizo zimetoa taarifa zake Bungeni na Serikali makini inatakiwa kuwa imeisha kuchukua hatua na watusika wa ubadhirifu, wizi na matumizi mabaya ya fedha za umma nao wanatakiwa kuwa wamechukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, kutokuchukua hatua kwa mapendekezo ya Chombo cha Kikatiba yaani Taarifa ya *CAG* ikipewa nguvu na Maazimio yanayotokana na Kamati za Bunge, ni udhaifu mkubwa sana kwa Serikali. Utashi wa Serikali wa kuchukua hatua, haujaonekana kama ulivyothibitishwa na utekelezaji wa Maazimio ya nyuma mathalan, aliyekuwa Balozi wa Tanzania Malawi aliyefanya *shopping* ya gari kwa kubeba fedha kwenye begi na kununua gari Dubai bila utaratibu wowote wa manunuzi ya umma (*tender*) na gari lenyewe likiwa limetembea zaidi ya kilomita 700,000. Gari hilo halikufanya kazi likarudishwa Dar-es-Salaam kwa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, Balozi huyo hatimaye aliishia kukatwa tu fedha kidogo tu wakati anastaafu. Taifa linapoteza mabilioni ya fedha na kisha linaendelea kuimba kuwa ni “Taifa Maskini”, linaenda kuomba fedha kwa wahisani lakini halichukui hatua kwa watusika wa ubadhirifu huo, japo hatua iliyochukuliwa katika Halmashauri ya Bagamoyo inatia moyo na hapa kwa namna ya pekee kwa mara nyingine ninapenda kumpongeza kwa dhati sana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo ambao wamesimamia vizuri zoezi hili. Ni imani yangu pia zoezi lililoanza katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza na Mkinga nayo itachukuliwa kwa umakini mkubwa na hatimaye watusika wote kufikishwa mbele ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambako tumeonyesha udhaifu mkubwa, ni pale ambapo Bajeti yetu Mwaka 2010/2011 siyo tu inaendelea kuwa tegemezi bali tumelazimika kukopa fedha kwa kinachoelezwa kuwa Wahisani wamejitoa kwa kuwa hatukutimiza masharti. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ni masharti yapi ambayo wahisani hao wameweka. Tanzania ni nchi ambayo tangu wakati wa Mwalimu imekataa kupewa masharti. Lakini je, masharti hayo ni ya aina gani? Ni vema Taifa likajua masharti hayo ili pia tufahamu ni nani hasa marafiki zetu.

Mheshimiwa Spika, lakini iwapo masharti hayo ni ya usimamizi wa uchumi wetu, hata Kambi ya Upinzani tutawaunga mkono kwani tusingelipenda uzembe, ufisadi wala wizi ndani ya Serikali yetu kwa manufaa ya Watanzania. Serikali ni Mtumishi wa Umma na ni lazima maadili ya uendeshaji wa Taifa yaheshimike kwa manufaa ya wote.

Mheshimiwa Spika, hatua ya kukopa mwaka huu ndani na nje tena kutoka vyombo nya kibiashara, si jambo zuri kwa uchumi wetu kwani inaashiria pia kuwa

tutapaswa kulipa kwa masharti ya kibiashara kama tunakopa kulipia mishahara (*Recurrent Expenditure*). Hali hii haikubaliki kabisa na kama hatua hiyo imefikiwa kutokana na uzembe wa Afisa kutotekeleza masharti yaliyokubaliwa. Ni vema Bunge likafahamishwa na Afisa huyo achukuliwe hatua zinazostahili kwa kuliingizia Taifa hasara ya shilingi takriban bilioni 200/=. Baadhi ya mikopo hiyo ni yenyé masharti yasiyo nafuu ya shilingi billioni 797,720/= (kufidia pengo lililotokana na wahisani kujitoa).

Mheshimiwa Spika, mikopo kwa shughuli za maendeleo, ni jambo la kawaida na Kambi ya Upinzani, haina pingamizi iwapo tu mikopo hiyo itasimamiwa na kutumika vizuri. Lakini kukopa kwa kuendeshea shughuli za Serikali yaani kulipa mishahara, posho mbalimbali, mafuta na kadhalika, si jambo linalokubalika hata kidogo. Mikopo mingi itakuja kulipwa miaka 30/40 ijayo hivyo si vyema kuwabebesha watoto na wajukuu zetu mzigo wa kulipia mikopo ambayo hawatakuwa wameonja matunda ya mikopo hiyo hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, kuna msemo wa mitaani kuwa “mbuzi hula kwa urefu wa kamba yake”. Iwapo Serikali imeona hakuna fedha kuititia njia za kawaida, wala misaada basi ilitakiwa kukata na kupunguza matumizi yake kuliko kuliingiza Taifa katika madeni ambayo hayana tija kwa Taifa. Madeni yote ya uendeshaji kwa kawaida hayana Tija.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana tulipiga kelele kuwa chai na vitafunio ofisini, vilikuwa na Bajeti kubwa kuliko hata fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mahakama Kuu kwa nchi nzima. Tunashukuru kuwa kilio chetu kimesikilizwa kwa kiasi fulani. Hata hivyo, kuna maeneo ambayo bado yangeliweza kupunguzwa zaidi, mathalan Kasma ya 410501, ununuvi wa Vyombo vya Nyumbani. Ni lazima Serikali itueleze ni kwa nini vyombo hivi vinanunuliwa kila mwaka na hata kama ni hivyo, mbona vilivyochakaa haivonekani kuingizwa kwa upande wa maduhuli ya Serikali kama mapato? Kuna mchezo gani hapa?

Mheshimiwa Spika, Serikali lazima iwajibike kwa wananchi na kutoa ufanuzi wa kina kunapotokea matumizi ya namna hii ambayo ni mabilioni kwa Serikali nzima. Mifano hai ni Ofisi ya Waziri Mkuu, Kasma ya 410501. Vivyo hivyo kwa kasma ya 410502, Ununuvi wa samani, mapazia na mazulia, kifungu ambacho nacho kinaenda kwenye mabilioni ya fedha.

Mheshimiwa Spika, hali hii bado iko kwenye Wizara na Idara zote, mathalan Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kasma ya 210503 kwa ununuvi wa chakula na viburudisho au kasma ya 410500 “*kitchen applicances, utensils and crockery*”. Swali la msingi ni kuwa vitu hivi vilikuwa kwenye Bajeti ya mwaka 2009/2010, je, ni kwa nini vinanuliwa tena kuititia bajeti ya 2010/2011? Iwapo ni hivyo vilivyochakaa vimekwenda wapi? Je, samani na hasa mazulia na fenicha zinachakaa kwa mwaka mmoja tu? Au watumishi wenye stahili wameongezeka? Iwapo hivi ndivyo, mbona Idara zimebakia zile zile? Kunahitajika maelezo ya kina.

Mheshimiwa Spika, hali hii haiwezi kabisa kukubalika katika nchi ambayo inakiri katika takwimu yake yenye kuwa watu zaidi ya 12.9 milioni wanaishi chini ya mstari wa umaskini (*below poverty line*) unaotambulika duniani (yaani ni maskini wa kutupa – ambalo ni ongezeko la watu 1,500,000 kati ya 2001/2008 (HBS 2007). Yaani tumekuwa na maskini wengi zaidi kuliko mwaka 2001. Hii ni hali ya kutisha na Serikali kwa takwimu hizi tu, inapaswa kuwa makini zaidi na kuondoa aina zote za matumizi ya anasa na kupanga mikakati imara zaidi ya kuwanyanya hawa ndugu zetu Watanzania milioni 12,9 ambaao ni maskini wa kutupa. Katika vigezo hivi vyote, ni dhahiri, Serikali ya Chama cha CCM haiwezi kusema kuwa imepata mafanikio. Ni ajabu kama kuongeza maskini, badala ya kufuta umaskini inaweza kuhesabika kama ni mafanikio.

Mheshimiwa Spika, kwa rasilimali na utajiri mkubwa tulionao, hali ya Mtanzania inatakiwa kuwa bora zaidi iwapo atawekewa utaratibu mzuri, mikakati mizuri ya ajira na matumizi bora ya rasilimali yenye kumjali zaidi mwananchi. Hali ya sasa ya matumizi ya rasilimali za Taifa haionyeshi dalili hiyo na tusipokuwa makini, madini, magogo yataisha na Taifa litabaki halina rasilimaili ya kuendeleza vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, je, tumefaulu katika kumletea Mtanzania Maisha Bora, ambayo ndio ilikuwa Kauli Mbiu nzito wakati wa Kampeni za Uchaguzi 2005? Kwa bahati mbaya, hakuna anayezungumzia tena kauli hiyo, hata Viongozi wenyewe wa CCM wameitelekeza.

Mheshimiwa Spika, wakati tunahesabu maisha ya Watanzania kwa vitu kama Radio, Baiskeli na Kochi, wako Watanzania wanaotuhumiwa kukwapua mabilioni ya hela, wamejenga maghorofa, wakiwa watumishi wa Serikali na mishahara yao inajulikana, posho zao wakisafiri zinajulikana na sio wafanyibiashara lakini wanaogelea katika starehe ya ajabu wakati watu milioni 11 hata mlo wao wa siku ni shida. Ni lazaima Serikali ya Awamu ya Nne, itafute vigezo vingine kuelezea ufanisi, kwa vyovypote si hivi ambavyo vinawagusa wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi ya Upinzani pia katika uchambuzi wake wa kina, inabaini kuwa Serikali hajjaweza kabisa kusimamia safari za nje. Haiwezekani, haina mantiki kabisa kila Wizara na katika kila Wizara takriban kila Idara na Kitengo inatenga mamilioni ya fedha kwa ziara za nje na za Mikoani.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inadhani sasa umefika wakati wa kufanya tu zile ziara zenye tija. Hivyo ndivyo wanavyofanya wenzetu siyo tu nchi za Ulaya lakini hata nchi kama Rwanda, Mozambique, Namibia ambazo zimetupiku sana kwa maendeleo, japo nchi hizo zote zimetoka kwenye mazingira ya Vita miaka michache tu iliyopita. Siyo tu hao wenzetu walikuwa kwenye vita, bali Tanzania ilikuwa katika mstari wa mbele katika ukombozi au kuleta amani kwa nchi hizo. Siri yao ni nini? Hakuna siri kubwa kama usimamizi thabiti wa mapato ya nchi na matumizi yake. Jambo hili linahitaji sana utashi wa Kisiasa siyo tu wa kutoa matamko matamu lakini pia wa kuchukua wakati mwingine maamuzi na hatua ngumu. Tanzania tuko nyuma sana katika hatua hii.

Mheshimiwa Spika, mathalan, kwa wale tulio pata uzoefu wa kusafiri kwenda nje ya nchi, mara ngapi tumesafiri na Mawaziri tena kutoka nchi hisani, wakisafiri katika ndege Daraja la Kawaida (*Economy Class*) wakati sisi tunaotegemea msaada toka kwao hata wa kulipa mishahara yetu tume panya Daraja la Wafanyabiasahara Wakubwa (*Business Class*). Hatutegemei Waziri Mkuu wetu asafiri katika *Economy Class* lakini tunahitaji kuthibiti zaidi ziara hizi na hatua ya kwanza ya kudhibiti ni si kila mwaliko au kila safari inayojitokeza lazima twende na siyo kila mukutano tunao alikwa lazima twende. Serikali ichague mikutano muhimu na yenye tija kwa nchi yetu na fedha za ziada ziwekezwe kwenye maendeleo zaidi. Uwiano wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ambayo mwaka huu ni Trilioni 5.9 dhidi ya Matumizi ya Maendeleo ya 3.8 ni sharti uangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, matumizi yasiyo ya lazima yadhibitiwe na matumizi yasiyo na tija ya moja kwa moja, nayo ya ondolewe na vyanzo vipyta vibuniwe kuwatoa Watanzania kwenye aibu hii ya kuitwa “Nchi maskini”. Mkakati tuliojiwekea wa 2025, unaelekeea dhahiri hautawatoa katika umaskini iwapo tutaendelea kwa mwendo huu tulio nao. Nio maana matumizi katika ziara kwa mfano isiyo na tija ya moja kwa moja lazima kuthibitishwa na mamlaka fulani. Ni kwa sababu hiyo Mauritius, Zambia, Uganda, safari zote za Mkuu wa Nchi, zinathibitishwa na Bunge na kila ziara nje ya zilizopitishwa na Bunge, zinahitaji “*Retrospective Approval*”(kibali cha Bunge cha Baadaye), baada ya hoja ya msingi kujengwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kauli ya Mwalimu kuwa wakati wenzetu “Wanatembea sisi lazima tukimbie”, ilikuwa na umuhimu mkubwa sana kusukuma maendeleo yetu, lakini ni dhahiri Mwalimu ameondoka na Kauli yake hiyo. Ni vigumu sana kufikiria maendeleo wakati wenye Diploma na Cheti cha Chuo kikuu ni asilimia 0.6. Serikali na washabiki wa CCM, watuelewe tunapozungumzia takwimu hizi. Hakuna Mtanzania anayetakiwa kuwa na ushabiki wa kisiasa kwa takwimu hizi na wote tunatakiwa tulie kwanza, tuweke vichwa pamoja ili tuelewe ni vipi tunajikwamua katika hili. Ni aibu kwa Tanzania yenye amani, utulivu kuwa na takwimu hizi, wakati wenzetu wa Rwanda, Uganda, Mozambique waliotoka kwenye mazingira ya vita wanazungumzia takwimu za juu zaidi.

Mheshimiwa Spika, hakuna asijeju kuwa Tanzania haina utaratibu wowote wa udhibiti wa fedha chache zilizoko na zinazohitajika sana kusukuma mbele maendeleo yetu ya nchi iwe katika ujenzi wa madarasa, zahanati na vituo vya afya au miundombinu. Tunajisifia kuwa na idadi kubwa ya madarasa lakini Taarifa ya *CAG* na Kamati inaonyesha jinsi idadi kubwa ya madarasa haya inavyokosa sifa na hivyo baada ya muda si mrefu tusipokuwa waangalifu hatutakuwa na madarasa kwa vile yatakuwa yamechoka. Hii haina maana kuwa kuna madarasa mazuri sana kati ya hayo. Wanaharakati na vyombo vya habari vimechambua sana ziara za Rais, na tija yake sina sababu ya kuzirudia hapa. Taarifa za *CAG* na Kamati kutofanyiwa kazi, hatuwezi kumaliza eneo hili la udhibiti bila kufanya marejeo kwenye Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (*CAG*) na Kamati za Bunge za Hesabu za Serikali, tangu Ofisi ya *CAG* ilipoanzishwa imekuwa ikilalamika miaka yote kuhusu matumizi yasiyo yakinifu ya fedha.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Rais alionyesha utashi mkubwa wa kiasiasa pale alipowaita viongozi wakuu wakiwemo Wakuu wa Mikoa (RCs), Wakurugenzi na Wenyeviti wa Halmashauri kujadili Taarifa ya CAG. Kambi ya Upinzani iliamini kuwa maagizo ya Rais yangelisimamiwa kikamilifu na watendaji wake na pale ambapo hayasimamiwi kikamilifu, hatua madhubuti zingelichukuliwa, hali imekuwa si hivyo hata kidogo kiutendaji. Nikitoa mfano wa mwaka 2009, Kamati za Bunge za Mahesabu zimetoa Taarifa zake Bungeni na Bunge kupitisha Azimio kukubali mapendekezo ya Kamati hizo.

Mheshimiwa Spika, kimsingi *CAG* amekuwa wakati wote akitoa Taarifa lakini Taarifa hizo zimekuwa hazifanyiwi kazi. Ushahidi ni vitabu na vitabu na hakuna taarifa yoyote ya utekelezaji iliyo wazi. Kama zingekuwepo *CAG* angeziona na kwa kuwa haziko tunaamini kuwa hakuna hatua iliyochukuliwa. Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kama rasilimali za Taifa hili zingesimamiwa na kudhibitiwa inavyotakiwa, leo hali yetu ya uchumi isingekuwa tofauti na Malaysia au Singapore ambapo wakati wa uhuru walikuwa na hali ya uchumi kama ya kwetu, Watanzania lazima wajilize Tanzania kuna nini? Rasilimali nyingi sana, ardhi kubwa sana, maji mengi sana, lakini Watanzania maskini wa kutupwa na Serikali lazima itupe jibu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani kwa miaka minne iliyopita tumekuwa tukitoa Bajeti mbadala lakini hakuna hatua zilizochukuliwa japo, Waziri Mkulo jana wakati wa kuhitimisha amesema kuwa “tungelimpelekea mapema”, tumpelekee mara ngapi?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ilitegemea kuwa Serikali, kwa maana ya Hazina, Tamisemi na Wakurugenzi husika, wangechukua hatua mara moja kuhusu maeneo yaliyobainishwa kuwa na ubadhirifu. Hali imekuwa kimya, Kamati za Bunge zimezunguka takriban Mikoa yote kwa gharama za wananchi, lakini matokeo yamekuwa kama hakuna lililotokea. Serikali kwa ujumla wake imenyamaza kimya, karibu maeneo yote, ukiacha tukio la Bagamoyo na sasa la Muheza/Mkinga ambayo nayo tunaamini yatasimamiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya *LAAC* imefika kwenye maeneo, inakuta hakuna nyumba ya Mwalimu iliyojengwa lakini vitabu vya Halmashauri vinaonyesha mradi umekamilika asilimia 100 (mfano wa Nyumba ya Mwalimu Migombani, Monduli), nyumba iliyoko imejengwa asilimia 100 na TANAPA), kisima cha maji ambacho hakipo Manispaa ya Arusha, Mradi wa Umwagiliaji Halmashauri ya Morogoro ambapo *CAG* amefanya kazi nzuri hadi kuwataka waliosababisha hasara siyo tu walipe hasara hiyo bali pia mamlaka husika iwachukulie hatua za kisheria na kinidhamu. Hali hiyo ya udanganyifu, ubadhirifu, matumizi yasiyo mazuri ya rasilimali, majengo yasiyofuata ramani na ubora, imejitokeza katika miradi mingi kama ilivyoonyeshwa na Taarifa ya Kamati ya *LAAC* iliyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, mifano ya miradi hiyo ambayo matumizi yake au hayakuridhisha kabisa au miradi haipo lakini fedha imetumika ni pamoja na miradi ya Shule ya Msingi Mlongo Kisiwani Mafia, Stendi ya Basi Manispaa ya Songea, stendi

ambayo haipo kabisa lakini fedha zimetumika, Zahanati ya Ndagoni ambapo ujenzi umesimama na fedha kuliwa; Mradi wa Ujenzi wa Nangaramo (Nanyumbu) ambapo mradi umejengwa lakini hautumiki na fedha za umma zimefungwa humo, ni dhahiri mipango haikuwa makini na wala hapakuwa na upembuzi yakinifu au Mradi mkubwa wa Maji Newala uliogharimu Tshs Milioni 172 lakini hauwezi kutumika kwa miaka mingi ijayo kwa ukosefu wa umeme na wananchi wa vijiji 11 wataendelea kutazama matenki 11 matupu bila manufaa yoyote kwao. Wakati huo huo Halmashauri nchini hazijajibu hoja mbalimbali za ukaguzi, zenyet thamani ya Tshs Bilioni 91,101, 051, 978.40, Kamati ya *LAAC* ilikwisha kutoa Taarifa Bungeni kuwa japo ni kweli fedha hizi si lazima ziwe zimeibowi, lakini kinachotokea ni kuwa Wakiisha kupita Wakaguzi, wahusika wanaenda kununua *receipt* bandia mitaani na kuwaita tena Wakaguzi kwa ukaguzi wa pili. Mtindo huu usipokomeshwa, fedha nyingi zitaendelea kuibiwa na risiti bandia kuwasilishwa kwa uhakiki na wakati huo hakuna kazi inayofanyika. Hali hii iligunduliwa pia na Kamati ya *LAAC* hivi karibuni kwa kupiga simu kwenye Kampuni iliyodhaniwa imetoa bidhaa lakini kampuni hiyo kukanusha kabisa kuhusika.

Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni 91 kwa wale wasiofahamu ni fedha nyingi kiasi gani, ni sawa na Madarasa ya Sekondari 65,000 kwa thamani ya Tshs.14 Milioni kwa darasa. Kiasi hiki kinahusu Halmashauri 126 tu. Halmashauri nyingi zimeshindwa kujibu hoja za miaka ya nyuma kabisa ya *CAG* yenye jumla ya Tshs.32, 903,395,306 ambayo nayo ni sawa na Madarasa 2,350 kwa gharama ya Tshs.14 Milioni kwa Darasa au ni sawa na Shule zilizokamilika Madarasa 16 kila mmoja, Shule 146. Wilaya ya Kongwa peke yake haijashughulikia hoja za thamani ya Tshs.6,813,262,872 ambazo thamani yake zinatosheleza kujenga Sekondari 30 bila mchango wa mwananchi hata mmoja.

Mheshimiwa Spika, nimeeleza haya kwa kuwa hii ni hali ya kutisha. Kambi ya Upinzani haina nia ya kumkebehi yejote, wala kuingiza ushabiki, inaumizwa na hali halisi na tunaumia tuapoona watu wanaingiza siasa kwenye mambo yasiyotaka siasa. *CAG* pamoja na kuwa anafanya kazi kwenye mazingira magumu sana, hana watumishi wa kutosha, hana vifaa na nyenzo za kazi za kutosha, lakini anafanya kazi nzuri sana na anatoa taarifa iliyo sahihi bila hila. Lakini hakuna ushirikiano wa kutosha kwa upande wa Uongozi wa Serikali, wahusika hawachukuliwi hatua au zikichukuliwa kesi nyingi, kama Kamati ya *LAAC* ilivyogundua zinaishia njiani kwa kuhujumiwa na Watendaji wa Halmashauri kwa kutokupeleka ushahidi na nyaraka za kutosha Mahakamani. Hali hii isipothibitiwa Taifa letu litaendelea kuimba wimbo wa Nchi maskini. Hadi leo hii, mamlaka husika hazijachukua hatua, imebaki kimya kana kwamba hakuna lililotokea. *CAG* amekagua, Kamati yako ya Bunge imekagua na kutoa Taarifa Bungeni. Hayo yote yanatumia fedha za wananchi wa Tanzania hao hao wanaokosa huduma. Mamlaka imekaa tuli kana kwamba hakuna lililotokea na mambo ni shwari tu. Hali hii haiwezi kuvumiliwa katika nchi inayojiita ‘Maskini’ miaka 50 baada ya uhuru, Kambi ya Upinzani nayo inajuliza baada ya wahusika kukaa kimya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kiongozi wa Shughuli za Serikali au Mheshimiwa Rais, kwa nini nao pia wamekaa kimya? Kuna nini katika mfumo wa Serikali na kwa utaratibu huo kauli za “mitaani” kuwa uwizi na ubadhirifu huo ni cheni hadi ngazi ya TAMISEMI na Hazina tutashindwaje kuiamini?

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kuwa Waziri Mkuu au Waziri wa Nchi, TAMISEMI atatolea ufanuzi wa kina hali hii. *CAG* mwaka jana amefanya siyo tu ukaguzi wa kawaida bali pia alifanya Ukaguzi Maalum (*Special Audit*) zipatazo tisa na ameenda mbali kufanya ukaguzi wa ufanisi na kupendekeza hatua mahsusizi za kuchukua. Wahusika wamekaa kimya tu rasilimali zinaangamia, umaskini unazidi kukua na kukithiri na wananchi wanazidi kupoteza matumaini kila kukicha. Ukaguzi wa ufanisi wa Babati ulihusu maeneo ya mafuriko na taarifa ile ingelifanyiwa kazi, athari iliyoletwa na mafuriko ya Kilosa huenda isingelitokea au isingelikuwa kubwa kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Nchi Utumishi, aliwahi kueleza kuwa kulikuwa na Watumishi “hewa” zaidi ya 3,000 kwenye *Pay Roll* ya Serikali. *CAG* na Kamati ya *LAAC* wamethibitisha pia kuwa wako watumishi wengi waliostaafu, waliofariki, walioacha kazi, waliofukuzwa majina yao bado hayajaondolewa kwenye Orodha ya Watumishi wa Serikali, hawa hawapo duniani au hawapo kazini lakini wamekwisha kulipwa kwenye akaunti zao, hivyo hizi fedha zimepotea. Watumishi wote Wilayani kwa utaratibu wa sasa wanalipwa na Halmashauri. Hivyo, hakuna maelezo yejote kwa majina hayo kutoondolewa kwenye orodha, wakati kila mwezi Afisa wa Halmashauri anapeleka orodha ya Watumishi Wizarani. Taarifa zote za kifo, kuacha kazi, ziko Wilayani, hivyo mishahara hewa kutokea ni dalili ya uzembe na au uwizi ambayo ni lazima ichukuliwe hatua mara mmoja kuokoa fedha nyingi zinazopotea. Kwa mwaka 2008/2009, fedha ambazo hazikurudishwa hazina ni bilioni 1,755,207,927 kwa mamlaka ya Halmashauri za Wilaya peke yake. Hizi ni fedha nyingi sana na kama zingelielekezwa kwenye ujenzi wa madarasa ni sawa na madarasa 125 au shule za Sekondari saba zilizokamilika za madarasa 16 kila shule. Lakini fedha hizi zimelipwa kwa watumishi hewa. Serikali imejua hilo, Waziri wa Utumishi alitangaza mwenyewe kuhusu Watumishi hewa, lakini Taifa halijajulishwa tena kuhusu hatua mahsusizi zilizochukuliwa dhidi ya waliosababisha hali hiyo, iwe ya kinidhamu au kisheria.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inadhani Serikali haijawa na mpango mkakati mahususi wa kudhibiti hali hii kuokoa fedha nyingi za walipa kodi, tukisema hili pia tunakebehi? Taifa hili tuache ushabiki, tataendelea kuditimiza Taifa na watoto na wajukuu zetu watatuhukumu. Tusiogope kusema ukweli pale unapostahili alimradi hatuyasemi kwa ushabiki. Ni vema na Serikali wakati wa kujibu ijibu hoja kwa hoja badala ya ushabiki na kuwa tu “*defensive*” yaani “kujitetea kwa kujitetea tu”. Ni kwa kuweka vichwa pamoja tutaokoa rasilimali chache za Taifa.

Mheshimiwa Spika, taarifa nyingine zinazoonyesha kuwa hakuna udhibiti imara ni Taarifa kuwa kwa mwaka 2008/2009, jumla ya Tshs 2,526,117587 zinazohusu Halmashauri 33 tu zilizolipwa bila kuwa na hati za malipo. Halmashauri nyingine 62 zilifanya malipo yenye thamani ya shilingi 5,313,071,671 zikiwa na nyaraka pungufu. Halmashauri zetu zote kwa sasa zina Wahasibu wenyе sifa, zina Wakaguzi wa Ndani na zina ikama zilizokamilika za Wahasibu Wasaidizi. Hakuna sababu kabisa, isipokuwa kuna uzembe na hila za uwizi ndio maana nyaraka hizo au hazionekani wakati wa ukaguzi au zinaonekana pungufu. Halmashauri nyingi ziko kwenye Mfumo wa Uhasibu wa *EPICOR* lakini hata pale ambapo mfumo huo umefungwa na *Computer* kuwekwa

wahusika wanaacha kuzitumia bila sababu za msingi. Hali hii inatia mashaka makubwa na kuashiria dalili isiyo nzuri. Japo *CAG* amelalamikia hali hiyo muda mrefu sasa lakini hakuna hatua inayochukuliwa na fedha zinaendelea kuteketea na Taifa linaendelea kulalamika kuhusu “Umaskini”.

Mheshimiwa Spika, kutokuwa na nyaraka au nyaraka zisizozokamilika za malipo ni kinyume na Agizo Na. 5(c) la Memoranda ya Fedha za Serikali ya Mitaa ya mwaka 1977. Ukiukwaji huu wa makusudi wa Memoranda unafahamika na madhara ya kutokuwa na nyaraka nayo inafahamika lakini hakuna hatua zinazochukuliwa. Kambi ya Upinzani inasema, ni vizuri sasa Waziri husika akatoa maelezo ya kina ya hali hii ya kuweka Kanuni na hatimaye Kanuni hizo hazisimamiwi? Viongozi wa chini wako wapi? Ngazi ya Mkoa, Wilaya na hata Wizara hawaoni hali hii? Tatizo liko wapi? Tumekwisha kusema Madiwani wapewe *breakdown* ya matumizi, ni imani yangu TAMISEMI itakuwa imeziandikia Halmashauri ili suala hilo litekelezwe ili Madiwani wawe na uwezo wa kusimamia na kudhibiti matumizi katika eneo lao kwa kuwa na Taarifa zinazowawezesha kusimamia.

Mheshimiwa Spika, Wilaya nyingi zimeingia kwenye Mfuko wa Afya ya Jamii. Watanzania wengi au wanachangia Mfuko huo kwa jinsi Wilaya ilivyoweka katika Sheria zake ndogo. Kwa ujumla, wale ambao hawachangii wanatakiwa kulipa Tshs.1500, kwa Kituo cha Afya na Shs.1000 kwa Zahanati. Fedha hizo hazirekodiwi vizuri na *CAG* ameshindwa kuzikagua. Hata hivyo, katika Wilaya ya Karatu tuliwahi kufanya *test* ndogo kwa ukaguzi wa dharura. Tulikuta kwa mwezi mmoja upotevu wa zaidi ya 100 milioni. Hii ni baada ya kuondoa watoto na wazee na wale wote wanaotibiwa bure.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Madiwani iliundwa na kutoa taarifa kwenye vikao vyote vya maamuzi na hatimaye Mkurugenzi kuachiwa kuchukua hatua. Hakuna hatua iliyochukuliwa na shilingi milioni 100 kwa mwezi ni hela nyingi sana. Hii ni hali ya kutisha. Watendaji na Serikali wote wanajua kuwa kutokutengeneza taarifa sahihi ya Mfuko huu ni kinyume na Agizo la 84(iii) ya Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa. Uvunjifu huu umeachwa muda wote bila kukemewa!

Mheshimiwa Spika, kwa mtindo huu, je, ni kweli Tanzania inastahili kuitwa nchi maskini au tunaifanya Tanzania kuwa Maskini kwa nguvu. Hapa sijaongelea rasilimali tulizopewa na Mwenyezi Mungu yaani madini ya kila aina ambayo nayo hatutumii vizuri, tunawapa misamaha ya ajabu ajabu, kinyume kabisa na Taarifa ya Kamati tuliyounda na kuihudumia kwa zaidi ya Tshs.2 bilioni. Ni dhahiri kwa mtu ye yeyote makini hali hii haiwezi kuingia akilini kabisa. Sijazungumzia rasilimali ya Bahari/Maziwa na Samaki tulio nao, sijagusia Misitu na Ardhi ambayo sasa inauzwa kwa bei ya kutupa na wakati mwengine ni wananchi wenyewe wanauzu ardhi yao bila kuangalia madhara ya siku zijazo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia masuala mbalimbali ya fedha na usimamizi au udhibiti, sasa niseme kidogo kuhusiana na uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2009. Oktoba, 2009 ilikuwa ni uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa viongozi wa ngazi ya Kijiji, Kitongoji na Mtaa. Uchaguzi huo kama tulivyotabiri haukuwa wa huru na haki kwa sababu mbalimbali nitakazoeleza hapa chini. Ni dhahiri Serikali yetu, japo kwa mdomo inazungumzia la kutaka kuona unafanyika uchaguzi huru na haki lakini matendo ya viongozi wetu mbalimbali, kuanzia TAMISEMI na Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya ambao ndio walikuwa Wasimamizi Wakuu wa Uchaguzi, walionekana dhahiri kuwa “wakiendeshwa” na mamlaka nje ya mamlaka zao. Aidha, ilikuwa dhahiri kabisa kuwa Serikali ilikula njama na Chama Tawala. Viashiria ya wazi ni kuwa:-

(i) Vyama vilishirikishwa na kwa pamoja tulikubaliana kutengeneza Kanuni ambazo tunaweza kuziita Sheria Mama. Baada ya Kanuni, TAMISEMI ilitengeneza kitu kilichoita “Mwongozo” ambao ulikuja kuwa na nguvu kuliko hata Kanuni zenyewe tulizokubaliana.

Mheshimiwa Spika, wakati Kanuni inatamka kuwa “Mgombea wa nafasi ya Uongozi atadhaminiwa na kiongozi wa Chama cha Siasa”, Mwongozo uliotengenezwa na TAMISEMI ulisema “...atadhaminiwa na kiongozi wa ngazi ya “chini kabisa” ya chama cha siasa”. Vyama vingine, ngazi za chini kabisa, mathalan ngazi ya “msingi” kwa Chadema sio ngazi ya uongozi bali ni ngazi ya uratibu tu hivyo haina mamlaka ya kudhamini.

Mheshimiwa Spika, katika utendaji, wasimamizi wasaidizi wakashikilia maelekezo ya Mwongozo na kukataa maelezo mengine yoyote. Hata tulipojulisha TAMISEMI tuliamiwa Wasimamizi watajulishwa lakini hakuna kilichotokea, matokeo na athari ya hatua hiyo ya kisheria ni kuwaondoa (*disfranchise*) wagombea wengi wa Vyama vya Upinzani, mathalan CHADEMA. Athari yake, ni kuwa wagombea wetu wengi waliondolewa kutokana na mchezo mchafu. Hali hiyo pia imetokea kwa Wagombea wa CUF.

(ii) Mheshimiwa Spika, CHADEMA tuliletewa kitabu cha Mipaka ya Vijiji, Vitongoji na Mitaa, siku moja baada ya CCM kumaliza zoezi la kura ya maoni. Mtu ye yoyote mwenye akili atajiuliza imewezekanaje kufanya kura ya maoni wakati mipaka hajulikani? Maelezo pekee ni kuwa TAMISEMI ilikula njama ya kutoa Taarifa kwa CCM hivyo CCM ikaitumia taarifa hiyo katika kura zake za awali, wakati vyama vingine tulianza kujipanga baada ya kujua mipaka.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya awali, nilieleza jinsi Waziri Celina Kombani alivyoshinikizwa katikati ya Uchaguzi hadi kumhamisha Msimamizi wa Uchaguzi Wilaya ya Karatu katikati ya Uchaguzi. Taarifa zote tunazo na simu zilikuwa zanapigwa tunazo mpaka muda walipowasiliana. Ni hali ya hatari sana Waziri ambaye kimsingi Uchaguzi uko chini yake anapoagizwa na Chama kimoja kwa vile tu ni Chama Tawala. Mheshimiwa Kombani amejitetea kwenye vyombo vya Habari kuwa yule Mkurugenzi amehamishwa kwa sababu za kiafya.

Mheshimiwa Spika, ninatoa “challenge”, kuwa Mheshimiwa Waziri atoe vyeti vya afya, kwa vile kiongozi anayeondolewa kwa sababu za afya kwanza awe ameomba yeye na pili kama Serikali inamwondoa iwe kwa Vyeti vya Daktari. Wakati wa kudanganyana umepita, Sheria na Kanuni tunazifahamu. Serikali inayopaswa kulinda Kanuni na Sheria inapokuwa ya kwanza kuzivunja, hali inakuwa mbaya sana. Ni dhahiri kitendo hiki peke yake kinaufanya uchaguzi ule usiwe wa huru na haki, lakini pia inaondolea Tanzania sifa ya kuwa nchi inayothamini demokrasia japo inahubiri sana demokrasia ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri hali hii siyo ya kistaarabu, haistawishi utawala bora wala misingi ya demokrasia. Hali hii inaondoa kabisa dhana ya kuwa TAMISEMI inaweza kuwa “*impartial*” na kusimamia uchaguzi bila kupendelea. Hoja ya Upinzani ya kuondoa Uchaguzi huo chini ya TAMISEMI inapata mantiki na tunasisitiza uchaguzi ujao uondolewe kabisa chini ya TAMISEMI na uwewe chini ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, yenyewe japo inalalamikiwa kwa mambo mengine lakini haijaonyesha “upendeleo wa wazi” kiasi hicho. Hivyo, kauli ya Katibu Mkuu wa CCM, Mheshimiwa Yusuf Makamba kuwa “CCM imepita bila kipingwa katika nafasi 24,000 ni lazima iangaliwe kwa umakini, siyo sahihi na inapotosha kwani uchaguzi haukufanyika katika mazingira yanayofanana, aidha, taarifa kuwa matokeo hayo yanaashiria CCM ndio Chama kinachopendwa, yanapotosha. Katika hili, lazima tuseme kwa ukali wote kuwa CCM imecheza faulu kubwa kwa kuwa wao ndio “*Linesmen, Refereee na Mchezaji*”, ikajiamulia aina ya mchezo inayotaka. Nchi hii ni yetu sote. Kuna siku Watanzania wataamka, watakataa udanganyifu huu wa wazi, watakataa kunyanyaswa. CCM dhahiri sasa kwa kung’ang’ania uongozi inataka kutupeleka pabaya na nikumbushie tu, nchi jirani ambako kila siku tunasikia siyo shwari, ni kutokana na vitendo vya aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, uchaguzi huo unaashiria nini kwa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani baadaye mwaka huu? Tayari kuna dalili zinazoashiria kuwa hila za namna hiyo zinaanza kuandaliwa, ikiwa ni pamoja na maadili yanayoandaliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, ambayo pamoja na mengine yanalazimisha Chama ambacho hakitasaini kitafutwa kugombea. Ni dhahiri vyama vinakataa kuweka saini kwa vile kuna mambo ya msingi ambayo hatujakubaliana na si utawala bora kulazimisha vitu ambavyo kwenye maziringira yetu hayafai na hatua hiyo inaweza masharti ambayo hata Katiba ya Jamhuri ya Muungano haiweki.

Mheshimiwa Spika, maeneo mbalimbali kila kukicha tunasikia matukio ya rushwa ndani ya Chama cha Mapinduzi, japo kifungu cha 25 ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi tuliyopitisha tu juzi inatakiwa idhibiti hali hiyo, watu wanapita kwenye vilabu, wanununa pombe, wanatoa hela, wanatoa jezi kwa vijana bila utaratibu unaojulikana na kadhalika. Hali hii haiathiri Wagombea wa Upinzani tu, bali pia wa CCM. Kinachoathirika ni maadili ya Taifa, hivyo suala hili lisiangaliwe tu kwa jicho la Vyama vya Siasa. Lakini pia, kutokuchukua hatua ni dalili ya wazi kuwa CCM haina tena uwezo wala dhamiria ya kudhibiti Rushwa ndani yake. Mtu anayeingia kwa kununua wapiga kura kwa jezi, pombe na hela, ni dhahiri hawezi kupiga vita rushwa na wala hawezi

kusimamia maendeleo na rasilimali ya nchi hii. Ni vizuri wananchi wakawa makini na watu wa aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe “Rushwa ni Adui ya Haki”, ni dhahiri Wabunge wakipatikana kwa rushwa, watashindwa kuwatetea wananchi maskini iwe ni kwenye kero zao mbalimbali, ushauri au hata kusukuma mbele maendeleo yao. Ni imani yangu, nia ya Mheshimiwa Rais ya kusukuma hadi ikatungwa Sheria ya Gharama za Uchaguzi, haitavurugwa na watu wasiozingatia maadili, ndani ya Vyama, lakini na hata wasiozingatia Sheria yenyewe.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imekuwa ikipokea malalamiko kutoka maeneo mbalimbali yanayohusiana na vitendo vya viongozi wa CCM kuwafuata kwenye nyumba zao, kuwataka wawaonyeshe kadi zao za kupigia kura, wanaandika namba hizo kwenye fomu au daftari zao. Kinachoudhi ni usumbufu, wakati mwingine usiku, hasa wasio wanachama au wapenzi wa CCM, kufuatwa na kulazimishwa kutaja namba zao za kadi za kupigia kura.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inafahamu kuwa Kadi ya kupigia kura ni mali ya Mpiga Kura na mwenye mamlaka ya kuiomba au kutaka chochote kifanyike kwenye Kadi hiyo, ni Tume ya Taifa peke yake na hakuna mtu au mamlaka nyingine yejote inayohusiska. Kwenye Uchaguzi mdogo wa Busanda na Biharamulo, kadi za wapiga kura zilichukuliwa kwa nguvu, tulitoa majina na taarifa kamili Polisi lakini hakuna hatua iliyochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, hivyo, ni vema Serikali ikatoa tamko na kuwataka viongozi wa CCM wa ngazi zote za chini kuanzia Mkoo, kwani Mkoo wa Arusha, kwa mfano zoezi hilo analiongoza Katibu wa Mkoo, Mary Chatanda mwenyewe. CCM iandikishe wanachama wake, lakini iache kufuata wananchi amba wanahakika si wanachama wao na waache tabia ya kuwaamsha wananchi kiholela. Kambi ya Upinzani, haina shida CCM kuandikisha watu wao wanavyotaka ilimradi hawaingilii uhuru wa wanachama wa vyama vingine na au hata Watanzania wasio na vyama. Vurugu hiyo imesababisha damu kumwagika Busanda na Biharamulo, ni imani yangu kuwa CCM inayokuwa mstari wa mbele kuhubiri uchaguzi wa amani na utulivu, haitakaa kuona damu ya Mtanzania hata mmoja itamwagika kama ilivyotokea kwenye Uchaguzi mdogo wa Kiteto, Tarime, Busanda na Biharamulo. Amani inatengenezwa haiteremki tu kutoka mbinguni, wala amani haiji kwa kuhutubia na kutoa maagizo ambayo hayafulitaliwi kiutendaji. Jeshi la Polisi nalo litakiwe kusimamia Sheria na kuacha kubeba Chama chochote cha Siasa.

Mheshimiwa Spika, matatizo yameishaanza kujitokeza sasa kwa mfano Wilaya ya Temeke ambako *OCD* wa Mkoo wa Temeke ameweka amri ambayo ni kinyume na Sheria kuwa vyama vinavyotaka vifanye mkutano vipeleke maombi kwa Mkoo wa Wilaya. Mfano halisi ni siku ya 10 Juni, ambako Chadema walipeleka “Taarifa” ya Mkutano kwa *OCD* kama sheria inavyotaka lakini akakataa kuipokea na kuagiza iende kwa Mkoo wa Wilaya. Afisa wetu alipoenda kwa Mkoo wa Wilaya, hakumkuta lakini akaambiya na *DAS* kuwa huo ndio utaratibu. Viongozi wasiofuata sheria za nchi ndio wanaosababisha fujo na vurugu nchini. Ni vema Serikali iwafunze vizuri, wasiipeleke

nchi pabaya kwa matakwa tu ya watu wachache. Huu ndio mwanzo wa kuvurugika nchi iwapo kila mmoja anajiwekea sheria zake. Ni imani yangu kuwa tumejifunza kutoka kwa majirani zetu na ni imani ya Kambi ya Upinzani kuwa misingi yote ya amani katika uchaguzi itafuatwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, utawala bora na demokrasia nchini, Mheshimiwa Waziri Mkuu na hata kwenye Kitabu cha Hali ya Uchumi, kazi iliyofanywa na Serikali katika eneo hili imefafanuliwa, mathalan Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, kufungua ofisi za Mashtaka na Upelelezi katika Mikoa ya Shinyanga, Lindi na Mtwara. Hii ni hatua nzuri, pia katika Hali ya Uchumi, Serikali imeeleza kuwa kesi za rushwa kubwa 15 zilifunguliwa Mahakamani. Kambi ya Upinzani, inaamini japo hii ni hatua mojawapo, utawala bora ni zaidi ya hapo. Mahakama zisipokuwa karibu na wananchi kwa umbali unaofikika misingi yenewe ya utawala bora haitakuwapo. Mahakama zimekuwa na usumbu mwingi, kesi zinachelewa sana mpaka maana ya haki inapotea. Wananchi wadogo wanashindwa kuzifuata haki zao kutokana na umbali mkubwa na hasa kesi zinapopigwa tarehe za mara kwa mara watu wa hali ya chini wanafika kukata tamaa na kupoteza haki zao.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Mabaraza ya Kata yenyе kushughulikia hata baadhi ya kesi za jinai. Lakini Serikali hadi leo haijatoa maelekezo ya kina jinsi Mabaraza hayo yatakavyoendeshwa. Jambo ambalo hili limefanya kesi za ardhi kuwa kero zaidi kuliko hata awali. Gharama za kufungulia kesi katika Baraza, ni kubwa mno ambayo wananchi wa kawaida hawawezi, mathalan 20, 000 kufungua file, wakati Mahakama ya Mwanzo kesi inafunguliwa kwa Shs.1,500 tu. Ni wakati sasa Serikali itazame upya utaratibu huu ulioanzisha Mabaraza haya, mamlaka yao, uendeshaji wao, ikiwa ni pamoja na usimamizi. Baadhi ya Wenyeviti wa Mabaraza ya Wilaya wamegeuka kuwa Miungu Watu na wanahukumu kesi wanavyotaka, wakati mwingine bila hata kuwasikiliza mashahidi inavyotakiwa. Niko tayari kumpa Mheshimiwa Waziri majina ya wahusika wanaolalamikiwa kwa kesi za aina hiyo. Vyombo hivi vimeundwa kutoa haki na vyombo vya haki vinapogeuка kuwa kinyume madhara yanakuwa makubwa zaidi na wananchi wanapoteza imani kwa Serikali yao moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo mengi, TAKUKURU ni sehemu ya matatizo na mfano ni matukio yaliyotokea Kijiji cha Chemechem, Wilayani Karatu, ambako wananchi wamelalamikia jinsi viongozi wa kijiji hicho walivyotafuna rasilimali za kijiji hicho na TAKUKURU wamefika mara kadhaa, lakini hakuna hatua inayochukuliwa wala hakuna taarifa. Taarifa hiyo imefika kwa Mkurugenzi Mkuu ambaye naye aliahidi atashughulikia lakini hadi sasa ni kimya zaidi ya miaka miwili. Kijiji kinaangamia, TAKUKURU ipo na wanalipwa mishahara kwa kodi ya wananchi hao hao. Hatuingili utendaji wa Takukuru, lakini mambo yanapokuwa hayaendi, ni lazima tuyaseme hapa Bungeni kama chombo kinachosimamia Serikali na vyombo vyake vyote. (Katiba Ibara ya 63(2)).

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora, Mheshimiwa Sofia Simba akifuatana na Mary Chatanda, Katibu wa CCM Mkoa wa Arusha, alitembelea Wilaya ya Karatu mwezi Mei 2010. Wananchi wa Karatu walifurahi sana kwa vile wanatembelewa na Waziri wa Utawala Bora, wakiamini kero zao kuhusu utawala bora zitapata ufumbuzi. Cha kushangaza Mheshimiwa Waziri, pamoja na mengine na kwa kushirikiana na Mary Chatanda, walianza kuwachochaea wananchi wa kijiji cha Gyekurum Lambo kuwa waandamane kugomea kijiji chao kuingizwa katika Mamlaka ya Mji mdogo wa Karatu. Waziri wa Utawala Bora, ambaye pia ni Mwanasheria, alipaswa kulinda Sheria. Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati akiwa Waziri wa Tawala za Mikoa, ndio alitangaza Mamlaka ya Mji mdogo 55 nchi nzima. Wakati Tangazo hilo linatolewa, Halmashauri husika wala hazikuulizwa. Leo Waziri anashawishi wananchi waandamane, badala hata ya kuwashauri wachukue hatua za kisheria kupinga hatua hiyo na Waziri ni sehemu ya Serikali. Wakati wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kulikuwa na mawasiliano ya kina na TAMISEMI na hata Waziri Celina Kombani. Sasa Serikali hiyo hiyo inajikanganya na kushawishi wananchi kugoma. Kwa hatua hiyo, ni dhahiri Serikali ya CCM haina utawala bora na kama inadhani inao, haina Waziri anayestahili Wizara hiyo na kwa kuwa Wizara hiyo matunda yake ndiyo hayo inatumia fedha za wananchi wa Tanzania kwa Wizara isiyo na tija.

Mheshimiwa Spika, usalama wa raia na mali zao, siku za hivi karibuni Taifa limeshuhudia matukio ya Watanzania, Raia wema kuvamia vituo vya Polisi na kuleta madhara ya kuumiza Polisi na kuharibu mali. Matukio haya yameongezeka kama vile yalivyoongezeka matukio ya raia kufa mikononi mwa Polisi na hatimaye kutafutwa visingizio vya kila aina. Matukio haya yametokea Iringa, Arusha, Dar-Es-Salaam, Karatu na maeneo mengine mengi. Tukio la aibu la hivi karibuni lililotokea Wilaya ya Tarime, linatia aibu Taifa, Polisi kutuhumiwa kuvamia nyumba za raia na kuwalazimisha kuvua nguo wanawake na wanaume na wanawake kulazimishwa kulamba sehemu za siri za wanaume, shemeji zao na mwanamke mwингine kulazimishwa kulala na mtoto wake si jambo la kawaida. Hii ni aibu kubwa, kama ni kweli na Serikali ikakaa kimya tu?

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha, ndani ya Jeshi la Polisi bado kuna viongozi wenye mawazo ya mgando, ni aibu kwa Afisa wa Polisi ambaye hajui kuwa Tanzania ni nchi ya Vyama vingi na kuwa njia za kawaida zinaposhindikana, raia ana haki ya kukimbilia mahali anapodhani atasaidiwa, kama walivyofanya wakina mama hawa kwa kukimbilia CHADEMA. Lakini Polisi anawalaamu hadharani eti ‘kwa nini walienda CHADEMA’ kana kwamba CHADEMA ni chama haramu nchi hii. Nashukuru akina mama hao hawakukata tamaa, walipata fursa ya kupiga kelele CHADEMA na hatimaye jambo likafika hadharani kwa Taifa zima. Mheshimiwa Waziri Mkuu, matukio haya, japo yanafanywa na watu wachache, lakini wanachafua sura ya Jeshi letu la Polisi ambao ndani yao wako wengi tu wanaofanya kazi nzuri sana na ya kijasiri, ni lazima Jeshi liwashughulikie hawa wachache wanaochafua jina la Jeshi.

Mheshimiwa Spika, matukio mengine yanayochafua jina na sura ya Jeshi letu ni pamoja Polisi kuwalinda wahalifu kama ilivyo kwenye kesi nyingi za Karatu ambapo nimekwisha kumjulisha Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani lakini hadi sasa hakuna hatua iliyochochukuliwa. Inatisha inapofika mahali watu wanaweza kukamatwa kwa amri ya mtu

binafsi tajiri. Tajiri huyo akipiga watu ni halali na hata pale anapokamatwa yeye tajiri anapelekwa na Askari kwa gari lake akiendesha mwenyewe na kusaidiwa Mahakamani kwa ‘*fast track*’ na akiisha kupata mdhamana anarudi na gari lake na Askari huyo. Hii ni sawa na kubinafsisha Jeshi la Polisi kwa matajiri wachache. Marehemu Boay Gichuru aliyeuawa katika kijiji cha Qanded Karatu, ambapo raia wema wakiwemo viongozi wa kijiji wamesaini *Affidavit*, licha ya kutoa *Statement*, kuwa wako tayari kutoa uishahidi popote, lakini Polisi wamenyamaza na wahusika wanatambaa mitaani kuwa wameweka Polisi wote mifukoni. Taarifa ya mazingira ya kifo hicho imepelekwa kwa *IGP* na mimi mwenyewe nimemjulisha Naibu Waziri, Mambo ya Ndani, wote wamekaa kimya. Taarifa za namna hii tumepokea kutoka Tarime, Bariadi, Kagera, Rukwa na meaeneo mengine mengi. Ni vema Mheshimiwa Waziri Mkuu akafahamu kuwa matendo haya yanakatisha tamaa wananchi na isitoshe matukio ya namna hii yanachafua jina la Polisi lakini pia la Chama Tawala kuwa kimeshindwa kusimamia haki za raia wake na inabeba matajiri kuliko raia maskini.

Mheshimiwa Spika, matendo ya unyanyaswaji kama yanayofanywa na Polisi kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Geita, katika kijiji cha Rwamgasa, Wilaya ya Geita ni vitendo ambavyo navyo havivumiliki katika utawala wa sheria. Viongozi wa Chama ambao kwa utaratibu wa kawaida, wametoa “Taarifa” kufanya mikutano yao ya Chama, wanakamatwa wakati hawakupewa hata ile taarifa ya “kukataliwa” hiyo mikutano. Shinikizo la kuwakamata linatoka kwa Mkuu wa Wilaya, ambaye Sheria ya Vyama vyta Siasa wala haimtambui.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa kijiji cha Mpuguso, Wilaya ya Rungwe nao wananyanyasika sana na manyanyaso yameanza baada ya Chama cha Upinzani kushinda katika kijiji hicho. Ni vizuri Serikali ikawaelimisha maafisa wake, Wakurugenzi wa Wilaya, Jeshi la Polisi katika maeneo mbalimbali, Maafisa wa *TRA* na Uhamiaji. Hakuna anayekataa viongozi hao kufanya kazi zao lakini wafuate maadili ya kazi zao na wale wanaokiuka washughulikiwe inavyostahili. Nchi hii ni yetu sote, hakuna mwenye hati miliki, hivyo wananchi wote, wa jinsia yoyote, rangi yoyote, imani ya dini yoyote na itikadi yoyote, wote tuna haki sawa na hakuna aliye juu ya mwingine. Serikali inawajibu wa kusimamia usawa huu bila upendeleo au ubaguzi wowote ule.

Mheshimiwa Spika, masuala ya ujisadi na uwizi wa mali ya umma. Mwaka wa 2007 mimi pamoja na Wenzangu na kwa kushirikiana na Wabunge wa Kambi ya Upinzani, nilitoa pale Mwembe Yanga, “*List of Shame*”, iliyokuwa yenye majina ya watu tuliovatuhumu kuhusika na Ujisadi mkubwa katika nchi yetu ikiwa ni pamoja na Ujisadi ndani ya *BOT*. Kwa kuwa baadhi ya kesi ziko Mahakamani sitaki kuzungumzia zile kesi ambazo ziko Mahakamani tayari. Hata hivyo, ninapenda kueleza kuwa wengi wa waliokuwa ndani ya Orodha hiyo ya Watuhumiwa wa Ujisadi walitishia kunipeleka Mahakamani. Nami nikasema wawahi kwenda Mahakamani kwa vile Taarifa nydingi zingeweza kutoka hadharani.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007, Shirika mmoja la Uingereza lilitangaza kufanya Mkutano wa “*Economic Forum*”, ambao ungelifanyika Hoteli ya Kempinski na kutangazwa katika Gazeti la “*The Economist*”. Waandalizi wa mkutano huo walitangazwa kuwa ni pamoja na Bwana Yusuf Manji, ambaye walimtaja kama ni moja wa nguzo kubwa ya uchumi wa Tanzania na pia angelikuwa mtoa mada mmojawapo. Nilipotakiwa maoni yangu na Waandishi wa Habari, nikapinga sana kuwa huyo Bwana hawezি kuwa nguzo ya Uchumi wa Tanzania kwa vile anahusishwa na kutumiwa mambo mbalimbali katika uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kauli hiyo kwenye Gazeti, Bwana Yusuf Manji alinifungulia Kesi katika Mahakama Kuu ya Tanzania, *Civil Case*, Na.140 ya mwaka 2008, Yusuf Manji (*Plaintiff*) vs Dr. Willibrod Peter Slaa (*Defendant*), kwa kosa la kumchafulia jina. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, nimeshinda kesi hiyo na nashukuru kuwa haki ya Watanzania inalindwa. Katika uamuzi wake, Jaji G.P. Shaidi, alioutoa tarehe 14 Januari, 2010 amekataa (*rejected not dismissed*) kesi hiyo katika hatua ya *PO*. Kwa maneno yake mwenyewe, Jaji anatamka “*Under the circumstances of this case, I hold the view that the plaint as drafted does not fully disclose cause of action against the defendant, I therefore reject it under Order V11 Rule 1 of the Civil Procedure Code*”.

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Tundu Lissu, Wakili wangu aliyesimamia kesi hiyo mpaka haki ikapatikana katika hatua ya *PO*, yaani kabla hata kesi yenyewe haijasikilizwa. Kwa ushindi huo, ninapenda kuwasisitiza Watanzania, wawe majasiri kulinda heshima ya nchi yetu, kulinda rasilimali za Taifa hili kwa gharama yoyote na nina hakika tukisimamia ukweli, Mungu atalinda Taifa lake kwa njia ya majasiri wachache. Ninapongeza pia Mahakama kwa kusimamia ukweli na haki.

Mheshimiwa Spika, masuala ya rushwa na ujisadi yameisumbua nchi yetu kwa muda sasa. Wako watu wanaosema tuache kuzungumzia ujisadi bali tuzungumze maendeleo. Ukweli ni kwamba, huwezi kuwa na maendeleo kama rushwa na ujisadi havitapigwa vita kwa hali na mali. Iwapo wananchi watalipa kodi na watu wachache wakazitumia kwa njia ya kifisadi, shule haziwezi kujengwa, zahanati hazitajengwa wala hazitapata dawa, barabara nazo hatajengwa na kadhalika. Ni kwa msingi huo, tunaoamini kuwa ujisadi na ubadhirifu wa mali ya umma, tutaushikia bango kuwa suala la ujisadi ni lazima Serikali ichukue hatua madhubuti.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Bunge hili Tukufu, Kambi ya Upinzani, imeendelea mwaka hadi mwaka kuuliza maswali ambayo hayajapata majibu. Mwaka huu ninarudia tena, kuuliza na kutaka maelezo ya kina kuhusu ujisadi uliofanyika kupitia Kampuni ya *Deep Green Finance Company Ltd*, ambayo ilisajiliwa 18 Machi 2004 kwa Taarifa za Brella, wanahisa waanzilishi wakiwa ni Mawakili Protase R.G. Ishengoma na Stella Ndikimi wa Kampuni ya IMMA Advocates. Mawakili hao walihamisha hisa zao kwa Kampuni ya *Needbank Ltd* na *Nedbank Africa Investment Ltd* tarehe 15 April, 2005. Tarehe 1 Mei 2004 siku ya Sikukuu, Kampuni hiyo ilifungua Akaunti benki ya NBC, *Corporate Branch*, Akaunti na 011103025840 na haikingiza hata senti moja katika

akaunti hiyo kwa zaidi ya mwaka mmoja. Kati ya Tarehe 1 August na Desemba, 2005 Kampuni hii ilipokea jumla ya bilioni 10,484,005 815.39 kutoka *BOT*. Bilioni 10 kutoka *BOT* kwenda kwa Kampuni tusiyoijua na Serikali haitaki kutolea taarifa, inaleta mashaka na wasiwasi mkubwa kuhusu uwajibikaji wa Serikali yetu. Serikali imekataa kujibu hoja hizi na Bunge hili na Watanzania tunahitaji kujua Kampuni hii ni ya nani, kwa dhahiri siyo ya kijeshi na hivyo hakuna usiri wowote. Jinsi fedha zilivyohamishwa kwa siku, tarehe, kiasi na njia iliyyotumika, niliwasilisha katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imefikishwa mahali kwenda kukopa fedha kwenye Benki ya Kibiashara wakati tuna fedha zetu zilizotoka Benki Kuu, imepelekwa kwenye Kampuni tusiyoifahamu na Serikali haitaki kutoa jibu. Kimsingi, hii ni dharau kubwa kwa Watanzania na Serikali imekiuka kabisa misingi ya uwajibikaji na misingi ya Katiba kuwa madaraka ya Serikali yenye yanatoka kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya pili ambayo Kambi ya Upinzani na Watanzania wanataka kujua ukweli, ni Kampuni ya *TANGOLD* ambayo ilisajiliwa katika kisiwa cha Mauritius tarehe 5 April, 2005 ikiwa na Hati ya Usajili Na.553334 na kupata *Global Business Licence (C2/GBL)* tarehe 8 April, 2005 na kupata Hati ya Kutimiza Masharti hapa nchini tarehe 20 Februari, 2006. Hata hivyo, taarifa zilizoko ni kuwa *Tangold* imekuwa na akaunti *NBC Corporate Branch*, No. Olll03024840 iliyofunguliwa tarehe 1 Januari, 2003, yaani miaka miwili kabla Kampuni hiyo haijasajiliwa Mauritius na takribani miaka minne tangu imepata Hati ya Kutimiza Masharti Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaweza kukataa kujibu maswali haya, inaweza kutumia ubabe, lakini kuna siku itafika Taifa haliwezi kukaa kimya, majibu lazima yatapatikana tu. Kambi ya Upinzani, inataka kupata majibu sahihi kwa vile ndani ya Bunge lako hili Tukufu Serikali imekuwa ikitoa kauli tofauti, mathalan, wakati aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini, wakati ule Mheshimiwa Karamagi, analiezeza Bunge kuwa *TANGOLD* ni mali ya Serikali kwa asilimia mia moja, Taarifa ya Kamati ya Bomanii inaeleza kuwa Kamati hiyo iliarifiwa kuwa *TANGOLD* ni mali ya watu binafsi. Isitoshe, tumeuliza na hatujapata majibu, Kifungu cha 7 cha *Memorandum* ya Usajili, kinasema kuwa “wenye hisa wanaweza kuhamisha ‘share zao’ kwa baba, mama, mke, watoto wapwa...” Swalii ambalo halijapata majibu na lazima sasa lipate majibu ni, je, Serikali inao watu hao?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ndani ya Bunge hili amekataa kujibu maswali yanayohusu Meremeta. Kambi ya Upinzani haitachoka kuweka na kuingiza kumbukumbu hizi ndani ya *Hansard* ya Bunge. Naomba kuwakumbusha Watanzania kuwa Kampuni ya Meremeta, inayotuhumiwa kwa matumizi ya Tshs.155 Bilioni, ambayo ni zaidi ya Bilioni 133 za *EPA*, iliandikishwa Uingereza ikiwa na Hati ya Usajili Na.3424504 ya Tarehe 19 August, 1997 na kupata Hati ya Kutimiza Masharti (*Certificate of Compliance*) nchini Tanzania kama Tawi la Kampuni ya Kigeni yenye Na.32755 ya tarehe 3 Oktoba, 1997.

Mheshimiwa Spika, kinachoshangaza katika Kampuni hii ni kuwa wenyе hisа wake tofauti na Bunge liliyoyelezwa marа nyingi (*Hansard*, Karamagi na Meghji, *Budget Speech* 2007), ni *Triennex* (PTY) Ltd ya Afrika Kusini yenye hisа asilimia 50%, Msajili wa Hazina mwenye hisа asilimia 50%, kwa niaba ya Serikali ya Tanzania na Kampuni mbili za *London Law Services Ltd* wa *Temple Avenue*, wenyе hisа 1% na *London Law Secretarial Services Ltd* ambaо anuani yao ni sawa na hao wenzao, nao pia wana hisа 1%. Jeshi la Wananchi halitajwi mahali popote, hata kama Meremeta ni Kampuni ya Jeshi, ni Kampuni iliyokuwa inafanya biashara kwani kuchimba dhahabu Buhemba, ni biashara ya madini na siyo siri ya Kijeshi. Hivi ni nini Serikali inaficha kuhusu Kampuni hii. Hata kama kuna Siri, ni kwa nini Taarifa ya Siri isitolewe kwa Kamati maalum ya Bunge au Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ulinzi. Kambi ya Upinzani, haioni kuwa ni sahihi Taarifa ya Kampuni ya Umma isitolewe kwa Bunge kwa utaratibu wowote ule. Kambi ya Upinzani haitaacha kufanya utafiti hadi ukweli wote ujulikane kuhusu Kampuni hii, Tshs Bilioni 155 ambazo Meremeta inatuhumiwa, ni fedha nyingi sana za wananchi na bila kupata maelezo ya kina basi ni dhahiri kuwa Serikali itakuwa inaficha ukweli fulani. Ni imani ya Kambi ya Upinzani, kuwa safari hii, Serikali angalau itakuwa tayari, basi kutoa maelezo japo mafupi na au kama haiko tayari kutoa taarifa hayo hadharani, basi angalau kwa Kamati ya Bunge ya Uongozi, ya Mambo ya Nje na Ulinzi au Kamati yoyote ile ambayo Serikali itaona inafaa.

Mheshimiwa Spika, Ripoti ya Uguzi wa *EPA*, uliofanywa na *Ernest and Young* katika Kifungu cha 3.20, 3.23 na 3.24, kinatamka wazi uwepo wa “*fraudulent supporting documents submitted to support claims*” yaani ufisadi uliotumika ni pamoja na kutumia hati za kugushi katika kutoa fedha kutoka *BOT*; malipo ya viwango visivyo sahihi au kutumia viwango visivyo sahihi vya kubadilisha fedha (yaani *incorrect amounts and incorrect exchange rate*). Uguzi ulionyesha kuwa kati ya Tshs 133 Bilioni malipo ya zaidi ya 90.3 bilioni yalifanyika kwa kutumia hati za kugushi (*invalid and fraudulent supporting documents*), nyaraka hizi zimeonyeshwa katika kiambatanisho C ikionyesha na majina ya Makampuni husika, ikiwa ni pamoja na Kagoda *Agriculture Ltd* ambayo peke yake ilichukua zaidi ya Bilioni 40.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imekaa kimya kabisa kuhusu Kampuni ya Kagoda, Kambi ya Upinzani imelazimika kueleza kwa kirefu tena kilichojiri kuitia Kagoda, taarifa mbalimbali zilizoko kuhusu kampuni hii na sura ya ufisadi inayoonekana wazi. Kampuni ya Kagoda *Agriculture Ltd* iliyosajiliwa nchini chini ya Sheria ya Makampuni, Sura ya 212 tarehe 29 September, 2005 na kupata Hati Na.54040, Wakurugenzi waliosajiliwa wa Kagoda ni watu wawili wenyе anuani za Kipawa *Industrial Area, Plot No.87*, Temeke, Dar-Es-Salaam na P.O. Box 80154 Dar-Es-Salaam, kinyume na utaratibu wa usajili Brella ambaо unahitaji Wakurugenzi wa Makampuni kujisajili kwa kuonyesha anuani ya mahali anapoishi na siyo Sanduku la Posta.

Mheshimiwa Spika narudia tena, ni lazima Serikali ilieleze Bunge kwa niaba ya Watanzania wote undani wote kuhusu Kampuni ya Kagoda na hatua zиpi imechukua au inafikiria kuchukua dhidi ya Kampuni na watendaji wake na au watendaji na viongozi wa Serikali waliohusika angalau hatua za kiutawala na au kinidhamu. Hiyo pia ni kwa

watendaji wake ambao labda hawakuwa makini wakati kampuni ya Kagoda iliposajiliwa, jambo linaloleteteza kuwa vigumu kwa kampuni hii kujulikana hasa ni mali ya nani, iwapo hivyo ndivyo ilivyo.

Mheshimiwa Spika, leo ni takriban miaka tisa tangu Kambi ya Upinzani ilipopinga ununuzi wa kinachoitwa Radar ya Jeshi, ndani ya Bunge lako Tukufu na hatimaye kupinga upitishwaji wa Bajeti na kutoka nje. Kumbukumbu za *Hansard* zinaonyesha kuwa Kambi ya Upinzani wakati huo ikiongozwa na Mheshimiwa Lwakatare, aliyekuwa Mbunge wa Bukoba Mjini, ilitoka nje ya ukumbi ambao leo ni ukumbi wa Msekwa, kuonyeshwa kuchukizwa kuburuzwa na Serikali na Wabunge wa CCM ambao walitumia turufu ya uwingi wao kuptisha Bajeti hiyo. Kambi ya Upinzani, inamshukuru sana aliyebuni na kutengeneza mitambo ya *Hansard* ambayo siyo tu inarekodi kilichosemwa ukumbini bali pia kama kuna kicheko, makofi na hata kuzomewa kama ilivyotokea siku hiyo.

Mheshimiwa Spika, miaka tisa baadaye, Kambi ya Upinzani inaona fahari kubwa, tulichokisimamia siyo tu kimeelekeea kuthibitika lakini imekuwa ni hadithi dunia nzima na imehusishwa na kitendo kikubwa cha ufisadi au rushwa au uwizi wa mali ya umma. Ufisadi huo umejadiliwa ndani ya Bunge la Uingereza (*House Commons*) mara kadhaa na uchunguzi kuanzishwa na Shirika la Upelelezi la Uingereza la *Serious Fraud Office (SFO)*, wenzetu wa Uingereza, ambao tunao mfumo unaofanana sana wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inayo furaha ya pekee kusikia kuwa Serikali iliyokuwa imekanusha katakata kuwa hakuna ufisadi wa aina hiyo, ndio inayotuma wataalam wake kwenda kudai mgawo wa Serikali ya Tanzania baada ya Serikali ya Uingereza kutamka kuwa itatoa mgawo huo kwa *NGO*. Kwa jambo kubwa kama hilo, Kambi ya Upinzani inaona ingelikuwa jambo la busara kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kutoa taarofa rasmi juu ya kitu gani kinaendelea kuhusu sakata hilo? Isitoshe, Sakata hilo linahusu pia bei ya Radar hiyo kupandishwa kuliko bei yake halali.

Mheshimiwa Spika, hii maana yake ni kuwa kuna fedha za Walipa kodi wa Tanzania imetumika vibaya, Serikali ya Tanzania imeingia hasara kwa kulipa bei kubwa kuliko bei halisi, je, wahusika walioliingizia Taifa hasara hiyo, wamechukuliwa hatua gani? Maswali haya yanagusa hadhi na heshima ya Serikali ya Tanzania, hivyo ni imani yangu kuwa Serikali haitakuwa na kigugumizi kuwaeleza Watanzania kilichojiri, hatua zilizochukuliwa au zinazotarajiwa kuchukuliwa dhidi ya wahusika waliosababisha hasara hiyo.

Mheshimiwa Spika kwa taarifa tulizonazo, *SFO* walifanya upelelezi wa tuhuma za rushwa (*kickback*) zinazoihusu Kampuni ya kwao ya *BAE*. Hata hivyo, kulinda heshima ya nchi yao, wakamaliza swala hilo nje ya Mahakama kwa kukubaliana *BAE* kulipa *fine*, kwa kosa la “kutokutunza kumbukumbu vizuri” badala ya tuhuma ya awali iliyokuwa ikichunguzwa ya rushwa. Kwa kuwa *SFO* walikuwa wakishirikiana na

Tanzania katika upelelezi na kwa kuwa walikwishawasilisha kwa Mwanasheria wa Serikali, kwa Barua yao yenyne Kumb. SPC01/D/MC ya tarehe 21 Machi 2001, majina ya wahusika wote wa kashfa hiyo kwa upande wa Tanzania, Kambi ya Upinzani inataka kufahamu Serikali ya Tanzania imechukua hatua gani au inachukua hatua gani sasa baada ya *SFO* kumaliza kazi kwa upande wa kwao? *SFO* wamekwenda mbali zaidi, kiasi cha kuonyesha fedha hizo zilikopelekwa na viongozi pamoja na wafanyabiashara wa Tanzania katika Akaunti za nje Uswisi, Lichtenstein na hatimaye katika kisiwa cha New Jersey, Uingereza.

Mheshimiwa Spika, iwapo Serikali ya Tanzania haijachukua hatua yoyote hadi sasa, je, ni sababu gani za msingi zimefanya Serikali yetu kutokuchukua hatua? Hali hii ya usiri katika mambo ya umma, ndio unaoleta hisia kuwa Serikali yetu haina uwazi, haisemi ukweli katika masuala yanayoihusu rasilimali na mali za Taifa letu. Ni imani yetu kuwa, Serikali itatoa Taarifa ya kina kwa Bunge lako Tukufu ili Taifa liweze kufahamu kinachoendelea. Hizi ni fedha za Wananchi na Serikali inawajibika kwa wananchi, Kambi ya Upinzani haioni kabisa msingi wa usiri huu. Hata hivyo, haya yametendwa na Serikali au ilikuwa inafahamu na kama haikufahamu basi inapaswa kuwachukulia hatua hao wote walioliingizia Taifa hasara hii kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mtu yejete mnyofu, mkweli na anayefanya upembuzi yakinifu wa hali ya siasa ya Tanzania, atakubali leo kuwa hali ya siasa ni tete katika maeneo na nyanja nyingi. Tusijidanganye kwa kusema kila mara kuwa hali ya kisiasa nchini ni ‘shwari’. Tusipojiangalia na kuwa makini tutakuwa tunacheza mchezo wa Mbuni wa ‘kuficha kichwa kwenye mchanga’. Kila kukicha kuna taarifa ya mgomo kwenye shirika hili au lile kutokana na wafanyakazi au kunyanyasika au kunyimwa haki zao au kubaguliwa. Pamoja na ukweli wa Msukosuko wa Kifedha wa dunia, ni vema waajiri wakakaa na wafanyakazi wao na kupanga pamoja namna bora ya kuhimili msukosuko huo ambao unaelekea kwisha. Waajiri wasiachiwe kufanya maamuzi ya kiimla ya kusimamisha wafanyakazi wao. Ninapenda kutoa pia wito wa jumla kwa vyama vyote vya Wafanyakazi kusimamia haki za wananchi kwa mujibu wa Katiba zao kwani malalamiko haya ya kutelekezwa na vyama katika maeneo ya kazi tunayapata karibu kila mahali.

Mheshimiwa Spika, hali katika Vyuo vyetu Vikuu si shwari. Chuo Kikuu cha Dodoma, kina hali isiyo ya kawaida ya unyanyasaji unaofanya kwa misingi ya kisiasa. Nashukuru kuwa tarehe 13 Juni, 2010, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, akiwa amevalia rasmi katika mavazi ya CCM, alipokea maandamano ya wanafunzi. Nimefarijika sana na maandamano hayo. Ni imani yangu kuwa manyanyaso katika Chuo hicho kwa vijana wanachama wa Vyama vya Upinzani, sasa utaisha na vijana wanawenza kufanya siasa kwa uwazi bila kunyanyaswa. Vijana hao walishiriki katika maandamano wakiwa katika Sare za CCM na Mheshimiwa Rais naye akiwa katika Sare rasmi,, akawapokea na kuwashudumia, iwapo hiyo inawezekana, basi kumbe wana haki ya kushiriki kwenye shughuli za vyama wanavyochagua wenywewe bila kulazimishwa.

Ninaamini sasa ukurasa mpya umefunguliwa kwa vijana wetu kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za siasa pale wanapoamua kufanya hivyo na kwa kuzingatia Sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ya ajabu kukataza ushiriki wa vijana wake katika shughuli za Siasa. Wanavyuo ni watu wazima, wana miaka zaidi ya 18 inayotambuliwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano kufanya shughuli za kisiasa, tena hao ndio wanaoandaliwa kuwa viongozi wa miaka ijayo. Kuwazuia kushiriki katika siasa ni kuwanyima haki zao za kisiasa. Mwalimu Nyerere alianza Siasa akiwa mwanafunzi na bila ushiriki wake katika Siasa, si ajabu Tanganyika isingelikuwa imefika hapa tulipofika leo. Ni muhimu vijana wakawa huru kushiriki shughuli za siasa, ili wapate ujuzi na uzoefu watakaohitaji katika maisha yao ya baadaye.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana (*Hansard*), nilieleza kuwa nimeletewa barua mbili rasmi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Singida Vijiji, wakati ule Mama Bernadetha Kinabo, akiwaandikia Watendaji wote wa Wilaya yake, kuwa Mtendaji yeoyote atakayeshirikiana na Kambi ya Upinzani, atachukuliwa hatua kali za kisheria na kinidhamu. Lakini wakati huo huo, barua ya pili, anayowaandikia Watendaji wa Vijiji na wa Kata, inawaagiza Watendaji hao watoe Shs.12,000 kwa kila kijiji ajili ya kuwasafirisha wajumbe wa Halmashauri Kuu wanaotoka Mkoa wa Singida kwenda kwenye Mikutano ya Kitaifa ya CCM. Ni dhahiri kabisa hapa kuna “*double standard*”, watakaoshirikiana na Upinzani watachukuliwa hatua, lakini siyo tu inaruhusiwa kushirikiana na CCM bali pia kuchangiwa fedha kutoka mfuko wa kijiji ambazo zinatokana na jasho au mchango wa kila mmoja wana CCM na wa Upinzani na hata wasio na vyama kabisa. Serikali iwe makini na kuingiza ubaguzi kupitia watendaji wa Serikali, ni jambo la hatari sana. Tuna taarifa kuwa, wafanyabiashara wanalazimishwa kuchangia Kampeni za Chama cha Mapinduzi, kuchangisha mwananchi yeoyote ni sawa lakini kulazimisha ni kinyume kabisa na Sheria za nchi hii. Ni imani yangu kuwa Serikali itatoa miongozo sahahi ili haki siyo tu itendeke bali pia ionekane inatendeka.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo ikiachiwa kuendelea itakuwa vigumu, kuamini kuwa Tanzania ni nchi ya demokrasia ya kweli, labda ya mdomo tu na mbele ya Taasisi za Kimataifa ili kuendelea labda kupata misaada yao. Kambi ya Upinzani inapenda kueleza masikitiko yake sana na pia kulaani vitendo hivi vya kulazimisha wananchi kuchangia au kufanya mambo ya kukipendelea Chama cha Mapinduzi na hasa kama vina baraka ya viongozi wa ngazi ya juu. Mfano wa hivi karibuni ni wa Waziri wa Utawala Bora, Mheshimiwa Sofia Simba ambaye kwa kushirikiana na Mary Chatanda, Katibu wa Mkoa wa Arusha, waliwalazimisha viongozi wa CCM Kijiji cha Gyekurum Lambo,Wilaya ya Karatu, kuvamia eneo la kijiji/mtaa na kujenga banda la mashine ya kusaga ambayo kwa mujibu wa ahadi hiyo atatoa Mheshimiwa Sofia Simba.

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha, ni kuwa eneo lililoshinikizwa ni eneo au mahali pasipofaa kwa kazi hiyo kwa kuwa eneo hilo liko mbele ya ofisi na karibu kabisa na uwanja wa mikutano wa wananchi. Waziri wa Utawala Bora, anadhaniwa kukuza na kulinda utawala bora na utawala wa Sheria. Lakini kwa Mheshimiwa Sofia Simba, ni tofauti, yeye ndiye anayeenda kuchochea uvunjifu wa Sheria kama alivyowahutubia wananchi wa Gyekurum Lambo, akidhani anabomoa ngome ya CHADEMA kumbe hafahamu Karatu, Wajinga ndio waliwao.

Mheshimiwa Spika, kama matendo hayo hayana baraka za viongozi wa juu, ni imani yetu kuwa wahusika hawa watachukuliwa hatua kwa kuichafulia jina CCM, Serikali na nchi yetu kwa ujumla. Vitendo hivi kutoka kwa watendaji wa Serikali vinashushia hadhi Serikali, wanaonekana kama viongozi wasio na maadili na wala hawajui wanaloofanya na badala yake wanawachanganya wananchi. Ni imani yangu kuwa, kwa kuwa Waziri Mkuu, Kiongozi wa Shughuli za Serikali yuko hapa, atakemea vitendo hivyo na kujenga heshima ya Serikali yake.

Mheshimiwa Spika, kutoka maeneo mbalimbali ya nchi, kuna taarifa mbalimbali za uonezi na unyanyasaji na wananchi wakati mwingine kuchukua Sheria mikononi mwao. Matukio ya wananchi kuvamia vituo vya Polisi na wakati mwingine kuondoka na wahalifu, au kuwapiga hadi kufa, yameendelea hata mwaka huu kuripotiwa kutoka maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Taarifa ya Mwaka 2007/2008 ya Tume ya Haki za Binadamu. Kama nilivyosema katika hotuba yangu mwaka 2006, 2007, 2008 na mwaka huu, pia ninaomba nigusie kuwa wananchi katika maeneo mengi ya vijiji wanapata unyanyaswaji mkubwa kutoka Polisi na Mahakama. Kwenye maeneo haya au wananyimwa haki, hawasikilizwi au wanadaiwa rushwa wazi wazi.

Mheshimiwa Spika, mahali pengine viongozi hasa ma-*VEO* bado wanawapiga wananchi au wanawaweka kwenye *lock up* zisizostahili kama vile kuwaweka kwenye maghala ya mbegu yenyе dawa. Wilaya kama Bukombe, Kishapu na zilikutwa hazina Mahakama za Wilaya na wananchi wake kuhangaika sana kufuata huduma za Mahakama Wilaya nyingine, tena kwa gharama kubwa na wakati mwingine kukaa *lock up* muda mrefu kwa vile ni vigumu kupata wadhamini katika mazingira ya Wilaya hizo za mbali. Manyanyaso haya yamejitokeza tena katika Taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu kwa kutozwa gharama kinyume na taratibu/rushwa. Tume ya Haki za Binadamu, ni chombo cha Serikali. Ziara zake zinagharamiwa kwa kodi za wananchi. Kambi ya Upinzani, inategemea kuwa, safari hii Serikali itatoa Kauli kali dhidi ya manyanyaso haya ambayo dhahiri yako chini ya uwezo wa Serikali kuyakomesha. Mheshimiwa Waziri Mkuu, alieleze Bunge hili ni hatua gani Serikali inachukua kukomesha manyanyaso haya.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyokuwa kwa Taarifa ya mwaka 2009, bado kuna unyanyasaji unaotokana na maamuzi mabovu katika ngazi ya Halmashauri za Miji, Manispa na Wilaya, kama vile utekelezaji usio na mpango wa kuwaondoa Wamachinga na Mama na Baba lishe ambayo imewasababishia upotevu wa mali na kuwarudisha

katika lindi kubwa la umaskini na upotevu wa mali pamoja na wengi kukosa kazi na hivyo familia zao kuathirika sana. Suala hili nalo liko chini ya uwezo wetu kuliweka sawa, hatuhitaji fedha za kigeni hata kidogo, inatakiwa mipango sahihi na bora tu kuwahudumia wananchi wetu hawa, ambao kwanza katika mazingira ya kawaida, wanahitaji msaada ili wajikwamue katika hali yao ya kiuchumi. Kwa kuwafukuza fukuza na kumwaga mali zao kidogo, tunawafukarisha zaidi, jambo ambalo ni kinyume kabisa na dhana na sera ya Taifa ya MKUKUTA. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa mwongozo na maelekezo stahiki kwa Halmashauri za Miji na Majiji, kusimamia utekelezaji bora wa Mipango Miji na kuondoa usumbufu. Mji au Halmashauri itakayoshindwa kutekeleza maagizo hayo, ichukuliwe hatua za kinidhamu na kisheria ikiwa lazima.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inarudia tena rai yake ya kuitaka Serikali kutazama upya mapema iwezekanavyo Sheria na 7 na 8 hadi 11 kwa na kuzihuisha na Sheria za Fedha ya Umma na Manunuzi ya Umma, kwa lengo la kuleta ufanisi zaidi katika Serikali za Mitaa na kuondoa migongano iliyoko sasa. Naipongeza sana Serikali kwa kukubali kuwa na mfumo maalum wa Wakaguzi wa Ndani hadi ngazi ya Taifa jambo ambalo tuna imani litaimarisha sana usimamizi na udhibiti wa fedha na rasilimali za umma katika ngazi ya Halmashauri. Ni imani yangu, Sheria inayohusu Mkaguzi wa Ndani, itawasilishwa Bungeni katika Bunge hili la 20 angalau kupitia *Written Laws Miscellaneous Amendment*. Hii ni kutokana na umuhimu wa Wakaguzi wa Ndani (*Internal Auditors*) katika kusimamia fedha za umma na rasilimali mbalimbali za Taifa letu katika ngazi ya Halmashauri, Wizara na Idara zinazojitegemea.

Mheshimiwa Spika, ni imani ya Kambi ya Upinzani kuwa kwa vigezo hivi tumejaribu kuonyesha maeneo mbalimbali ya udhaifu katika utekelezaji wa mipango mbalimbali ya Serikali. Kwa tathmini hii na kwa Bajeti Mbadala ya Kambi ya Upinzani iliyowasilishwa na Mheshimiwa Hamad Rashid, Mbunge wa Wawi na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, ni dhahiri kuwa kuna upungufu mwingi sana katika utekelezaji wa Sera, Ilani na Kauli ya CCM. Ni dhahiri kuwa, umaskini wetu haukuletwa na Mwenyezi Mungu bali unatokana na Sera zisizo sahihi, vipaumbele vilivyopinda vya Serikali ya CCM, Kauli nyingi tamu katika maandishi lakini zisizoendana na hali halisi katika tarakimu katika vitabu vya fedha, usimamizi usio makini wa fedha na rasilimali za umma. Kwa upungufu huu, Watanzania ndio wenyewe kuamua kama wanaridhika na Chama Tawala, CCM ama la, wananchi wakiwa makini na kama hakuna mchezo mchafu na kwa jinsi wananchi walivyochoka na CCM, Kambi ya Upinzani ina uhakika ukweli utajulikana mwezi Oktoba katika Sanduku la Kura. Watanzania wanastahili kupewa Taarifa zenye kuwasaidia kuingia katika uchaguzi wakijua masuala mbalimbali yanayohusu maisha yao. Kambi ya Upinzani, inapenda kupata Taarifa na majibu ya kina kuhusu hoja hizi. Mwenyezi Mungu atupe busara zake kama tunavyoomba kwenye Dua kila siku asubuhi.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa namna ya pekee, niwashukuru sana Dr. Kashillilah, Katibu wa Bunge na timu yake ya wataalamu wa Bunge, kwa huduma nzuri

waliyotoa kwa Kambi yetu kipindi chote cha miaka mitano. Ninatoa pia shukrani za dhati kwa Mratibu wa Kambi ya Upinzani, Ndugu Oliver Mwikila, kwa kuhudumia Kambi kwa muda wa zaidi ya miaka 6 sasa, Ndugu Frank Mbumi, Mama Salvina Mahundu (*Secretary*) na Grace Gwivaha (Mhudumu), kwa huduma nzuri walizotoa kwa kipindi chote.

Mheshimiwa Spika naomba nikushukuru tena kwa kunipa fursa hii na pia nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na nakushukuru lakini siungi hoja mkono. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, nikuhakikishie tu na pamoja na Kambi yote ya Upinzani kwamba hotuba hii kama ilivyo, inaingia kwenye *Hansard*. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, basi tumefikia tamati ya kazi ya mchana huu, kama nilivyosema maombi ya kuchangia ni zaidi ya 86, lakini Katibu amefanya hesabu hapa, tuna dakika 620 za kuchangia. Kwa hiyo, tutawezesha wachangiaji 62 kwa dakika 10, 10. Kwa utaratibu huo, basi michango itaendelea hadi kesho kutwa Ijumaa, saa 6.00 mchana ili kutoa nafasi kwa Mawaziri, Waziri wa TAMISEMI na Naibu Waziri pia kuanza kujibu hoja hadi saa 7.00 mchana, ni saa moja kwa hao wawili...

**MBUNGE FULANI:** Watatu.

**SPIKA:** Ndio watatu, kila mara tunamsahau Waziri wa Nchi, Sera, Uratibu na Bunge, ni mwenzetu sana huyu. Kwa hiyo, watakuwa watatu mpaka saa 7.00 mchana na saa 11.00 jioni siku ya Ijumaa, Mheshimiwa Waziri Mkuu, atahitimisha hoja yake na tunadhani basi kuanzia saa 12.00 siku hiyo tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi. Mkumbuke kwamba Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ina mafungu saba ambayo yote inabidi tuyapitie. Ndiyo maana tumetenga muda wa kutosha ili tuweze kuyapitisha, muda usipotosha basi tutakwenda kwenye Kanuni ya 104 isiyopendwa kabisa inaitwa *guillotine*, lakini natumaini saa mbili hizo zitatusaidia hoja za msingi zikaweza kujadiliwa.

Kuanzia saa 11.00 jioni wale Waheshimiwa 80 wataanza hawa wafuatao ili wajiandae. Wa kwanza ni Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, atafutiwa na Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Diana Chololo, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu na wa saba ni Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa. Watakaofuata baada ya hapo ili nisitumie muda mrefu kuwataja watatajwa saa 11.00 jioni.

Hakuna tangazo lingine, ningeomba kuwakumbusha Waheshimiwa Mawaziri kwamba tulivyotengua Kanuni, hotuba za kuwasilisha Makadirio ni dakika zisizozidi 30. Kwa hiyo, waje na vitabu lakini wawe wameandaa muhtasari ambao unaelezea malengo

muhimu, hiyo inatosheleza kabisa. Waheshimiwa Wabunge, sasa nasitisha Shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

(*Saa 7.30 mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 jioni*)  
(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

*Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Ishirini Kikao cha Nane.

## **HOJA ZA SERIKALI**

**Kama** alivyowaeleza Mheshimiwa Spika asubuhi, tunaendelea na Hoja ya Waziri Mkuu na niwakumbushe Waheshimiwa, dakika zetu ni zile zile, kwa hiyo, ukianza, anza moja kwa moja. Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, atafuatiwa na Mheshimiwa Castor Ligalama.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kushukuru kwa kupata nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza lakini itabidi nizungumze kwa uchache mengine niandike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Same Mashariki, kwa heshima walionipa, wakani-expose kitaifa, kimataifa, ni kwa sababu ya kura zao. Kwa hilo, nawashukuru sana na nitaendelea kuwashukuru wakati wa kura za maoni. Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, niwashukuru wapiga kura wangu kwamba katika kipindi cha takribani miaka mitano, tumeshirikiana pamoja kuibua miradi na tumefanya kazi nyingi sana za pamoja, naomba niseme, ukweli maendeleo mtu unajilettea mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije mahali ambapo ningependa kupaongelea vizuri. Naomba niipongeze sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya Awamu ya Nne. Naomba nitumie mfano mdogo tu kwa kifupi. Watu tujue kuna tofauti ya mke na kimada au mke na hawara, kuna tofauti kubwa sana. Siku zote kimada anamkosoa mke kwamba hajui kumwangalia mume, hajui hivi, ndiyo kawaida. Kwa hiyo, naomba mpaka hapo tuelewani. Mfano si mbaya lakini ndiyo maisha ya kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, naomba niizungumzie, kwangu mimi kwenye Jimbo la Same Mashariki imefanya mambo

makubwa ambayo yalikuwa hayajawahi kufanywa katika Jimbo la Same Mashariki tangu ulimwengu umeanza kuumbwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina Kata nne tambarare, nina Kata kumi ziko milimani na ni milima mirefu sana, ni Awamu ya Nne tu ambayo imeweza kufanya mambo makubwa kwenye Kata zangu kumi za milimani. Naishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Sasa hivi ukienda Miamba, ukienda Lugulu, ukienda Mtii, ukienda Bombo, ukienda Kirangare, ukienda Vuhna, barabara zote ziko kama barabara za tambarare. Yote hii ni kazi ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Naomba niseme ukweli Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya jitihada kubwa katika kuleta maendeleo kwa wananchi wake kwa sababu Jimbo langu lipo Tanzania na kila mtu mwenye Jimbo lake atazungumzia Jimbo lake. Kwangu mimi naomba niisifu Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwamba wenyewe wanaoishi kule milimani wanasema tangu wameanza kuishi milimani hawajahi kuona barabara za namna ile. Leo hii nikizungumza hapa nina Kata nne za tambarare, lami imenzia Maore inakwenda Mkomazi. Hivi niilaumu tena hiyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi? Siwezi. Mtu yejote akienda Same Mashariki, atakayeisema Serikali ya Chama cha Mapinduzi vibaya, nakwambia ukweli atalogwa. Naomba niseme ukweli Serikali ya Chama cha Mapinduzi Awamu ya Nne, chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Jakaya Kikwete, imefanya maajabu sana. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongee tatizo moja ambalo naomba Serikali mlifanyie kazi, nimwombe mwenyewe Mkuu wa Kazi za Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliangalie japo nitaliandika kimaandishi. Tuna msitu unaitwa Msitu wa Shengena. Huu msitu ndio unaofanya Same Mashariki iishi lakini umeingiliwa na majangili ambao wamekwenda kuchimba dhahabu kwa njia batili, wanakata miti kwa njia batili. Ninaiomba Serikali kwa sababu ina mkono mrefu, nafahamu Wilaya inajua, Mkoa unajua lakini Serikali Kuu naomba mchukue nafasi mwende kwenye msitu wa Shengena kuna mambo makubwa yanafanya huko. Nitaandika kimaandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumze na Watanzania. Naomba kuzungumza na Watanzania wote kwa ujumla wao. Tupo wakati wa uchaguzi sasa. Tunakwenda kwenye uchaguzi mkuu twendeni kwa amani. Uchaguzi sio vita, twendeni kwa amani ili nchi yetu iendelee kuheshimika. Lakini niwaambie Watanzania kura zenu, ni mali zenu. Kura ya Mtanzania mmoja ni mali yake. Hebu mchague kiongozi unayeona kwamba anatetea maslahi yako na maslahi ya Taifa. Sisi sasa hivi tunataka mabadiliko, tunataka wanaoingia humu ndani wawe wanakuja kutetea maslahi ya wananchi na maslahi ya Taifa. Tunawaomba Watanzania msije mkaanza kulaumu Wabunge, Wabunge, mnawachagua nyie wenyewe. Angalia huyu Mbunge, je, ataenda kutetea maslahi yangu huyu, angalia huyu Mbunge ataenda kutetea maslahi ya Taifa huyu? Wananchi wa Same Mashariki, mimi mwenyewe Anne Kilango Malecela, mkiona kwamba sikutetea maslahi yenu, sikutetea maslahi ya Taifa hili, msinichague na sitawalaumu kwa sababu nitakuwa nimefanya makosa, sikufanya kazi niliyostahili, nitawaomba radhi. Tunachotaka sasa, tunataka viongozi wakuja kuitoa hii nchi hapa

kuipeleka pale na ninawasihi Watanzania kasitokee kakundi kadogo kakawachagulia viongozi, hiyo ni dharau. Yaani wanawaonesha nyie kwamba hamna akili timamu, hamjui anayefaa, hamjui asiyefaa wanaojua wao? Hapana, chagueni viongozi nyie wenyewe. Mimi kule kwangu, Jimbo la Same Mashariki, unamwangalia kabisa huyu katumwa huyu, unajua kabisa huyu katumwa, pikipiki na vitu vingine, hakuna, acheni wananchi wachague viongozi wao wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, nizungumze jambo la kulalamika. Magazeti mawili haya, haya hapa, Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakuomba uandike nakusihi. Kuna Gazeti linaitwa Tazama na lingine Mkakati. Haya magazeti mimi nashangaa Waziri wa Habari, magazeti mengine yakitelea kidogo, anayafungia, haya hata siku moja sisikii yakifungiwa na kazi ni kutukana viongozi mchana na usiku. Leo yatamtukana Spika, kesho watamtukana Mudhihir, kesho kuwa Anne Kilango, mtondogoo Mwakyembe, hawajitukane wenyewe na kinachoniudhi wenyе magazeti haya wamo humu humu ndani. Nitamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anafunga atoe kauli ya Serikali kuhusu magazeti haya ambayo yanatukana viongozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kitu cha ajabu, magazeti haya hayauzwi, yanatolewa bure. Kwangu mimi milimani kule yanapandishwa na maroli, asubuhi watu wakiamka yamemwagwa magazeti 10,000 ili tu waone Mbunge wao asivyofaa. Wanantoa picha yangu Anne Kilango, hapa kando wanamtoa mtu atakayegombea lakini eti huyo atakayegombea kamuegemea mke wa Kiongozi Mkuu wa Nchi. Huyo anafaa huyo? Kwa nini asijitoe yeye picha yake na yangu mimi, yeye kamwegemea mtu mkubwa, ina maana hana miguu, mbavu zake ni mbovu, hana kiuno imara, kwa hiyo, hawezi kujisimamia mwenyewe, ni mpaka aegemee mtu mwengine, hafai huyo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba viongozi wakienda kutafuta uongozi, waende kwa sifa zao, wasitumie majina ya viongozi wetu. Wengi wanakwenda wanamtaja Kikwete, kule Jimboni kwangu wanasesma ametumwa na Makamba. Mimi naomba Mheshimiwa Makamba atokeze wazi akatae maana wanalala mchana na usiku kule, wanatoa pesa, wanafanya kazi zao kutwa wanasesma, “mimi nimetumwa na Makamba, mimi nimetumbwa na Makamba”, ni uongo, Makamba atatumaje mtu aende kwenye Jimbo ambalo si lake? Makamba kwao ni Bumbuli, Same Mashariki ni kwetu, akutume wewe uende kule ili nini? Wanatumia majina ya viongozi vibaya kwa sababu hawana uwezo. Naomba viongozi wote amba majina yenu yanatumika vibaya, muwashushue hawa watu wazi, kwamba waende wakatafute kura wao wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusicheze na amani ya nchi jamani tutajuta...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Hiyo ni ya pili?

**WABUNGE FULANI:** Ya pili.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Haya naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana, hasa kuhusu Msitu wa Shengena uelekee *Mkomazi National Park*. Sasa namwita Mheshimiwa Castor Ligalama atafuatiwa na Mheshimiwa Diana Kilolo.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda nichukue nafasi hii, kuwashukuru wananchi wa Kilombero, kwa ushirikiano walionipa miaka hii mitano ya uwakilishi hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda pia niishukuru Serikali, wananchi wengi wamenipigia simu hasa wakulima wa miwa, wakishukuru kuondolewa kwa kodi lakini nataka niseme kitu kimoja. Imejitokeza dhana hapa Bungeni ambayo jana nimeisikia kwa mara ya pili ambayo kama haitakemewa, itatuweka pabaya katika Bunge letu. Kuna dhana ya *Regionalization*, sijui inatoka wapi? Suala zima la mchakato wa msamaha wa kodi, ni mchakato ambao sisi katika Wilaya yetu tulianza mwaka 2006 kabla hata Mheshimiwa Mkulo hajawa Waziri wa Fedha. Mwaka jana katika kipindi kama hiki, wakati tunazungumzia miundombinu ya barabara, Waziri Mkulo naye alishambuliwa hivyo hivyo, kwa sababu anatoka Mkoa wa Morogoro kafanya hivi. Jana tena kauli hiyo imetoka na kauli hizi zinatoka sehemu moja katika nchi yetu. Kama tutaacha kauli hizi ziendlee, kwa kweli *regionalization* itakuwa inaanza kidogo kidogo. Nchi hii ni moja, sisi kwa mfano tuchukue suala la maji kupelekwa Shinyanga, Kahama, ule mradi ume-cost shilingi bilioni 250 kwa Mkoa mmoja lakini tulielewa katika nchi na Utaifa wetu kwamba wale wenzenetu wanashida ya maji, *no body complained*, sasa inapotokea sehemu nyingine kidogo tu, tayari tunasikia maneno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Cheyo kama angekuwepo angeweza kuja kwangu aulize tumefanyaje, tulimuajiri *Tax Consultant* kuieleza Serikali jinsi gani wakulima wa miwa wanavyoweza kulipa kodi ile mara tatu kwa sababu kama analipa VAT kwa kukata miwa, VAT kwa kupakia kwenye roli, VAT kusafirisha kwenda kiwandani na VAT kwa sukari atakayotumia maana ni kodi ya mlaji inatozwa mwishoni. Kwa hiyo, tukajenga hoja mwaka 2006/2007 na 2008, tukamuajiri *Tax Consultant*, ndiyo huyo Serikali ikamuelewa zikafutwa zile mbili za kukata na kupakia na mwaka huu

wametoa hii. Kwa hiyo, tusiende kuleta mambo ya *regionalization* ambayo yanatokea hapa katika Bunge letu Tukufu, tuikemee mapema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano sisi tuna vyanzo viwili vyaa umeme, Kidatu na Kihansi. Lakini sisi tunaangalia nyaya zinapita juu hatuna umeme, vijiji vyetu viko gizani. Mimi naweza kuropoka, nikasema *brand statement* kwamba Ngeleja hapeleki umeme katika Wilaya ya Kilombero, umeme wote anapeleka Sengerema tu. Nitakuwa mtu wa ajabu, ndiyo maana tunaendelea kuiomba Serikali jamani kule wananchi wale vyanzo vile vimeanzia kule wanajisikia vibaya, wasaidieni. Kwa mara ya tano katika Bunge hili tangu niingie, naeleza jambo hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimo Kwanza. Kuna Mikoa minne ambayo inazalisha chakula kwa wingi ambayo ni Rukwa, Mbeya, Iringa na Ruvuma na sasa hivi wameingia Morogoro na Kigoma. Mimi nimewaza sana juu ya huyu mkulima anayezalisha, mkulima huyu kwa sasa anakuwa kama ni mkulima wa kuzuia njaa nchini kwa sababu yeye mwenyewe binafsi hana maendeleo sana, sana sana Mkoo ule unazalisha kwa wingi ukijumlisha Mikoa yote sita nchi inakuwa haina njaa lakini Serikali inaogopa njaa kwa sababu kuna Mikoa mingine haina mvua nyingi na hii inajulikana, takwimu zinajulikana, hali ya hewa inajulikana. Mimi nina wazo moja, ile Mikoa ambayo haina mvua nyingi, bahati nzuri Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala katika taarifa yake aliiata, Mikoa hii ambayo haina mvua nyingi walazimishwe kulima mtama mfupi halafu Serikali inunue ule mtama na ikishanunua ule mtama wale kama hawataki kula mtama, Serikali itaweka mtama kama akiba ya njaa ili wale wa Mikoa ile sita wanaolima mahindi na mpunga, wawe huru kuuza popote, wabadilike hali zao za maisha. Nafikiri naeleweka katika hili. Ukiwa na njaa, huwezi ukachagua chakula, hata mtama utakula tu na bahati nzuri hawa wenzetu wanye mvua chache wana kitu kingine mbadala, wana ufugaji, kwa hiyo, anaweza akaiza ng'ombe akapata hela akanunua mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana, sisi tulipata mpunga wa kutosha lakini mpaka mwezi Machi, bei ilikuwa chini sana. Nimetoka huko juzi, mwaka huu *Alhamdulillah*, Mwenyezi Mungu ametupa mapato mazuri lakini bei ya mpunga debe moja ni Sh.3,000/-, gunia la debe nane ni Sh.24,000/-, huyu mkulima ambaye mwaka huu amenunua hata mbolea ya ruzuku, gharama za uzalishaji zimeongezeka na kuwa Sh.24,000/- kama akipata gunia labda 20 jumla 480,000/- zitambadilisha vipi? Lakini mwaka juzi kulikuwa na ka-*free trade* ka-namna fulani, bei ya mpunga ilifika mpaka Shs.60,000 – Shs.70,000/-, mara gunia 20, anapata Shs.1,400,000/- pale ana uwezo wa kumsomesha mtoto, ana uwezo wa kula vizuri, anaweza kununua bati akaezeka nyumba yake na hali ya maisha ikabadilika na tukasema kwamba kweli mkulima huyu anabadilika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tutafanyaje? Tumeunda ile Bodi ya Mazao Mchanganyiko, sijui Bodi yenye we imeshaundwa lakini Sheria ya Mazao Mchanganyiko, tumeshaipitisha. Wale ndiyo wangewasaidia wakulima hawa kuwatafutia masoko chini

ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Sasa Sheria tumepitisha, Bodi haijaundwa, mazao ndiyo hayo tumepata, wakulima wetu wanabaki vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi namsemea sana mkulima huyu ili tumbadilishe na ili Kilimo Kwanza kiwe cha manufaa kwake. Kule kwetu katika Wilaya ya Kilombero tayari wawekezaji wakubwa wamekuja na wengine wengi zaidi wanakuja, hivyo tunahitaji umeme uende sawa sawa na uwekezaji kwa sababu ndiyo utafumua *agro processing industries*. Zile *agro processing industries* zitamsaidia mkulima kubadilika badala ya kuuza mpunga auze mchele, badala ya kuuza mahindi auze unga ambao umekuwa *packed* kupeleka kwa wenzetu ambao hawana chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mashamba wananchi wame-*improve*, maafisa ugani wamefanya kazi zao, tija imeonekana kwa *acre* ukifananisha mwaka 2005 na sasa hivi *production per acre* ni kweli imeongezeka kutoka katika takwimu zilizotolewa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu. Ni kweli imefikia karibu tani tano kwa hekta moja. Tulianza na tani tatu. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu kupitia hotuba hii ya Waziri Mkuu pamoja na Waziri wa TAMISEMI. Kabla sijaanza kutoa mchango wangu, naomba nitoe pongezi kubwa sana kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi ambavyo amekuwa mahiri sana katika kusimamia Ilani ya Uchaguzi akiwa kama Mtendaji Mkuu, Mungu ambariki sana. Vile vile nampongeza Mheshimiwa Celina Kombani, Mama ambaye ametuwakilisha vizuri, ameonyesha uwezo wa juu kiasi kwamba akina mama wenzake tunajivunia uwezo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitamtaja Mheshimiwa Philip Marmo - Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mchango wake mkubwa katika Serikali hii ya Muungano wa Tanzania. Vile vile naomba niwakumbuke Watendaji kuanzia Makatibu Wakuu, Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Katibu Mkuu Ofisi ya TAMISEMI pamoja na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa hotuba hii kwa kumsaidia Waziri Mkuu. Napenda nisimsahau *best* wangu Mheshimiwa Mwanri kwa kazi kubwa anayofanya kumsaidia mwanamke mwenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi, naomba nionyeshe masikitiko yangu katika hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Hotuba hiyo ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Spika alisema kwamba aghalabu hakuisoma yote, lakini itaingia jinsi ilivyo katika *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni habari kubwa, inasomwa dunia nzima. Ukitosha hotuba hiyo ukurasa wa 29 kifungu kidogo cha 117, ningependa kupata maelekezo yako, anasema Chama Tawala kimejaa rushwa. Rushwa mpaka kwenye vilabu tunatoa hela, tunatoa jezi, sijui tunatoa na nini huku siyo kukichafua Chama Cha Mapinduzi? Kwa nini msemaji huyu asithibitishé kama yupo aliyemkamata si athibitishé hapa ndani ya Bunge la Muungano wa Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Bunge hili linataka tuseme kweli tumekula viapo baada ya kuomba hilo ambalo ninajua utalifanyia kazi, naomba niendelee kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niipongeze na Serikali ya CCM kwa jinsi ambavyo inajitahidi kutuletea maendeleo Watanzania pamoja na Mkoa wa Singida. Kwa kweli Mkoa wa Singida ni mambo mengi sana mazuri yaliyotekelizwa ambayo yamebadilisha kabisa hali ya Singida. Singida ya leo siyo Singida ambayo mlikuwa mnaijua Waheshimiwa Wabunge tembeleeni Singida. Vilevile nitamnyima haki Dr. Kone kwa jinsi ambavyo amekuwa mahiri katika kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi katika Mkoa wa Singida kwa kweli Mkuu wa Mkoa huyu nadhani kufika kwake Singida ni mpango wa Mwenyezi Mungu kwasababu aliyotufanyia ni mambo mengi sana ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuu wa Mkoa huyu amefika, ameanzisha ujenzi wa Hospitali ya Rufaa. Mimi nilikuwa namhoji kwenye *RCC*, hivi mwenzangu umewasiliana na Serikali kuna hela? Akasema Diana tuanze hivyo hivyo na nguvu za wananchi tutatafuta na Wahisani mpaka tulipofika inatia moyo kwelikweli. Shahidi ni Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipofika kwenye ziara ya Mkoa wa Singida ameona ujenzi wa hospitali hiyo. Ombi langu kwa Serikali mwaka jana bajeti iliyokwisha walitutengea bilioni mbili na mwaka huu wametenga hivyo hivyo kwa jinsi hospitali hiyo ambavyo itakuwa kubwa ikikamilika itakuwa na majengo makubwa 28, kwa utaratibu huo tutajenga hospitali hiyo sijui kwa miaka sijui 28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiambia Serikali, hebu itafute njia mbadala kutusaidia ili tuweze kujenga hospitali hiyo kwa muda mfupi. Nilikuwa ninaiomba Serikali, hebu tujaribu kuangalia mpango uliotumika kujenga *UDOM* - Chuo Kikuu cha Dodoma tumetumia njia nzuri tu, tumeomba Mashirika mbalimbali *NSSF*, *PPF*, *PSPF*, *LAPF* na mashirika mengine, hebu naomba nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu afikirie namna ya sisi wana Singida kutuunganisha na haya mashirika wapate zamana ya Serikali waweze kutusaidia kujenga hospitali hiyo ili hospitali hii tuweze kuimaliza kwa muda mfupi, hospitali ambayo itakuwa mkombozi kwa Mkoa wa Singida, hospitali ambayo itakuwa mkombozi kwa Mikoa ya jirani Dodoma, Tabora na hata Manyara, ukizingatia Singida sasa hivi kwa suala la usafiri hatuna tatizo ni lami kila upande. Singida, Manyara tayari mradi umeanza, kwa hiyo, hospitali hii ikikamilika itakuwa ni msaada mkubwa sana kwa suala la matibabu kuliko ilivyo sasa hivi wananchi wanakwenda Muhimbili mbali, wanahangaika ukizingatia wananchi wetu kipato chao ni duni sana. Ninaamini Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa tabia yake na kwa jinsi alivyopendezwa na mradi huo atatamka lolote wakati tunafanya majumuisho katika hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba niongelee suala la ujenzi wa vituo vya kilimo. Sisi Singida tumeitikia wito huo kwa kuona ni suala muhimu sana, hata wakati wa ziara yake Mheshimiwa Waziri Mkuu alikiona Kituo cha Gumanga. Sasa kituo hicho kama tutakuwa na vituo vya aina hiyo kwa kila Kata tayari ni ukombozi katika suala zima la kilimo kwasababu elimu ya kilimo, Maafisa Ugani watatumia vituo hivyo, hata Maafisa Mifugo watatumia vituo hivyo, Maafisa Uvuvi watatumia vituo hivyo, hata

wenzetu hawa wakala wa pembejeo watatumia vituo hivyo na hata mambo yote yanayousika katika Kilimo Kwanza yatatumika katika vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, niendelee kuisihi Serikali, Singida tunajitahidi sana kupiga hatua lakini tunahitaji sasa *support* ya Serikali. Ni kweli kuwa kila Mkao unahitaji *support* ya Serikali lakini Mikoa inapishana kimaendeleo. Iko Mikoa ambayo imepiga hatua sana, mimi ninadhani kuna kila sababu kuangalia Mikoa ambayo ilibaki nyuma kwa muda mrefu kupewa kipaumbele ili na sisi tusogee mahali wenzetu walipo. Nitashukuru sana katika miradi ambayo imeibuliwa Singida na Mkuu wetu wa Mkao ambaye ameonyesha imani na Singida, akipata *support* ya Serikali sisi Singida tutakuwa tumeondoka mahali tulipo, kwa sababu hata sisi viongozi wote wa Mkao wa Singida tuko bega kwa bega na Mkuu wetu wa Mkao wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, naomba nizungumzie kuhusu suala la mambo ya UKIMWI. Ninaipongeza Serikali kutoa ajira kwa waratibu wa masuala ya Ukimwi kwa kila Mkao. Sasa nawamba viongozi wa Mikoa wawatumie hawa Watendaji wa TACAIDS ili Watendaji hao waweze kufanya kazi zao vizuri na itakuwa ni vyema zaidi iwapo Serikali itafkiria kuwa karibu zaidi ifikirie pia kuwaajiri pia Waratibu hao kwa ngazi ya Wilaya ili huyu mratibu aliyeko Mkoani, apate wenzake wa kumpa taarifa ili janga hili la UKIMWI liweze kupata nguvu kubwa ya kupambana nao ili tuweze kulitokomeza.

Ndugu zangu, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana, naunga mkono hoja.  
(*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Diana Chilolo. Katika mchango wako, umelalamikia suala la hotuba ya Kambi ya Upinzani ukurasa 29, nadhani kifungu cha 17. Jambo hili tutampelekea Mheshimiwa Spika na yeze atalitazama na kwa wakati muafaka atalitolea maelezo kwa sababu lingekuwa ni la Mheshimiwa Slaa ningelifuatilia kwa karibu, lakini yeze ni msemaji Mkuu wa Kambi hiyo kuhusiana na suala lililoko mbele yetu. Kwa hiyo, hili limesemwa na Kambi nzima ya Upinzani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, atalifanya uamuzi siku zijazo. Tunaendelea. Namwita Mheshimiwa Anna Abdallah atafuatiwa na Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga.

**MHE.ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote katika ofisi yake Naibu Waziri, watendaji kwa hotuba nzuri na kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika kipindi chao chote cha Uongozi. Ninaomba nianze kwa kipongeza hotuba hii na kwanza kabisa niunge mkono hotuba ya Waziri wa Nchi (TAMISEMI) katika ukurasa wa 46 wa hotuba hii Waziri Mkuu ameeleza juu ya utekelezaji wa dhamira ya Serikali ya kuongeza uwakilishi wa wanawake katika ngazi mbalimbali za maamuzi na kwa mujibu wa taarifa hii tumefikia asilimia 31.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasema na ninasema kwamba dhamira ya kufikia *fivey fifty* ipo na ninamwomba Waziri Mkuu kuwa dhamira hii itekelezwe kwa mujibu wa Sheria kwa mfano, tungependa akina mama waingie katika ngazi za maamuzi kwa kura

hasa kwenye Udiwani pamoja na Ubunge. Hii asilimia nyingine ya Viti Maalum tunaiheshimu, iendelee, lakini tunaomba suala la wanawake kugombea kwenye Majimbo lizingatiwe.

Napenda kukishukuru sana chama cha *TWPG*, tulifanya Semina mwezi wa Pili kikawaalika Wenyeviti wa Vyama vya Siasa na tukakubaliana kwenye semina ile kwamba kila chama kihakikishe kwamba kinateua angalau asilimia 40 ya wagombea kwenda katika majimbo. Sasa kila chama kina taratibu na taratibu nyingine ni kura za maoni. Ninachoomba ni kwamba kama hakutakuwa na sheria ya kuhakikisha na kuvilazimisha vyama kuteua wanawake kwenda kwenye Majimbo na kwenye Kata hawataateua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hasa hili tatizo sijui niseme tatizo la kura za maoni, inaweza ikawa ndiyo kisingizio. Tumeanza kuona matokeo ya baadhi ya maeneo katika kura za maoni, sasa tukiendeleza namna hii, mimi sijui tutaischia wapi. Kwa hiyo, naomba suala la uteuzi kwenye vyama mtuachie hiari. Hatutafika! Wanashau kabisa kuwa vyama vinasahau kabisa kuwa wanawake ndiyo wapigakura wao wa kuaminika kwa vyama vyote. Kwa kutambua udhaifu uliopo, Jumuiya za Wanawake za Vyama vya Siasa hasa wenye uwakilishi Bungeni, tumeanzisha kitu kinaitwa Ulingo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kwamba tunautumia Ulingo kuhakikisha hivi vyama vinateua wanawake kugombea. Lakini kwa masikitiko katika kipindi hiki cha watu kupitapita huko kutangaza nia, kwa masikitiko makubwa tumeanza kusikia taarifa kwamba baadhi ya akina baba ndugu zetu, watoto wetu, wajukuu zetu wengine wakiona mwanamke amejitokeza katika Jimbo lake wanamwandama kwa matusi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna viongozi wengine wakubwa tu, wanashema ah, huyo mwanamke ye ye anapaka *lipstick*, huyo ni Malaya! Ebo! Wewe una mke nyumbani kwako, una mama yako aliyezuzaa, unachukua mke wa mwenzako kwa kuwa anataka kugombea unamwita Malaya! Kwa nini usimwite huyo uliye naye nyumbani mwako wewe? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashema hivi, sisi hasa mimi ambaye ndiye Mwenyekiti wa ule Ulingo sitajali Chama kama kuna mwanaume atamtukana mwanamke katika hatua za kutaka ye ye ndio apate, tunashema kuwa tutawahamasisha wanawake wote wa vyama vyote hivyo wasimpe kura huyo mwanaume. Haijalishi ni wa Chama gani! Kwa kweli ni mambo ya ajabu sana, tena utakuta sehemu nyingine wako sita, saba, wanagombea lakini kila akigombea mwanamke tu inakuwa nongwa. Tena mwanamke akijitetea akisema jamani mimi nimeolewa, sina hiyo sifa mnayosema, wanashema ah, kwani ni mwanaume huyu aliywao? Alah! Kama siye mwanaume sasa kaolewa na nani? Dharau hizi za nini kwa wanawake? Mnamtukana mwanamke na mnamtukana na mume wake!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hili jambo halikubaliki hata kidogo! Halikubaliki! Ninasema Ulingo tulikwishesemba hatutakubali wanawake kudhalilishwa.

Tunaomba vyama viteue wanawake na mimi nikiwa Mwenyekiti wa Ulingo huu nimekutana na wanawake wenyewe uwezo mkubwa sana, vyama vyote, wapo, lakini wanaogoa kugombea kwa sababu ya taratibu za ajabu ajabu tu kwenye vyama vyetu. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu hili jambo tulifanyie kazi, tukingojea hiari tu wateue kwa kupenda kwao hatutafika. Lakini naomba tu nitoe angalizo kuwa kwa kweli hatutakubali mwanamke kudhalilishwa wakati anatafuta haki yake ya kikatiba, hatutakubali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao akina baba wengi sana na baadhi yao ni Wabunge humu mpo, wapo wengine huko nje wanatuheshimu sana wanawake. Hawa ninaowasema ni wale wachache ambao hawajui kabisa kuwa walizaliwa na wakalala kwenye tumbo la mwanamke hawajui. Kwa hiyo, tulikuwa tunataka kusema hivi, mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi, akina mama wajitokeze na mimi ninawaomba wanawake wa vyama vyote wajitokeze wagombee. Akina mama ni wengi, tuna uwezo, tumejiandikisha na tutachaguana. Ule mtindo wa kusema kwamba ah, adui wa mwanamke ni mwanamke, haupo. Rafiki wa mwanamke ni mwanamke na kama wapo wanawake wenzetu ambao hawaungi mkono wanawake wenzao walegee na wapotee kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mimi nimeshangaa sana, nimesikia kwamba eti *UDOM* siyo sera ya CCM. Kwenye hotuba ya Waziri Mkuu ameeleza idadi ya wanafunzi walioko *Primary*, walioko Sekondari na walioko *High Schools*, hao ndio wanao-feed Vyuo Vikuu tulivyo navyo. Sasa hawa wanaosema ni sera yao, wanafunzi wa Vyuo hivi wangewatoa wapi kama hawatokani na sera ya CCM? Sasa tusipokuwa na tabia ya shukrani tusije tukalalamika kuwa watoto wetu au vijana wetu hawana shukrani kwa wazee wao, kwa sababu wanayasikia kutoka kwenu nyinyi mnaoanza kusema kwenye majukwaa. Kama kitu ni kizuri, sema hiki kizuri; kama kibaya sema hiki ni kibaya. Lakini kizuri, kibaya na kibaya kibaya kila kitu kibaya, kipi kizuri? Nasema huu siyo uungwana wala siyo tabia nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema kuhusu Kilimo Kwanza. Mheshimiwa Waziri Mkuu tukitaka Kilimo Kwanza kiendelee, lazima kiwe endelevu kiendane na mafunzo toka mtoto anapokuwa mdogo shulenii na nini. Lakini *JKT* ndiyo mahali pake na kule siyo hiki cha kupanda na kunini, hapana hata matengenezo ya matrekta, haya matrekta mnayoyataja humu yatatengenezwa wapi? Mimi naomba vijana wetu wa *JKT* watakopwenda kwa mujibu wa Sheria, wasomi wafundishwe mambo haya yakiwaingia kichwani watakuwa nayo, watakopokuwa Viongozi wa baadaye watakuwa wanajua kilimo bora maana yake nini na Kilimo Kwanza maana yake nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi sana suala la Magereza, sawa. Lakini pale Magereza anafanya kazi ile ya kilimo hicho kwanza kama ni adhabu wakati hii ya *JKT* ni jambo zuri na ni la hiari. Kwa kuwa wanaokwenda pale ni watu wenyewe nguvu, nina hakika tunaweza tukapata mafanikio makubwa. Ahsante sana na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mama Anna Abdallah. Sasa namwita Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga atafuatiwa na Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na afya katika siku hii ya leo nami nikasimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu kuweza kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja hii. Katika hotuba ya Waziri Mkuu, amesema kwamba Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ulikuwa huru na wa haki. Siwezi kupinga maneno yake, haya ni mawazo yake, lakini sisi tuliokuwa kwenye uchaguzi huo mstari wa mbele, uhuru ulikuwa mdogo na haki haikuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, walipita Watendaji wa Kata kama Wasimamizi wa Uchaguzi, walikuta matatizo vituoni na wakaelezwa, lakini hawakuweza kuchukua hatua yoyote na walisema uchaguzi uendelee, mtakutana Mahakamani, sasa mimi nikajiuliza kama mtendaji unasema uchaguzi uendelee mtakutana Mahakamani, wakati uchaguzi una matatizo, kweli hapa watu walitendewa haki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine watajua wananchi wenye we waliokuwa kwenye uchaguzi, na wanayaelewa wazi na uhakika uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, pamoja na kwamba kuna takwimu CCM imeshinda kwa asilimia 92, hayo ni mahesabu ya wafanya mahesabu, mimi sipo huko kwenye mahesabu. Tuangalie nini baada ya ushindi huu wananchi wananaufaika nacho au wanafaidika nacho? Au hao Wenyeviti ni kazi zipi zinakuwa nyepesi kwao na zipi zinakuwa ngumu kwao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza, karibu ya uchangazi kumeunganishwa Mitaa, Kata kama ya Nyamanoro ilikuwa na Mitaa arobaini ikawa na Mitaa tisa. Zoezi hilo la kuunganisha Mitaa limefanywa wiki moja kabla ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa, sasa huo ndiyo uchaguzi huru na wa haki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuunganisha Mitaa, mtu hajui mpaka wake unaishia wapi. Mtu mmoja anapiga kura zaidi ya mara mmoja, huo ndio tunasema ni uchaguzi wa haki na wa huru? Tunaomba uchaguzi mkuu usije ukafanywa kama uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupata Wenyeviti wa Mitaa na Mitaa imeungwa, kuna Mwenyekiti ameongezewa Mitaa saba au sita, Mwenyekiti huyu anafanya kazi kwa muda wote, anaweza akaamshwa saa saba usiku kulingana na hali yetu ilivyo, anaweza akaamshwa saa sita za usiku, asubuhi, mchana. Mwenyekiti huyu ameunda Kijiji ndani ya Mtaa na wakati mwininge anakuwa hata wale wananchi wanaoishi katika Mtaa wake hawaelewi vizuri. Ningewaomba Serikali waliangalie hili kwa sababu kutakuja hata wakimbizi ndani ya Mitaa tukiambiwa hawa ni wakazi wa mitaa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wenyeviti hawa wa Mitaa wanafanya kazi ngumu sana ya kuweza kuwahudumia wananchi wetu, lakini hawana posho ya uhakika, hawana mshahara, wao wanafanya kazi kutwa nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale pale Serikali ikamleta Mtendaji wa Serikali ya Mtaa. Mtendaji huyu wa mtaa ameajiriwa, anafanya kazi kwa masaa manane tu, akiingia saa mbili na nusu asubuhi saa tisa anaondoka na haishi katika Mtaa huo. Anaweza akaishi Kata mbili, au tatu mbele ya mtaa huo, au hata akaishi Wilaya nyingine kwa sababu haya Majiji yanaingiliana. Lakini pia Mtendaji huyo hana hata ofisi. Tuliamua kuunganisha Mitaa tukawaweka Watendaji wa Mitaa hawana ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtendaji kama huyu utamtafuta wapi? Utakapokwenda kwa Mwenyekiti, atakuandikia barua, atakwambia nenda kwa mtendaji akakugongee muhuri kwa sababu Serikali imesema Mtendaji ndiyo atakaa na Muhuri. Huyo Mtendaji hana ofisi, sijui *TAMISEMI* hawapeleki hela za ofisi, waliamua tu kuunganisha Mitaa na kuweka watendaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ningeomba Serikali iliangalie sana kwani linawapa adha wananchi wanaoishi kwenye Mitaa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, sijui Serikali inatumiaje uteuzi wa Watendaji hao wa Mitaa? Nina kaka yangu huwa nikimwambia neno moja huwa analichukulia haraka Mheshimiwa Mwanri, lakini hili nilimwambia Mheshimiwa Mwanri suala hili sijui alilichukulia viper!

Mhehimiwa Mwenyekiti, Watendaji wa Mitaa baadhi yao ni Walimu wa Shule za Msingi, sasa ofisi ya Mtaa inahamia shulenii, kati ya haya mawili sijui Mtendaji afundishe kwanza, au huyu Mtendaji kwanza ahudumie wananchi, kwa hiyo, utakuta shulenii watu wamejaa wakimsibiri Mtendaji wa Mtaa aidha, amalize kipindi aje awahudumie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali kupitia Wakurugenzi wa Halmashauri za Miji au Majiji kwa Mkurugenzi aliyefanya kitu kama hiki awaondoe Watendaji wale wa Mitaa kuwa Walimu, ama wachague kuwa Walimu ama wachague kuwa Watendaji wa Mitaa kwa sababu mambo yote ni muhimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja kusema elimu ya msingi inashuka wakati huo huo Mtendaji hana muda wa kufundisha, anawaza kazi mbili kwa wakati mmoja na zote zinatakiwa zifanyike. Atakapokaa darasani huku wananchi wanamtafuta mtendaji huyu yupo wapi. Kwa hiyo, naiomba Serikali ikalifanyie kazi jambo hilo, Mwalimu achague, ama abaki darasani afundishe watoto kwa kutuliza akili yake, ama anataka kuwa Mtendaji wa Mtaa aondoke kwenye ualimu tujue tuna upungufu wa Walimu, kuliko kusema tuna walimu wakati ni Watendaji wa Mitaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Kilimo Kwanza, Kilimo Kwanza nami sikikatai ni suala zuri, lakini tumejiandaaje na Kilimo Kwanza? Kwa sababu mtu ana shamba, ameshapita Serikali ya Kijiji, kijiji kimeshakaa kimemkabalia, anapofika katika

Halmashauri ya Mji anaambiwa kalete hati ya nyumba, Je, hivi kweli hata sisi watu wa Mjini wote tuna hati za nyumba? Sembuse huyu mtu wa kijijini pale Dodoma ana nyumba ya udongo Chini na Juu atakuwa na hati ya nyumba ile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafutwe urahisi wa mambo haya, huyu Mkulima atawezaje kupata mkopo ili na yeye ajiendeleze katika kuendeleza familia yake, lakini tukisema kwamba mpaka alete hati ya nyumba sisi wenyelewa wa mjini hatuna, hao wa Vijijini je? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka hapo unamkuta Afisa Kilimo wa Wilaya badala ya kumuweka chini na kumwelesha anamwambia hayo ni maneno ya wanasiasa tu. Kwa hiyo, mrudi huko huko kwa wanasiasa, hii si kauli ya Mtendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali ifuatilie Watendaji hawa, hawafai. Muwaeleweshe mtu ajue ni nini anachotakiwa kukifanya ili na yeye aweze kupata pembejeo, aweze kulima ajenge nyumba yake nzuri, asomeshe watoto wake na mmuachie auze mazao yake kwa bei anayoihitaji yeye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali kuitia hili, wajaribu kuwapa angalau darasa hata hao walimaji wa vijijini kwa sababu wao wameshajua watapata mikopo, lakini hawajui wataipata wapi. Likija zoezi la mafunzo wanapewa maofisa. Maofisa ndiyo hao wanaowajibu majibu hayo wananchi wa kule chini, sasa hao wananchi wanauliza, ina maana Kilimo Kwanza ni kwa matajiri peke yao? Kwa sababu tajiri ndiye atakuwa na hati ya nyumba hata kama anazo tatu ama nne zote atazikopea. Je, wasiokuwa na hati wataishia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala moja ambalo nilikuwa ninaomba nilifahamu kidogo. Katika bajeti ya mwaka 2008/2009 nilimwomba Waziri Mkuu kutenganisha Halmashauri ziwe Manispaa katika Jiji la Mwanza katika Wilaya ya Ilemela na Nyamagana. Kuna fununu tu ambazo ni za chini chini nimezisikia kwamba hili Waziri Mkuu amelikubali, lakini wengine hatujui limefikia wapi. Utekelezaji wake utakuwepo lini? Ni katika hizi fununu za chini chini tulidhani kwamba katika bajeti hii Halmashauri hizi mbili kila mmoja itajitegemea ili kuleta maendeleo katika Wilaya husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameweka Wilaya mbili katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza kwa kuwapunguzia wananchi safari ndefu, lakini watalaamu wote wako katika Halmashauri ya Jiji mjini, lakini kuna wananchi wanatoka mbali na wengine wanatumia nauli, wengine wanapanda mabasi mawili. Lakini wakimhitaji Mkuu wa Wilaya wanampata kiurahisi kwa sababu tayari Mkuu wa Wilaya yupo katika eneo husika. kwa hiyo, ninaiomba Serikali katika hili angalau liongezewe nguvu Halmashauri hizi ziweze kujitenga na kila mmoja ijitegeme ili kuleta mashindano ya maendeleo katika Halmashauri za Jiji la Mwanza.

## **MWONGOZO WA MWENYEKITI**

**MWENYEKITI:** Mwongozo Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikutaka kumwingilia Mheshimiwa Mbunge wakati akiongelea kuhusu Mwalimu wa Shule ya Msingi ambaye pia ni Mtendaji wa Mtaa, hili jambo ni jipya, pengine atuambie baadaye ni shule gani hiyo, Mwalimu anaitwa nani na pia ni Mtendaji wa Mtaa gani, la sivyo afute usemi huo kwa sababu utaratibu huu ni mgeni kabisa katika utendaji wa shughuli zetu.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitathibitisha usemi huo.

**MWENYEKITI:** Sijakupa nafasi bado. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga umemsikia Waziri wa Nchi, amezungumzia kuhusu hotuba yako, naomba upitie maelezo yako.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitathibisha kwa sababu hata hapo awali nimesema kwamba nilishamweleza Naibu Waziri wa TAMISEMI suala hili, nitathibitisha na siyo shule moja, na nitamwambia Waziri. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tuendelee na meza itapenda kujuu uthibitisho huo. Namwita Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu baada ya kumsikia Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga Jecha atafuataiwa na Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa.

**MHE. ISMAIL JUSSA LADHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Tunajadili hotuba ya bajeti ya Waziri Mkuu ambaye kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano Ibara ya 52, Ofisi ya Waziri Mkuu ndiye mwenye dhamana ya kusimamia udhibiti, usimamiaji na utekelezaji wa shughuli za siku hadi siku za Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, tunapozungumzia Ofisi ya Waziri Mkuu tunazungumzia kwa hakika utendaji wa Serikali nzima iliyopo hapa. Kwa sababu hotuba ya Waziri Mkuu ilijikita katika kufafanua mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Nne, yakielezwa kwamba ni utekelezaji wa ilani, ningeomba na mimi nijikite hapo kuitathmini Serikali hii kwa miaka minne imefanya nini katika kutekeleza ahadi zake na kama kweli inastahiki sifa ambazo zimeelezwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa mkononi ninayo Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ambayo imekuwa gumzo kubwa humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 157 kifungu cha 126 inasema: "Ilani hii ya CCM ya mwaka 2005-2010 inatangaza vita ya kuutokomeza umaskini nchini Tanzania. Utekelezaji wa dhati wa majukumu makuu mawili yaliyoainishwa na Ilani, yaani kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea na kuwawezesha wananchi kiuchumi ndiyo njia ya uhakika ya kuutokomeza umaskini hatua kwa hatua. Tangazo hili la vita dhidi ya umaskini ni ahadi iliyotolewa na CCM kwa wananchi

kwamba, wakiichagua tena itaongoza mapambano hayo dhidi ya umaskini katika nchi yetu.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasikitika sana kusema kwamba ukitazama hali halisi malengo hayo ya Ilani yameshindwa na nitathibitisha maneno yangu. Naomba wenye jazba kidogo wazitulize. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 159 kwa sababu Ilani hii nimeisoma sana na haikunivutia ndiyo maana nikaamua kubakia CUF mpaka leo. Inasema kwamba utekelezaji wa haya unapaswa kuwa wa vitendo. Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa amesema kwamba Serikali hii imefanya maajabu, mimi nataka nikubaliane naye kabisa kwamba imefanya maajabu kabisa katika kuzidi kuperomosha maisha ya Watanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hapa inazungumzwa kwamba malengo mawili makubwa ni kujenga uchumi wa kisasa na kuondokana na utegemezi, lakini tunapotazama hali halisi, tunaona kwamba utegemezi haujaondoka na ushahidi wa wazi ni bajeti hii ya mwaka huu ambayo imepitishwa hapa juzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii vyanzo vya ndani ni trilioni sita tu kati ya trilioni 11 ambazo zinategemewa zitumike, maana yake ni kwamba kiasi kikubwa zaidi kinategemea kutoka katika ufadhilli au kuendelea kukopa. Hii maana yake ni kwamba bado suala la utegemezi liko pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi katika suala la ujenzi wa uchumi, inasikitisha kwamba miaka mitano hii hata yale mafanikio machache yaliyokuwa yamefikiwa hadi kufikia mwaka 2005 chini ya Serikali ya Awamu ya Tatu nayo pia yamepotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Awamu ya Tatu ilipochukua Serikali ilikuta uchumi unakua kwa asilimia 3.6 lakini wakati inaondoka madarakani ikauacha uchumi unakua kwa asilimia 6.7. Lakini leo kwa takwimu hizi tunaambiwa uchumi unakua kwa asilimia 6.9 maana yake mafanikio kwa miaka mitano yote ni kuongeza asilimia 0.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi unaona utendaji wa Serikali hii tunapoangalia suala la mfumuko wa bei ambao ndiyo unamuathiri mwananchi sana, kwa sababu unazungumzia kuongezeka kwa bei ya bidhaa ambazo anazitumia kila siku. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali hii inaingia madarakani ilikuta Serikali ya Awamu ya Tatu imefanikiwa kuangusha kiwango cha mfumuko wa bei kutoka asilimiaa 27 mwaka 1995 hadi asilimia 4.5 lakini juzi Waziri mwenyewe ametuambia hapa kwamba sasa mfumuko wa bei mwaka uliopita umerudi kuwa asilimia 12.2. Haidhuru wametuambia kwamba kuna takwimu zinazoonesha kwamba eti mfumuko wa

bei unaendelea kuporomoka, lakini tunapozitazama bei za vitu halisi huko mtaani hazioneishi hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuthibitisha hoja yangu zaidi tunapoangalia utafiti wa bajeti ya kaya (*Households Budget Survey*) wa mwaka 2007, inasema mfumuko wa bei ukitazamwa katika hali halisi kabisa, basi umeongezeka mara mbili zaidi ya ule unaotangazwa na Serikali na hii *Household Budget Survey* hata Serikali inaitumia. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba imeikubali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa *Household Budget Survey*, masikini nchi hii wameongezeka kwa milioni 1.5 kutoka masikini milioni 11.4 mwaka 2001 hadi kufikia masikini milioni 12.9 mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata hapo unapozungumzia kiwango hicho cha kuongezeka ukitazama vigezo vyenyewe vilivytumika ndiyo vinakuacha hoi, kwamba mtu ambaye anahesabiwa kuwa sio masikini nchini Tanzania ni yule ambaye akiwa Dar es Salaam ana uwezo wa kutumia Sh. 641/= au zaidi kwa siku, au akiwa ana uwezo wa kutumia Sh. 532/= au zaidi katika Miji mingine na Sh. 469/= au zaidi katika Vijiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika sisi tuliomo humu ndani tuijilize, nani anaweza kuishi kwa Sh. 641/= Dar es Salaam kwa siku? Au Waheshimiwa Wabunge tupewe sisi Sh. 641/= tuambiwe tukaishi Dar es Salaam kwa siku tuone tunaweza kuishi katika hali gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa hakika ukitazama umasikini umeongezeka sana na ukitumia kigezo cha Benki ya Dunia, ambapo mtu anahesabiwa kuwa ni masikini wa kutupwa iwapo anaishi chini ya dola moja kwa siku utagundua kwamba ukichanganya na hii *Household Budget Survey* basi asilimia 90 ya Watanzania ni masikini wa kutupwa na hao ni sawa sawa na Watanzania milioni 36 kati ya Watanzania milioni 43 ambao tunao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inasikitisha sana kwa sababu badala ya kuwasaidia wananchi hawa kunyanyuka sisi tunaendelea kuwakomoa kwa kodi kama zilivyoonekana hapa. Leo Serikali hii inatoa misamaha ya shilingi bilioni 752 ambazo wapinzani tumepiga kelele sana kwamba zipunguzwe angalau kwa asilimia 50 lakini mfanyakazi wa chini nafuu aliyopewa ni kuondolewa 1% katika kodi ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yapo mengi sana ya kuthibitisha hoja kwamba katika miaka hii mitano (5) kwa hakika hali ya maisha ya Mtanzania imezidi kwenda chini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia hapa ni ajira. Tunaambiwa kwamba, lengo la Ilani, lilikuwa ni kutoa ajira milioni moja katika kipindi cha miaka mitano hii. Tumepewa takwimu kwamba ajira hizo zimefikiwa na zimevuka kiwango, lakini kitu cha kufurahisha ukisoma Taarifa ya Hali ya Uchumi

ambayo Waziri wa Fedha na Uchumi alitusomea hapa yeye mwenyewe anatuthibitishia katika ukurasa wa sita kwamba, kwa mujibu wa utafiti wa *ILFS* kunakuwa na watu 760,000 wanaoingia soko la ajira kila mwaka na katika hao ni 40,000 tu ndio wanaopata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa takwimu hizi Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi anaziamini maana yake katika miaka mitano 40,000 x 5 tumetengeneza ajira 200,000 na hivyo ajira milioni moja zilizoahidiwa hazipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ukiangalia katika hotuba tulizoletewa katika uvuvi, madini, miundombinu hali imeharibika kabisa. Leo katika miaka mitano, reli imekwama kufanya kazi. Nilikuwa nazungumza na Balozi mmoja siku moja akaniambia anashangaa reli hii ilikuwa inafanya kazi vizuri mwaka 1914, leo mwaka 2010 reli ya kati haifanyi kazi, anashangaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi *ATC* ambayo haijawahi kufa tangu mwaka 1977 ilipoanzishwa kwa maana ya kuwa *grounded*, imekuwa *grounded* katika miaka mitano hii. Ukienda katika Bandari kila siku tunalalamikiwa kwamba hali imekuwa mbaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kutokana na hali hiyo, nasema siungi mkono hoja. Ahsante sana! (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili, Mheshimiwa Jussa anasema haungi mkono hoja. Nilikuwa namkumbusha tu kwamba, unajua Waheshimiwa Wabunge wote wanapochangia humu ndani wanazingatia sana majimbo yao? Sasa sijui Mheshimiwa Jussa amazingatia vipi Jimbo. Nakupongeza kwa kazi nzuri. (*Kicheko*)

Baada ya Mheshimiwa Jussa, atafuata Mheshimiwa Mlingwa na atafuata Mheshimiwa Haroub.

**MHE. DR. CHARSE O. MLINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya wananchi wa Shinyanga Mjini, naunga mkono hoja na kwa hiyo, nianze na pongezi na shukrani kwa wafuatao:-

Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga na timu yake yote, Mkurugenzi wa Halmashauri na timu yake yote, Viongozi wa Chama changu cha CCM katika ngazi zote, Waheshimiwa Madiwani wangu, Watendaji wa Kata na Vjiji, Mabalozi wote na Wananchi kwa ujumla kwa kuwezesha na kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005. Kwa hiyo, nitakuwa nafuta yale ambayo yameongelewa muda uliopita ya kukibeza Chama Cha Mapinduzi kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ndio msingi wa kuunga mkono hoja na hapa tunajaribu kuanisha mambo machache tu kama mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu tumejenga shule 15 za Sekondari na zina wanafunzi ukilianganisha na shule tatu zilizokuwepo awali katika kipindi cha miaka 44 ya uhuru. Kwa hiyo, sasa tuna shule 19 na kati ya hizo shule 15 ni mpya na zinasomesha watoto. Kwa hiyo, hili haliwezi likabewza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekamilisha ujenzi wa chuo cha ufundi (*VETA*) pale Kizumbi, ni chuo kizuri kabisa na tunaona fahari kuwa nacho kuifanya *Shycom* kuwa Chuo cha Ualimu cha kwanza katika Mkoa wa Shinyanga na tayari kuna wanafunzi Watanzania wanasoma pale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitaifa ujenzi wa Chuo Kikuu cha mfano Afrika cha Dodoma, haya ni mafanikio ambayo tunaona fahari kuyasema na wala hakuna sababu ya kuogopa ubezo wa aina yoyote ile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, maji. Tumekamilisha ujenzi wa Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria, huduma ya maji ilizinduliwa na Mheshimiwa Rais tarehe 31, mwezi wa Tano, 2009 na sasa maeneo mengi ya Jimbo la Shinyanga mjini yanapata maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sehemu ambazo hazijapata maji, mpango wa Serikali upo pale pale. Maji hayo hayajapatikana katika Kata zote kwa muda mrefu, na tunaona fahari ya kupata maji haya kwa sababu ulikuwa ni mpango wa Serikali wa muda mrefu na sasa tunafurahi kwa hayo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tumechimba na visima vidogo vidogo kuhakikisha kuwa tunapata maji kwa ajili ya matumizi mengine ya binadamu pamoja na mifugo kwa sababu Mkoa wa Shinyanga ikiwa ni pamoja na Jimbo langu ni Mkoa wa kwanza kwa kuwa na ng'ombe wengi, hivyo maji ni suala la msingi sana katika ufugaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hapa katika suala la maji ni *KASHWASA* na *SHUASA* kuhakikisha kuwa kuna ubora wa hali ya juu katika kuhakikisha kuwa kuna huduma bora ya maji yanayopatikana wakati wote na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kwenye eneo la afya. Serikali imekubali kujenga Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Kama tunavyofahamu, awali Mkoa wa Shinyanga haukuwa na Hospitali ya Mkoa. Hadi sasa tunayo hospitali ambayo imekuwa ikitumika kama Hospitali ya Mkoa, ambayo imekarabatiwa katika kiwango cha juu sana na tunaipongeza Serikali katika hilo, lakini sasa kwa kutambua kuwa tunahitaji Serikali ya Mkoa, tumetenga eneo la ekari 100 na tayari katika bajeti hii nimeona kuna kifungu kinachozungumzia ujenzi wa hospitali ya Mkoa na kwa hiyo, kuna kila sababu ya kuipongeza Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alikubali mbele ya wananchi wa Shinyanga katika ahadi hii muhimu na tunaona fahari tutakapokuwa na Hospitali hii ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa barabara, awali mji wa Shinyanga ulikuwa unafahamika kuwa ni mji wenyewe vumbi sana, lakini sasa hivi kwa watu wanaoingia mjini Shinyanga wanashangaa kuona kuwa Shinyanga imebadilika sana na watu wanavutiwa sana. Kwa hapa nimpongeze sana kwa namna ya pekee Mheshimiwa Celina Kombani - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMI kwa sababu amefanya kazi kwa karibu sana na mimi kuhakikisha kuwa barabara hizo za lami zinajengwa na kwenye bajeti hii kuna pesa nyingi tu za kuhakikisha kuwa tunajenga barabara za lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kulikuwa na madaraja matatu ya kero, Mshikamano Kata ya Ngokoro, Ndara inayounganisha na Kambarage, yalikuwa ni kero kubwa sana, sasa sio kero tena. Kazi hiyo imekamilika. (*Makofii*)

Kuna daraja la tatu kule Kata ya Kizumbi sehemu ya Lyandu linakamilishwa ili kusudi kero hiyo ya watu wa Lyandu na wengineo waweze kupita bila matatizo. Tunaona fahari kwa mafanikio haya makubwa ambayo Halmashauri ya Shinyanga imeshirikiana kwa karibu sana na Ofisi ya TAMISEMI kuhakikisha kuwa haya mambo yote yanafanyika na wananchi wa Shinyanga Mjini wanafurahi sana na wanaipongeza sana Serikali kwa usikivu huo na ndivyo Chama Cha Mapinduzi kinavyofanya kazi zake, hakidanganyi wananchi. Hayo mengine wanayosema ni maneno tu na wala hatuna sababu sana ya kupata taabu nayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni changamoto katika elimu. Ninajiuliza, kwanini Mkoa wa Shinyanga kwa miaka miwili mfululizo unakuwa wa mwisho katika matokeo ya vijana wanaomaliza Darasa la Saba? Kwangu mimi naona hili sio suala la Shinyanga peke yake kulijadili kwa sababu kuna mambo ambayo yanaweza yakafanyika ndani ya Mkoa, lakini kuna mambo ambayo hayawezi yakafanyika ndani ya Mkoa na kwa hiyo, tunahitaji msaada wa Serikali katika kukabiliana na hili jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wanapomaliza Darasa la Saba na wakaishia hapo, mimi ninajiuliza inatokea hivyo ili kusudi wawe akina nani katika miaka 50 ijayo? Hawawezi kuwa rasilimali ya kutegemewa sana kama wataishia Darasa la Saba. Mimi ndoto yangu ni kuhakikisha kuwa wale wote wanaosoma Shule za Msingi waingie Sekondari na hapo ndipo tutakapokuwa na nguvu kazi ya kutosha kuhakikisha kuwa tunahimili changamoto hapa duniani katika suala la maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukamilishaji wa Shule za Sekondari pia ni changamoto katika kuboresha elimu hii ya Sekondari kwa vijana wetu ambao kwa sasa wako mashulenii kwa shule ambazo nyingi hazijawa na mioundombini ya kutosha, lakini nafurahi kwamba katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia mpango mzuri sana wa kuhakikisha kuwa kazi hii inakamilika mapema na kuwa na shule kamilifu katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine katika eneo hili la elimu ningependa kuona Serikali inakuwa wazi zaidi katika kuhakikisha kuwa kuna mpango mahsus wa

kuwa na hosteli za wasichana katika Shule za Sekondari. Wasichana ndio wanawake wa baadaye na wanawake ni muhimu sana katika jamii. Tusipowalinda leo tutakuwa tunajitengenezea matatizo ambayo baadaye tutakuja kuathirika nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa kuona kuwa wasichana wanaosoma Shule za Sekondari wanachukuliwa kwa namna ya pekee ili kuhakikisha kuwa wakiingia Sekondari wanamaliza shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kuzungumzia mambo ya ndani. Mimi ninajiuliza hivi sera yetu na mipango yetu ya ujenzi wa nyumba bora za Askari Polisi na Magereza ikoje? Maana pale Shinyanga mjini Askari Polisi na Magereza wako kwenye nyumba duni sana. Nyumba nyingine nilipozaliwa nilizikuta, ni duni sana! Lakini huu ni mfano tu katika nyumba nyingi za Askari tulionao hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanini tusiwe na mpango kwa mfano, *National Housing* ikajenga nyumba na kuwapangisha hawa Askari? Au mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii kwa mfano, *NSSF* ikajenga nyumba kama ilivyofanya kwa Dar es Salaam ili kusudi tukamalize tatizo la nyumba kwa Askari? Au Serikali ikawa inatenga kila mwaka fedha za ujenzi wa nyumba za Serikali? Au nimesikia Serikali ya China iko tayari kukopesha Jeshi la Polisi, dola kama milioni 65 kwa ajili ya ujenzi huo, Waziri wa Fedha angeridhia hilo ili Askari wetu hawa ambao wanafanyakazi kubwa sana wakaweza kuishi katika nyumba bora zinazolingana na kazi yao. Mimi ninasikitika sana pale Shinyanga Mjini Askari polisi wako kwenye nyumba duni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, katika changamoto ni hospitali ya Mkoa, kwamba wananchi wale waliopisha ujenzi wa hospitali hii kule eneo la Negezi basi wafidiwe haraka na nadhani kwenye bajeti hii zipo fedha za kuwafidia ili kusudi waweze kukaa sawasawa na kusema kwamba tulitoa eneo hili na sisi tukalipwa haki yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kwamba sisi tungependa kuona ujenzi huu unakamilika haraka iwezekanavyo ili kusudi wananchi wa Mkoa wa Shinyanga waweze kupata huduma inayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo masuala ya msingi yanayonifanya nimalizie kwa kusema tena ninaunga mkono hoja. Ahsante sana! (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa - Mbunge wa Shinyanga Mjini. Kabla sijamwita Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Waheshimiwa Wabunge naomba nichukue fursa hii kutambua uwepo wa Mheshimiwa Luhahula. (*Makofi*)

Mheshimiwa karibu tena Dodoma, karibu Bungeni baada ya matatizo makubwa sana uliyoyapata kutoka kwa baadhi ya wapiga kura wabaya kabisa. Karibu sana! (*Makofi*)

Mheshimiwa Masoud, atafuatiwa na Mheshimiwa Gosbert Blandes.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Kwanza kabisa, nisije nikasahau baadaye, naunga mkono hoja mia kwa mia hotuba hii ya Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaeleza yale yangu niliyokuwa napenda kumuunga mkono Mheshimiwa Anna Abdallah, kwa mambo mawili aliyooyazungumza. Moja, suala la Chuo Kikuu cha Dodoma. Kama hao wanaozungumza wanazo Ilani za Uchangazi kuanzia mwaka 2000 na kuendelea waangalie Na. 63 ya Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 inaeleza kabisa kuhusu habari ya elimu ya juu katika Vyuo Vikuu vyote vya Tanzania. Sasa nashangaa leo wanasema hii ni sera ya upinzani. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile jambo la pili ambalo ninataka kumuunga mkono mama Anna Abdallah, mimi nawasihi ndugu zangu wanaume, tena nawasihi sana, chonde chonde, wanawanake wamewakosea nini? (*Makofi*)

Wanawake ni mama zetu, wewe, mimi, Mheshimiwa Malecela hatuwezi kuipata pepo kama hatukufuata nyanyo za akina mama. Kwa hiyo, tuwape uongozi waongoze, tusiwaogope. Sasa naendelea na mambo yangu niliyokuwa nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nazungumzia suala la rada ya Kigamboni. Nazungumzia kwa sababu leo Mheshimiwa Mwinchoum amekuja na wanafunzi pale ambao walimbana juzi kwenye mkutano wa hadhara wakamwambia Mheshimiwa, daraja halijajengwa ndio kawachukua leo pale. Sasa mimi namsemea kwanza leo, kama hatapata nafasi kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyoelewa kwamba daraja la Kigamboni limo katika Ilani ya Uchaguzi vile vile. Mimi naelewa sio kama wale wengine hakuna jambo ambalo unaweza kuyapanga mambo yote ukayafanya siku moja. Hata nyumbani kwetu wenyewe familia zetu huwezi kufanya kila unalomwambia *wife* wako au *wife* kumwambia mume ukalifanya siku moja. Leo hii, kesho na kuendelea. (*Makofi*)

Katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 ilisisitiza kuhusu ujenzi wa Daraja la Kigamboni. Naamini kuna matatizo kadha wa kadha yalijitokeza ambayo kwa kweli tukitaka tuisitake Serikali imepoteza hela nyingi sana. Labda niseme tu kwa ufupi, ilipoamuliwa tangu wakati wa awamu tatu lakini tulipoingia mwaka 2005 ujenzi wa daraja lile ulikuwa *una-cost Euro* milioni 45. Kwa wakati ule Serikali ya Uhulanzi ilikubali kutoa asilimia 50 ya gharama zile ambayo ni asilimia 22.5. Lakini kutokana na urasimu vile vile walikubali kutoa mkopo nafuu asilimia 33 ya *cost* yote ya mradi. Lakini matatizo yakaenda huko yakaenda huku mpaka leo daraja halijajengeka na naamini mimi kwa nguvu zake zote. Mheshimiwa Jakaya Kikwete na Waziri Mkuu safari hii watalisimamia na tuone daraja linajengwa. Kwa sababu nilivyosikia na ninavyoelewa mimi kwamba Waziri Mkuu ametoa agizo maalum sasa hivi kwa shirika la Hifadhi ya Jamii lihakikishe kwamba daraja lile kwa kila mbinu linajengwa. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu uwatosheleze wale wanafunzi pamoja na Mbunge maana Mbunge kiroho kinampiga kuhusu daraja lile.

Kwa hiyo, ukitutolea kauli pale tutakuwa sisi tuna furaha hasa Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Kwa sababu kabla ya mwaka 2005 ilikuwa Kamati yetu hii ambayo mimi ni Makamu Mwenyekiti, tumepiga kelele sana, tumewaita Mawaziri kila mmoja, lakini naamini kwamba mwaka huu daraja litajengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kabla hajaja Tido Mhando hapa kutoka Uingereza akaja wakati ule *TVT*, *TVT* ilikuwa inasota ilikuwa imeshakufa, mbovu kabisa. Nasema kwa uchungu kwa sababu tangu nimeingia mwaka 2005 Kamati yangu inasimamia na inasema maneno kadha wa kadha kuhusu hali mbaya ya majengo. Majengo yale yaliyojengwa miaka mingi iliyopita yamewekwa mawe ya msingi na Marais wa nchi hii, lakini matokeo yake hatujasikilizwa Kamati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri Mkuu aeewe, Kamati yangu pamoja na Mwenyekiti Mhagama tulikwenda kutembelea siku moja wakati ule *TVT* tukakuta ndoo za maji katikati ya vyumba. Mimi binafsi niliuliza mnaoga humu ndani? Wakatuambia siyo Mheshimiwa samahani maji haya ni nyumba inavuja. Tulisikitishwa sana. Tukatoa rai tukawaita Hifadhi ya Jamii *NSSF* katika kikao maalum ambacho Naibu Waziri wa Fedha alikuwepo. Hebu jamani tusaidieni, hawa walishakubali *NSSF* kumaliza majengo haya kwa mujibu wa taratibu zote za Serikali miaka mitano. Taratibu gani hazikamiliki hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi *TBC* wanaruka kule kusota, hakuna tena, wanaruka na ndio maana tulikuwa tuna mipira yote hii. Tena tunampongeza sana Mheshimiwa Spika, amezuia kuonyesha Bungeni amesema tuone mashindano yote ya Afrika Kusini Kombe la Dunia. Sasa ile ingekuwa wamewezeshwa zaidi hawa angefanya miujiza mingi zaidi kuliko hii. Naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu akiniiita Ofisini kwako nitakuja nilie mbele yako. Nitakuja kulia, lakini tuhakikishe Waziri Mkuu kwa nguvu zako zote *TBC* majengo yale wanapewa shirika lolote la Hifadhi ya Jamii. Wenzetu nje huko siku hizi hakuna Mheshimiwa Waziri Mkuu hakuna Serikali inayofanya kila kitu yenye.

Kuna Wabunge wamezungumza hapa kuhusu habari ya nchi za nje mpaka barabara. Madaraja yote yanapewa makampuni yanajenga. Yakishajenga wanaambiwa endesheni, lipeni, tozeni ada. Sasa sisi tuna tatizo gani? Sasa mimi nasema hebu na sisi tufuate rai hizo, mimi nimesikia kwamba kuna watu walikwenda Malaysia kusoma taratibu hizo na katika hao waliokwenda huko Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya alikwenda na ye. Hebu aje atueleze miujiza gani wamefanya Malaysia imekuwa barabara zao zote za vijiji na za mjini na madaraja yote hakuna lililojengwa na Serikali hata moja na wala hawana shida yoyote. Hebu na sisi hapa tufanye yale kama wanavyofanya wenzetu. Mifuko yetu ipo, ina uwezo kamili, mifuko yetu tuipe kazi, tuipe watujengee barabara, halafu watalipwa kidogo kidogo. Majengo makubwa kama walivyofanya Chuo Kikuu kile pale. Leo tunaipongeza sana mifuko yote isipokuwa hili nasema taratibu na nanong'ona tu na wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimepata habari kwamba udhamini wa mifuko ile haujatolewa kujenga majengo yale.

Sasa hebu tupekue, kuna nini huku ndani? Kwa sababu hii mifuko ni fedha za umma. Fedha za wananchi zile pale na wale ili tuwape moyo wapate karatasi za udhamini tu hawana tatizo, wale hawatafilisika kabisa. Lakini kama iko kimya mpaka leo hali mbaya hairidhishi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu naamini kuwa haya yote utasimamia vizuri na nina hakika kwamba yatakelezwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile niendelee katika suala la akina mama maana naona dakika zangu nizimalie hapo. Jamani hata mimi nimesikia baadhi ya wanaume wakiingia wanaume hata saba hawanuni, akiingia mwanamke ananuna. Jamani kwa nini? Hebu wanawake waje kwangu kugombea. Siyo kugombea tu, kama anajitokeza mwanamke na namwona kweli uwezo anao namwachia, kaa hapa Mwana Abdallah wewe gombea hapa, Mheshimiwa Chilolo gombea Jimbo langu. Mnaogopa nini? Kwa sababu kwanza anafanya kazi za CCM anatekeleza Ilani ya Uchaguzi. Kuna jambo gani la kuogopa? (*Makofî*)

La mwisho kabisa, hata Serikalini tuwatazame wale waaminifu zaidi nani? Sisi ME au KE?

#### **WABUNGE: KE.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Namwita Mheshimiwa Haroub Masoud. Isipokuwa nikwambie tu mamlaka ya kuhoji Wabunge ni ya kwangu tu, wewe huruhusiwi. (*Kicheko*)

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi mimi nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Celina Kombani, Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ya kwangu leo kwa kweli ni kuelezea mafanikio ambayo yamepatikana kwenye Jimbo langu, wala sina mambo ya kulalamika kama siku za nyuma kwa sababu kazi zimefanyika, wenyе macho wanaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna mtu anakuwa na ubishi, basi atembelee Jimbo la Uchaguzi la Karagwe ambako mimi ndiyo Mbunge wa huko. Ukifika Jimbo la Karagwe tumejenga barabara zote za vijiji zinapitika kwa asilimia mia moja.

Ukija Karagwe tunajenga Chuo cha Ualimu kwenye Jimbo langu la Karagwe. Kwenye Jimbo langu la Karagwe tunajenga Chuo Kikuu - *University of Karagwe*. Kwenye Jimbo langu la Karagwe barabara ya lami iliyokuwa inatusumbua kutoka Kyaka mpaka Bugene tayari Mkandarasi ameshapatikana na inaanza kujengwa. Karagwe tulikuwa na matatizo makubwa sana ya ujambazi lakini sasa hivi mtu unatembea hata usiku wa manane kuna hali ya utulivu na amani. Karagwe tumejenga Zahanati nyingi vijijini karibu kila kijiji tumekipatia Zahanati tunajenga, lakini pia Jimbo langu la

Uchaguzi Karagwe tumeplizia dawa ya mbu kila Kijiji. Bei ya kahawa Karagwe sasa hivi inakwenda kuanzia Sh. 700/=, Sh. 800/= mpaka Sh. 900/= tofauti na zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ni mengi sana, nikianza kuzungumza hapa pengine sitamaliza, lakini kama mwenzangu alivyosema Dr. Mlingwa Jimbo langu la Karagwe nimefanikiwa kujenga Sekondari 17 za Kata na zinakwenda vizuri sana. Mafanikio yote hayo yamepatikana kwa ushirikiano mkubwa sana na wenzangu hasa Mkuu wa Mkoa - Mzee Mohamed Babu. Nampongeza sana Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Karagwe, Mama Consolata Kamwaba na Watendaji wenzake, Mwenyekiti wetu wa Halmashauri amenipa msaada mkubwa, Mheshimiwa Kashunju - Mkuu wetu wa Halmashauri, Mzee Masawe, Kanali Masawe anajitahidi pia na wadau mbalimbali.

Katika Jimbo langu la uchaguzi la Karagwe wakati naingia madarakani kulikuwa hakuna redio hata moja. Sasa hivi tunazo redio mbili ambazo ni Redio Karagwe pamoja na redio Fadeko. Mawasiliano ni makubwa sana, mitandao ya simu huko kote imejaa. Haya yote yamefanywa na Chama cha Mapinduzi. Nitamshangaa mtu ambaye anabeza maendeleo haya tena ya muda mfupi sana. Mimi kwa kushirikiana na Waheshimiwa Madiwani kwa kweli tumechapa kazi za kutosha na nina imani wananchi wangu wa Jimbo la Karagwe, haya wanayaona na hawataniangusha hata kidogo wakati wa uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipekee niombe kwa mara ya kwanza nitaje majina ya Waheshimiwa Madiwani ambao kwa kweli tumeungana kwa pamoja kuchapa kazi hizi. Nianze na Mheshimiwa Robinston Mutafungwa, Mheshimiwa Yusuph Kagande, Mheshimiwa Cornel Kabigumira, Mheshimiwa Jane Adam, Mheshimiwa Josia Katanga, Mheshimiwa Esejia Bimurilo, Charles Bechumira, Justin Bechumira, Justin Kaihula, Ezbon Ishunga, Joseph Kibate, Sbi Rwazo, Raphael Kinyina, Wales Mashanda, Stanton Mugenyi, Cleophas Gervas, Felix Mukuchu, Ilimina Mshongi, Jane Bilalo, Twabu Kasenene, Zidina Murishidi na Jovita Kombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawataja hawa kwa sababu wamekuwa ni nguzo zangu muhimu sana katika kutekeleza na kusimamia ilani ya Chama cha Mapinduzi. Moja tu ambalo labda nikumbushie kidogo, nilikuwa naomba tu wakati namalizia hapa kwamba bajeti ya mwaka jana Serikali ilinipatia fedha kwa ajili ya kupeleka umeme vijijini kwa maana ya vijiji vya Bisheshe, Nyankayanja, Nyaihodzi, Ihymbe na sehemu nyingine nimeambiwa na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwamba tayari Mkandarasi ameshapatikana na nimepewa taarifa kwamba tayari ameshafika Bukoba.

Nilikuwa naomba wamhimize afanye haraka sana aweze kupeleka umeme katika maeneo haya kwa haraka, lakini pia nimekuwa nikizungumza na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kuhusiana na umeme wa ukanda wa Bushanga sasa ameniahidi kwamba utakuja kwenye bajeti ya mwaka huu. Nimejaribu kudodosa kitabu sijaona vizuri.

Mheshimiwa Ngeleja ni rafiki, nilitaka apate salamu huko aliko kwamba kama safari hii umeme huu hautakwenda ukanda wa Bushangara kwa maana ya Tarafa ya

Nyabionza, hapa ndani hatutaelewana. Siku ya bajeti ya Mheshimiwa Ngeleja nimeshajipanga sana kuhakikisha kwamba kwa kweli tunakabana koo kwa sababu ameniahidi ni karibia miaka mitano yote ambayo nimekaa hapa Bungeni. Kwa hiyo, ninaomba apate salaam hizo, atafute pesa mapema apeleke umeme kule maeneo ya Bushangara.

Lakini pia kuna umeme wa kwenda Kituntu, Igurwa na Rwambahizi. Ule umeme tayari nguzo zimesimama mpaka maeneo fulani, lakini umeme haujafika, wananchi wanandai umeme, hawataki nguzo wanataka kuona umeme unawaka na mimi kabla sijamaliza kipindi cha kwanza hiki na kuingia cha pili nilitaka nione umeme unawaka maeneo hayo. Kwa hiyo, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini wajipange katika maeneo hayo wakati wanaleta bajeti ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine moja tu nililonalo ni kuhusiana na wanafunzi wa Shule za Sekondari hasa za Kata. Tumekuwa na matatizo katika Jimbo langu la Karagwe, kuna baadhi ya wazazi ambao wanakuwa wameshindwa kulipia watoto wao karo katika hizi Shule za Sekondari za Kata. Sasa baadhi ya walimu wanawarudisha majumbani, kwa hiyo, watoto wanapata shida. Sasa nilitaka nipate kauli pengine ya Serikali itupe msimamo kwamba kwa kuwa elimu ni haki ya kila mtoto, basi kwa wale ambao wameshindwa kabisa kama ambavyo tumesamehe wazee kulipa kodi za nyumba basi na wenyewe wasaidie watoto wao waweze kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami niwashukuru wananchi wa Jimbo la Manyoni Magharibi kwa kuniamini kwa muda wa miaka mitano na kama asubuhi mlivyoona kwenye *screen* pale mmeiyona ofisi nzuri sana ya Jimbo langu. Ningeliomba wanipe nafasi niitumie, basi hiyo ofisi sio tena baada ya miezi miwili waweke mtu mwengine ndani humo. Nadhani nitasema kweli pia kwamba kwamba dunia sasa hivi inazizima kwenye suala la michezo. Mchezo wa mpira ni muhimu sana na siku ya Jumanne wakati tunaanza Bunge hapa kulikuwa kuna swalii kuhusu Wizara inayohusika na kuna timu zilipongezwa sana hapa, ile ya *coca-cola*, timu ya Taifa, timu ya Twiga, Timu ya Taifa ilipongezwa japo nayo ilitandikwa magoli mengi, lakini sikusikia Timu ya *Kindai Shooting Stars* ya Mkoa wa Singida. Sasa mnatuonaje sisi baada ya kuchukua Kombe la Taifa hakuna hata pongozi kwa upande wetu na Bunge halifarifi na pia wameondoka na kitita cha shilingi milioni 35, lakini hatukusikia pongozi zozote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lwanji kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote tunapongeza Singida kwa kuchukua Kombe.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana maana ni uchumi huo na wenzetu wa Afrika Kusini nadhani wamepata neema kubwa sana kuwa wenyeji wa Kombe la Dunia, halafu ni heshima. Sasa hivi wachezaji wanaingia uwanjani wanalia kwa hamu y a kupata *glory*, ni heshima kubwa sana. Baada ya kusema hivyo,

narudi kusema kwamba tuko hapa kugawana keki ya Taifa na kwa kweli nadhani tungekuwa *serious* sana kwa suala hili. Baada ya kusemea suala la mpira, kana kwamba haitoshi, Mkoa wa Singida na Mkoa wa Lindi ni za mwisho kwenye bajeti, kwa maana kwamba ni Mikoa midogo na sababu yenyewe mimi ninavyoiangalia sioni wivu. Lakini wivu wa maendeleo unakubalika. Uongo? Wivu wa maendeleo unakubalika, tusije tukaleta *sentiments* za *Regionalism* kama Mheshimiwa Ligalami alivyosema hapa na nisingependa kufanya hivyo, lakini ukweli ndio huo na sababu yenyewe tu ni kwamba hatuna Wilaya za kutosha, ni miaka mingapi hapa toka Mkoa uundwe ni Wilaya tatu mpaka leo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lindi nayo ukiiangalia kwa kweli haina Wilaya za kutosha. Kwa hiyo, mimi ningeomba operesheni maalum ifanyike kama ilivyofanyika kwa Wilaya ya Masai. Utakumbuka Wilaya ya Masai ilikuwa ni moja, haikuwa kwa sababu ya vigezo vyta watu, lakini ni kwa sababu ya maeneo mapana. Watu sio kwamba wamekuwa *grouped* pamoja kama zizi la ngombe, watu wametawanyika, wana maeneo mapana. Sasa unawahudumiaje hawa watu wenye maeneo mapana?

Sasa Wilaya ya Masai pekee yake ilizaa Wilaya tano. Monduli, Ngorongoro, Kiteto, Simanjiro na Longido, kilomita za Mraba 64,755 sawa na Mkoa wa Rukwa au sawa na Mkoa wa Lindi. Hiyo ilikuwa ni Wilaya moja tu na watu wake mpaka sasa hivi hawafikii laki saba wako laki sita na tisini na tano, Wilaya tano. Maana yake watu hawa wanaweza kukaa Wilaya moja ya Bukombe au Wilaya moja ya Kinondoni. Kwa hiyo, mimi naomba hoja yangu hapa kwamba hii *factor* ya idadi ya watu kwa kweli isiwe ndio kipaumbele cha kwanza, yaangaliwe maeneo. Nchi hii ni kubwa ukiunganisha Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi, nchi hii bado inazidi, ina kilomita za mraba karibu laki tisa. Hata Uingereza sijui inaingia mara nne, au mara ngapi hapo! Lakini tutaendelea kuwa nyuma kama hatukuweza kuya-*manage* vizuri maeneo yetu.

Nisingependa ku-*dwell* kwenye takwimu lakini tuuangularie upana wa maeneo na ndio maana maeneo mengine yalipewa kipaumbele. Ukiangalia kwa mfano Longido ni Wilaya, ndugu yangu sio kwamba namwonea wivu, lakini ina watu 86,000, haifiki hata laki moja na eneo la mraba ni elfu 7,900. Liwale watu 83 elfu, Pangani watu 50 elfu, Mafia watu 44 elfu sijui nitaje na Siha labda, lakini Siha, Nanyumbu, Rwangwa hizi zilipewa hadhi hiyo hata hazijafikia watu laki moja.

Naomba tuangularie mapana jinsi yalivyo. Nimelizungumza sana katika Kamati, nadhani hilo niliache, lakini ni muhimu tuangularie maeneo na maeneo hayo kwa mfano ni makubwa sana, mapana. Watu tuko elfu 80 kama watu wa Longido, lakini eneo ni kilomita za mraba elfu 18 *how do we manage such a place?* Juzi tumegundua kwamba kuna *uranium* kwetu, *how do you manage these resources?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni utajiri mkubwa sana. Mimi nashukuru kama litakuwa limefika mahali pake angalau watuangularie kama wanaona Wilaya ni ngumu kutupa, basi watuangulariez kwa upande wa Halmashauri tuenze kijianda tuweze *ku-manage resources* zetu vizuri. Kitu cha pili kwamba, hii sheria iliyompa mamlaka

makubwa namna hiyo, huyu Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani imekuaje? Jimboni kwangu nina watoto takribani 200 wamefutiwa mitihani mwaka jana. Barua ile nilivyoisoma imehusisha Mikoa kumi, labda kule kumekuwa *spoiled*, lakini kwangu unakuta darasa zima limefutiwa, watoto sitini na tano. Shule ya pili, watoto 45, na ya tatu 40 inasemekana waliibia mitihani na wakaundiwa Tume kwenda kuwahoji.

Ndugu zangu kweli mnaweza kwenda kuwahoji watoto wa Darasa la Saba? *Is it fair?* Kwa sababu wale watoto wameagizwa kufanya vitendo hivi. Kwa hiyo, ningeliomba suala hili liangaliwe na wanasema Sera inakataza kutunga mtihani mwingine. Ni kwanini wasitungiwe mtihani mwingine wakafanya? Sisi tunajenga shule usiku na mchana, tunawachangisha watu na shule tumejenga, *then* katika *level* hiyo ya sekondari watoto kutoka Mikoa mingine kujaza hizo shule. Shule zilizofutiwa matokeo ni Itigi-Reli, Sanjaranda na Furaha, inasikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tuwaonee huruma, hili jambo sio la mchezo tumeandikisha watoto milioni moja nchini mwaka huu katika taarifa ya Waziri Mkuu, waende mashulenii na tunajenga shule usiku na mchana, lakini hawa watu hawaangali. Nadhani nimejitahidi sana kulieleza suala na Wizara husika na kila kitu nimepeleka wakubwa wengi, tumewahuishisha lakini uamuzi hautoki. Huyu Katibu Mtendaji amebanwa anasema kwamba haiwezekani, basi suala hilo nadhani niliache mikononi mwa wahusika liweze kuangaliwa, nimalizie kwenye suala la hospitali ya Singida.

Ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Diana Chilolo kuna mradi mkubwa. Huo mradi ni wa bilioni mia moja ishirini. Serikali imekuwa ikitoa shilingi bilioni mbili kwa mwaka, maana yake ni kwamba hiyo itachukua miaka sitini. *Simple arithmetic, sixty years to build that hospital!* Sasa katika ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliona na akaahidi kwamba ataangalia sasa tungeliomba mtuangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunisikiliza. (*Makofii*)

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hii hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza, awali ya yote napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri, lakini naishukuru Serikali yote kwa ujumla kwa namna ambavyo tumeshirikiana pamoja na wananchi wa Jimbo langu la Musoma katika utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Kusema kweli mwaka 2005 tulikuwa mbali sana kwa maana tulikuwa nyuma lakini kwa ushirikiano huo yako mambo ya kimsingi yale tuliyoyatarajia karibu yote sasa tumeweza kuyatekeleza kwa asilimia sio chini ya tisini. Tulikuwa na tatizo kubwa la elimu. Leo katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo kila mtoto anayefahulu anapata nafasi ya kwenda Sekondari. Tulikuwa na tatizo la afya leo kila Kata ina Zahanati na zimeendelea kuboreshwa. Tulikuwa na tatizo kubwa la maji, leo maji Musoma zimebaki tu *place* ndogo na chache ambazo hazina maji. Tulikuwa na tatizo la barabara ya

Musoma mjini, ilikuwa moja tu ya kuingia, karibu eneo la mjini pale sasa tunazo barabara za kutosha za lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kumbe nina kila sababu ya kuipongeza Serikali, lakini na wananchi wa Musoma kwa namna ambavyo wamenipa ushirikiano na hata wakati naaga nakuja Bungeni walisema nije, lakini wanaendelea kuwa pamoja na mimi na ni imani yangu kwamba katika kipindi kijacho watanirudisha mjengoni ili tuendelee kufanya kama ambavyo tumefanya.

Pamoja na hayo mafanikio makubwa ambayo yamefanyika, lakini kwangu yapo mambo matatu ambayo yamenipa kero, vile vile yamewapa kero sana wananchi wangu wa Jimbo la Musoma na kusema kweli yametupa huzuni na mambo haya leo nadiriki kusema kwamba yananifanya nachelewa kusema kwamba kwa kweli kama hayakurekebishwa sitaunga mkono hoja. Mambo haya ni mambo ambayo yako kwenye uwezo wa Serikali na Serikali ikiamua leo yote yanafanyika. Suala la kwanza ni suala la watumishi waliokuwa wafanyakazi wa kiwanda cha *MUTEX* Musoma, kiwanda kile kimefungwa mwaka 1994. Wale watumishi wameendelea kutaabika hadi hivi tunavyozungumza bado wanadai mafao yao lakini pasipokuwa mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe binafsi nimelifuatilia, nimemchukua Waziri Kapuya mpaka kule kama Waziri wa Kazi, ameliangalia suala na ameona kwamba wale watu wana haki ya kulipwa mafao yao. Lakini hadi leo hakuna kilichofanyika. Sikuishia hapo, niliwaleta viongozi wao nikaja nikaomba *appointment* kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Bunge lililopita na mimi namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba aliweza kuwapokea na akawasikiliza vizuri na kwa kweli akaona kwamba kuna haja wale watu wapate mafao yao wakapumzike makao.

Kile kiwanda kilikuwa na watumishi zaidi ya 900, ombi langu katika hili sasa labda wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuwa anahitimisha ajaribu kuwaambia wale wananchi wa Musoma waliokuwa watumishi wa *MUTEX* kwamba mafao yao kama kweli watayapata, basi ni lini Serikali itayashughulikia? Kwa sababu sasa ni zaidi ya miaka ishirini.

Suala la pili ambalo linanifanya nachelea kuunga mkono hoja ni kama nilivyouliza juzi kwenye maswali kwa Waziri Mkuu. Tuna tatizo kubwa la hospitali ya Kwangwa, hospitali ile wananchi waliuza mali zao wakatumia na hata kuna baadhi ya wananchi waliokua kwa sababu ya kuhangainia ujenzi wa hospitali hiyo. Hospitali hiyo ilijengwa na ikafikia ghorofa tatu na ni hospitali kubwa ambayo ndio ilitakiwa iwe hospitali ya Mkoa.

Lakini kwa bahati mbaya sana kwa kuwa wananchi walitegemea nguvu za Serikali, Serikali kwa wakati ule haikuwa na fedha, ndio ikamwombwa Baba Askofu

ajenge hospitali hiyo. Baba Askofu alikubali, lakini akaomba kwamba akabidhiwe hati kwa kuwa kulikuwa na suala la ulipaji wa fidia, fedha zilizokuwa zinadaiwa za fidia zilikuwa kama shilingi milioni 33.

Fedha hizo nilizifua tilia na nimeuliza swali Bungeni, Serikali ikasema fedha hizo anazitafuta na itazilipa mara moja. Baba Askofu amesubiri na hatimaye mwisho ameleta barua ya kusema haendelei na mradi huo. Juzi mwanzoni mwa mwezi huu, mwisho *RCC* ikakubali ikasema sasa italitazama suala hilo ili sasa Serikali ianze kujenga hospitali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa jengo lile lilikuwa na vifaa, lilikuwa na matofali mengi, yameendelea kuibiwa, ombi langu kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu ukubali kwa haraka kwamba katika mwaka huu na katika Bajeti hii kianze kutengwa kiasi cha fedha ili tuweze kunusuru jengo lile na wananchi waone kwamba nguvu yao ile haikupotea bure.

Kwa hiyo, nadhani kwamba kwa kufanya hivyo basi tutakuwa tumewatendea haki wale wananchi wa Jimbo la Musoma na kusema kweli kwa kutambua umuhimu wa Hospitali ya Mkoa na kwa kuangalia Hospitali iliyopo kwa namna ilivyokuwa ndogo ndiyo maana tunadhani kwamba hospitali ile ikijengwa itaweza kuwasaidia wananchi wa Jimbo lile la Musoma lakini na wananchi wa Mkoa wa Mara kwa ujumla. Kwa hiyo, hayo nayategemea kwamba yako kwenye uwezo wa Serikali ambayo ni imani kwamba kama ityaweka sawa basi tutaweza kuwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ambalo kusema kweli na lenyewe linatutia kero kubwa, ni suala la mipaka ya Manispaa. Mimi nimesikia hapa wapo watu wanalia wanasesma maeneo yao ni makubwa, cha kusikitisha Manspaa ya Musoma ina *square kilometre* 63 peke yake. Urefu wa kutoka eneo la kwanza kwenda lingine, mfano Bweli kwenda Makoko hapavuki kilomita 15, upana wake hapavuki kilomita 8. Sasa matokeo yake kale kamji kamejifinya wakati hako ndiko Makao Makuu ya Mkoa wa Mara. Sasa kilichokuja kutokea yako baadhi ya matatizo ambayo tumeendelea kuhangaika nayo. Leo tumeshindwa kupata hata uwanja wa ndege, maana uwanja wa udege uliopo uko katikti ya mji na ni mdogo. Matokeo yake ni kwamba kwa sababu hatuna eneo, uwanja ule Serikali imeshindwa kuujenga kwa sababu inasema uko mjini. (*Makofi*)

Lakini vilevile kwa kuwa tumekosa eneo, ndiyo maana tumeendelea kukaa hivyo hivyo na uwanja huo ukiwa mbovu. Lakini hatua zote za kupanua mji tumezipitia. Tumeomba Kata tatu zitoke vijijini ziingie mjini. Zile hatua zote tumezipitisha vizuri kwa kushirikiana na wenzetu wa Halmashauri ya Wilaya, tumeenda kwenye *RCC* na hatimaye mambo yako kwenye Ofisi yako Waziri Mkuu. Lakini kwa bahati mbaya sana na kwa masikitiko makubwa ni kwamba hadi leo inaonekana sijui ni kwa sababu gani, tumeshindwa kupewa maeneo hayo ambayo wala hayana gharama kwa Serikali, kwa sababu ni suala la kuhamisha mipaka na kusema kweli hilo limekuwa ni tatizo kubwa kwetu kwa sababu linazuia hata yale maendeleo ya mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo viwanda kama viwanda vikubwa vyta samaki tulivyo navyo mjini Musoma vinashindwa kufanya kazi kwa sababu ili uweze kupakia

samaki lazima uhamishe upeleke Mwanza au upeleke Nairobi. Leo watalii ambao wangekuja Musoma ndiyo wakaingia Serengeti lazima washukie Arusha na kwingineko, ndipo waje Serengeti na hii yote ni kwa sababu ya tatizo la eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutatua matatizo ya nyumba za watumishi, tulizungumza na watu wa NSSF. Wakakubali kutujengea nyumba 500. Wakaomba tuweze kuwapatia viwanja. Kwa sababu ya ufinyu wa eneo kama nilivyosema *square kilometre* 63, huo mradi tumeukosa kwa sababu wamekuja wanataka eneo na sisi Musoma Mjini hatuna eneo. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema kwamba haya yote yako kwenye uwezo wa Mheshimiwa Wazairi Mkuu na mimi nasema kwa kweli nitaunga hoja pale ambapo yatakuwa yamepata majibu mazuri. Ahsante. (*Makofî*)

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda moja kwa moja kwenye mchango wangu. Utaratibu tuliokuwa nao uliotumiwa na Serikali huko nyuma wa kupeleka madaraka mikoani umekuwa ni utaratibu mzuri na mfumo mzuri wa kuweza kuwapa wananchi madaraka na hivyo kuweza kusimamia miradi yao na maendeleo yao kwa ukaribu zaidi na kwa ufanisi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha sasa kwamba Halmashauri nyingi ambazo fedha nyingi sana za wananchi tunazopitisha hapa Bungeni zinakwenda kwenye Halmashauri zimeshindwa kusimamia vizuri fedha za wananchi kwa ajili ya maendeleo yao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia fedha nyingi karibu asilimia 80 ya fedha tunazopitisha hapa zinakwenda Wilayani. Lakini kutokana na Serikali kuwa *so loose* yaani imekuwa haina ufuatiliaji wa karibu Wilayani, ndiyo maana fedha nyingi sana zinatumika tofauti na malengo. Ukijaribu kuangalia ripoti ya CAG fedha nyingi zimetumika tofauti na mipango, zimetumika tofauti na malengo, zimetumika kwa jinsi ambavyo watendaji wameona wafanye. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetumika kwa muda mrefu. Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema kwenye taarifa yake kwamba suala la matumizi kinyume ya matumizi Wilayani linatiliwa msisitizo na watendaji wanaelekezwa. Lakini siyo leo hili limetokea, kila siku linatokea. Lakini ni kwa sababu ya kuendelea kukumbatia watumishi ambao wamekuwa siyo waadilifu ndiyo sababu matatizo haya yanaendelea. Ni kwa nini Serikali inashindwa kuchukua hatua kwa haraka? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Wilaya moja tu, Halmashauri inahamisha shilingi milioni 75 kutoka kwenye akaunti ya Mfuko wa Jamii inapeleka kwenye akaunti ya Amana, inaweka kule bila ridhaa ya mtu yoyote. Akaunti ya Amana inazalisha faida, ni kwa ajili ya nani, hakijulikani. Wilaya hiyo hiyo inachukua fedha za wananchi mfuko wa jamii shilingi milioni 41 inakwenda kununua hisa kwa ridhaa ya nani, fedha za

wananchi. Wilaya hiyo hiyo inachukua fedha za wananchi shilingi milioni 100 inapeleka kwenye Akaunti ya Amana ya Funge inatoa faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote haya hayatiliwi maanani. Hivi mpaka tunavyoongea bado watumishi hawa wako kazini, hivi wanasubiri nini? Kwa nini tunalea uzembe makazini? Mtu kama ameweza kutumia karibu shilingi milioni 300, akina mama wanajifungua kwa matatizo, hawana huduma za afya, wanachajiwu hata mipira ya kujifungulia, watoto hawapewi huduma, *dispensary* hazina dawa, fedha za huduma za afya zinakwenda kufanya kazi tofauti. Ni kwa nini haya yanafumbiwa macho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali au ndiyo ule utaratibu kwamba kila mmoja yupo kwenye nafasi yake anachukua chache mapema, kwa sababu hii ni hatari. Serikali inachelewa sana kuchukua hatua. Kwa hiyo, naomba sana Serikali ichukue hatua. CAG anavyotoa taarifa pale pale Serikali ichukue hatua za haraka. Kwa kufanya hivyo tunaweza kutoa fundisho. Lakini kwa kuwa tunakuwa wataratibu wa kuchukua hatua ndiyo maana watumishi wanajiona kwamba wana haki ya kufanya chochote na wanaoteseka ni wananchi wetu kwa sababu hii fedha imeenda kwa ajili ya kuhudumia wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la elimu, pamoja na kuwa kuwepo na juhudhi nyingi na Serikali na hapa hata hotuba nyingi zimesema na Wabunge wa CCM wanasema zimejengwa shule nyingi. Kweli tumeziona shule za Kata ambazo kwa kiasi kikubwa wananchi wameshiriki sana kujenga wenyewe, wamechangishwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado shule hizi zina matatizo makubwa sana na hasa maeneo ya vijijini. Kwa mfano shule zilizoko Urambo, shule ina mwalimu mmoja, shule haina madawati, shule haina maktaba, shule haina maabara na mwanafunzi anasafiri kilometra saba mpaka 10 akapate huduma ya elimu pale shulenii. Lakini cha kusikitisha ambacho najiuliza, tunaomba Serikali ituambie, mwanafunzi huyu huyu anayesoma kwa matatizo kiasi hiki, mwisho wa mwaka anapewa mtihani mmoja na mwanafunzi anayesoma Shaban Robert, anayesoma Azania, anayesoma shule nyingine zozote ambazo zina kila aina ya kumwezesha afaulu vizuri. Hapo siyo kuwakosea wananchi wakulima haki? Kwa maana nyingine ni kwamba watoto wa wakulima waendelee kuwa wakulima, kwa sababu hawesi kufaulu kwa kiwango cha kufika Chuo Kikuu kwa mazingira ya shule anayosoma. Kwa vyovoyote lazima atafaulu kwa kiwango cha *division four au zero*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, akifika hapo haonekani kwamba amefanya kitu kwa sababu kafeli, kwa hiyo, lazima atarudi kuwa mkulima. Lakini mwanafunzi anayesoma Azania Sekondari Dar es Salaam, *Kibo Boys* na shule nyingine ambazo ni mzuri atafaulu kwa sababu mazingira yanamruhusu. Ni kwa nini kusiwepo na kuangalia kwamba wanafunzi hawa ambao wanakosa huduma nzuri waangaliwe vipi kwenye mitihani? Ni kwa nini wapewe mtihani mmoja ule ule bila kuzingatia kwamba wana mazingira magumu na wengine wana mazingira mazuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kwa Serikali kwa hilo iliangalie, vinginevyo wanafunzi wa watu wa kubwa, watakuwa watu wakubwa na mwanafunzi wa mkulima ataendelea kuwa mkulima siku zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la huduma za afya. Mkoa wetu wa Tabora ni Mkoa ambao kwa suala la huduma za afya, niseme ni mkoa wa mwisho kwa Tanzania na ni mkoa ambao una wahudumu wachache sana na hata vituo vya afya vichache tofauti na mikoa mingine Tanzania na *specifically* kwa Wilaya yetu ya Urambo tatizo bado ni kubwa. Nimekuwa naongea hapa karibu kila mwaka, lakini bado tatizo ni kubwa. Nasikitika sana kwamba hapa nyuma kuna angalau *dispensary* au vituo vya afya vilikuwa na wahudumu wawili. Kwa sasa hivi wameondolewa, mhudumu mmoja amebaki mmoja, yaani kama hospitali ina wahudumu wawili anaondolewa mmoja, mwingine anapelekwa kwenye *dispensary* nyingine ambayo ilikuwa haijafunguliwa.

Kwa hiyo, tunasababisha tena matatizo mengine zaidi pale. Kwa mfano, *dispensary* moja tu Kijiji cha Usinge, Wilaya ya Urambo, ina mhudumu mmoja. Kata hii ina vijiji vitano, vijiji vina vitongoji kibao, mwananchi anatoka nyumbani saa 12 asubuhi anafuata huduma. Ni mama huyo ana mtoto mgongoni anafuata huduma saa 12 ili akahawi foleni. Anakaa hospitali siku nzima mpaka saa 12 jioni. Pengine aandikiwe dawa tu akanunue *pharmacy* pengine asipate huduma kabisa. Kwa hiyo, wengi wao wanaishia kwenda kutafuta dawa kwenye *pharmacy* za vichochoroni na tunafahamu *pharmacy* za vichochoroni hazina wataalamu. Kwa hiyo, watoto wanakuwa katika *risk* za kupata dawa ambazo hazistahili, kupata ushauri ambao haustahili, kwa sababu tu kwamba huduma za afya bado ni duni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali iangalie Mkoa wa Tabora kwa namna ya pekee, naomba sana ituangalie kwa namna ya pekee kwa sababu watoto wanaopoteza maisha kwa kukosa huduma ni wengi. Kina mama wanaojifungua bila kupata huduma za kujifungua kwenye hospitali ni wengi. Wengi wao wanajifungulia tu nyumbani. Kwa hiyo, ni matatizo. Miaka 45 bado wananchi hawajaweza kujikomboa bado kutokana na huduma za afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia nchi yetu ni nchi ambayo inafuata mfumo wa vyama vingi na kila chama ambacho kimesajiliwa kisheria kina haki ya kuingia kwenye uchaguzi na chaguzi ambazo tunaendesha zinashirikisha vyama vyote kwa sababu ni haki yao ya Kikatiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nina suala la kusikitisha, kwenye chaguzi za Serikali za Mitaa ambazo zilipita, sehemu ambazo vyama vya upinzani vimechukua nafasi, Serikali za Vijiji, Vitongoji, kumetokea tabia ya viongozi wa Chama cha Mapinduzi kuweka pingamizi kwa kushinikiza Watendaji wa Vijiji na wa Kata. (*Makofi*)

Kwa hiyo, wanawawekea viongozi wa CUF pingamizi, wanawasumbua Mahakamani kwa sababu ambazo hazina msingi. Mwananchi ameshachagua wameona ni chaguo lao. Ni kwa nini msikubaliane na huyo kwamba wameona anafaa kwa sababu

wamemchagua kati yao hawakushinikizwa, ameshinda kwa kura hakuna upendeleo. Ni kwa nini utaratibu huu unakuwepo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu afuatilie. Urambo yapo maeneo mengi sana ambayo wamebandikwa kesi. Kesi zipo Mahakamani, wanafanya kazi ya kukimbia barabarani badala ya kukaa wahudumie wananchi ambao wamewapitisha kwa kura nyingi na wanastahili kuwahudumia na kwa ajili maendeleo ya wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi ya mimi kuchangia katika hoja hii ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Pia napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, kwa hotuba yake nzuri sana alioitoa ndani ya Bunge lako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kusema yale niliyonayo ningependa tu kuwaambia ndugu zangu wa Chama cha Mapinduzi wajibu wa Kambi ya Upinzani si kuunga mkono na kupiga makofi tu, tuna uwezo wa kutambua mazuri na tutayapongeza, lakini hatuwezi kusifia kila kitu na ndiyo wajibu wetu na ndiyo maana tuko ndani ya Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni Wabunge kama Wabunge wengine, tutaendelea kusema pamoja na kuwa wanatuita majina mengi na leo nimesikia jina jipya la kimada. Lakini sisi hatuogopi kuitwa majina hayo, tutaendelea kusema. Tunamwogopa Mungu na wananchi tu waliotuleta ndani ya Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo napenda sasa niende kwenye hoja. Nina wasiwas sana na takwimu ambazo zinaletwa aidha, kwenye Wizara au ndani ya Bunge lako Tukufu. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (*LAAC*) na hivi majuzi wenzetu wakiwa wanapitia Bajeti, Kamati yetu ilikuwa inatembelea miradi katika Mikoa mbalimbali, nilibahatika kwenda katika Mikoa ya Kaskazini yaani Mikoa ya Arusha na Manyara na kule tulitembelea miradi mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba nizungumzie suala la maji, katika kitabu cha Hali ya Uchumi, tumeambiwa miradi ya maji vijijini ni 2,060 imekamilika kwa mwaka 2009. Naomba nitoe mifano miwili tu na hii niliona kwa macho na siyo kwamba ninazua na kwa bahati nzuri tunaongozana na Wabunge wa Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitembelea Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto. Katika miradi tuliyochagua, tulichagua miradi miwili ya maji. Tulichagua mradi mmoja wa maji Kijungu ambao ulikuwa chini ya *TASAF*. Mradi huu ultumia shilingi milioni 36 na kwenye kitabu walichokileta cha *LAAC* walituambia mradi huu umekamilika, lakini tulipofika kutembelea eneo lile mradi ule haufanyi kazi. Tulichokuta pale ni mabomba, wananchi wa Kijungu hawana maji mpaka leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaposimama hapa na kusema Ilani ya Chama cha Mapinduzi imetekelzeza, sina tatizo na hilo, ningefurahi zaidi kama Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ingetekelzeza wananchi wa Kijungu wakapata maji. Hiyo ingekuwa Ilani imetekelzeza wananchi wangepata maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi milioni 36 zimetumika, maji hakuna, kitabu wameandika mradi umetekelzeza. Mradi wa pili ni mradi wa Sunya. Huu ni mradi wa WSDP ambao ulitakiwa ukabidhiwe toka Novemba, 2009 na huu ninaamini kwamba ulikuwa katika ile miradi tuliambiwa imekamilika mwaka 2009. Mradi huu umetumia shilingi milioni 174.4. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifika eneo la tukuo ambako mradi huo ulikuwa unatekeleza na tulikutana na wananchi wengi sana na walikuwa wana kilio kikubwa sana cha maji. Mradi ule haujakamilika, haujaanza kutumika na huku tunaambiwa miradi 2,060 imekamilika kwa mwaka 2009. Ndiyo maana ninasema kwamba takwimu ambazo wanatuletea aidha, zinazopelekwa Wizarani si za kweli ama viongozi wetu wanaogopa kufukuzwa kazi na wakubwa zao ndiyo maana wanaamua kuandika taarifa za uongo. Kibaya zaidi tulipita katika kijiji kimoja kinaitwa Laiti na kingine kinaitwa Embulei Murutagozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nilikuta kitu kikubwa sana na cha kushangaza. Tulikuta wakulima wanabadilisha debe la mahindi na debe la maji. Biashara iliyofanywa na mababu zetu, leo ni miaka 50 baada ya Uhuru wananchi wanabadilishana mahindi na maji katika Tanzania halafu tunasema Ilani ya Chama cha Mapinduzi imetekelzeza na wananchi wanashindwa kupata huduma ya maji safi na salama!! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji wanayokunyuwa Watanzaia walioko huko vijijini na niliyoyashuhudia mimi, ng'ombe wanakunyuwa humo humo, binadamu humo humo, mbuzi, mbwa, wote wanakunyuwa maji hayo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji wanayokunyuwa wananchi hao mimi na wewe hatuwezi kunywa na hata kama tunakunyuwa kwa ajili ya kuwaridhisha kwamba tupo pamoja nao au tupate kura, basi baada ya saa chache lazima twende hospitali kwa sababu tutakuwa tumeshapata maradhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tena mradi mwingine tulitembelea ulikuwa katika Halmashauri ya Mji wa Babati. Tulitembelea shule ya sekondari na shule hii ilipewa jina la Mbunge wa Babati kwa heshima, Mheshimiwa Kwaangw' na kwa bahati nzuri nimetembelea shule hiyo kwa mara ya pili. Mara ya kwanza nilitembelea Kamati yangu ilipokwenda hapo mwaka 2009. Tulikuta tena ujenzi wa madarasa na vyoo, tulikuta haujakamilika mwaka 2009 mwezi Januari. Tukatoa maelekezo kwamba wasitishe miradi mingine na wahakikishe nyumba za walimu na vyoo vinamalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Kamati yangu imerudi tena mwezi jana. Tulichokiacha Januari 2009, ndivyo kilivyo mpaka ninavyozungumza leo. Lakini kwenye taarifa ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za

Mitaa (TAMISEMI) wanasema wamejenga nyumba 204 kama sikosei, hizi taarifa nawaambia si sahihi kwa sababu walimu au wakuu wa Idara waliopo kwenye Halmashauri zetu hawaleti taarifa sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusemea jambo lingine ambalo tumekutana nalo katika Kamati yetu, ni mfuko wa vijana na wanawake. Kamati yetu ilizitaka Halmashauri zitoe taarifa za mfuko huu toka ulipoanza mpaka sasa una faida kiasi gani, ni kiasi gani kilichokopeshwa, ni kiasi gani cha watu wanaodaiwa na mchango wa Halmashauri na michango kutoka Serikalini au wafadhili wengine. Lakini mpaka sasa ninavyosema ziko Halamshauri zaidi ya 40 zimeshindwa kuleta mchanganuo huo mbele ya Kamati yetu na hii inatutia wasiwasije, pesa hizi zipo au zimeshaliwa? Kwa sababu fedha hizi zingekuwepo zingewasaidia vijana pamoja na akina mama kunyanya uchumi wao na hata wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katiika Bajeti ya Waziri wa Fedha, Wabunge walilalamika kwamba vijana wako vijiweni, hawafanyi kazi, wanacheza bao na *pool*. Lakini mimi ninaamini kama fedha hizi zingekuwepo na zingetumika vizuri, zingeweza kuwasaidia vijana wetu wakaachana na kucheza bao na kucheza *pool*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwapa vijana *t-shirt*, kanga na kofia, hatuwasaidii bali tunawaendeleza umaskini. Tunawatumia vijana hawa wakati wa kampeni kwa kuwapa vitu hivyo lakini ninaamini kama tungewasaidia kwa mikopo, watu wa maendeleo ya jamii kwenye Halmashauri wangetoa masomo kwa vijana hawa na akina mama hawa, kweli umaskini ungepungua kwa wananchi wetu wa vijijini na pato la maskini lingekuwa. Lakini kusema tu Ilani imetekelvezeka wakati wananchi wanaendelea kuwa maskini hata mlo mmoja wa siku unawashinda, sikubaliani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

**MHE. DR. LUKE J. SIYAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuhusu Bajeti ya Ofisi yake na Bajeti ya Ofisi ya Bunge ikiwa ni pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, kuhusu utendaji wa Wizara ya TAMISEMI kwa mwaka huu wa 2010 hadi 2011. Awali ya yote naomba nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi wa Wilaya ya Mbozi, hususan wale wa Jimbo la Mbozi Magharibi, ambao kwa miaka hii mitano wameweza kushirikiana na mimi kwa dhati katika majukumu yangu ya kuhakikisha nawawakilisha katika Jimbo lao. (*Makofi*)

Napenda niseme niko nao na leo hii napenda nitamke kwamba waendelee na ule ushirikiano walionipa kwa hii miaka mitano na ninaamini wataendelea kuwa na imani hiyo ili waweze kunipitisha katika uchaguzi ujao niweze kushirikiana nao tena kwa miaka mitano inayofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo sasa naomba nichukue fursa ya kipee kabisa kuishukuru Serikali ya Awamu ya Nne, kwa yale mambo mazuri ambayo imeyafanya katika Jimbo hili la Mbozi Magharibi ambalo kwa hakika ni Jimbo lililopo

pembezoni mwa nchi na kwa kiasi kikubwa ni Jimbo la Vijijini ambalo kwanza kabisa hadi miaka mitano iliyopita kulikuwa hakuna kitu ambacho tumeweza kukusema na cha kujivunia. Lakini hivi sasa napenda nianze kwa kusema kwamba katika hii miaka mitano, Serikali ya Awamu ya Nne imeweza kuboresha mambo yafuatayo; tulikuwa hatuna barabara kabisa lakini hivi sasa kwa sehemu kubwa Jimbo hili linafikika. Tulikuwa pia na shule nne tu za sekondari, hivi sasa tunazo 15 na mojawapo ikiwa na *high school*. Kwa kiasi kikubwa vijiji vyetu vilikuwa havina maji kabisa kama alivyosema Mheshimiwa wa Upinzani kwamba, mbwa na ng'ombe walikuwa wanashirikiana lakini hivi sasa naweza kusema robo tatu ( $\frac{3}{4}$ ) ya hivi vijiji vina maji ya uhakika. Kwa hiyo, hili ni suala la kipekee la kujivunia kwetu na tunaamini katika miaka mitano ijayo kila kijiji kitakuwa na maji yakutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ni wakati wa kampeni ya Mheshimiwa Rais hapo mwaka 2005 pale Mjini Tunduma, kulikuwa hakuna maji kabisa. Ilikuwa ama watu wanachukua kwa mikokoteni kutoka mji wa Nakonde upande wa Zambia ama anafuata kilometra 10 kutoka Kijiji cha Mpemba njia panda ya Ileje, hivi sasa maji Tunduma kutoka kwenye vile visima virefu vilivyoimbwa ni mengi ya kutosha; tatizo letu sasa hivi ni kupata mtandao wa kuyasambaza katika ule mji ili kila mtu aweze kuwa na maji ya uhakika. Lakini kwa hakika napenda nichukue fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Mbozi Magharibi kwamba Serikali katika usambazaji wa maji imetusaidia sana na tunashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee napenda pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, ambaye mwaka jana tarehe 31 Oktoba, aliweza kufika Jimboni kwetu na hususan kule kwenye tarafa ya Kamsamba, sehemu ambayo ilikuwa haifiki na alikuwa hajapata kufika Rais ye yeyote kwa miaka 28 iliyopita, lakini yeye akafika na kuahidi kumalizia ujenzi wa kilometra 25 za ile barabara ambayo ilikuwa imebakia pamoja na daraja kubwa ambalo litaunganisha mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Rukwa na hivyo kulturahisishia sisi namna ya kuweza kufika hadi Kigoma, Kagera, Rwanda na Burudi na mpaka hivi sasa napenda niseme daraja lile usanifu unaendelea na kwa hiyo, litaanza kujengwa hivi karibuni na kwa uhakika kabisa nimeambiwa kwamba zile pesa za kujenga kilometra 25 za mwisho kati ya Kamsamba na Itumbula, nazo zimepatikana, barabara hiyo itamaliziwa wakati wowote na hivyo kutupa matumaini ya kuweza kusafiri kwa urahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda niseme zile barabara nyingine za mkoa, barabara za Sangano, Igamba, Utambalila pamoja madaraja yake Serikali imeahidi kuzijenga. Pia barabara kutoka Kakozi kuambaa na mpaka wa Zambia, Kasinde na kuungana na ile barabara inayokwenda Kasanga Ziwa Tanganyika, Serikali ina mpango wa kuijenga na hivyo basi inatupa matumaini kwamba sasa hivi tunaweza tukasafiri kwa urahisi. Pia napenda niseme Serikali imeweza kutoa fedha kwa ajili ya umwagiliaji mkubwa kabisa huko katika Bonde la Ufa la Bonde la Rukwa, sehemu ya Naming'ongo ambayo Serikali imeahidi kutoa shilingi bilioni 5.6 ili iweze kumalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine wa umwagiliaji uko kijiji cha Iyendwe mpakani na Zambia unaogharimu karibu shilingi nusu bilioni na hii yote ni

katika kuhakikisha kwamba tuna kilimo bora. Baada ya hapo napenda niseme kwamba pamoja na hayo, tungependa Serikali iangalie mambo yafuatayo; moja ni katika wilaya yetu ya Mbozi na hususan Jimbo hili la Mbozi Magharibi, suala la pembejeo za kilimo limekuwa na utata. Msimu uliopita kulikuwa na vocha zilizopotea zikawa zimekamatwa zikapelekwa Mahakamani, lakini jambo la kushangaza tunaambiwa kwamba sasa hivi hata Mahakamani zimepotea. Tunaomba Serikali ifuutilie ili tuweze kujua hatma ya hizo vocha za pembejeo zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kwamba tuna matatizo ya miji midogo ambayo ninaamini kwa nchi nzima. Kwetu tunayo miji midogo ya Tunduma na Vuawa ambapo tuna Mwenyekiti wa Mji Mdogo pamoja na Afisa Mtendaji na wakati huo huo tuna Diwani kwenye hiyo miji midogo, sasa hatuelewi kwa kweli kwamba hivi sasa katika muundo wetu kama huduma zile za mji mdogo ziko chini ya Mamlaka ya Mji, Diwani anafanya nini kwenye hizo mamlaka?

Pia napenda niseme kwamba pamoja na shule zetu, tumekuwa na upungufu wa walimu kiasi cha kwamba uwiano wa walimu na wanafunzi ni mwalimu mmoja kwa wanafunzi kati ya 57 na 67, kwa hivyo tunaomba Serikali itusaidie walimu. Pia napenda niseme lengo letu ni kuwa na wanafunzi nusu kwa nusu lakini mwaka huu wanafunzi wetu waliofanya mitihani katika wilaya ya Mbozi, kati ya wale wanafunzi 18,500, 16,500 walikuwa ni wavulana, wasichana walikuwa ni 2,500. Sasa hii yote tunaamini kabisa pengine ni kutokana na upungufu wa walimu, watoto wa kike wanashindwa kuwa wavumilivu kukaa shulenii na hivyo wanakwenda kwenye shughuli zao nyingine ama wanaolewa, ama hawaoni haja ya kwenda shule kama hakuna walimu na kwa hiyo, matokeo yake tuna uwiano mbovu wa wanafunzi 16,000 wakiume kwa wanafunzi 2,500 wakifanya mtihani wa darasa la saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimalizie kwa kusema kwamba katika hotuba ya Waziri Mkuu, kwenye ujenzi wa viwanja nimeona viwanja mbalimbali vyta ndege vimetajwa, lakini uwanja wa ndege wa Songwe haukutajwa kabisa katika ile hotuba yake. Hatuelewi kuna nini kinachoendelea wakati uwanja tulitegemea wakati wowote mwaka huu ufunguliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, naomba niseme naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii adimu na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na maeleo ya kiutendaji yaliyotolewa na Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Celina Kombani. Napenda kutamka kuwa naunga mkono hoja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Ranya, natoa shukrani na pongezi nyingi sana kwa Serikali ya Awamu ya Nne, chini ya uongozi shupavu, usioteteraka wa Rais Mheshimiwa Jakaya Kikwete na chini ya utendaji thabiti unaosimamiwa na jemadari wa maendeleo, mtoto wa mkulima na mfugaji, Waziri Mkuu,

Mheshimiwa Mizengo Pinda, pamoja na timu yake ya askari shupavu amba ni Mawaziri, Naibu Mawaziri, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, nawapongezeni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Rarya hawatasahau jinsi Serikali ya Awamu ya Nne ilivyoshughulikia kero sugu kuhusu wizi wa mifugo wilayani Rarya, hasa wavamizi na wauwaji wa wananchi wasio na hatia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutamka hapa Bungeni tatizo hili sugu, Mawaziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Waziri wa Mambo ya Ndani pamoja na viongozi wote wa dola wakiwemo viongozi wa Jeshi la Polisi na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, walihamia Rarya na wakaweka kambi pale. Waliwahakikishia wananchi wa Rarya kwamba Serikali ya Awamu ya Nne, haitavumilia kuona wananchi wanapoteza mali zao na maisha yao na waliwahakikisha kwamba tatizo hili sasa litakuwa ni la kihistoria baada ya kukubali kuunda Kanda Maalum ya Polisi Mkoa wa Rarya na Tarime. Kwa hivyo, nawapongezeni sana na wananchi wamefurahi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu alipokuja katika kijiji cha Changuge ilikuwa ni mara ya kwanza kumuona na mara ya kwanza kuiona helikopta inatua kijijini. Iliwatia moyo sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, na naomba ufikishe shukrani za wananchi wa Rarya kwa Mheshimiwa Rais na Mawaziri wote na wapiganaji wote na Jeshi la Polisi kwa jinsi walivyoshughulikia na wanavyoendelea kushughulikia tatizo hili sugu la wananchi wa Rarya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pamoja na ponezi hizi wamenituma niwakilishe kwako maombi yao kama ifuatavyo; kwanza wanasema Mheshimiwa Waziri Mkuu, wewe ni mtoto wa mkulima na mfugaji, na walifurahi sana jinsi uliviyowatia moyo lakini wanaomba tukio la uvamizi na mauwaji yaliyotokea Rarya, Serikali iyachukue kama maafa. Wananchi waliopoteza maisha yao ni 40, ng'ombe walioibwa ni 2,600, wananchi waliopata ulemavu wa kudumu ni watu 20. Wanaomba Serikali iwasaide kuwapatia fidia na kama haitawezekana, basi hata kifuta machozi. Wananchi hawa sasa wamebaki maskini, nguvu kazi hawana na mifugo yao pia imepotea na kazi imepungua.

Pili, wanaiomba pia Serikali itoe hadharani orodha ya wezi wa mifugo walipigiwa kura za siri. Kama Serikali itasita, wananchi walioathirika na wananchi wengine wa Rarya watawataja kwa kupitia magazeti. Nasema kwa masikitiko makubwa kwamba majambazi hawa bado wanaishi kama watakatifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu wananchi wa Rarya, wanawapongeza walinzi wetu na Jeshi letu la Polisi na Jeshi la Ulinzi kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wilaya ya Rarya. Wanaomba vijana hawa wapatiwe tuzo maalum na kama itawezekana wapandishwe vyeo kwa uchapaji wao hodari wa kazi, utiifu wao kwa Amiri Jeshi Mkuu na kwa nchi yao. Waongezewe posho na vitendea kazi.

Mwisho nawashukuru sana wananchi wangu kwa imani yao kwangu na ninawahakikishia kuwa nitakuwa pamoja nao na sitawaangusha. Tumefanya mengi,

barabara zote za mkoa zinapitika wakati wote, barabara zote za wilaya zinapitika, sasa tumeanza kujenga barabara ya lami mpaka mpakani na Kenya. Tumeweza kuchimba mabwawa na malambo 43, tumeweza kujenga shule za sekondari 30 na sasa upo mpango wa kujenga vyuo vinne vya ufundu stadi katika wilaya ya Ranya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana wananchi wangu na nataka niwahakikishie kuwa niko pamoja nanyi na sitawaangusha. *Aluta Kontinua*, mapambano bado kabisa yanaendelea. (*Makofi*)

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na ile ya Mheshimiwa Waziri Wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – (TAMISEMI) ambazo zimetolewa asubuhi ya leo. (*Makofi*)

Naomba nikiri kwamba kwenye orodha nilikuwa najiona kwamba nitakuwa mchangiaji wa pili kesho, hata hivyo ninashukuru kwa kunipa nafasi hii, nitatoa yale ambayo nilikuwa ninayafikiria niyazungumze hiyo kesho na mimi nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri sana, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, mama Celina Kombani, kwa kutoa hotuba nzuri sana ya utendaji wa kazi katika kipindi cha mwaka huu, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba nianze kama wenzangu wengi walivoanza kwamba ni lazima tukiri kwamba hakuna nchi hapa duniani ambayo inaweza ikamaliza matatizo yake yote siku moja na tunajua kwamba maendeleo ni hatua au mchakato, kwa maana hiyo hatuwezi kumaliza matatizo yetu yote tuliyonayo siku moja na mimi ninaamini kwamba zipo nchi tajiri duniani kama Marekani, Uingereza, Japan na nyinginezo ambazo mpaka leo zina matatizo yake na zinaendelea kuyatatua kwa kadri ya nafasi zao kiuchumi na hata Tanzania, tutaendelea kumaliza matatizo yetu taratibu na iko siku yote yatakuwa yamekwisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri wapinzani wanasema ni lazima waseme kwa sababu kama wengi walivyosema kwamba hawawezi wakawa wanatupigia makofi lakini ukweli ni kwamba tunafanya vizuri sana katika maeneo mengi. Naomba niseme na nitoe mifano kidogo; kule Mbozi, Wilaya ya Mbozi Mashariki, wakati mimi nakuwa Mbunge mwaka 2005, tulikuwa na sekondari za Kata 13. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika kipindi cha miaka mitano tumejenga sekondari mpya 26, kwa hivyo, Wilaya ya Jimbo la Mbozi Mashariki leo lina sekondari 39, haya ni mafaniko makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mbozi yote Magharibi na Mashariki tuna jumla ya sekondari 54, nani anaweza akabeza mafanikio makubwa namna hii. Ni mafanikio makubwa na mimi nampongeza kweli Mheshimiwa Rais kwa uamuzi ule walioamua wa kwamba lazima tuwe na sekondari kwenye kata zote, tumefanikiwa kwa sehemu kubwa sana katika kufuta ujinga kwa maana vijana wetu wengi ambao wangebaki nyumbani ambao leo wengine wangkuwa wanauzu baa, wangkuwa

wanafanya kazi isiyoeleweka wako sekondari, tunabeza yote haya kwa vyovytote vile wengi hatuna shukrani. Mimi naipongeza sana Serikali ya Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa uamuzi wake huo kwa kufanya mambo mengi mazuri ya namna hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo naomba nichangie haya mengine yafuatayo, ukizungumza kilimo Mbozi unazungumza siasa na ukizungumza siasa unazungumza kilimo na mimi nimewahi kusema kila ninaposema mbele ya Bunge lako kama naweza nikazungumza hotuba ya dakika kumi nisiguse kilimo maana yake nitakuwa sijawawakilisha wananchi wa Mbozi wa Mashariki ambao wamenileta ndani ya jengo hili.

Kwa hiyo, naomba nichangie kuhusu kilimo, naomba nianze mbegu pamoja na mbolea hasa zile ambazo zinatolewa chini ya utaratibu wa *voucher*. Wilaya ya Mbozi tuna karibu kaya 120,000 kwa ujumla wake. Lakini mwaka jana ni kaya karibu 80,000 peke yake ambazo zilipata mbolea za ruzuku, kwa maana hiyo kaya zaidi ya 40,000 hazikupata mbolea hiyo au *voucher* za ruzuku kwa ajili ya mbegu na mbolea.

Sasa tunazinyima kaya hizo 40,000 na hili linatuweka pabaya maana yake tunakuwa tunawapa Watanzania mbolea kwa ubaguzi kwamba wewe unstahili na wewe hustahili. Hili linatupa taabu kubwa sana, viongozi tunatumia vigezo gani kumpa huyu na kumnyima huyu pamoja na kwamba tunaweka vigezo kwamba unashiriki shughuli za maendeleo. Lakini kimsingi suala hili linaonyesha ubaguzi na mimi namuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu hebu wawe na utaratibu mzuri wa kuhakikisha Watanzania wengi wanapata mbolea ya kutosha, kama hili haliwezekani basi tuhakikishe kwamba taasisi nyingi za mikopo zinakuwepo na nyingi zinaweza zikawafikia Watanzania kule vijijini ili waweze kupata mbolea ya kutosha na kwa maana hiyo waweze kuzalisha inavyostahili. Lakini kwa utaratibu uliopo bado tutakuwa tunaendelea tunawabagua baadhi ya Watanzania jambo ambalo naamini halitatupeleka sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala ununuzi wa matrekta makubwa pamoja na *power tillers*, suala hili namuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu alisimamie sana, nilikuwa kwenye kikao cha RCC Mbeya nadhani kipindi cha mwezi uliopita jambo moja ambalo lilinishitua sana kila wilaya Mkurugenzi alipokuwa anatakiwa na Mkuu wa Mkoa aeleze amefikia wapi katika ununuzi wa *power tillers* zile, kila Mkurugenzi alikuwa anasema sisi tumenunua trekta tayari au wengine tumeagiza. Lakini kilichoshangaza ni bei ambazo *power tillers* hizi zinazwa, wengine wanasema tumenunua kwa shilingi milioni tano, wengine kwa shilingi mlioni saba, wengine kwa shilingi milioni tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi hii ilinishangaza, hii ni Serikali moja kwa nini tununue *power tiller* ya aina hiyo hiyo moja, pengine kutoka sehemu moja lakini kwa bei zinazotofautiana? Mimi hili nililihoji, magazeti yakaandika walisema Dhambi afichua dhambi nyingine ingawa mimi siyo dhambi naitwa Zambi, lakini wakasema dhambi afichua dhambi nyingine. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani haya ni makosa hebu tuyasimamie, kama matrekta haya tunaweza tukayanunua kutoka China au mahali pengine kama ni India kwa

nini tusiwe na *source* moja kama Serikali? Kwa nini kila Wilaya, Mkoa ununue kwa bei yake? Mimi nadhani haya ni matumizi ya pesa ambayo siyo mazuri sana na mimi ninamuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika hilo pengine alitolee maelezo ili tuweze kujua kwamba pesa Serikali inatumika vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa nilizungumze ni suala la mikopo kupitia dirisha la kilimo ndani ya Benki ya Rasilimali ya Taifa (*TIB*). Niliuliza Serikali wiki iliyopita ni masharti gani ambayo yanahusika na ukopaji wa pesa hizi? Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu alitoa masharti ambayo kwa hakika mjomba wangu kule kijijini, nina hakika hata kule kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kule Mpanda na maeneo mengine Watanzania wengi hawawezi wakakamilisha masharti haya na kwa mtazamo wangu mimi ninaona benki hii tunaianzisha kwa faida ya watu wachache lakini tukisahau Watanzania wengi wa kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nimuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu waangalie yale masharti upya ili benki hii iwe ya Watanzania, lakini isiwe ya watu wachache ambao tayari wanaweza wakayakamilisha yale masharti bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kulizungumza hilo naomba nizungumze jambo lingine kama nilivyosema suala la sekondari. Pamoja na mafanikio makubwa ambayo tumeyapata katika sekondari zetu hili Watanzania wengi tunazungumza, tunakwenda vijijini bado tunaona kuna taabu ya walimu kuishi katika maeneo yetu. Nyumba za walimu ni tatizo kubwa pengine kuliko tatizo lingine lolote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua hatuna maabara za kutosha, lakini wanafunzi wako darasani, walimu wanashindwa pa kulala. Mwalimu mmoja analazimika atembee kilomita 10 kwenda kufundisha sekondari moja. Sasa kwa mazingira yaliyopo walimu wengine wanalazimika kuacha shule. Kwa hiyo, mimi naomba pamoja na jitihada zinazoonekana za dhati kabisa za Serikali, lakini tuwe na mpango wa makusudi kabisa wa kujenga nyumba nyingi za walimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa Bajeti hii tunayoitenga ya kujenga nyumba za walimu nina hakika hatutafanikiwa sana. Ninaomba sana ili walimu watulie mashulenii suala la kujenga nyumba za walimu pamoja na hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa kwamba tutatenga shilingi bilioni 50 kila mwaka basi naomba hilo lifanyike *seriously* ili tuweze kujenga nyumba nyingi na walimu ili waweze kukaa kule vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko tatizo pia la kujenga hosteli katika shule hizi na hili liwe la lazima kujenga hosteli katika maeneo yale. Watoto wengi wa kike leo ni waathirika wakubwa wa kukaa mbali na sekondari zile. Mimi naomba nitoe mfano mmoja, kuna shule yangu moja ya sekondari iko Kata ya Isansa inaitwa Iganya. Utashangaa na ni ukweli, watoto wa kike 74 wamepata mimba katika mwaka mmoja na mazingira ndiyo yanayofanya jambo hili litokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba ili kuwalinda hawa watoto wa kike, tujenge hosteli nyingi ili watoto hawa waweze kukaa salama zaidi na waweze

kusoma vizuri zaidi. Tukiacha hivi Watanzania hawa wengi, vijana wetu wengi hawa badala ya kuwaendeleza na kuwajenga, tutakuwa tunawaharibu. Kwa hiyo, mimi naomba sana huu mkakati wa hosteli uwekwe madhubuti kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine tujenge maabara katika sekondari hizi. Kuna mpango wa Serikali mzuri lakini naomba na wenyewe uende sanjari na ujenzi wa hosteli lakini pia na ujenzi wa nyumba za walimu. Watoto wengi wanasoma bila vitendo, wanasoma kwa kuoneshwa kitu lakini hawaendi maabara. Pamoja na utaratibu wa Serikali kwamba mtenge chumba kimoja mfanye mazoezi lakini nashauri Serikali ifanye hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ninashukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. OMARI S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza nitumie nafasi hii kwa kweli kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wote kwenye ofisi yake kwa kazi nzuri wanazozifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba niungane na wenzangu wanaosema kwamba tusibeze juhudzi za wananchi za kujenga shule za msingi na za kata. Tutafanya makosa makubwa sana kubeza juhudzi za wananchi. Shule hizi nyingi zinajengwa na wananchi kutokana na nguvu zao. Tunachotakiwa sisi kufanya ni kujenga uwezo wa rasilimali na tuzielekeze kule, lakini tusibeze nguvu zao ambazo wanazitumia katika kujenga shule hizi. Shule zina matatizo mengi lakini bila shaka tukiendelea kuelekeza rasilimali kwenye hizi shule zetu za sekondari na msingi, mimi nina hakika kwamba, tutasonga mbele na bila shaka Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu atakapotoa hotuba yake tutapata mwelekeo mzuri wa kwamba nyumba za walimu zinajengwa kwa namna gani na tatizo la maabara na vitabu. Kwa hiyo, mimi ninaungana na wale wanaosema kwa kweli tusibeze nguvu za wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kusema kwamba niipongeze Serikali kwamba kwa kweli sisi Mkoa wa Manyara katika majedwali kadri nilivyoangalia kwenye fedha za ujenzi za maendeleo kwa kweli tumekuwa Mkoa wa tano kwa hiyo, tunashukuru na vilevile kwenye fedha za ujenzi wa Hospitali. Hospitali ambazo zimetajwa zinazojengwa upya ni tatu ambazo ni Manyara, Singida na Mbeya na kwa kweli Serikali imeendelea kutenga fedha kwani Singida wamepata shilingi bilioni mbili na sisi Manyara vilevile tumepata shilingi bilioni mbili. Nadhani kwamba hizi ni juhudzi nzuri, tunaipongeza Serikali kwamba ujenzi hautasimama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni vizuri tuangalie kwamba miradi hii mikubwa tukiendelea kuweka fedha hizi kidogo kidogo kwa kila mwaka itachukua miaka mingi. Ni vizuri miradi hii mikubwa ambayo inagusa afya za wananchi ikatengewa mafungu maalum ili ujenzi wake ukamilike kwa muda mfupi iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitumie nafasi hii kwa kweli kuishukuru Serikali mwaka huu kwa namna ambavyo Mkoo wa Manyara ulivyopata bahati ya kuwasha Mwenge wa Uhuru. Tumepata bahati hiyo na nitumie nafasi hii kumshukuru Mkuu wa Mkoo wa Manyara na Mkoo wa Wilaya ya Babati kwa juhudini walizofanya kuhakikisha kwamba shughuli za mwenye zilikwenda vizuri sana na kwa wale ambao huwa hawaamini kwamba mwenye unaleta maeendeleo waje Babati waone. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi iliyofanyika ni nzuri, tumepata na uwanja wa michezo na juhudini zimekuwa nzuri na miradi mingi kwa kweli imefunguliwa kwa hiyo, nataka nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri ambayo kwa kweli imeifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache ningependa nijielekeze kwenye jambo muhimu sana ambalo nilidhani kwamba kwenye hotuba ya Waziri Mkuu lingetiliwa mkazo zaidi na hasa katika miaka ijayo ni hili suala la menejimenti ya kuzuia na kupunguza maafa yanavotokana na mafuriko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Babati imepata athari kubwa ya mafuriko kwa miaka mingi, tangu miaka ya 1960, miaka ya 1970, miaka ya 1990, na sasa miaka ya 2000 mpaka sasa 2010. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya hiyo imeendelea kupata athari kubwa sana, mwaka 1990 tulipata athari mbaya sana za mali na vilevile kupoteza uhai wa watu, lakini na mwaka 1997 na mwaka 1998 vilevile tulipata mafuriko makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwaka 1990 baada ya Serikali kuona kwamba matatizo ya mafuriko ni makubwa katika sehemu mbalimbali za nchi ilitungwa Sheria mwaka 1990 ya kudhibiti maafa (*Disaster Relief Coordination Act No. 9*) na ambayo ilikuwa imepanga mambo makubwa manne; kuhakikisha kwamba watu wanakuwa na utayari, kuhakikisha kwamba kunakuwa na mipango ya kuzuia mafuriko, kuhakikisha kwamba kunakuwa na mwitikio kwa wananchi, lakini kuhakikisha kwamba baada ya tatizo kutokea kunakuwa na mipango ya kujenga upya au kufanya ukarabati katika maeneo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya Serikali kuona tatizo hili ni kubwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali alikwenda kufanya ukaguzi na alitolea mfano wa Wilaya ya Babati. Katika ukaguzi huo mambo yaliyojitekeza ni kama yafuatayo na ninadhani yanapaswa kuwa mfano kwa nchi nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza alisema kuongezeka kwa hatari ya kutokea mafuriko katika miaka inayokuja na kwa Babati imeonesha kwamba katika miaka inayokuja hatari itakuwa kubwa. Lakini vilevile Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu aliona kwamba hakukuwepo na hali ya utayari kwa mkoa na Wilaya zake, kwa maana ya zile Kamati zinazohusika, lakini vilevile kukosekana kwa misaada toshelezi kutoka Idara ya Maafa kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile aliona mipango ya miji siyo mizuri kwamba makazi ya watu wakati mwingine viwanja vinapimwa kwenye maeneo ambayo maji yanapita na makazi ya biashara yanajengwa kwenye maeneo ambako mafuriko yanapita. Lakini vilevile ukarabati wa barabara aliona kuna upungufu mkubwa sana, kwamba hauzingatii matatizo ya mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile aliona kwa nchi nzima hakuna rejestya ya maafa ya mafuriko. Kama kungekuwa na rejestya ya maafa basi ina maana kwamba mifano ingeweza kutumika na kuhakikisha kwamba hiyo ndiyo inakuwa chanzo kizuri cha kuhakikisha kwamba tunadhibiti mafuriko katika maeneo mengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la pale Babati ni kwamba sasa hivi kuna eneo la Kigongoni, daraja litajengwa kwa sababu kuna utaratibu wa Serikali kujenga barabara ya lami. Lakini tatizo linalojonesha pale ni kwamba korongo linachimbika zaidi chini na linachimbika kurudi nyuma, itakapofika kwenye daraja pale Kigongoni, ziwa lote litahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo litakuwa tatizo kubwa sana kwa kuwa ziwa litakuwa juu na korongo litakuwa liko chini. Kwa hiyo, uchimbikaji wa makorongo unaporudi nyuma na kuvuta kina cha ziwa pale chini basi ziwa lote litahama na itakuwa maafa makubwa sana katika maeneo mengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kuipongeza sana ofisi ya Waziri Mkuu, kupongeza hotuba hii yetu ya leo na kumpongeza sana kipekee Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Manaibu Mawaziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nijikite kwenye jimbo, kwenye sekta ya afya katika jimbo letu la Kigamboni kuna maeneo ambayo yamechukuliwa kwa ajili ya maendelezo na kazi maalum. Lakini tumekuwa na matatizo makubwa juu ya ulipaji wa fidia katika maeneo hayo, kwa mfano tuna eneo la kutoka Govu, kata ya Govu, kata ya Kijaka na kata ya Kisarawe tu ni eneo kubwa lenye ekari nyingi tu lilichukuliwa na

jeshi la wananchi wa Tanzania kwa ajili ya kazi maalum. Lakini tokea mwaka huo walipochukua wananchi hawajalipwa fidia zao mpaka leo, ni jambo la kusikitisha, na la kusikitisha zaidi ni kwamba walizuiwa wasiendeleze chochote na eneo ni kubwa sana inahusisha wananchi wengi sana. Tuna eneo la DAWASA ambao kuna mradi wa maji wanachimba visima ishirini pale katika eneo la Kata ya Kisarawe tu ambao utagharimu kiasi cha shilingi bilioni 161, ni mradi mkubwa sana ambao utalisha wilaya yote ya Temeke. Ni mradi mzuri na ni maendeleo lakini tuna tatizo vilevile la malipo ya fidia, wananchi wamezuia kuendeleza na wao ndiyo wakulima, ndiyo uti wa mgogo wa maisha yao, hawajui wafanye nini wamechanganyikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo la fidia vilevile katika barabara ya Kilwa, watu wamebomolewa nyumba zao na maeneo ya biashara zao lakini namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba hilo ameliona, tumepeleka hoja kwake amelikubali na Serikali inalishughulikia. Lakini naomba tu kwa upande wa fidia hii ya barabara ya Kilwa kwamba Serikali iongeze juhudili wananchi nao watokane na adha na uzia uliowakabali kwa miaka mingi. Naishukuru sana Serikali kwa uamuzi wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la uvuvi, niishukuru Serikali imetujibu hapa kwamba kuna maeneo mengi ya kodi, lakini ningeomba Serikali itoe kipaumbele cha kutosha kwenye sekta hii ya uvuvi. Mimi naweza kujiita ni mvuvi, nimewahi kuvua sana wakati wa utoto wangu, bahari ina tija sana, maziwa yana tija sana, naomba Serikali ichukue maamuzi ya makusudi ili sekta ya uvuvi ipewe kipaumbele na iweze kuleta tija zaidi katika mapato ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano uvuvi wa samaki aina ya kamba yaani *prawns* hasa katika ukanda ule wa Rufiji, tukiweka utaratibu mzuri tutapata mapato na Serikali itashangaa, nilishaijulisha sana Serikali kuona uvuvi huu nao ni muhimu kwenye ukanda ule wa kutoka Rufiji hadi Mafia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na taasisi iliyokuwa ikiitwa *TAFICO*. *TAFICO* imekufa lakini kuna miundombinu pale, inasikitisha sana kwani miundombinu ile imetupwa kwa muda mrefu, ukienda pale mali walizoacha ndugu zetu Wajapani kwa kweli inasikitisha. Naiomba Serikali ilifanyie kazi suala hili la *TAFICO*, wataalamu ambao walikuwa wanaitumikia *TAFICO* wapo, ile miundombinu iendelezwe na kuna mtambo mkubwa sana pale wa kuhifadhi samaki. Pia kuna vyama vyaya wavuvi angalieni uwezekano wa kuwakabidhi huu mtambo wa kuhifadhi samaki kwenye soko la *ferry* waweze kuutumia ili usiendelee kuharibika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna msongamano barabara ya Kilwa kipande kidogo tu, kwa taarifa nilizonazo Serikali imechukua juhudili itaongeza kilomita moja ya lami kuondoa msongamano ule lakini mpaka leo amri na maagizo hayo toka yatolewe hakuna kinachotekelizwa na kikubwa tukiuliza tunaambiwa ni taratibu za manunuzi. Nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo yeche ndiye msimamizi mkubwa wa shughuli za Serikali waangalie utaratibu huu ili adha na uzia tuondokane nao kwani tunapata taabu sana,

tunaomba tuondokane na tatizo hilo na hiyo kilomita moja tulioahidiwa na Serikali kumaliza tatizo hilo iweze kufanyiwa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naitahadharisha Serikali vilevile kwenye sekta ya bima. Sekta ya bima ni muhimu sana, kuna nchi nyingine katika Afrika wao waliwekeza, wamechukua, wameingia kwenye mkondo wa kuweka bima mali zote za Serikali. Hii nakumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu aliwahi kulitolea changamoto. Sasa naomba kuitahadharishe vilevile Serikali kwamba ione umuhimu wa kuwekea bima mali za Serikali na kama mchakato upo basi uendelezwe kwa nguvu zake zote, tumepatwa na majanga makubwa ndugu zangu kama kuungua kwa Benki Kuu ya Tanzania, kuungua kwa Wizara ya Mambo ya Ndani, kuzama kwa *MV Bukoba* na kadhalika yote haya kama tungkuwa na utaratibu kama huu ungetusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mabasi kwa ajili ya usafiri wa wanafunzi Dar es Salaam, naipongeza sana Benki ya CRDB lakini kama Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye hotuba yake alivyotoa wito kwenye mashirika ya umma basi naomba hili nalo walipe kipaumbele, watusaidie mkoaa wa Dar es Salaam. Ukiona wanafunzi wanatoka Temeke, Tandika na kadhalika wanakwenda sehemu Pemba Mnazi, Mji Mmwema, Kisota na kadhalika wanapanda malori, ni hatari na inasikitisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa changamoto kwa mashirika ya umma mengine pamoja na benki nyingine waangalie hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mfuko wa maafa. Mfuko wa Maafa uko kwa ngazi ya Taifa, lakini tuna maafa ambayo yanampata mtu mmoja mmoja na maafa hayo kwa kweli yanakuwa huwezi kuyaacha matokeo yake anayebeba mzigo ni Mbunge, Diwani, Mwenyekiti wa Mtaa na kadhalika. Sasa naomba kuiomba Serikali na Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaomba sana hilo kwamba mziagize Halmashauri zetu aidha, kuanzia mwaka huu wafanye *reallocation* au kuanzia mwaka ujao wa fedha lakini Halmashauri ziwe na mfuko wa maafa ili linapotokea janga ambalo huwezi kulifumbia macho liweze kumsaidia huyu mtu mmoja aliyeunguliwa na nyumba yake na kadhalika. Sasa tupunguzieni mgizo kidogo Wabunge na Madiwani mtusaidie hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala la leseni za makazi, tulisema kwenye ilani yetu hili tutalisimamia lakini linasuasua hasa kule Wilayani Temeke kuna masikitiko mengi tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwinchoum na Waheshimiwa Wabunge, naomba niwapongeze sana kwa michango mbalimbali ambayo imetoka kwa siku ya leo, tutakubaliana kwamba kwa kweli shughuli yetu inaendelea vizuri na mjadala wetu unaendelea kesho ambapo Mheshimiwa Paschal Degera, atatufungulia mjadala baada ya kipindi cha maswali na atafuatiwa na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa na Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa. Nimewataja watatu wa mwanzo na wengine

waendelee kijiandaa na orodha imebandikwa katika Jengo la Utawala, kwa hiyo, anayetaka kujua orodha ya majina. (*Makofî*)

Ninapenda kuwasisitiza Waheshimiwa ambao wako katika orodha ni vizuri kuwepo ili kutoleta usumbufu kwa kuja baadaye wakati orodha imeshasogea mbele itakuwa si sawa. (*Makofî*)

Basi baada ya maneno hayo naomba kuchukua nafasi ya kuahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. (*Makofî*)

(*Saa 1.45 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,  
Tarehe 17 Juni, 2010 saa tatu asubuhi*)